# Ujumbe – Sehemu Ya Kwanza

# Ujumbe - Sehemu Ya Kwanza



Ja'far Subhani

Kimetafsiriwa na
Dhikiri U M Kiondo

Al-Islam.org

## Author(s):

Ja'far Subhani [1]

## Publisher(s):

Al Itrah Foundation [2]

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, The Message, kilichoandikwa na Sheikh Ja'far Subhani. Sisi tumekiita, Ujumbe. Kwa vile kitabu hiki ni kikubwa, tumekigawa katika juzuu nne ili kuwarahisishia wasomaji wetu kukisoma kwa makini katika kila sehemu. Hii uliyonayo mkononi ni Juzuu ya Kwanza.

Kitabu hiki kilichoandikwa na mwanachuoni mkubwa Sheikh Ja'far Subhani kimekuwa ni miongoni mwa vitabu bora vilivyofanya utafiti wa kina kuhusu historia ya Uislamu na Waislamu. Haya ni matokea ya utafiti wa kielimu pamoja na hoja zenye nguvu na utumiaji sahihi wa akili uliofanywa na mwanachuoni mwandishi wa kitabu hiki juu ya maudhui haya yaliyotaja hapo juu.

Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kuchapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Get PDF [3] Get EPUB [4] Get MOBI [5]

## Translator(s):

Dhikiri U M Kiondo [6]

## Topic Tags:

History [7]
Knowledge [8]
Shariah [9]
Arabs [10]
Surah [11]

**Person Tags:**

Imam Ali [12]

Prophet Muhammad [13]

Imam Ja'far al-Sadiq [14]
Prophet Ibrahim [15]

# Kuhusiana Nasi

(Inawahusu watoaji wa toleo la Kiingereza ambalo kitabu hiki ni tafsiri yake)

Leo hii, akili iliyo macho huyaona mabadiliko kwenye maisha ya kiakili ya mwanaadamu. Sayansi na teknolojia, vikiwa kwenye ustawi wake wa juu zaidi, vyaelekea kukifikia kipeo chake cha mwisho. Mahitaji ya kimwili pamoja na tamaa ya mamlaka na tawala vimemwongoza mwanaadamu kwenye ufisadi wa dhahiri wa maadili yake. Katika hali hii ya kukatisha tamaa, mtu alazimika kutulia na kuitathmini hatari iliyojificha na inayowatishia wanaadamu wote kwa ujumla. Mwanaadamu, tayari kaisha mkodolea macho tena Allah, Mwingi wa rehema, Rahimu, kwa kuwa, sasa kaishatambua ya kwamba ufumbuzi wa matatizo yake na wokovu wake umo kwenye kuzifuata Amri za Allah.

Mgeuko huu, wa kutoka kwenye fikara za kimwili na kuja kwenye fikara za kiroho unaafikiana kabisa na malengo na shabaha za hii Seminari ya kiislamu. Mafundisho ya dini yanakwenda sambamba na maendeleo ya huu wakati wetu, yakitoa kimbilio lihitajiwalo mno na akili yenye kusumbuka na mashaka. Haya ni matokeo ya mtanabahisho, ya kwamba sasa inatambulikana ya kwamba siri ya kuishi maisha ya kiuchamungu kwenye ulimwengu huu huongoza kwenye baraka ya milele ya maisha ya Ahera. Huu ndio ujumbe wa UISLAMU kwa ulimwengu mzima.

Hii Seminari ya kiislamu inadhamiria kuinua juu kurunzi ya mwongozo wa kiroho na kusaidia kwa juhudi zote katika kuukuza urithi wa mwanaadamu. Inaionyesha njia ya maisha ifundishwayo na Qur'ani katika utukufu wake wa asili. Inayaonyesha yale yenye nguvu na yaliyo ya kweli tu. Vitabu vyake vimekusudiwa kufaa katika kuyafikia mahitaji ya kiroho ya zama zetu hizi. Vitatumika kama kijito kitiririkacho maji daima, kwa wale walio na kiu ya elimu.

Hii Seminari ya kiislamu ni taasisi ya ulimwengu mzima yenye kujitahidi katika kudumisha udugu wa kiislamu. Inafurahia mchango wa akili zilizo bora zaidi, zaidi ya kuwa na msaada wa kimataifa kwa ajili ya kuyafikia malengo yake makuu. Inavyo vituo Canada, na Mashariki ya Mbali.

Orodha ya anwani iko kwenye kurasa za mwisho za kitabu hiki. Msomaji (wa Kiingereza) anaweza kukiandikia barua chochote miongoni mwa vituo hivi ili kuvipata vitabu vyetu.

**Islamic Seminary Publications**

# Kwa Ndugu Msomaji

**Asalaam Alaykum**

Kitabu hiki kinatolewa na Seminari ya kiislamu (S.L.B. 5425, Karachi, Pakistan). Vitabu vyake vimelengwa kuyatimiza mahitaji ya kiroho ya zama zetu hizi, na msisitizo maalum juu ya kuzisafisha akili na fikara. Juhudi nyingi zimefanywa na Seminari hii kuweka kwenye vitabu vyake yale yaliyo na nguvu na yaliyo ukweli halisi kwenye Uislamu. Unaombwa kukisoma kitabu hiki katika hali iliyodhamiriwa. Vilevile unaombwa kuwasiliana nasi, kuhusu maoni yaliyo huru kuhusu vitabu vyetu, jambo tutakalolipenda mno.

Kuubalighisha ujumbe wa Uislamu ni jukumu lihitajilo ushirikiano wa watu wote. Seminari hii inakukaribisha ushiriki kwenye jukumu hili ukiuitika mwito wa aya ya Qur'ani Tukufu isemayo:

{قُلْ إِنَّمَا أَعِظُكُمْ بِوَاحِدَةٍ ۖ أَنْ تَقُومُوا لِلَّهِ مَثْنَىٰ وَفُرَادَىٰ ثُمَّ تَتَفَكَّرُوا ۚ {46

***"...Sema: Mimi ninakuahidini jambo moja tu, ya kwamba msimame kwa ajili ya Allah, wawiliwawili na mmoja-mmoja..."*** (***As-Saba 34: 46***).

**Allah na Akubariki.**
**Nduguyo katika Uislamu,**
**Katibu wa Uchapishaji.**

# Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, The *Message,* kilichoandikwa na Sheikh Ja'far Subhani. Sisi tumekiita, *Ujumbe.* Kwa vile kitabu hiki ni kikubwa, tumekigawa katika juzuu nne ili kuwarahisishia wasomaji wetu kukisoma kwa makini katika kila sehemu. Hii uliyonayo mkononi ni Juzuu ya Kwanza.

Kitabu hiki kilichoandikwa na mwanachuoni mkubwa Sheikh Ja'far Subhani kimekuwa ni miongoni mwa vitabu bora vilivyofanya utafiti wa kina kuhusu historia ya Uislamu na Waislamu. Haya ni matokea ya utafiti wa kielimu pamoja na hoja zenye nguvu na utumiaji sahihi wa akili uliofanywa na mwanachuoni mwandishi wa kitabu hiki juu ya maudhui haya yaliyotaja hapo juu.

Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika

nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kuchapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, Maalim Dhikiri Kiondo (Allah *'Azza wa Jalla* amkubalie amali zake na amweke karibu na Maasumina 14 [a.s.] – Amin) kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

**Mchapishaji:**
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar-es-Salaam, Tanzania

# Utangulizi

**Kwa Jina La Allah, Mwingi Wa Rehema, Rahimu.**

Tangu zamani za kale, mwanadamu amekuwa akiitafuta elimu kupitia milango yake ya fahamu. Hivyo basi, kwa kuvitambua vitu, hujaribu kulitatua tatizo lake. Katika mchakato huu, amekuwa akifanya majaribio, na hatimaye kwa kubahatisha alifikie kwenye ufumbuzi uwezekanao wa matatizo yake. Ikiwa imetegemea juu ya dhana na utendaji huu, sayansi ilistawi kwa ukubwa mno kwenye maeneo na nyanja mbali mbali za matumizi yake.

Kwenye zama hizi mpya za sayansi, mamia na maelfu ya maabara ya utafiti yanavutia nadharia ya wanasayansi ambao hufanya ugunduzi na ubuni- fu mkubwa mno wa kiwango cha kutoaminika cha usahihi wa ala na zana. Vivyo, kitu pekee ambacho hadi sasa sayansi imeshindwa kukikamata ni tatizo la kijamii. Ni dhahiri kwamba matatizo ya kijamii ni matatizo ya wanadamu. Na matatizo ya wanadamu ni ya hali ambayo haiwezi kuingizwa kwenye neli ya majaribio/testityubu (test-tube). Ili kuisadiki habari hii, mtu yuatambua vizuri mno kwa mfano, ya kwamba bado sayansi haijatoa jibu la kutoafikiana na chuki iliyomo miongoni mwa watu au tofauti za kimatabaka zinazokithiri kwenye matabaka ya jamii za wanaadamu.

Historia inatuambia kuhusu ustaarabu mkubwa uliopita hapo kale na mwishowe ukapotea. Hivi sasa tumebakiwa na masalio na magofu bubu yanayotukumbusha zama za kale za wanaadamu, zilizochakaa. Hakuna shaka kwamba sayansi inagundua habari za maisha kwa njia ya ufukuaji wa mashimo yanayodhaniwa kuwa na vitu vya kale kwa ajili ya uchunguzi, na kwa kujifunza masalio ya vitu

visisivyo na uhai (relics) na (vikisukuku) vile vyenye uhai vilivyogeuka kuwa mawe (fossilis), vilivyogandamana na miamba ya ardhi. Lakini tukiyaachilia mbali yote hayo, hakuna matokeo ya dhahiri yaliyopatikana kuhusiana na matatizo mengi ya wanaadamu.

Imam Ali (a.s.) alimpa dokezo la fikara zake mwanawe ambalo ni lenye kuhusika na jambo hili. Alisema: “Mwanangu mpenzi! Ingawa muda wa maisha yangu si mkubwa kama ule wa watu wengine waliofariki dunia kabla yangu, lakini nilijichukulia hadhari kubwa kujifunza maisha yao, kwa juhudu nyingi niliyapitia matendo yao, nilizifikiria fikara na matendo yao. Niliyachunguza masalio ya vitu vyao visivyo na uhai na magofu; na nikayafikiria maisha yao kwa makini mno kiasi kwamba nilijihisi kana kwamba niliishi na kufanya kazi pamoja nao tangu kwenye zama za awali za historia hadi kwenye hizi nyakati zetu, na ninayajua yaliyowatendea mema na yaliyowadhuru.”

Hakika, historia imeandika habari zote, zile zenye kupendeza na zenye kuchukiza, lakini lile lisikitishalo ni kwamba hakuna yeyote aliyejali kuzama ndani ya kina cha sababu za habari hizo. Ama kuhusu ufumbuzi halisi wa tatizo, liwe kubwa au dogo, hakuna juhudi katika upande wa mwanaadamu uonekanao kwenye historia. Ni yale mambo yasiyo muhimu ndiyo yaliyoshughulikiwa kwa maelezo marefu yaogofyayo.

Kwa kuwa historia ni masimulizi ya matukio ya kale yaliyoandikwa, yana- pata kuwepo kwake kutoka kwa mwandishi wake. Watu walioiandika historia hawakuwa huru kutokana na kiburi cha ubinafsi, rangi au sehemu atokayo mtu, na hivyo basi, lengo lake hasa laonekana kushindwa.

Mbele ya tafsiri mbaya na uzushi wa habari za kihistoria, msomaji wa kawaida wa historia yumo kwenye hasara ya kuuelewa ukweli wa jambo hilo. Ni kama daktari ambaye, kama hana taarifa sahihi kuhusu maradhi ya mgonjwa wake anayemwuguza, hataweza kuchunguza maradhi halisi ya mgonjwa wake huyo.

Hakika sifa moja ya historia iangazayo mno ni kwamba, inazichukua taarifa za maisha ya watu wakuu wa kale. Hakika watu hawa waliiunda historia kwa kuwa walileta mapinduzi na mabadiliko kwenye mtindo wa maisha ya wanaadamu.

Miongoni mwa hawa watu wakuu hakuna hata mmoja aliyeishi maisha yenye mambo mengi, ya kimapinduzi na yenye maana kama aliyoishi Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.).

Hakuna yeyote miongoni mwao aliyeziacha athari za kudumu kwenye jamii aliyojitokeza kama alivyofanya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Huu ni ukweli uliokubaliwa na karibuni wanahistoria wote, wawe ni wa Mashariki au wa Magharibi.

Kujifunza maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w), mkuu zaidi miongoni mwa wanaadamu wote, kunachukuliwa kuwa ni kwenye kuleta hofu na kujierevusha. Nyororo ya matukio ya kabla na ya baada ya kuzaliwa kwa huyu mtu mkuu kunatoa mawazo kwa ajili ya kila mtu aliye na japo punje ndogo tu ya akili na hisia za ulinganifu.

Kuzaliwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) akiwa yu mtoto aliyezaliwa baada ya baba yake kufariki dunia, na kifo cha mama yake, Bibi Amina (a.s.), alipokuwa na umri wa miaka sita tu, na kulelewa kwake, kwanza na babu yake na kisha na ami yake ni mambo yasiyo kifani.

Baada ya kuyapitisha maisha yenye mambo mengi, kujitenga kwake kwenye Pango la Mlima Hira na Ufunuo wa Allah uliofuatia, kuwaitia watu kwenye dini ya Allah, upinzani wa makafiri na wenye kuabudu masanamu, maonevu na mateso yao, umadhubuti wake uliodumu katika kuimarisha ujumbe wa Allah kwenye kipindi cha miaka kumi na mitatu ya mwanzo ya Utume wake mjini Makkahh hadi kwenye muda wa kuhamia kwake Madinah, ni matukio yasiyo kifani kwenye historia.

Miaka kumi ya mwisho ya maisha yake mjini Madina, kuimarisha kwake juhudi za ujumbe wake kwa ajili ya uenezaji wa Uislamu, kushiriki kwake kwenye vita nyingi dhidi ya makafiri na hatimaye kutekwa kwa Makkahh bado ni matukio makuu yenye kuonekana kuwa si ya kuaminika, lakini yameandikwa kwenye historia kuwa ni mafanikio ya kimiujiza.

Mamia ya vitabu yameandika kuhusiana na maisha na ujumbe wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) lakini vitabu hivi haviwezi kuchukuliwa kuwa ni wasifu kamili juu ya sifa na mafanikio yake. Hasa yale maandishi ya mustashrik yameingiliwa na chuki, makosa na tafsiri potofu.

Kitabu hiki sio tu kwamba kinatoa mambo yenye kuongoza, bali vile vile kimezitegemeza taarifa zake kwenye maandiko ya kihistoria yaliyo ukweli. Moja ya sifa zake zijidhihirishazo mno ni kwamba mwandishi amechukua hadhari kubwa katika kuyasimulia matukio ya kihistoria, na wakati huohuo amejitahidi, akiwa yu mwanachuoni mtafiti, kuyaendea matukio hayo kwa fikara zenye kuchanganua mambo pia.

Sifa nyingine, ya kitabu hiki yenye kuvutia ni kuwa kiko huru kabisa kutokana na uzushi na hadithi zilizobuniwa zilizozushwa na faida zilizofichwa.
Kwa maneno mengine ni kwamba, kiko kabisa kwenye hali ya kusalia kwenye kiwango kihitajikacho cha ukweli wa kihistoria. Kwa kifupi ni kwamba, kinapelekwa kwa Waislamu kwa ujumla, bila ya upen- deleo na kiburi.

Tunategemea ya kwamba kitabu hiki kitalifikia lengo lake la kukiongoza kizazi kichanga chenye shauku kuu ya kujipatia taarifa za kweli na zenye kutegemewa juu ya huyu Mtume Mkuu wa Uislamu (s.a.w.w), na tunaamini ya kwamba vijana wetu wa kiislamu watajipatia mwongozo kutokana na kitabu hiki katika kuyatengeneza maisha yao kwa mujibu wa maamrisho ya Allah pamoja na sifa tukufu za Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na Dhuria wake Wateule (a.s.).

# Sura Ya Kwanza: Rasi Ya Bara Arabu

## Chimbuko La Utamaduni Wa Kiislamu

Arabia ni Rasi kubwa iliyoko Kusini-Magharibi mwa Bara la Asia. Eneo lake ni kilometa za mraba milioni tatu, karibuni maradufu ya eneo la Iran, mara sita ya lile la Utaliani na mara themanini ya lile la Uswisi.

Rasi hii ina umbo la pembe nne zisizo sawa na inapakana na Palestina na jangwa la Sham kwenye upande wa Kaskazini, na Hira, Mto Tigri, Mto Frati na Ghuba ya Uajemi kwenye upande wa Mashariki, na Bahari ya Hindi kwenye upande wa Kusini, na Bahari ya Sham kwenye upande wa Magharibi.

Hivyo, kwenye upande wa Magharibi na Kusini imepakana na bahari, na kwenye upande wa Kaskazini na Mashariki imepakana na jangwa na Ghuba ya Uajemi.

Tangu kwenye Zama za Kale, nchi hii imekuwa ikigawanywa katika mikoa mitatu:

Mkoa wa Kaskazini na Magharibi unaoitwa Hijaz;
Mkoa wa Kati na Mashariki, uitwao Jangwa la Uarabuni; na
Mkoa wa Kusini, uitwao Yemen.

Kwenye Rasi hii, mtu huyaona majangwa mengi yaliyo mapana na maeneo ya mchanga yenye joto kali ambayo karibuni si yenye uwezo wa kukaliwa na watu. Moja ya majangwa haya ni Baadyah Samawah ambalo siku hizi huitwa Nafusi. Vilevile liko jangwa pana jingine linalotanda hadi kwenye Ghuba ya Uajemi na sasa laitwa Rub'ul Khaali. Hapo awali sehemu moja ya majangwa haya iliitwa Ahqaaf na ile nyingine iliitwa Dahna.

Kutokana na kuwapo kwa majangwa haya, karibuni theluthi moja ya eneo la Rasi hii ni kame na isiyofaa kwa makazi ya wanaadamu. Ni katika nyakati fulani-fulani tu kiasi kidogo cha maji chaweza kupatikana kwenye maeneo machache, ikiwa ni matokeo ya mvua kwenye joto la majangwa hayo, na baadhi ya makabila ya kiarabu huwapeleka ngamia na mifugo yao mingine kwenye maeneo hayo kwa ajili ya malisho.

Hali ya hewa ya Rasi hii ni ya joto sana na kavu kwenye majangwa na kwenye maeneo ya kati. Kwenye maeneo ya pwani kuna unyevunyevu na hali ya hewa isiyo ya joto kali wala baridi kali kwenye baadhi ya sehemu. Ni kwa sababu ya hali yake ya hewa isiyofaa kwamba idadi yake ya wakazi haizidi milioni kumi na tano.

Kwenye nchi hii mna safu ya milima inayonyooka tangu Kusini hadi Kaskazini, kilele chake kina urefu wa meta 2470.

Tangu kwenye Zama za Kale, migodi ya dhahabu na fedha na mawe mengine ya thamani imekuwa asili

ya utajiri wa Rasi hii. Kutoka miongoni mwa wanyama waliofugwa na Waarabu, wamo ngamia na farasi. Ama kuhusu ndege, njiwa na mbuni walikuwa wengi kuliko ndege wengine. Siku hizi asili kuu zaidi ya mapato ya Uarabuni ni uchimbaji wa mafuta na gesi. Kituo cha akiba ya mafuta cha Rasi hii ni mji wa Dhahraan ambao Wazungu huuita Dahraan. Mji huu umo kwenye wilaya ya Saudia iitwayo Ahsaa jirani na Ghuba ya Uajemi.

Ili kwamba mheshimiwa msomaji aweze kufahamishwa zaidi kuhusu hali ya Uarabuni, sasa tunaendelea kukupa maelezo marefu kidogo ya ile mikoa mitatu tuliyoitaja hapo juu:

**Hijaz**: Inajumlisha ukanda wa Kaskazini na Magharibi wa Uarabuni nao unatanda tangu Palestina hadi Yemen, unapakana na pwani ya Bahari ya Sham. Hili ni eneo lenye vilima na lenye majangwa mengi yaliyo kame na maeneo ya mawe mawe.

Mkoa huu una sifa njema zaidi kwenye historia kuliko ile mingine. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba hizi sifa njema zilitokana na msururu wa mambo ya kiroho na kidini. Kwa mfano hata kwenye huu wakati wa sasa, Al- Ka'ba, Nyumba ya Allah iliyoko kwenye mkoa huu ni Qiblah cha mamia ya mamilioni ya Waislamu wa Ulimwengu mzima.

Eneo linaloizunguka Al-Ka'ba limekuwa likiheshimiwa na Waarabu na wale wasio Waarabu pia kwa karne nyingi za kabla ya Uislamu. Ikiwa ni dalili ya heshima kwa eneo hili, waliamini kuwa kupigana vita ndani ya mipaka ya Al-Ka'ba ni haramu na hata Uislamu umelitambua eneo lizunguukwalo na mipaka hii kuwa ni lenye kustahili heshima.

Miji ya Makkahh, Madinah na Taa'if ndio miji muhimu ya Hijaz. Tangu kale Hijaz imekuwa na bandari mbili. Ya kwanza ni Jiddah inayowahudumia watu wa Makkahh, na nyingine ni Yanbu, ambayo kupitia hapo, watu wa Madinah huingiza baadhi ya mahitaji yao. Hizi bandari mbili zimo kwenye pwani ya Bahari ya Sham.

## Makkah:

Ni mmoja miongoni mwa miji maarufu ya ulimwenguni na ni mji wa Hijaz wenye wakazi wengi zaidi, nao uko kiasi cha meta 300 juu ya usawa wa bahari. Kwa vile mji huu uko baina ya safu za milima miwili, hauwezi kuonekana kwa mbali. Idadi ya wakazi wa Makkahh hivi sasa ni watu 200,000.

## Historia Fupi Ya Makkah:

Historia ya mji wa Makkahh huanzia kwenye wakati wa Nabii Ibrahim (a.s.). Nabii Ibrahimu (a.s.) alimpeleka mwanawe Nabii Isma'il (a.s.) pamoja na mama yake Haajar (a.s.) kwenye nchi ya Makkah kuishi hapo. Mwanawe alioa kwenye kabila lililokuwa likiishi karibu na hapo. Nabii Ibarahim (a.s.) aliijenga Al-Ka'ba kwa amri ya Allah na baada ya hapo yalianza makazi ya watu hapo Makkahh.

Ardhi ya viungani mwa mji wa Makkahh kidogo ni ya chumvi na hailimiki kabisa. Kwa mujibu wa baadhi

ya wataalamu wa elimu ya nchi za Mashariki, hali yake ya kijiografia iliyo mbaya haina kifani hapa duniani.

## Madinah:

Madinah ni mji ulioko umbali wa *leagues* 90 (Kilometa 432) kaskazini mwa mji wa Makkahh.
Una mabustani na mitende kwenye sehemu zote zizungukazo mji huu na ardhi yake ni yenye kufaa kwa mashamba ya miti na kilimo cha nafaka.

Kabla ya Uislamu mji huu uliitwa Yathrib, lakini baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kuhamia mjini humu, ukaitwa Madinatur-Rasul (Mji wa Mtume). Hata hivyo, baadae neno la Mwisho liliachwa ili kuweza kulifupisha na hapo ukaitwa Madinah tu. Historia yatueleza ya kwamba watu wa kwanza kuishi mjini hapa walikuwa ni kikundi cha Amaaliqah. Wale ambao waliowafuatia hao ni tapo moja la Wayahudi na makabila ya Aws na Khazraj ambao baadae walifahamika miongoni mwa Waislamu kwa jina la Ansar (Wasaidizi).

Ukiwa tofauti na mikoa mingine ya Uarabuni, Hijaz ulisalia kuwa salama kutokana na mashambulio ya maadui, na dalili za ustaarabu wa Urumi na Uajemi; falme mbili kubwa za ulimengu wa kabla ya Uislamu, haziwezi kuonekana hapa. Ilikuwa hivyo kwa sababu ardhi yake kame na isiyokalika haikuwezesha kuwafaa wageni kufanya safari za kijeshi ili kuichukua na kisha warudi mikono mitupu, baada ya kuyakabili maelfu ya matatizo yaliyotazimiwa katika kuichukua.

Kuhusiana na jambo hili, mtu anaweza kujifunza hadithi ifuatayo kwa makini. Hadithi hii imenukuliwa na mwanahistoria wa kigiriki aliyeitwa Deodre (aliyeishi kwenye miaka ya kabla ya Masih). Aliandika hivi: "Chifu Mkuu wa kigiriki, Demetrius alipofika Patra (mmoja wa miji ya kale ya Hijaz) kwa lengo la kuitwaa Arabia, wakazi wa mji huo walimwambia: 'Ewe chifu wa Kigiriki! Kwa nini wapigana nasi? Tunaishi kwenye jangwa ambalo umasikini wa kila namna ndio chanzo cha maisha. Tumelichagua hili jangwa kame ili kwamba tusihitaji kuzitii amri za mtu yeyote. Hivyo basi, tafadhali zipokee zawadi na tuzo zetu duni na uache kuikalia nchi yetu.

Na kama ukiendelea kuishikilia azma yako, basi sisi tunatamka dhahiri ya kwamba, hivi karibuni utakabiliwa na maelfu ya matatizo na magumu. Na ufahamu ya kwamba 'Wanabti' hawaelekei kuuacha mtindo wa maisha yao.

Hivyo basi, iwapo utawateka kwa nguvu baadhi ya watu wetu, na ukataka kuwachukua nje ya nchi hii, hili halitakusaidia, kwa kuwa watakuwa watumwa waovu na wenye tabia mbaya tu, na hawatakuwa tayari kuubadili mtindo wao wa maisha."

Yule chifu wa kigiriki aliukubali ujumbe wao wa amani na kutakiana heri na akaliacha lile wazo la kuishambulia na kuikalia nchi ya Uarabuni."[1]

**Mkoa wa Kati Na Mashariki:** Unaoitwa 'Jangwa la Uarabuni' na unaujumuisha Ukanda wa Najd. Ni

uwanda wa juu unaokaliwa hapa na pale.

Baada ya familia ya Saudi kushika madaraka, wilaya ya Riyadh, ambayo ndio mji wao mkuu, imekuwa moja ya vituo muhimu vya Uarabuni.

**Urefu wa Yemen:** Mkoa wa Kusini-Magharibi wa Rasi hii ni kiasi cha kilometa 750, tangu kaskazini hadi kusini na kiasi cha kilometa 400 tangu magharibi hadi mashariki na eneo lake limekisiwa kuwa ni maili za mraba elfu sitini. Hata hivyo, hapo awali, eneo lake lilikuwa hata zaidi ya hapo na kwenye nusu karne iliyopita, sehemu ya mkoa huu (Aden) ilibakia kuwa kwenye hifadhi ya Kiingereza. Hivyo basi, Najd ikawa mpaka wake wa Kaskazini na Aden ikawa mpaka wake wa Kusini.

Bahari ya Sham iko magharibi kwake, na masharikini kwake inaligusa jangwa la ar-Rub'ul Khaali. Mji maarufu wa Yemen ni mji wa kihistoria wa San'a na bandari yake maarufu zaidi ni Hudaydah, iliyoko kwenye pwani ya Bahari ya Sham.

Nchi ya Yemen ndio tajiri zaidi kwenye Rasi hii. Hapo kale ilikuwa na ustaarabu mzuri na mtukufu. Yemen ilikuwa ndio makao makuu ya serikali ya wafalme wa ki-Tababi'ah, waliotawala kwa kipindi kirefu mno. Kabla ya Uislamu Yemen ilikuwa kituo kikuu cha uchumi na biashara, na kwa kweli ilifikiriwa kuwa ni 'njia panda' ya Uarabuni. Ilikuwa na migodi tajiri mno ya vito kama vile dhahabu, fedha, na mawe mengine ya thamani yaliyochimbwa huko. Madini hayo yalisafirishwa kwenda kwenye nchi nyingine.

Dalili na mabaki ya ustaarabu wa Yemen wa siku hizo bado vinapatikana. Kwenye kipindi ambacho mwanaadamu hakuweza kupata zana za kutekelezea kazi zenye udhia, watu mastadi wa Yemen waliweza kujenga majengo yapendezayo na marefu kutokana na kufanya kazi kwao kwa nguvu.

Wafalme wa Yemen, kupitia watawala wa nchi waliokubaliwa na watu wote, hawakusita kuhakikisha ya kwamba katiba iliyoandikwa na iliyothibitishwa na wataalamu wa nchi hiyo inatumika, na wakawazidi watu wengine katika kukikuza kilimo na kilimo cha bustani. Amri ndogondogo zinazohusu kilimo cha mashamba na unywesheaji wa makonde na bustani ziliandikwa na zikafuatwa. Kuhusiana na jambo hili, nchi hii yaaminiwa kuwa moja ya nchi zilizokuwa zikisifika na zilizoendelea kwenye zama hizo.

Mwanahistoria maarufu wa Kifaransa, aliyeitwa Gustave Le Bon, anasema: "Uarabuni kote hakuna mkoa uliostawi na ulio na rutuba zaidi ya Yemen."

Idrisi, mwanahistoria wa karne ya kumi na mbili aliyesifiwa mno anaandika hivi kulihusu jiji la San'a: "Hapa ndipo ulipo mji mkuu wa Uarabuni na makao makuu ya serikali ya Yemen. Majengo na Ikulu za jiji hili ni maarufu ulimwenguni kote. Hata yale majengo na nyumba zake za kawaida zimejengwa kwa mawe ya kuchonga."

Hizi kumbukumbu zenye kustaajabisha, zilizogunduliwa zikiwa ni matokeo ya ufukuaji na uchunguzi uliofanywa na mustashirik, zathibitisha kuwako sehemu mbalimbali za Yemen ya siku za kale, ambazo ni Ma'arib, San'a na Bilqis.

Kwenye jiji la Ma'arib (jiji maarufu la Saba) yalikuwako majengo marefu mengi yaliyokuwa na milango na matao yaliyotarizwa kwa dhahabu. Halikadhalika vyombo vya dhahabu na fedha pamoja na vitanda vya samadari vilivyotengenezwa kwa metali vilipatikana kwa wingi huko."[2]

Moja ya kumbukumbu za kihistoria za Ma'arib ilikuwa ni bwawa lake maarufu, ambalo dalili zake bado zinapatikana. Bwawa hili liliharibiwa na mafuriko yaliyozungumziwa katika Qur'ani Tukufu kwa jina la 'Mafuriko ya Iram.'

1. Tamaddhun-i-Islam wa Arab, Uk. 93-94
2. Tamaddun-i- Islam wa Arab, uk. 96.

# Sura Ya 2: Uarabuni Kabla Ya Uislamu

Ili kuielewa hali iliyokuwapo Bara Arabu kabla ya Uislamu vyanzo vifuatavyo vinaweza kututosha: Agano la Kale (licha ya kuwa na mabadiliko yote ambayo yaliyofanywa humo).

Maandishi ya Wagiriki na Warumi kwenye Zama za Kati.

Historia ya kiislamu iliyoandikwa na wanachuoni wa kiislamu, na Masalio ya zamani, yaliyopatikana kutokana na ufukuaji uliofanywa na mustashirik, ambao ulidhihirisha habari kwa kiasi fulani.

Licha ya vyanzo tulivyovitaja hapo juu, mambo mbalimbali yahusianayo na historia ya Uarabuni bado hayajaeleweka kwa ukamilifu, na yanasalia kuwa fumbo lisilofumbuka.

Hata hivyo, kwa vile kujifunza hali ya Uarabuni ya kabla ya Uislamu ni utangulizi tu wa mazungumzo yetu; lakini azma yetu hasa ni mchanganuo wa maisha ya Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w) hivyo basi, tunatoa hapa chini mukhtasari wa taarifa za baadhi ya watu na hali za mambo zilizo maarufu za Waarabu wa kabla ya Uislamu.

Ni ukweli ukubalikao kwamba tangu kwenye siku za kale, Rasi ya Bara Arabu ilikuwa ikikaliwa na makabila mengi, ambayo baadhi yao yamekwisha kupotea kutokana na kupita muda mrefu. Hata hivyo, kwenye historia ya nchi hii, makabila matatu yafuatayo, ambayo baadae yaligawanyika na kuwa koo nyingi tofauti, yalipata sifa kuu kuliko mengineyo:

**Waba'idah:** Neno 'Ba'idah' lina maana ya iliyokufa, isiyokuwepo tena, na watu hawa waliitwa hivyo kwa sababu, kutokana na uasi wao uliodumu, walifutiliwa mbali kutoka usoni mwa ardhi, ikiwa ni matokeo ya misiba ya mbinguni na ya duniani. Inawezekana kwamba watu hawa ndio waliokuwa makabila ya Waadi na Wathamudi waliokuwa wakitajwa mara kwa mara kwenye Qur'ani Tukufu.

**Waqahtani:** Hawa walikuwa ni vizazi vya Ya'rab bin Qahtani. Watu hawa waliishi nchini Yemen na

sehemu nyingine za Bara Arabu ya Kusini na waliitwa Waarabu wa damu kamili. Wayemeni wa siku hizi na makabila ya Aws na Khazraj, ambao waliyajumlisha makabila mawili makuu ya Madina, kwenye siku za awali za Uislamu ni wa kizazi cha Waqahtani. Walifanya juhudi za nguvu kwa ajili ya maendeleo ya Yemen na wameacha idadi kadhaa ya ustaarabu ukiwa ni kumbukumbu yao. Sasa watu wanajifunza maandishi yao, kwa mujibu wa njia za kisayansi, historia ya Waqahtani imegundua hivyo kwa kiwango fulani. Lolote lile lisemwalo kuhusu utamaduni wa kabla ya Uislamu na ustaarabu wa Bara Arabu linahusiana kabisa na kundi hili la Waarabu na linauhusu mkoa wa Yemen.

**Waadnani:** Hawa ni dhuria wa Nabii Isma'il (a.s.). Maelezo marefu ya nasaba ya kabila hili yatatolewa kwenye hatua itakayofuatia baadae, lakini tukizungumzia kwa kifupi tu, hali ni hii: Nabii Ibrahimu (as) aliamrishwa na Allah kumloweza mwanawe Isma'il (a.s.) na mamie Haajar (a.s.) kwenye nchi ya Makkahh. Hivyo basi akawasafirisha kutoka Palestina na kuwapeleka kwenye bonde lenye kina kirefu (Makkahh) lililokuwa kame kabisa. Allah Aliwahurumia na akawajaalia chemchemi ya Zamzam. Nabii Isma'il (a.s.) alioa kwenye kabila lililoitwa Jarham, lililokita mahema yao kwenye sehemu iliyokuwa karibu na Makkahh. Dhuria wake (Nabii Isma'il a.s.) walikuwa wengi. Mmoja wao alikuwa ni Adnan ambae alisogezwa mbele kwa vizazi vichache kutoka kwa Nabii Isma'il (a.s.).

Dhuria wa Adnan waligawanyika katika makabila mengi. Kabila lililojipatia sifa kutoka miongoni mwao lilikuwa ni lile la Quraysh, na Bani Hashim walikuwa sehemu ya kabila hili.

## Maadili Ya Waarabu Kwa Ujumla

Tunaposema hivi tuna maana ya maadili na tabia za kijamii zilizokuwapo miongoni mwa Waarabu kabla ya Uislamu. Baadhi ya desturi zikifuatwa na Waarabu wote. Sifa za Waarabu wote na zenye kustahili kusifiwa kwa ujumla zingaliweza kuelezwa kwa ufupi hivi, katika sentensi chache:

"Waarabu wa Zama za Ujinga (zama za kabla ya Uislamu) na hasa vile vizazi vya Adnan walikuwa wakarimu na wenye tabia ya ukaribishaji. Walivunja ahadi kwa shida mno. Waliamini kuwa kuvunja ahadi ni dham- bi isiyosameheka. Walikuwa wakiishika dini yao na walijaaliwa sifa kamili ya ufasaha wa lugha. Walikuwa na akili zenye uwezo mkubwa wa kukum- buka mambo. Kwa urahisi sana waliweza kujifunza beti (za mashairi) na hotuba kwa kukariri. Kwenye sanaa ya utunzi wa mashairi, waliwazidi wengineo wote.

Ushujaa wao ulikuwa ukifahamika kote. Walikuwa na ustadi mkuu kwenye mbio za farasi, na upigaji mishale. Waliamini kuwa kumkimbia adui ni jambo lenye kuchukiza na lisilopendeza kabisa.

Na pengine tungaliweza kuzitaja hapa sifa zao zilizokuwa njema zaidi. Hata hivyo, kinyume na hivi, silsila ya utovu wao wa maadili mema na tabia zao mbaya, ambazo kwa kiasi fulani, zimewafanya waichukue tabia ya pili, hufutilia mbali utukufu wa mafanikio, na kama wasingalifunguliwa dirisha kutoka kwenye yasiyoonekana, msokoto (scroll) wa maandishi wa maisha yao ya kibinaadamu ungekunjwa, nao wangeliangukia kwenye shimo lenye kina kirefu na lenye kutisha la kutokuwapo. Kwa kauli nyingine

ni kwamba, kama jina la Uislamu lilishalo nafsi lisingaliziangaza nyoyo zao katikati ya karne ya sita Masihiya, siku hizi usingaliziona dalili zozote za Waarabu na hadithi ya Waarabu wa Baaidah ingalirudiwa.

Kutokana na kukosekana kwa mwongozo na maelekezo sahihi, na kuwepo kwa utovu wa maadili mema, na imani za kishirikina, Waarabu walikuwa wakiishi maisha yaliyo sawa na yale ya wanyama. Historia imetuwekea kumbukumbu za hadithi za vita vya miaka hamsini na vita vya miaka mia, na hizo pia ni kwa sababu ndogo ndogo na zisizo na maana.

Huu utawala huria, ukosefu wa sheria na taratibu na kukosekana kwa serikali yenye mamlaka ambayo ingeliweza kuitawala hali ya mambo na kuwashughulikia waasi vipasikavyo, vilikuwa sababu ya Waarabu kuishi maisha ya kibedui na ya kuhama hama kwao kwa kila mwaka pamoja na wanyama wao wakiziendea sehemu za majangwa ambako maji na malisho viliweza kupatikana. Kila walipopata maji na majani mabichi mahali popote pale walikita mahema yao karibu na hapo. Hata hivyo, mara tu wapatapo mahali pafaapo zaidi, waliendelea na kuhamahama kwao kwenye jangwa.

Kuhamahama na hali ya kutokuwa na maskani maalum kulitokana na mambo mawili; kwanza ni ile hali mbaya ya jiografia ya eneo hili, na jingine ni kujitia kwao kwenye umwagaji wa damu uliokithiri, jambo lililowawajibisha kufanya misafara ya mara kwa mara na uhamiaji.

## Je, Waarabu Wa Kabla Ya Uislamu Walistaarabika

Kama matokeo ya mafunzo yake juu ya hali ya Waarabu wa Zama za Ujinga, mwandishi wa kitabu kiitwacho *'Tama-ddun-i- Islam wa Arab'* amemalizia kwa kusema kwamba Waarabu hao walikuwa wamestaarabika kwa karne nyingi.

Kwa mujibu wa maoni yake, majengo matukufu na marefu waliyoyajenga kwenye sehemu mbalimbali za Uarabuni na uhusiano wao na mambo ya kibiashara na mataifa mbalimbali yaliyoendelea, kunathibitisha kustaarabika kwao, kwa kuwa, watu walioweza kujenga majumba makubwa kama hayo hata kwenye kipindi cha kabla ya kuja kwa Warumi, na wakawa na uhusiano wa kibiashara na mataifa makuu ya ulimwengu, wasingeliweza kuitwa washenzi.

Tena, kwenye sehemu nyingine, ameitaja fasihi ya Waarabu na kuwa kwao na lugha kamili kuwa ni ushahidi wa kuliunga mkono dai lake hilo la kwamba walikuwa na ustaarabu uliokuwa na mizizi ya kina. Anasema: "Kwa mfano, tusikijue cho chote kile kihusianacho na historia ya Waarabu wa kale, vivyo, tungaliweza kuikataa dhana ya kuwa kwao watu wasiostaarabika, kwa sababu, chochote kile kihusianacho na lugha ya taifa, vilevile chahusiana na kustaarabika na utamaduni wa taifa hilo. Haiwezekani kwamba lugha nzuri mno yenye kuhusiana na uandishi wake, ijitokeze bila ya chanzo chochote. Zaidi ya hapo, udumishaji wa uhusiano na mataifa yaliyoendelea daima huwa ni njia ya maendeleo kwa watu wenye uwerevu."

Mwandishi tuliyemtaja hapo juu amezitumia kurasa kadhaa za kitabu chake kuthibitisha kuwapo kwa ustaarabu wa hali ya juu miongoni mwa Waarabu wa zama za kabla ya Uislamu na akaliweka tumaini lake kuhusiana na jambo hili kwenye mambo matatu, ambayo ni:

(1). Kuwa kwao na lugha nzuri zaidi.
(2). Kudumisha kwao uhusiano na mataifa yaliyoendelea
(3). Majengo mazuri mno ya Yemen yaliyotajwa na Herodote na Artemidor, wanahistoria mashuhuri walioishi mwenye zama za kabla ya kuzaliwa Nabii Isa (a.s.) pamoja na Mas'udi na waandishi wengine wa historia ya kiislamu.[1]

Hakuna shaka kuhusiana na ukweli uliopo kwamba, zilikuwapo staarabu za nyakati fupifupi kwenye sehemu mbalimbali za Uarabuni, lakini hoja alizozitoa mwandishi huyu hazitoshelezi kuthibitisha ya kwamba ulikuwapo ustaraabu na utamaduni kwenye sehemu zote za nchi hii.

Kwanza, kukamilika kwa lugha kunaandamana na dalili nyingine za ustaarabu, lakini kimsingi, kiarabu hakiwezi kudhaniwa kuwa ni lugha yenye kujitegemea, isiyohusika na Kiebrania, Kishamu, Kiassiria, Kikaldayo, kwa sababu, kama ilivyothibitishwa na wanafalsafa, lugha zote hizi zilihusiana kwenye wakati fulani na zote zilitokana na lugha moja. Katika hali hiyo, uwezekano uliopo ni kwamba, kiarabu kiliufikia ukamilifu wake pamoja na Kiebrania, na Kiassiria na ilijitokeza katika hali ya lugha binafsi baada tu ya kuufikia ukamilifu huo. Kuwa na uhusiano wa kibiashara na mataifa ya ulimwenguni yaliyoendelea bila shaka ni ushahidi wa maendeleo na ustaarabu wa Waarabu.

Hata hivyo, swali liibukalo hapa ni kama sehemu zote za Bara Arabu zilikuwa na uhusiano huo na mataifa mengine, au yawezekana kwamba Hijaz haikuwa nao? Zaidi ya hapo, uhusiano na Iran, na Wagiriki wa majimbo mawili ya 'Hira' na 'Ghassan' yaliyoko kwenye jimbo la Hijaz vile vile hauwi ushahidi wa kustaarabika kwao, kwa kuwa hali yao iliweza kuwa kama ile ya 'setalaiti', ambayo kwa kweli twaweza kuiita makoloni. Hata katika zama zetu hizi ziko nchi nyingi barani Afrika, zilizo sehemu ya makoloni ya nchi za magharibi, lakini hazina dalili zozote za ustaarabu na utamaduni wa kizungu.

Hata hivyo, haiwezekani kukana kwamba ulikuwako ustaarabu mzuri zaidi huko Saba na huko Ma'arib kwenye jimbo la Yemen. Kwa kuwa, tukiyaachilia mbali yale tuliyokwisha kuyasema kuhusiana na jambo hili, kwenye Agano la Kale, na yule mwanahistoria Herodote na wengineo, mwanahistoria mashuhuri, Mas'udi anasema hivi kuhusu mji wa Ma'arib: "Ulizungukwa na majengo mazuri, miti ya kivuli na vijito vitiririkavyo kwenye pande zote.

Eneo la jimbo hili lilikuwa pana mno kiasi kwamba hata mpandafarasi mwepesi wa mwendo asingaliweza kuumaliza urefu na upana wake kwenye muda wa mwezi mzima; na msafiri, awe anampanda mnyama au anasafiri kwa miguu, haweza kuliona jua anapoikata nchi kutoka mwishilizio mmoja hadi mwingine, kwa kuwa barabara zilifunikwa na miti ya kivuli kwenye pande zote mbili. Nchi hii iliendelea kustawi na maji yalipatikana kwa wingi. Na serikali yake iliyokuwa imara, ilikuwa maarufu duniani kote.[2]

Hata hivyo, iwekwe akilini kwamba habari hizi hazituongozi kwenye ustaarabu uliopasika kuwako mwenye majimbo yote ya Bara Arabu na hasa kule Hijaz, ambako kwa hakika hakukuwa na dalili zozote za ustaarabu huu, kiasi kwamba hata Bwana Gustave Le Bon, kuhusiana na jambo hili, anasema hivi: “Ukiiachilia mbali mipaka yake ya Kaskazini, Bara Arabu ilisalia kuwa huru kutokana na mashambulizi ya wageni na hakuna yeyote aliyeweza kuikalia. Washindi Wakuu wa Iran, Urumi na Ugiriki waliouteka ulimwengu mzima hawakuijali Bara Arabu hata kidogo.”[3]

Na hata kama tukichukulia kwamba hadithi hizi ni za kweli kuhusiana na majimbo yote ya Rasi ya Bara Arabu, yale yote tuwezayo kuyasema kwa uhakika ni kwamba, kwenye wakati wa kuingia kwa Uislamu haikuonekana dalili yoyote ya ustaarabu huo, kwa kuwa Qur’ani Tukufu inalitaja jambo hili na inasema:

{وَكُنْتُمْ عَلَىٰ شَفَا حُفْرَةٍ مِنَ النَّارِ فَأَنْقَذَكُمْ مِنْهَا ۗ {103

***“…; Na (enyi Waarabu! Kabla ya kusilimu kwenu) mlikuwa ukingoni mwa shimo la Moto wa Jahanamu Naye (Allah) Akawaokoeni nalo (kwa Uislamu)…” (Al- Imran 03: 103)***

Kurasa za Nahjul Balagha zilipokuwa zikiisimulia hali ya Waarabu wa kabla ya Uislamu, zina ushuhuda ulio hai kwamba, ukiliangalia jambo hili la mtindo wa maisha, akili, uchafu na kuharibika kwa maadili, waarabu walikuwa katika hali ya kuhuzunisha. Hapa tunanukuu maneno yaangazayo ya Sayyidna Ali, Amirul Muuminiina (a.s.). Kwenye moja ya hotuba zake anaielezea hali ya mambo ya Bara Arabu kwenye siku za kabla ya Uislamu hivi: “Mola Alimteua Muhammad kuwaonya watu wa ulimwenguni na kuwa mdhamini wa Ufunuo Wake na Kitabu chake.

Nanyi waarabu mlikuwa mkizitumia siku zenu kwa dini iliyokuwa mbaya zaidi ya zote na kwenye sehemu mbaya zaidi. Mlikuwa mkiishi kwenye sehe- mu za mawe na miongoni mwa nyoka walio vipofu (wasiosogea kwa sababu ya sauti yoyote ile). Mlikunywa maji ya tope na kula chakula duni (kama vile guruguja, na unga wa mbegu za tende). Mlimwaga damu yenu wenyewe na mkajitia kwenye kukata udugu. Mmewaweka masanamu miongoni mwenu. Hamkuziambaa dhambi.”

(**Nahjul Balagha, Hotuba ya 26**).

Hapa, mifano ya hali ya kishenzi ya Waarabu wa Zama za Ujinga imenukuliwa. Ikiwa kama mfano, tunanukuu hapa chini hadithi ya As’ad bin Zurarah inayotupa mwanga kwenye tabia mbalimbali za watu wa Hijaz:

## As’ad Bin Zurarah Akutana Na Mtukufu Mtume (S.A.W.W)

Kwa muda mrefu vita kali ilipiganwa baina ya makabila mawili (ya mjini Yathrib) Aws na Khazraj. Katika wakati huo, As’ad bin Zurarah, mmoja wa machifu wa Khazraj alifunga safari kwenda Makkahh kwa ajili ya kuimarisha nguvu ya kabila lake. Lengo lake lilikuwa kwenda kutafuta msaada wa kijeshi na kiuchumi

kutoka kwa Waquraishi ili kumshinda adui yake mwenye umri wa miaka mia moja (yaani kabila la Aws). Kutokana na uhusiano wake wa tangu kale na 'Atbah bin Rabiyyah, alifikia kwake. Alimweleza shabaha ya safari yake ile na akamwomba msaada. Hata hivyo, huyu rafiki yake wa tangu kale ('Atbah), alimjibu kwa maneno haya:

"Hivi sasa hatuwezi kuridhia ombi lenu kwa sababu sisi wenyewe tumo mwenye mashaka ya ajabu. Ameamka mtu kutoka miongoni mwetu. Anawatusi miungu wetu, anaamini kuwa jadi zetu walikuwa wapuuzi na wajinga. Kwa maneno yake matamu amewavutia baadhi ya vijana wetu na hivyo amejenga mfarakano mkubwa baina yetu. Anatumia muda wake mwingi kwenye 'Sha'ab (Njia ya Mlimani) ya Abu Twalib ila kipindi cha wakati wa Hajj. Hata hivyo, katika wakati huo wa Hajj, hujitokeza kutoka huko na kukaa kwenye Hajjar Isma'il. Hapo huwaitia watu kwenye dini yake."

As'ad aliamua kurudi nyumbani bila ya kukutana na machifu wengine wa Kiquraishi. Hata hivyo, ili kuitimiza desturi ya Waarabu ya tangu kale, aliamua kufanya ibada kwenye Nyumba ya Allah (Al-Ka'ba) kabla ya kuondoka kwake. Lakini 'Atbah alimwonya asije akayasikia maneno yenye kuroga ya yule Nabii mpya wakati atakapokuwa akifanya tawafu, na akavutika naye. Ili kulitatua tatizo hili, 'Atbah alimshauri As'ad kushindil- ia pamba masikioni mwake ili kwamba asiweze kumsikia yule Nabii.

Pole pole As'ada alishuka na kuingia kwenye Masjidul Haraam na akaan- za kufanya tawafu kwenye ile Ka'abah. Kwenye mzunguko wa kwanza alimtupia jicho Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na akamwona ameketi kwenye Hajjar Isma'il wakati Bani Hashim kadhaa walikuwa wakimhami. Akiuchelea uchawi wa maneno ya Mtume (s.a.w.w), yeye (As'ad) hakumwendea.

Hata hivyo, hatimaye, alipokuwa akiizunguuka Al-Ka'ba (kwenye ile ibada ya tawafu) aliwaza akilini mwake na akajihisi kwamba alikuwa akitenda jambo la kijinga kwa kumwepuka Mtume (s.a.w.w) kwa sababu, inawezekana kwamba watu wanaweza wakamwuliza kuhusu jambo hili atakaporudi Yathrib na itakuwa ni lazima kwake yeye kuwapa jibu litoshelezalo. Hivyo basi, aliamua kupata taarifa za awali kuhusu hiyo dini mpya, bila ya kuchelewa zaidi.

Alijitokeza mbele na akamsalimu Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kwa maneno: *"Awam Sabahan"* (Habari za asubuhi), kwa mujibu wa desturi zilizokuwako kwenye zama za ujinga. Hata hivyo, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alimjibu; akamwambia kwamba Allah Ameamrisha aina iliyo bora zaidi ya kusalimiana. Alisema kwamba watakapokutana watu wawili, hawana budi kusema: *"Salaamun 'Alaykum."* Kisha As'ad alimwomba amfafanulie lengo na madhumuni ya dini yake. Ili kumjibu A'sad, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alimsomea Aya mbili zifuatazo:

قُلْ تَعَالَوْا أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبُّكُمْ عَلَيْكُمْ ۖ أَلَّا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۖ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۖ وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ مِنْ إِمْلَاقٍ ۖ نَحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ ۖ وَلَا تَقْرَبُوا الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ ۖ وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ۚ ذَٰلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ {151}

وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ أَشُدَّهُ ۖ وَأَوْفُوا الْكَيْلَ وَالْمِيزَانَ بِالْقِسْطِ ۖ لَا نُكَلِّفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۖ وَإِذَا قُلْتُمْ فَاعْدِلُوا وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۖ وَبِعَهْدِ اللَّهِ أَوْفُوا ۚ ذَٰلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ {152}

***"Sema*** (*ewe Rasuli Wetu Muhammad*)***: 'Njooni nikusoneeni Aliyokuharimishieni Mola wenu; ya kwamba msimshirikishe na kitu chochote na kuwatendea hisani wazazi*** (***wenu***)***, wala msiwauwe watoto kwa*** (***kuchelea***) ***umaskini; Sisi Tutakupeni riziki na wao pia; wala msiyakaribie manbo maovu, ya dhahiri na ya siri, wala msiiue nafsi Aliyoharamisha Allah ila kwa haki; hayo Anakuusieni kwayo ili mzingatie. Wala msiikaribie mali ya yatima ila kwa njia iliyo bora mpaka abalehe; na kamilisheni vipimo na uzani kwa uadilifu, Hatuikalifishi nafsi ila*** (***kuipa majukumu***) ***kwa kadiri ya uwezo wake, na mnaposema, basi fanyeni uadilifu japo iwe ni dhidi ya jamaa*** (***yako***)***; na itimizeni ahadi ya Allah; hayo Anakuusieni kwayo ili mpate kukumbuka."*** (***Al-An'am 06:151-152***).

Aya hizi hutoa taaswira ya kweli ya fikara na mtindo wa maisha wa Waarabu wa zama za ujinga. Hizi Aya mbili zinazotaja maradhi pamoja na tiba ya watu waliokuwa wakigombana wao kwa wao kwa miaka mingi mno kiasi cha kufikia mia moja na ishirini, zilimwibua As'ad mawazo ya ndani zaidi. Alisilimu mara moja na akamwomba Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kumpeleka mtu huko Yathrib akawe mbalighishaji wa Uislamu.

Tunaona kwamba kama tukienda ndani zaidi ya hizi aya mbili itatosha kuondoa majadiliano na mafunzo (marefu zaidi) kuihusu hali ya Waarabu wa Zama za Ujinga, kwa kuwa aya hizi zatosheleza kuifafanua kadiri ya maradhi ya siku nyingi ya kimaadili yaliyokuwa yakitishia kuwako kwa watu hawa. Hapa chini tunayatoa mambo yaliyomo kwenye Aya hizo pamoja na mukhtasari wa maelezo yake:

Nimetumwa kwenye huu ujumbe wangu wa Kiutume kuuondoa ushirikina na ibada ya masanamu.

Kuwatendea wema wazazi huichukua nafasi ya juu zaidi kwenye Ujumbe wangu.

Kwa mujibu wa sheria takatifu kuwaua watoto kwa kuchelea umaskini ni tendo baya zaidi awezalo kulitenda mtu.

Nimeteuliwa ili kuwazuia watu wasitende matendo maovu na kuwaon- dolea uchafu wa kila aina, uwe wa dhahiri au wa siri.

Sheria yangu inasema kwamba kuua mtu na kumwaga damu bila ya sababu ya haki, vimeharimishwa kabisa.

Kuitwaa mali ya yatima pasi na haki, kumeharimishwa.

Sheria yangu imesimama kwenye msingi wa uadilifu, hivyo basi, kwa mujibu wa sheria hii, kuuza vitu kwa uzani pungufu ni haramu. Simpi mtu jukumu zaidi ya lile awezalo kulibeba.

Ulimi na kauli ya mtu, vitu ambavyo ni kioo chenye kung'aa, chenye kuzieleza fikara zake, havina budi kutumika katika kuunga mkono ukweli na uhakika, na mtu asikiseme cho chote kile ila ukweli japo umsababishie hasara.
Uwe mkweli katika ahadi umwahidizo Allah. Hayo yameamrishwa na Mola wako na ni lazima juu yako kuyafuata.4

Kutokana na mambo yaliyomo kwenye hizi aya mbili na jinsi Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alivyozungumza na As'ad, inaweza kufahamika vizuri mno kwamba, Waarabu walikuwa walishajijengea sifa zote hizi zilizo mbaya na kwa sababu hiyo, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) akamsomea As'ad aya hizi mbili mwanzoni kabisa zikiwa ndio shabaha ya Ujumbe wake.

Kwenye hali hiyo, je, yawezekana kukubaliana na dai la watu wale wasemao kwamba ulikuwako ustaarabu wa hali ya juu zaidi kwenye sehemu zote za Bara Arabu kwa karne nyingi?

## Dini Bara-Arabuni

Nabii Ibrahimu alipoitweka bendera ya ibada ya Allah na akainua misingi ya Al-Ka'ba tukufu, akisaidiwa na mwanawe Nabii Isma'il (a.s.) baadhi ya watu walimkusanyikia, na miali ya utukufu wake iliyomulika kama jua iliziangaza nyoyo zao. Hata hivyo, kiasi ambacho hii roho tukufu iliweza kupambana na ibada ya masanamu na kuunda safu imara za wenye kumwambudu Allah hakifahamiki kwa uhakika.

Kwenye nyakati nyingi, na hasa miongoni mwa Waarabu, mara nyingi itikadi ya ibada ya Mungu iliandamana na ushirikina na itikadi ya kwamba masanamu yalikuwa udhihirisho wa Mungu. Kutokana na itikadi zao mbalimbali, Qur'ani Tukufu imeitaja itikadi moja ya aina hiyo, ikisema:

{وَلَئِنْ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ خَلَقَهُنَّ الْعَزِيزُ الْعَلِيمُ} 9

***"Na kama ukiwauliza* (*makafikri wa kiarabu*)*: 'Ni nani aliyeziumba mbingu na ardhi?***
***'bila shaka watasema: 'Ameziumba Mwenye nguvu, NMwenye kkujua"*** (***Az-Zukhruf 43:9***)

{أَوْلِيَاءَ مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ} 3

***"... Sisi hatuwaabudu hawa*** (***masanamu***)***, ila wapate kutufikisha karibu zaidi na Allah;***
(***Az-Zumar, 39:3***)

Sayyidna Ali, Amirul Muuminin (a.s.) anaielezea hali ya kidini ya Waarabu kwa maneno haya: "Watu wa zama hizo walikuwa na itikadi mbalimbali na uzushi wa aina mbalimbali na walikuwa wamegawanyika kwenye madhehebu nyingi. Kundi moja lilimfananisha Allah na viumbe Wake (na liliamini kwamba Alikuwa na viungo). Wengine walileta mabadiliko kwenye Majina Yake (kwa mfano wenye kuabudu

masanamu walijichukulia jina la 'Lat' kutokana na Allah na Uzza kutokana na Jina Aziz). Pia lilikuwako kundi lililowaelekea wengine ghairi Yake. Baadae Allah Aliwaongoza kupitia kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na Akawafanya kuwa wajuzi wa elimu ya Allah."[5]

Watu wenye elimu miongoni mwa Waarabu waliabudu jua na mwezi. Mwanahistoria mashuhuri wa kiarabu, aliyeitwa Kalbi aliyefariki dunia kwenye mwaka wa 206 Hijiriya, anaandika hivi:

"Kabila lililoitwa Bani Malih liliabudu majini, kabila la Tamim liliabudu Dabaran (moja ya nyota zilizomo kwenye mafungu kumi na mawili ya nyota iitwayo Taurus), kabila la Lakhan liliabudu sayari ya Jupita (Sumbula), kabila la Ta'i liliabudu nyota Shiraa, na kabila la Asad liliabudu sayari Zebaki. Hata hivyo, sehemu iliyotwezwa ya jamii iliyo na wengi wa wakazi wa Bara Arabu, zaidi ya kuabudu masanamu ya familia na makabila yao, vilevile waliyaabudu masanamu 360 na wakayahusisha matukio ya kila siku na moja yao."

Sababu ya kuasisiwa kwa ibada ya masanamu kwenye eneo la Makkahh baada ya kufariki dunia kwa Mtukufu Nabii Ibrahim (a.s.) itajadiliwa baadae. Hata hivyo, ni ukweli ukubalikao kwamba, kwenye siku za mwan- zoni tendo hili halikukamilika kabisa. Hapo awali Waarabu waliyafikiria masanamu kuwa ni waombezi tu na polepole wakaanza kuyadhania kwamba yanao uwezo. Masanamu yaliyopangwa kwa kuizunguka Ka'bah yaliheshimiwa na makabila yote, lakini masanamu ya makabila yaliabudiwa na kundi maalum tu. Kila kabila liliweka sehemu maalum kwa ajili ya masanamu yake, ili kuuthibitisha usalama wao. Wadhifa wa utunzaji wa funguo za hekalu yalimowekwa masanamu hayo ulishikwa kwa urithi na ulishikwa tangu mtu mmoja hadi mwingine.

Masanamu ya familia yaliabudiwa na watu wa familia ile mchana na usiku. Walipokwenda safarini waliyasugua na miili yao. Walipokuwa safirini waliyaabudu mawe ya jangwani. Walipofika kwenye kituo fulani, walichagua mawe manne. Miongoni mwa mawe hayo, waliliabudu lile lililokuwa zuri zaidi na wakayatumia yale matatu yaliyosalia kuwa mafiga ya jiko la kupikia chakula.

Watu wa Makkahh walikuwa na huba nyingi kwa Al-Ka'ba. Walipokuwa wakisafiri waliokota mawe kutoka karibu nayo na kuyaweka na kuyaabudu kila walipotua. Yawezekana kwamba watu hawa ndio waliokuwa '*ansaab*' (mawe yaliyowekwa) ambayo yalifasiriwa kuwa ni mawe meroro na yasiyo na umbo wala sura maalum. Kinyume na mawe haya, yalikuwapo yale yaliyoitwa '*awthaan*', neno lenye maana ya masanamu yenye umbo na yaliyonakshiwa yaliyotengenezwa kutokana na mawe ya kuchonga. Ama kuhusu '*asnaam*', haya yalikuwa ni masanamu, yaliyotengenezwa kwa dhahabu au fedha ya kusubu au yaliyochongwa kutokana na mti.

Kwa kweli, unyenyekevu wa Waarabu mbele ya masanamu ulishangaza mno. Waliamini kwamba kwa kutoa kafara watapata upendeleo wao. Na baada ya kutoa kafara ya mnyama waliipaka damu ya mnyama yule kichwani na usoni mwa lile sanamu. Vilevile walitaka ushauri wa masanamu kwenye mambo yao makuu na yaliyo muhimu. Ushauri huu ulipatikana kwa vijiti ambavyo kimoja walikiandika "fanya" na kingine wakakiandika

‘Usifanye’. Kisha walinyosha mkono na kuokota kimojawapo na kutenda kama kilivyosema kile kijiti.

## Fikara Za Waarabu Kumhusu Mwanadamu Baada Ya Kifo

Waarabu walilifafanua suala hili la kifalsafa na lililo gumu hivi: Baada ya kifo cha mwanaadamu, roho yake huutoka mwili wake kwa umbo la ndege aitwaye ‘*Hamah wa Sada*’ afananaye na bundi na ndege huyo huomboleza kandoni mwa maiti yule bila ya kukoma. Maombolezo yake huwa yenye kuogofya na kutisha. Yule maiti atakapozikwa, roho yake hutwaa makazi kwenye hali tuliyoitaja, karibu na kaburi lake na hukaa hapo daima.

Wakati mwingine ndege huyu huenda na kukaa juu ya paa la nyumba ya watoto wake na kuwa na mazoea na hali zao.

Kama mtu akifa kifo kisicho cha kawaida (kwa mfano akauawa), ndege yule hulia bila ya kukoma: *“Asquni … Asquni…*” (Yaani nizimeni kiu yangu kwa damu ya muuaji wangu) na hanyamazi hadi alipiziwe kisasi kwa muuaji wake.

Hapa ndipo mahali ambapo hali halisi yaeleweka dhahiri kwa mheshimiwa msomaji na anafahamu ya kwamba historia ya Bara Arabu kabla ya Uislamu na ile ya baada ya kuja Uislamu hazifanani. Inapokuwa kwamba ile ya awali ni hadithi ya mauaji, na mazishi ya mabinti walio hai, utekaji nyara, msiba na shida na kuabudu masanamu, ile ya pili inatueleza kuhusu upole kwa yatima, ukarimu na huruma kwa binadamu na ibada ya Mungu Mmoja.

Kwa kweli kikundi cha Wayahudi na Wakristo vilevile waliishi kwenye jamii hii hii lakini waliidhihirisha chuki yao dhidi ya ibada ya masanamu. Makao makuu ya Wayahudi yalikuwa ni mji wa Yathrib, ambapo Wakristo waliishi Najran. Kwa bahati mbaya jamii hizi mbili pia zilihusika na upotovu kuhusiana na upweke wa Allah.

## Fasihi Au Stirioskopu (Kinasa Picha Mbili Kwa Pamoja) Ya Fikra Za Taifa

Njia iliyo bora zaidi ya uchambuzi wa mtazamo na weledi wa taifa ni zile kazi za uandishi na hadithi zilizorithiwa na taifa hilo. Fasihi, ushairi na hadithi za kila jumuiya huwakilisha itikadi yake, huwa kama ndio kipimo cha utamaduni wake, na huidhihirisha namna ya fikira zake. Fasihi ya kila taifa ni kama picha ya rangi ya watu waliojipanga tayari, ambayo hutufanya tupate taswira akilini juu ya maisha ya familia pamoja na nyororo ya matukio ya kawaida na wingi wa machafuko au mandhari ya vita na utekaji nyara.

Ushairi wa Waarabu na methali zitumiwazo hivi sasa miongoni mwao zaweza zaidi ya kitu cho chote kingine, kuionyesha tabia halisi ya historia yao. Mwanahistoria mwenye kutaka kuujua mtazamo halisi wa taifa fulani, anapaswa kwa kadiri iwezekanavyo asizipuuze alama za ukumbusho mbalimbali za

kisomi za taifa hilo, kama vile ushairi, semi, methali, hadithi n.k. Bahati nzuri, wanachuoni wa kiislamu wameandika na kuweka katika kumbu kumbu kwa kadiri ya uwezo wao, fasihi ya Waarabu ihusianayo na Zama za Ujinga.

Abu Tamaam Habib bin Aws (aliyefariki dunia katika mwaka wa 231 Hijiriya) anayehesabiwa kuwa mmoja wa waandishi wa Kishi'ah, na aliyesifiwa kwa mashairi yanayowasifu viongozi wa kidini wa Kishi'ah, amekusanya idadi kubwa ya mashairi yaliyotungwa katika Zama za Ujinga na ameyapanga katika sehemu kumi ambazo ni Mashairi ya kitenzi – Fasihi ya kimaombolezo – Mashairi yenye hisia yahusianayo na kipindi cha ujana. Tashtiti za watu binafsi na za kabila – Mashairi yaliyolengwa upole na ukarimu – wasifu – sifa za kimaumbile, tabia – ujuaji na ucheshi – na kuwazulia wanawake.

Wanachuoni na waaandishi wa kiislamu wameandika tafsiri ya Kitabu hiki ili kuieleza maana ya maneno na kusudio la mashairi. Kitabu hiki kimetafsiriwa mwenye lugha nyingi za kigeni, baadhi yao zimetajwa mwenye kitabu kiitwacho "*Mu'jamul Matbu'aat*" (Uk. 297).

## Daraja Ya Wanawake Miongoni Mwa Waarabu

Sehemu ya kumi ya kitabu tulichokitaja hapo juu inaonyesha wazi vya kutosha kwamba wanawake waliwekwa chini ya fedheha ya kipekee mion- goni mwa watu hawa na waliishi maisha ya kuhuzunisha sana. Katika Qur'ani Tukufu pia zimeteremshwa aya zinazolaumu kitendo cha Waarabu, na kutoa mwanga juu ya kushusha kwao maadili. Inakitaja kitendo chao kichukizacho cha kuwaua wasichana, na inasema:

{وَإِذَا الْمَوْءُودَةُ سُئِلَتْ {8

{بِأَيِّ ذَنْبٍ قُتِلَتْ {9

***"Na mtoto mwanamke aliyezikwa hai atakapoulizwa, ni kwa kosa gani aliuawa?"* (*At-Takwir, 81:8-9*).**

Yaani wasichana waliozikwa wakiwa hai wataulizwa swali hili katika Siku ya Hukumu. Ni dhahiri kabisa huu ni uvunjaji wa hali ya juu wa maadili kwamba mtoto wake mtu aishapo kukua au ndio kwanza kuwasili ulimwenguni, mtu amzike chini ya tani za udogo na asihuzunishwe hata kidogo na kilio na maombolezo yake.

Watu wa kwanza kukitenda kitendo hiki walikuwa ni watu wa kabila la Bani Tamim. Nu'man bin Munzir, mtawala wa Iraq aliwashambulia maadui wake (ikiwa ni pamoja na hawa Bani Tamim) akiliongoza jeshi kubwa na akawashinda. Alizinyakuwa mali zao na akawachukua mateka wasichana wao.

Wawakilishi wa Bani Tamim walimwendea mtawala huyu na kumwomba awarudishie wasichana wao. Hata hivyo, kwa kuwa baadhi yao walikuwa tayari walishafunga uhusiano wa ndoa katika kipindi cha kutekwa kwao, Nu'man aliwapa uchaguzi wa kukata uhusiano na wazazi wao ili wabakie na waume zao au wapate talaka na warudi majumbani kwao. Mmoja wa wawakilishi wa Bani Tamim alikuwa mzee aliyeitwa Qays bin 'Aasim.

Binti wake alichagua kubakia na mumewe. Tusi hili lilimchoma moyo mzee yule na akaamua kwamba hapo baadae atawamalizia mbali mabinti zake mara tu wazaliwapo. Pole pole kitendo hiki kiliingia kwenye makabila mengine pia. Qays bin 'Aasm alipoipata heshima ya kufika mbele ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) mmoja wa Maansar alimuuliza kuhusu mabinti zake. Qays alijibu akisema: "Nimewazika mabinti zangu wote wakiwa hai na sikuhuzunishwa hata kidogo nilipokuwa nikifanya hivyo (ila safari moja tu). Safari moja nilikuwa nikisafiri na wakati wa mke wangu kujifungua ulikaribia.

Kwa bahati safari yangu ilikuwa ndefu. Niliporudi nyumbani nilimwuliza mke wangu kuhusu jambo hilo. Akajibu kwamba kutokana na maradhi alizaa mtoto asiyetimiza siku zake. Hata hivyo, ukweli ni kwamba alizaa mtoto wa kike, na kwa kuniogopa alimweka mtoto huyo chini ya ulinzi wa dada yake. Miaka mingi ilipita na yule msichana akaufikia ujana wake. Sikupata taarifa hata kidogo, juu yake. Hata hivyo, siku moja nilipokuwa nimeketi nyumbani mwangu, aliingia msichana kwa ghafla na akamulizia mama yake. Alikuwa msichana mzuri na alivaa kidani shingoni mwake. Nilimwuuliza mke wangu ni nani msichana yule apendezaye kiasi kile. Mke wangu akiwa anatiririkwa na machozi machoni mwake alinijubu akisema: "Huyu ni binti yako. Ndie yule msichana aliyezaliwa ulipokuwa safarini.

Kwa kukuogopa, nilimficha." Kimya changu kilichukuliwa na mke wangu kuwa ni dalili ya kuridhika kwangu na akafikiria kwamba sitaipaka mikono yangu damu ya msichana yule. Hivyo basi, siku moja alitoka nyumbani mle na uhakika wa kwamba sitamdhuru. Kisha, kufuatana na ile ahadi na nadhiri yangu nzito, niliushika mkono wa binti yangu na kumpeleka kwenye sehemu ya mbali. Huko nikaanza kuchimba shimo. Nilipokuwa nikijishughulisha na kazi hiyo binti yangu aliniuliza kwa kurudia rudia ni kwa nini nilikuwa niki- ichimba ardhi? Baada ya kwisha kuchimba niliushika mkono wa binti yangu, nikamtumbukiza shimoni, na nikaanza kumtupia udongo kichwani na usoni mwake bila ya kuvisikiliza vilio vyake vyenye kuupasua moyo.

Aliendelea kupiga kite na kusema: "Baba yangu mpenzi! Unanizika ardhini? Je, utarudi kwa mama yangu baada ya kuniacha hapa peke yangu?" Lakini mimi niliendelea kumimina udongo hadi ukamfunika kabisa. Ni kwenye tukio hili tu kwamba nilipatwa na kiasi kidogo mno cha fahamu."

Masimulizi ya Qays yalipokoma, machozi yalibubujika machoni mwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na akasema: "Hili ni tendo la ugumu wa moyo na taifa lisilo na hisia za huruma na upole halitapata rehema za Allah." [6]

# Nafasi Ya Kijamii Ya Wanawake Miongoni Mwa Waarabu

Miongoni mwa Waarabu, mwanamke alikuwa kama bidhaa ya kibiashara iliyoweza kununuliwa na kuuzwa na hakuwa na haki ya kibinafsi wala kijamii hata ile haki ya kurithi. Watu wenye elimu miongoni mwao waliwaweka wanawake chini ya jamii ya wanyama na kwa sababu hii alichukuliwa kuwa kimoja miongoni mwa vyombo vya nyumbani na mahitaji muhimu ya maisha. Kutokana na itikadi hii, methali isemayo: "Akina mama ni wazuri tu kama vile vilivyo vyombo, nao wameumbwa ili wawe vyombo vya kuwekea manii" ilikuwa ikitumika mno miongoni mwao.

Kwa kawaida kuhusiana na hofu ya njaa na fadhaa yenye kuogofya, mara kwa mara waliwakata vichwa mabinti zao katika siku ya mwanzoni mwa kuzaliwa kwao au kuwasukumizia chini kutoka kwenye mlima mrefu na kuwatupia kwenye bonde lenye kina kirefu au wakati mwingine kuwafisha maji.

Qur'ani, Kitabu kikuu cha dini, ambacho chakubaliwa hata na mustashirik wasio Waislamu kwamba kwa uchache ni maandiko ya kihistoria na yenye mafunzo yasiyoharibiwa, kina maandiko ya ajabu juu ya jambo hili. Inasema:

{وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُمْ بِالْأُنْثَىٰ ظَلَّ وَجْهُهُ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ {58

{يَتَوَارَىٰ مِنَ الْقَوْمِ مِنْ سُوءِ مَا بُشِّرَ بِهِ ۚ أَيُمْسِكُهُ عَلَىٰ هُونٍ أَمْ يَدُسُّهُ فِي التُّرَابِ ۗ أَلَا سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ {59

***"Na mmoja wao anapopewa habari ya (kuzaliwa) binti, uso wake huwa mweusi, naye kajaa chuki. Hujificha kutokana na kaumu (yake) kwa sababu ya habarimbaya aliyoambiwa (anafikiria) je, amweke kwa fedheha au amzike udongoni (akiwa hai)? Tazama! Ni uovu (kiasi gani) wa wanavyohukumu." (Al-Nahl, 16:58-59).***

Jambo lenye kusikitisha zaidi lilikuwa ni utaratibu wa ndoa zao ambao haukusimamia kwenye msingi wowote wa sheria yenye mtindo utumikao ulimwenguni mwa zama zile. Kwa mfano, hawakuamini kuwapo kwa mipaka yoyote ile katika idadi ya wake. Ili kuepuka kulipa mahari, waliwatesa wanawake na kama mwanamke atakoma kuwa msafi wa tabia, aliikosa mahari yake kabisa.

Wakati mwingine walijinufaisha visivyo haki kutokana na sheria hii na wakawasingizia wake zao kiasi cha kuweza kukataa malipo ya mahari. Kitokeapo kifo cha mtu au kumtaliki mkewe, ilihesabiwa kuwa ni halali kwa mwanawe kumwoa mke yule, na hadithi ya Ummayyah bin Shams kuhusiana na jambo hili imehifadhiwa kwenye vitabu vya historia.
Mwanamke anapojipatia talaka kutoka kwa mumewe, haki yake ya ndoa ya pili ilitegemea ruhusa ya mume wa awali na kwa kawaida ruhusa hiyo ilitolewa kwa yeye kuiachilia mahari yake. Kinapotokea kifo cha mtu, warithi wake waliwatwaa wanawake kama vilivyo kwa vyombo vyote vya nyumbani mle, na kujitangaza kuwa ndio wamiliki kwa kuwatupia nguo ya kichwa juu ya kichwa chake.

## Ulinganisho Mfupi

Kama mtukufu msomaji akiziangalia haki za mwanamke kwenye Uislamu na akapuuza ugomvi na migogoro ambayo hujitokeza ghafla kwenye nyakati fulani, bila shaka atatambua ya kwamba sheria na kanuni na hatua zenye kufaa za kuzitengeneza haki za mwanamke na kuzifanya kuwa za kawaida zilizochukuliwa kupitia kwa Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w), zenyewe ni ushahidi wa dhahiri kabisa wa ukweli wake na mawasiliano yake na ulimwengu wa ufunuo.

Kwani ni huruma gani na kuwatendea mema wanawake kuwezako kuwa bora zaidi ya hapo (ukiyaachilia mbali matangazo ya haki za wanawake kwenye aya mbalim- bali za Qur'ani Tukufu na kwenye Hadithi na pia kutoa mifano ya kivitendo kuhusiana na jambo hili kwa ajili ya wafuasi wake kuweza kufanya hivyo). Kwenye hotuba ya Hija yake ya mwago aliyoifanya, ambapo kwa kuamrishwa na Allah aliurudia rudia ujumbe huo kwa ufupi, akamteua mrithi wake na kwenye wakati huohuo, vilevile aliwakabidhi wanawake kwa wanaume kwa maneno yafuatayo:

"Enyi watu! Mnayo haki juu ya wanawake wenu nao pia wanayo haki juu yenu. Waamrisheni kutenda mema kwa kuwa wanakusaidieni na kukunusuruni. Walisheni vile mvilavyo ninyi wenyewe na wavisheni vile mvivaavyo wenyewe."

## Waarabu Kama Wapiganaji

Hakuna shaka yoyote kuhusu habari kwamba Waarabu walikuwa na moyo wa kupenda vita usiokuwa na kifani na waliyazidi mataifa mengi kwenye sanaa ya vita. Bila shaka moyo huu ulikuwa wa kusifika na kustahili kuthaminiwa mno kiasi kwamba hata Uislamu uliutumia mno mwelekeo wao huu baada ya kuurekebisha. Na ni jambo la heshima kuu kwa Uislamu kwamba baada ya kufanya marekebisho yafaayo kwenye mielekeo ya mataifa mbalimbali, iliitumia katika kuyafikia malengo na shabaha tukufu. Hata hivyo, kabla ya Uislamu, moyo huu wa Waarabu ulikuwa daima ukitekelezwa kivitendo kuyaharibu matengemeo ya maisha ya makabila mbalimbali na haukutoa matokeo yoyote yale ila umwagaji wa damu, mauaji na utekaji nyara.

Waarabu walizidisha mno tabia ya umwagaji wa damu, na utekaji nyara kiasi kwamba wakati wa kujisifu mtu, waliuhesabu utekaji nyara kuwa moja ya heshima zao. Ukweli huu ni wa dhahiri kabisa kutokana na ushairi na maandiko yao.

Mmoja wa washairi wa Zama za Ujinga, alipokuwa akiiangalia hali duni na nyonge ya kabila lake kuhusiana na mauaji na utekaji nyara, alihuzuni- ka mno na akaielezea tamaa yake kwa maneno haya: "O (ningalifurahi mno) kwamba badala ya kuwa wa kabila hili nyonge na lisilo na faida yoyote ningalikuwa mtu wa kabila, ambalo watu wake wamewapanda wanyama au watembeao kwa miguu, daima walijifurahisha kwa utekaji nyara na unyang'anyi, na kuyaishilizia maisha ya watu."

## Hitimisho

Sasa tuishajipatia dokezo la ujumla juu ya ustaarabu wa Waarabu wa Zama za Ujinga. Pia, sasa ishatudhihirikia kwamba hakuna mtu mwadilifu wala mwenye elimu awezaye kuyakubali maoni ya kwamba hali ya kijamii ya Hijaz, iliyojaa machafuko, ukatili na utwezaji wa utu na wema, ingezaa chama kikuu na cha ulimwengu mzima (Uislamu) ambacho kingeliweza kuzitumia nguvu za kiakili zilizo dhahiri kwenye ulimwengu wote wa zama zile na kuirudisha amani na taratibu njema kwenye eneo lile lililosumbuliwa kwa njia ya mpango ulio bora zaidi.

Na vilevile imedhihirika kwamba dai lililotolewa na baadhi ya watu wasioona mbali kwamba Uislamu ni matokeo ya kawaida ya jamii ile, ni lenye kushangaza mno. Bila shaka maoni kama haya yangelikuwa ya haki kama chama hiki kikuu kingelijitokeza kwenye maeneo yaliyostaarabika, lakini itakuwa ni fikara itokanayo na mapenzi ya mtu tu kutoa dai la aina hii kuhusiana na Hijaz.

Sasa, kwa lengo la kuyamalizia mazungumzo yetu juu ya maudhui hii, tunatoa hapa chini taarifa za itikadi na fikara za Waarabu wa Zama za Ujinga kuhusiana na mambo mbalimbali.

## Ushirikina Na Ngano Za Waarabu

Qur'ani Tukufu imetaja malengo ya Ujumbe wa Mtukufu Mtume wa Uislamu kwenye sentensi fupifupi. Moja ya sentensi hizi ipasikayo kuchunguzwa vizuri ni hii isemayo:

{وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَالْأَغْلَالَ الَّتِي كَانَتْ عَلَيْهِمْ ۚ {157

***"...Na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao..."*** **(*Al-A'araf, 7:157*).**

Yaani Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w) aliwaondolea matendo magumu na akawaondolea minyororo iliyoifunga mikono na miguu yao. Sasa haina budi kufahamika wazi maana ya minyororo iliyokuwa ikiifunga mikono na miguu ya Waarabu wa Zama za Ujinga wakati wa kuanza kwa Uislamu. Bila shaka hii haina maana ya minyororo na pingu za chuma bali ilikuwa na maana ya itikadi na ushirikina usiokuwa na msingi uliozifunga akili zao kutokana na fikira na maendeleo.

Na ukweli ni kwamba, minyororo na ugwe ulioifunga akili ya mwanaadamu ni vyenye hatari na madhara zaidi kuliko hiyo minyororo ya chuma, kwa kuwa baada ya kupita muda fulani, hiyo minyororo ya chuma huondolewa na mfungwa huibuka tena kwenye maisha na akili yenye afya timam, akiwa huru kutokana na fikara zote za kiufujaji, lakini minyororo ya ushirikina na uduni unaoifunga akili na utumiaji wa akili ya mwanaadamu kama uzi uliojisokota, humweka mwanaadamu kwenye hali ya kufungwa hadi kwenye kifo chake na humzuia kufanya juhudi zozote zile – hata ile juhudi ya kuviondoa vifungo na pingu hizi.

Na kuwa mtu mwenye akili timam anaweza kubuni mbinu ya kuivunjilia mbali minyororo au fito za chuma

kwa msaada wa akili na matumizi ya akili hizo, matendo na juhudi za mtu asiye na akili timam na dhana huishilizia patupu na hubakia kuwa ya bure.

Moja ya heshima na sifa kuu za Mtukufu Mtume (s.a.w.w) ni kwamba alipigana dhidi ya ushirikina, itikadi potovu na ngano, na alisafisha bongo za wanadamu na sababu ya imani za kuchukiza za ushirikina.

Alikuwa kila mara akisema: “Nimekuja kuikamilisha nguvu ya akili za mwanaadamu na kuiinua juu, kupiga vita imara dhidi ya aina zote za ushirikina japo ziwe zenye msaada kwa maendeloa ya Ujumbe wangu.”

Wanasiasa wa ulimwenguni wasio na nia wala lengo lolote jingine zaidi ya kuwatawala watu daima hutumia kila tukio kwa faida zao wenyewe kiasi kwamba, kama ngano za kale au itikadi ya ushirikina ya taifa fulani ni zenye faida kwa nchi na serikali zao, hawasiti kuzibalighisha. Na kama ni watu wenye fikara nyingi na hoja, basi huzipa msaada ngano na ushirikina usio na hoja chini ya dhana ya kuziridhia fikara za walio wengi na heshi- ma kwa itikadi ya walio wengi.

Hata hivyo, Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w) hakuzikomesha itikadi za kishirikina zilizokuwa na madhara kwake na kwa jamii tu, bali hata ngano ya eneo fulani au wazo lisilo na msingi lililokuwa lenye kutoa msaada kwa ajili ya maendeleo ya ujumbe wake alilifanyia kampeni dhidi yake kwa nguvu zake zote na akajitahidi kwamba watu waufuate ukweli na wala si ngano na ushirikina.

Kijana Ibrahim, mtoto wa kiume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alifariki dunia. Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alishikwa na masikitiko na akahuzunika kwa sababu ya kifo chake. Na akatiririkwa na machozi kutoka machoni mwake bila kujizuia.

Jua lilipatwa kwenye siku ya kifo cha mtoto huyu. Waarabu wapenda ngano na ushirikina walikuchukulia kupatwa huko kwa jua kuwa ni dalili ya ukuu wa huzuni za Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na wakasema: “Jua limepatwa kwa sababu ya kifo cha mwana wa Mtume.” Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alipata kuyasikia maneno haya. Aliipanda mimbari na akasema: “Jua na mwezi ni ishara kuu mbili za uwezo wa Allah, navyo huzitii amri Zake. Havishikwi kwa sababu ya kifo au uhai wa mtu yeyote. Kila kutokeapo kupatwa kwa jua au mwezi salini sala ya Ishara.” Baada ya kuyasema hayo alishuka mimbarini na akasali Swala ya Ishara pamoja na wengine.[7]

Ingawa wazo la kwamba kupatwa kwa jua kulitokea kutokana na kifo cha mwana wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) lingaliweza kuiimarisha itikadi ya watu juu yake, na hivyo ingaliweza kumsaidia katika maendeleoa ya ujumbe wake, katu hakupenda kwamba cheo chake kiimarike nyoyoni mwa watu kwa njia ya ushirikina. Kampeni yake dhidi ya hekaya na ushirikina, ambayo mfano wake ujidhihirishao mno ni vita aliyoipanga dhidi ya ibada ya masanamu na aina zote za dini za uongo, halikuwa jambo lenye kifani kwenye kipindi cha ujumbe wake wa kiutume. Amepigana dhidi ya ushirikina kwenye maisha yake yote hata kwenye siku za utotoni mwake.

Siku moja wakati umri wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w) haukuwa zaidi ya miaka minne na

alipokuwa akiishi na mlezi wake, Bibi Halima (r.a) aliidhihirisha tamaa ya kufuatana na kaka yake wa kunyonya kwenda naye porini.

Bibi Halima (r.a) anasema: "Siku iliyofuatia nilimwogesha Muhammad, nikazipaka mafuta nywele zake na nikayapaka wanja macho yake. Na vile vile nilimvika ushanga wa Yemen, uliotungwa kwenye kamba shingoni mwake kwa ajili ya usalama wake, ili asidhurike na pepo wabaya. Muhammad aliuvua ushanga ule kutoka shingoni mwake na akaniambia: "Mama yangu mpenzi! Moyo wako na utulie. Mungu wangu aliye nami daima yu Mlinzi na Mhifadhi wangu." 8

## Itikadi Za Kishirikina Za Waarabu Wa Zama Za Ujinga

Wakati wa kuanza kwa Uislamu itikadi za mataifa na jamii zote za wanaadamu wa ulimwenguni kote walikuwa wamefungwa na aina mbalimbali za ushirikina na visaasili na mithiolojia za Kigiriki na Kisasaniaa zilizotawala akili za mataifa yaliyochukuliwa kuwa ndio mataifa yaliyoendelea kwenye siku hizo. Na hata kwenye zama zetu hizi ushirikina mwingi umeenea miongoni mwa mataifa yaliyoendelea ya nchi za mashariki na ustaarabu wa kisasa bado haujafaulu kuufuta kutoka akilini mwao. Hata hivyo, kukua kwa visaasili na ushirikina kuko sambamba na kiwango cha elimu na mafunzo kwenye jamii. Jinsi jamii iwavyo nyuma kwenye mambo ya elimu na mafunzo, ndivyo idadi ya ushirikina itakavyokuwa kubwa humo.

Historia imesajili idadi kubwa ya visasili na ushirikina uhusianao na Waarabu, na Sayyid Mahmud Aalusi, mwandishi wa kitabu kiitwacho *Bulughul adab fi ma'rifa ahwaalil Arab*9 amekusanya mwingi miongoni mwao kwenye kitabu hicho pamoja na nyororo ya wasimulizi waliozirejea taarifa hizo kwenye maandishi yao. Ukikipitia kitabu hiki na vinginevyo mtu utaweza kuuona ushirikina chungu nzima. Haya mafundisho yasiyo na msingi ya itikadi zisizoeleweka kiakili yalikuwa moja ya sababu zilizolifanya taifa hili kukawia nyuma ya mataifa mengine. Ni jambo la kawaida kwamba, taifa ambalo idadi ya wasomi wake katikati ya mkoa wa Hijaz haikuzidi watu kumi na saba10 liwe ni lenye kukamatwa na ushirikina na visasili.

Visasili hivi vilikuwa kizuizi kikuu kwenye njia ya maendeleo ya Uislamu, na kwa sababu hii, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alijitahidi kwa kadiri alivyoweza kuzifutilia mbali hizi dalili za 'Ujinga' zilizokuwa na huu ushirikina na visasili. Alipokuwa akimpeleka Bwana Ma'az bin Jabal huko Yemen, alimpa maelekezo yafuatayo: "Ewe Ma'az! Ondoa kutoka miongoni mwa watu dalili za ujinga na fikara na itikadi za kishirikina na zihuishe hadith za Uislamu ambazo hutulingania kutafakari na kuitumia akili." 11

Kwa vile ilikuwa kinyume na jamii kubwa ya Waarabu waliotawaliwa kwa miaka mingi na itikadi za kishirikina, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alikuwa akisema: "Dalili zote za ujinga ziko chini ya miguu yangu." – yaani kwa kuja Uislamu, desturi, itikadi na njia za kupatia vyeo vimeharibiwa kabisa na vimekanyagwakanyagwa chini ya miguu yangu.

Sasa, ili kufafanua uzuri wa mafundisho ya Uislamu, tunatoa hapa chini mukhtasari wa maelezo ya itikadi za Waarabu wa Zama za Ujinga.

## 1. Kuwasha Moto Kwa Ajili Ya Kuja Kwa Mvua

Maeneo mengi ya Peninsula ya Uarabuni yanakabiliwa na ukame. Ili kuhakikisha upatikanaji wa mvua, watu wa maeneo hayo walikuwa na kawaida ya kujipatia matawi ya miti iitwayo *Sala* na '*Ushr* ambayo hushika moto upesi. Huyafunga matawi hayo kwenye mkia wa ng'ombe jike na kumpeleka ng'ombe huyo juu ya mlima. Baadae huyachoma matawi hayo.

Kutokana na kuwako kwa vitu vinavyoshika moto kwenye yale matawi ya '*Ushr* miali ilitokea mwenye moto ule na kuuchoma mwili wa yule ng'ombe jike. Kutokana na maumivu yatokanayo na kuungua, ng'ombe yule alianza kukimbia na kulia.

Watu hawa walilitenda jambo hili chafu na kulichukulia kuwa ni ishara ya kufanana na ngurumo na radi ya mbinguni. Waliichukulia ile miali ya moto kuwa inawakilisha radi na mlio wa ng'ombe kuwa unawakilisha ngurumo na kukifikiria kitendo hiki kuwa kinaleta mvua.

## 2. Kama Ng'ombe Jike Hakunywa Maji Walimpiga Ng'omba Dume

Waarabu waliwapeleka majike na madume ya ng'ombe kwenye kingo za vijito ili wakanywe maji. Wakati mwingine hutokea kwamba madume hunywa maji lakini majike yakaacha kunywa maji. Kutokana na jambo hilo walifikiria ya kwamba, hilo lilitokana na pepo wabaya waliokaa baina ya pembe za madume na ambao hawakuwaruhusu majike yao kunywa maji. Hivyo basi, ili kuwafukuza pepo wabaya hao, walizipiga nyuso za yale madume.

## 3. Waliwapiga Chapa Ya Moto Ngamia Wenye Afya Njema Ili Wengine Wapone.

Kama kukitokea maradhi miongoni mwa ngamia au kidonda au yakaonekana malengelenge midomoni na makooni mwao, alitafutwa ngamia mwenye afya timam na midomo yake, sehemu ya juu ya mguu wake na nyonga yake vilipigwa chapa ya moto ili kuyazuia maradhi hayo yasienee miongoni mwa wanyama wengine. Hata hivyo sababu ya kufanya hivyo haijulikani. Inaweza ikachuliwa kwamba kitendo hiki kinaweza kikawa na hali ya kuzuia maradhi na kilikuwa aina fulani ya tiba ya kisayansi, lakini tunapouangalia ukweil uliopo kwamba kutokana na ngamia wengi waliokuwapo, ni ngamia mmoja tu aliyechaguliwa katika mateso ya namna hiyo, tunaweza kusema kwamba jambo hili nalo lilikuwa kitendo cha ushirikina na kilisimamia kwenye msingi wa uongo.

## 4. Ngamia Aliwekwa Pembeni Mwa Kaburi

Mtu mwenye cheo kikuu alipofariki dunia, ngamia aliwekwa kwenye shimo karibu na kaburi lake na alikuwa hapewi maji wala malisho ili kwamba afe, na huyo mtu aliyekufa apate mnyama wa kumpanda katika Siku ya Kiyama na asifufuke akiwa yu atembea kwa miguu.

### 5. Waliikata Miguu Ya Ngamia Karibu Na Kaburi

Kwa kuzingatia ukweli kwamba mtu alipokuwa hai alikuwa na kawaida ya kuchinja ngamia ili kuwafurahisha ndugu na wageni wake, na kama kuonyesha heshima na malipo kwa marehemu huyo, warithi wake huikata miguu ya ngamia karibu na kaburi lake katika namna ya kumsababishia maumivu makali mnyama huyo.

## Uislamu Wapambana Na Ushirikina

Vitendo hivi (tukiachilia mbali ukweli uliopo kwamba hakuna chochote miongoni mwao kinachoafikiana na akili na sababu za kisayansi, kwa sababu mvua hainyeshi kwa kuwasha moto, kumpiga ng'ombe dume hakuna athari zo zote kwa ng'ombe jike, kumpiga chapa ngamia mwenye afya hakuwaponyi ngamia wagonjwa n.k.), ni aina fulani ya ukatili kwa wanyama. Kama tukilinganisha vitendo na itikadi hizi, na sheria thabiti zilizoamrishwa na Uislamu kwa ajili ya hifadhi ya wanyama, bila shaka tutasema kwamba sheria ya dini hii imetangaza vita ya dhahiri dhidi ya fikara za jamii ile.

Ziko kanuni nyingi za kiislamu zenye kuuhusu ulinzi wa wanyama na tunaweza kutaja kuhusiana na jambo hili kwamba, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) amesema: "Mnyama wa kupanda ana haki sita juu ya bwana wake":
Anapokuwa safarini na akatua (ili kupumzika) ampe malisho mnyama huyo;
Anapopita mahali penye maji amruhusu mnyama yule kunywa maji yale; Asimpige mnyama yule usoni;
Anapokuwa na mazungumzo marefu na mtu, asiendelee kukaa mgongoni mwa mnyama yule;
Asimbembeshe mzigo mzito zaidi ya uwezo wake.
Asimlazimishe mnyama yule kusafiri umbali ulio zaidi ya uwezo wake.[12]

### 6. Tiba Ya Wagonjwa:

Kama mtu aliumwa na nyoka au na nge, alivikwa shingoni mapambo ya dhahabu. Waliamini ya kwamba mtu wa aina hiyo akibeba shaba au bati mwilini mwake, angeweza kufa. Kuhusu kichaa cha mbwa (yaani maradhi yasababishwayo na kuumwa na mbwa) waliyatibu kwa kupaka kiasi kidogo cha damu ya chifu wa kabila kwenye kile kidonda.
Na kama mtu akitokewa na dalili za wendawazimu, alikwenda kukaa kwenye matambaa machafu na alivikwa shingoni mifupa ya wafu ili kumfukuza pepo mchafu.

Ili kuthibitisha kwamba mtoto wao hajeruhiwi na pepo wachafu, walifunga jino la mbweha na paka kwenye kamba kisha wakamvika shingoni. Mtoto anapoota majipu au chunusi mwilini mwake, mama yake alimtwisha chungio kichwani mwake na wakaiendea kila nyumba ya mtu wa kabila lao wakikusanya mikate na tende, vitu ambavyo baadae humpa mbwa, ili kwamba majipu na chunusi za mtoto yule ziweze kupona. Wanawake wengine wa kabila lile walijihadhari kwamba watoto wao wasizile tende na mikate ile ili wasije nao wakapatwa na maradhi yale.

Kama mtu alipatwa na ugonjwa wa ngozi (kwa mfano ugonjwa wenye athari za mikwaruzo mwilini) alikuwa akijitibu kwa kukipaka chungu mate yake.

Kama maradhi ya mtu yalichukua muda mrefu kupona, walidhania kwamba mgonjwa yule alimuuwa nyoka au mnyama yeyote mwingine aliyekuwa na uhusiano na pepo wabaya. Hivyo basi, ili kuwaomba radhi hao pepo wabaya walifinyanga masanamu ya ngamia ya udongo na kisha wakayasheheni shayiri, ngano na tende.

Walivipeleka na kuviacha vitu hivi mkabala na tundu kwenye mlima na kisha wakarudi tena kupatembelea hapo siku iliyofuatia.

Kama wakikuta kwamba vitu vile vimeliwa, walilichukulia jambo hilo kuwa ni dalili ya kukubaliwa kwa zawadi zile na hao pepo wabaya na waliamua kwamba yule mgonjwa atapona. Hata hivyo, kama mambo yakienda kinyume na hivyo, walifikiria kwamba zawadi zile, kwa vile zilikuwa ndogo, wale pepo wabaya hawakuzipokea.

## Jinsi Uislamu Ulivyofanya Kampeni Dhidi Ya Ushirikina Huu

Uislamu ulifanya kampeni dhidi ya ushirikina huu kwa njia kadhaa. Walikuwako mabedui wa kiarabu waliokuwa wakiwaagua wagonjwa wao kwa viambatisho vya kichawi na mikanda iliyosheheni mawe na mifupa. Walipotokea mbele ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na wakamwuliza kuhusu namna ya kutibu wagonjwa kwa miti shamba na madawa, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema:

“Ni lazima kwa kila mgonjwa kuitafuta dawa, kwa kuwa Allah Aliyeumba ugonjwa pia Ameumba dawa yake.[13] Na Sa’ad bin Abi Waqqas alipopatwa na maradhi ya moyo, Mtukufu Mtukume (s.a.w.w.) alimwambia: “Nenda ukamwone Harith Kaldah, mganga maarufu wa Thaqif.” Baadae Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe alimshauri Sa’ad atumie dawa maalum.[14]

Vilevile kuna simulizi nyingine zinazotangaza viambatanisho vya kiuchawi ili kuondokana na athari zozote ziwazo. Hapa tunanukuu mbili katika hizo:

“Mtu mmoja ambaye mwanawe alikuwa akiugua kutokana na maumivu ya koo alikwenda kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akiwa na viambatanisho vya kiuchawi. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwambia: “Usiwaogofye watoto wako kwa viambatanisho hivi vya kiuchawi. Huna budi kuyatibu maradhi haya kwa mafuta ya mti wa Aloe (*aloe-wood-oil*).[15]

Imam wetu wa sita, As-Sadiq (a.s.) amesema: “Nyingi ya hirizi na viambatanisho vya kichawi huwa sawa na ushirikina.[16]

Kwa kuwaongozea watu kwenye matumizi ya dawa nyingi (ambazo maelezo yake maalum yote, yamekusanywa na wanavyouni wa kiislamu wakuu wa hadith chini ya kichwa cha habari cha “*Tibur Rasul*” (Tiba za Rasuli), “*Tibur Ridha*.” (Tiba za Ar-Ridha), n.k. Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na Warithi

wake watakatifu kwa mara nyingine tena walishambulia kwa nguvu ushirikina huu, na kusema kweli, waliwakasirisha Waarabu wa Zama za Ujinga.

## Ushirikina Mwingine

Walizitumia njia zifuatazo katika kujikinga na fadhaa na woga: Kila walipofika kwenye kijiji, waliogopa baadhi ya magonjwa ya kuam- bukiza au pepo wabaya. Ili kuiepuka hofu hiyo, walilia kama punda mara kumi kwenye lango la kijiji hicho. Wakati mwingine pia walining'iniza mifupa ya mbweha shingoni mwao. Kama wakipotea njia wakati wa kusafiri jangwani, waliyavaa mashati yao baada ya kugeuza ndaninje. Wakati walipokuwa wakisafiri walihofia vitendo vya kifasiki kwa upande wa wanawake wao.

Kupata uhakika kuhusiana na jambo hili walifunga uzi kwenye vikonyo au matawi ya mti. Kama uzi ule ukibakia kufungika vizuri wakati wa kurejea kwao, waliridhika kwamba wanawake wao hawakutenda makosa ya uasherati. Hata hivyo, kama wakiukuta ule uzi ukiwa umefunguka au haupo, waliwakashifu wanawake wao. Kama meno ya watoto wao yaking'oka waliyakamata kwa vidole viwili na kisha wakayarushia kuelekea kwenye jua wakisema: "Ewe jua! Wape meno yaliyo mazuri kuliko haya."

Kama watoto wa mwanamke fulani hawakuishi (yaani walikufa kwenye kipindi cha utotoni), waliamini kwamba watoto wake wataishi kama akitembea mara saba juu ya maiti ya mtu mashuhuri aliyeuawa.

Haya ni maelezo mafupi ya ushirikina mwingi mno ulioyatia kiza maisha ya Waarabu wa Zama na Ujinga na umezizuia akili zao kutokana na kuendelea zaidi.

1. "Tamaddun-i- Islamic wa Arab", uk. 78 -102
2. Murujudh Dhahab, Juzuu ya 3, uk. 373.
3. Kitabu hiki kinatolewa kwa Kiingereza na "Islamic Seminary" kwa kichwa cha habari cha "Peak of Eloquence."
4. Rejea: A'lamul Wara, Uk. 35 – 40, na Bihaarul Anwaar, Juzuu ya 19, Uk. 8 –11.
5. Nahjul Balaghah, Hotuba ya 1.
6. Mwenye kitabu 'Usudul-Ghaba', Ibn Athir anamnukuu Qays akisema kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimuuliza ni mabinti wangapi aliowazika wakiwa hai na akajibu ya kwamba idadi yao ilikuwa ni kumi na wawili.
7. Bihaarul Anwaar, Juzuu ya 22, uk. 155.
8. Bihaarul Anwaar, Juzuu 6, uk. 92.
9. Biharul Anwaar, Juzuu ya 2, uk. 286 – 369.
10. Tazama 'Futuhul Buldaan,' Balazari, uk. 458.
11. 'Tuhaful'Uqul', uk. 29
12. Man la Yahzaruhul Faqih, uk. 228
13. At-Taaj. Juzuu 3, uk. 178. Mtukufu Mtume (saw) alikuwa na maana ya kusema kwamba hivyo viambatisho wa kichawi "appendages" havikuwa tiba itoshelezayo
14. At-Taaj, Juzuu ya 3 uk. 179
15. At-Taaj, Juzuu ya 3, uk. 184.
16. Safinatul Bihar, neno la asili ni "raqa."

# Sura Ya Tatu: Hali Ya Dola Za Kirumi Na Ki-Iran

Ni muhimu mno kujifunza mazingira mawili yafuatayo ili kuweza kutath- mini harakati takatifu za kiislamu: Mazingira ya kuteremshwa kwa Qur'ani Tukufu – yaani ile sehemu ambayo kwayo Uislamu ulianzia na kupiga hatua ya maendeleo.

Jinsi ya fikara za watu walioishi kwenye sehemu zilizostaarabika kwenye zama zile, na ambao fikara zao na tabia zao ziliaminiwa kuwa ndizo zilizoendelea na zilizokuwa bora zaidi. Historia yatueleza kwamba sehemu zilizoelimika zaidi kwenye zama zile, zilikuwa falme za Urumi na Iran.

Ili kuukamilisha mjadala huu ni muhimu kwamba hatuna budi kujifunza hali ya hizi falme mbili, kila moja peke yake, ili kwamba iwezekane kukadiria thamani ya ustaarabu ulioletwa na Uislamu.

Katika siku hizo Urumi haikuwa na hali njema ikilinganishwa na mpinzani wake, yaani Iran. Upinzani wa ndani na vita vilivyokuwa vikiendelea kutoka nje, vilivyopiganwa na Iran juu ya Armenia, n.k. vimewaweka watu wake kwenye hali ya kuyakubali mapinduzi. Zaidi ya jambo jingine lolote lile, kutofautiana katika maoni ya kidini kumezifanya tofatuti hizi kuwa pana zaidi.Ugomvi baina ya Wakristo na wenye kuabudu masanamu haukukoma. Wakuu wa kanisa walipozitwaa hatamu za serikali, mikononi mwao, waliwakandamiza mno wapinzani wao, na jambo hili lenyewe, lilitengeneza njia ya ujenzi wa kikundi cha raia wachache wasioridhika; jambo ambalo laweza kuhesabiwa kuwa kipengele kikubwa cha kusilimu kwa taifa la Kirumi na ukaribisho wa furaha waliotoa kwenye harakati hii lilikuwa ni kunyimwa haki walikokuhisi watu wa makundi mbalimbali kwa sababu ya ukali na utesaji wa wakuu wa Kanisa.

Siku baada ya siku, hofu na nguvu ya dola ya Kirumi ilikuwa ikipungua kutokana na tofauti zilizokuwapo miongoni mwa makasisi katika upande mmoja na kuwako kwa madhehebu nyingi za kidini, kwa upande mwingine.

Zaidi ya hapo, mataifa meupe ya kaskazini na ya njano ya mashariki yalitamani sana kulitwaa eneo lenye rutuba la Ulaya, na kwenye wakati fulani walileteana madhara makubwa wao kwa wao kwa vita baina yao.

Jambo hili, lenyewe likawa sababu ya kugawanyika kwa Dola ya Kirumi na kuwa na pande mbili ambazo ni upande wa Mashariki (wa Kigiriki) na upande wa Magharibi wa (Urumi –Kilatini au Utaliani wa kale). Wanahistoria wanaamini ya kwamba hali za kisiasa, kijamii na kiuchumi za Urumi kwenye karne ya sita Masihiya zilivurugwa mno. Kiasi kwamba hawakuweza kuifikiria hata ile nguvu ya Urumi juu ya Iran kuwa ni ushuhuda wa uwezo wake wa kijeshi. Na hivyo walikuhusisha kushindwa kwa Iran na utawala mbaya wa serikali ya Iran. Hizi Dola mbili zilizokuwa viongozi na watawala wa ulimwengu, zilikuwa kwenye hali ya ghasia na utovu wa serikali wakati wa kuanza kwa Uislamu. Dalili zake zilizaa nyoyoni mwa watu shauku na tamaa kubwa ya sheria maalum zitaka- zoweza kuwathibitishia ustawi wao.

## Majadiliano Ya Msimu Nchini Urumi

Kwenye baadhi ya nchi watu wazembe na wenye tamaa za kimwili wali- toa mijadala kadhaa juu ya matatizo yasiyo na maana na yaliyo duni kwa lengo la kuwarudisha nyuma watu kutokana na aina zote za maendeleo ya kisayansi na kiviwanda na hivyo kuyafanya maisha ya watu wa hali ya juu kuwa yasiyo na maana yoyote.

Kuhusiana na jambo hili tunayo idadi kubwa ya mifano na matukioa ya kale yafananayo na haya ya sasa kwenye nchi nyingi za kiislamu ambayo hayawezekani kuyataja hivi sasa. Ilitukia kwamba Urumi ya siku hizo ilikuwa zaidi ya mambo yote, ikitatanishwa na matatizo ya aina hii. Kwa mfano, mfalme na watu wa baraza lake, chini ya ushawishi wa baaadhi ya taasisi za kidini, waliamini ya kwamba Nabii 'Isa (a.s.) alikuwa na asili mbili na utashi namna mbili, ambapo baadhi ya Wakristo wa Kiya'qubi walikuwa wakiitakidi ya kwamba alikuwa na hali moja tu na utashi mmoja tu.

Jambo hili lisilo na msingi liliushambulia uhuru na amani ya Urumi, na likajenga mfarakano mkubwa miongoni mwa watu hao, kwa kuwa serikali ililazimika kuzihami itikadi zake, na hivyo basi, ikawatia wapinzani wake kwenye mateso makali. Kwa matokeo ya shinikizo na chuki kubwa, baadhi yao walikimbilia Iran.

Hawa ndio wale watu ambao, katika kulikabili jeshi la Waislamu, waliyakimbia mahandaki yao na kuwapokea Waislamu kwa mikono miwili. Urumi ya siku hizo ilikuwa kama Ulaya ya Zama za Kati. Mnajimu maarufu wa Kifaransa aliyeitwa Camile Flammarion anaisimulia hadithi ifuatayo kuhusu kiwango cha elimu huko Ulaya katika Zama za Kati:

"Kitabu kiitwacho *Majmu'a-i Lahutiah* (Kitabu cha Elimu ya tabia na sifa za Mungu – mkusanyo wa kitheolojia) kilikuwa ni mdhihiriko kamili wa falsafa ya kiuwanachuoni katika Zama za Kati na kilifundishwa barani Ulaya kwa muda wa miaka mia nne kikiwa ndicho kitabu cha mafundisho. Sehemu ya kitabu hiki inajadili kama inawezekana kwa malaika wachache hivi kuishi kwenye ncha ya sindano au ni umbali wa *'league'* (maili) ngapi kutoka mtoto wa jicho la kulia hadi yule wa jicho la kushoto la Baba wa Mbinguni?"

Imekuwa na bahati mbaya kiasi gani Urumi! Katika wakati ule ule ilipokuwa imetatizwa na vita kutoka nje yake, mfuriko wa tofauti za ndani, ambazo nyingi kati yao zilijidhihirisha kwenye vazi la dini, zilikuwa zikiikokota, siku hadi siku, karibu zaidi na genge. Wakati Wayahudi, ambao walikuwa watu waovu na wenye makri walipoona kuwa shinikizo la Mfalme wa Kikristo wa Urumi limeivuka mipaka waliyoiweka, wakapanga kuiangusha serikali ya Kirumi na hata kuukalia mji wa Antakia katika wakati fulani na kuyakata masikio, pua na midomo ya Askofu Mkuu.

Baada ya muda fulani Serikali ya Urumi ililipiza kisasi kwa kuwachinja Wayahudi wa Antakia.Mauaji ya kikatili ya aina hii yalirudiwa mjini Roma kwa mara kadhaa baina ya Wayahudi na Wakristo na kwenye nyakati fulani, hizi hisia za kulipiza kisasi zilikuwa na matokeo hasi yake hata nje ya mipaka ya Dola

hiyo. Kwa mfano, safari moja Wayahudi wal- inunua Wakristo elfu themanini kutoka kwa Wairani na wakawachinja kama kondoo kwa lengo la kulipiza kisasi kwenye jamii ya Kikristo.

Hapa ndipo mahali ambapo msomaji mwenye ujuzi anaweza kuuona msingi wa giza na ghasia wa ulimwengu unaoendana na zama za kuja kwa Uislamu na kukubali kwamba haya mafundisho yaliyo bora zaidi yaliyothibitisha wokovu wa mwanaadamu kutokana na hali ya hewa ile ya giza, hayatokani na akili za mwanaadamu, na huu upepo wa kusisimua na wenye kuburudisha wa umoja na makubaliano ya pamoja, na huu ujumbe wa amani na uaminifu, ambao ndio lengo la dini ya kiislamu, hauna chanzo kingine badala ya kile cha ghaibu.

Yawezekanaje kusemwa kwamba Uislamu, uliotoa haki ya kuishi hata kwa wanyama, ni mtoto wa mazingira kama haya ya umwagaji wa damu?! Uislamu uliweka kando mijadala yote hii isiyo na msingi na ya kipuuzi kuhusu utashi na Nabii ‘Isa (a.s.) na ukamtambulisha kwa maneno yafuatayo:

{مَا الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ وَأُمُّهُ صِدِّيقَةٌ ۖ كَانَا يَأْكُلَانِ الطَّعَامَ ۗ {75

***“Masihi mwana wa Mariamu*** (***si chochote kingine***) ***ila ni mtume*** (***tu***)***; bila shaka mitume*** (***wengi***) ***wamekwishapita kabla yake; na mama yake ni mwanamke mkweli; wote wawili walikuwa wakila chakula*** (***kama watu wengine***)***...”*** (***Al-Ma’idah, 5:75***)***.***

Kwa Aya hii, Uislamu uliikomesha idadi kubwa ya mijadala ya kipuuzi ya wakuu wa Kanisa juu ya roho, damu, na upekee wa Nabii Isa (a.s.). Wakati huo huo, ulimshawishi mwanaadamu kuachana na ugomvi na umwagaji wa damu kwa kumfunza mafundisho yaliyo bora zaidi na kuzihuisha sifa zake bora za kibinadamu.

## Iran Au Chanzo Cha Ustaarabu Wa Zama Zile

Wanachuoni wa elimu ya jamii wanaona kwamba ubovu wa serikali ya Iran katika zama zile ulitokana na hali yake ya kidhalimu na utawala wa mtu mmoja juu ya watu wengi.

Waarabu wajinga, pamoja na ushenzi wao, walikuwa na aina fulani ya serikali ya kidemokrasia. Kwa kuwa kwao na ‘*Darul Nadwah’* iliyokuwa na cheo cha Baraza la Mashauriano la Kitaifa, kwa kadiri fulani walikuwa wameiondoa hitilafu ya utawala wa Kiimla. Ingawa serikali, iwe ya kikatiba au ya kiimla, haiwezi kutatua matatizo bila ya utawala wa kidini, na imani na ulinzi wa askari kanzu, na vile vile haiwezi kuidumisha sheria na utaratibu mwema, kitu ambacho ndio hasa lengo la serikali yoyote ile, lakini ni ukweli ukubalikao kwamba hekima na busara za mtu mmoja haziwezi kuwa sawa na utambuzi wa kundi la watu.

Makri na ugomvi ni kidogo mno katika serikali ya kidemokrasia. Ni kwa sababu hii kwamba utukufu na uwezo au unyonge na fedheha ya Wairani umehusika mno na udhaifu au nguvu ya serikali yao ya mtu

mmoja. Uchunguzi wa kipindi cha serikali ya Wasasani uliotokea katika kipindi kile unaudhihirisha usemi huu kwa ukamilifu kabisa.

## Hali Ya Ujumla Ya Iran Pamoja Na Mapambazuko Ya Uislamu

Kuja kwa Uislamu na uteuzi kwenye ujumbe wa kiutume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) katika mwaka wa 611 Masihiya ulikwenda pamoja na utawala wa Khusro Pervez (mwaka 590 hadi 628 Masihiya). Kuhajiri kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kutoka Makkahh kwenda Madinah pia kulitokea kwenye kipindi cha utawala wake (mnamo siku ya Ijumaa. Tarehe 16 Julai, 622 Masihiya) na tukio hili likawa mwanzo wa historia ya Waislamu.

Katika siku hizo, dola mbili zilizokuwa kubwa na zenye nguvu (Ugiriki na Usasani) Iran ilitawala sehemu kubwa ya ulimwengu uliostaarabika wa zama zile. Walikuwa wakigombana na kupigana wao kwa wao kwa kipindi kirefu kila moja ikitaka kumiliki na kuutawala ulimwengu.[1]

Vita virefu walivyopigana Wairani dhidi ya Warumi vilianza katika zama za utawala wa Anushirwan (aliyetawala tangu 531 hadi 589 Masihiya) na ikaendelea kwa kipindi cha miaka ishirini na minne yaani hadi kwenye zama za utawala wa Khusro Pervez.

Hasara kubwa na matumizi makubwa mno ambayo yalibebwa na dola hizi mbili, Iran na Urumi kutokana na vita hivi yalizipiga nchi hizi mbili zilizokuwa kubwa pigo kali mno na hakuna chochote kilichoachwa kwenye nchi hizi ila umbo tu, bila ya kiini hasa.

Ili tuweze kuielewa hali ya Iran vizuri mno, kutoka kwenye kila pembe, itatulazimu kujifunza kwa mukhatasari hali ya serikali mbalimbali tangu mwishoni mwa utawala wa Anushirwan kwenda mbele hadi kwenye wakati Waislamu walipojitokeza.

## Huba Ya Anasa Katika Kipindi Cha Wasasani

Kwa kawaida Wafalme wa Kisasania walipenda mno anasa na raha. Fahari na mapambo ya baraza la Kisasania viliyastaajabisha macho.

Katika kipindi cha utawala wa Wasasani, Wairani walikuwa na bendera iliyoitwa '*Dirafshi – Kaavyaani*'. Wasasani waliitweka bendera hiyo kwenye uwanja wa vita au waliiweka juu ya paa la Ikulu wakati wa sherehe. Bendera hiyo ilinakshiwa kwa kila aina ya vito. Kwa mujibu wa mwandishi mmoja, bendera hii isiyo na kifani ilinakshiwa kwa njumu za vito na vitu vingine vyenye thamani, ambavyo gharama yake ilikasimiwa kuwa dirhamu 1, 200, 000 (au pauni 30,000).[2]

Kwenye Ikulu za kustaajabisha za Wasasani kulikuwa na vito vingi na vitu vingine vya thamani, na yamekusanywa masanamu ya ajabu na michoro mingi mno kiasi kwamba macho ya watazamaji yalishangazwa mno.

Kama tukitaka kuyajua maajabu ya ikulu hizi itatutosha kama tukilitazama zulia jeupe kubwa walilolitandaza mwenye ukumbi wa moja ya ikulu hizi. Zulia hili, lililoitwa *'Sabaristan-i Kisra'* lilitengenezwa na watawala wa Kisasania kwa lengo la kwamba, katika nyakati za furaha waweze kuwa kwenye mielekeo mizuri na ili daima waweze kuwa na mandhari nzuri na za uchangamfu za majira ya kuchipua machoni mwao.[3]

Imesemekana kwamba zulia hili lilikuwa na urefu wa dhiraa mia moja na hamsini na upana wa dhiraa sabini. Pindo lake lote pamoja na nyuzi za pindo hilo zimesukwa kwa dhahabu, na vito vilitomewa humo.[4]

Miongoni mwa wafalme wa Kisasania aliyekuwa akipenda mno anasa alikuwa ni Khusro Pervez. Kwenye Ikulu yake alikuwa na maelfu ya wake, wajakazi, malenga na wanamuziki. Kwenye kitabu chake kiitwacho '*Sanii Mulukul Ardh*' (wafalme wakuu wa duniani) Hamza Isfahani anayaelezea maisha ya anasa ya mfalme huyu kwa maneno haya:

"Khusro Pervez alikuwa na wake elfu tatu na wajakazi elfu kumi na mbili waliokuwa wacheza muziki. Alikuwa na wanaume elfu sita waliokuwa wakifanya kazi ya ulinzi. Farasi wapatao 8,500 walikuwa wamewekwa alama za masikioni kuwaainisha kwamba ni kwa ajili ya yeye kupanda. Alikuwa na tembo (ndovu) 960 na nyumbu 12,000 kwa ajili ya kubeba mizigo yake. Vile vile alikuwa na ngamia elfu moja."[5] Kisha Tabari anaongezea juu ya hayo kwa kusema kwamba: "Mfalme huyu alipenda sana vito na vyombo vya thamani n.k. zaidi ya mtu ye yote mwingine."[6]

## Hali Za Kijamii Nchini Iran

Kwa vyovyote vile hali za kijamii ya Iran katika zama za Wasasani hazikuwa nzuri zaidi ya hali ya kisiasa iliyokuwako mwenye baraza la Mfalme. Utawala wa kitabaka uliokuwako nchini Iran tangu zamani, ulilichukua umbo lake kali zaidi kwenye zama za utawala wa Wasasani. Watu wa koo zilizo bora na wakuu wa dini walikuwa bora zaidi kuliko watu wa matabaka mengine. Ofisi zote za umma na kazi zilizo muhimu ziliwekwa kwa ajili yao.

Mafundi na wakulima walinyimwa haki na upen- deleo wote wa kijamii. Ukiachilia mbali kule kulipa kodi na kushiriki kwenye vita, hawakuwa na kazi yoyote nyingine ya kutenda.

Mwandishi mmoja, Bwana Nafisi anaandika hivi kuhusu utofautishaji wa matabaka ya watu kwenye zama za utawala wa Wasasani: "Jambo lililokuwa sababu hasa ya kupandikiza ugomvi miongoni mwa Wairani ilikuwa ni utofautishaji wa kitabaka uliokuwa mkali zaidi na uliodumish- wa na Wasasani nchini Iran. Mizizi ya jambo hili ilitokana na ustaarabu wa kale, lakini ilikazwa mno kwenye kipindi cha utawala wa Wasasani."

Hapo awali familia saba za ukoo bora na baada ya hizo, tabaka nyingine tano zilifaidi upendeleo na mtu wa kawaida alinyimwa upendelea huo. Karibuni 'umilikaji' wote ulipewa zile familia saba. Idadi ya watu

wa Iran katika zama za Wasasani ilikuwa karibuni watu milioni 140. Kama tukichukulia kwamba idadi ya watu wa kila moja ya familia hizi ni laki moja, idadi ya watu wa familia zote itakuwa ni laki saba.

Na kama tukichukulia ya kwamba maafisa mabwana wa mipakani na ambao nao walifaidi haki ya kumiliki kwa kiasi fulani, nao walikuwa laki saba, hali itakuwa kwamba, kati ya watu milioni 140, ni watu milioni moja na nusu tu waliokuwa na haki ya kumiliki na wale wote wengine walinyimwa hii haki ya kimaumbile ambayo Allah Amempa mwanaadamu.[7]

Mafundi na wakulima, walinyimwa haki na upendeleo wote lakini walipasika kubeba mabegani mwao mzigo mzito wa gharama za zile koo bora, hawakuona kuwa ni jambo lenye thamani kuzihifadhi hali hizi. Hivyo basi, wengi wa wakulima na watu wa tabaka la chini walizikana kazi zao na wakakimbila kwenye majumba ya watawa ili kuepuka ulipaji wa kodi nzito.[8]

Baada ya kutoa maelezo ya misiba ya mafundi na wakulima wa Iran, mwandishi wa kitabu kiitwacho '*Iran-dar Zaman-i- Sasaniyan'* ananukuu maelezo haya ya mwanahistoria mmoja wa kizungu aliyeitwa Amyan Marcilinos: "Mafundi na wakulima waliishi maisha ya kimaskini na fedheha katika zama za utawala wa Wasasani. Ilipotokea vita walitembea kwa miguu na ndio waliounda mstari wa nyuma wa jeshi na wasio na faida yoyote, kana kwamba wameamriwa utumwa wa daima, na hawakuweza kupewa mishahara au zawadi kwa kazi waliyoifanya."[9]

## Haki Ya Kupata Elimu Ilihifadhiwa Kwa Ajili Ya Watu Wa Matabaka Ya Juu Tu

Katika zama za Wasasani ni watoto wa matajiri na wa koo bora tu waliopasika kupata elimu, na umma na matabaka ya katikati walinyimwa kupata elimu na heshima.

Hii dosari mbaya mno katika utamaduni wa Iran ya kale ilikuwa bayana mno kiasi kwamba hata waandishi wa tenzi (Khudainamah na Shahnamah) wameitaja kwa maneno ya dhahiri, ingawa mada yao hasa ilikuwa ni maelezo ya mafanikio ya mashujaa.

Bwana Firdausi, mwandishi maarufu wa tenzi nchini Iran, ameitaja hadithi moja kwenye Shahnamah yenye ushuhuda wa dhahiri juu ya jambo hili. Hadithi hii ni ya wakati wa Anushirwan yaani katika muda ule ule ambao utawala wa Kisasania ulikuwa ukipita katika zama zake zilizo bora zaidi. Na hadithi hii yaonyesha kwamba watu wengi ukiwamo umma wote hawakuwa na haki ya kuelimika na hata yule mpenzi wa hekima na uadil- ifu, Anushirwan hakuwa tayari kuwapa haki ya elimu watu wa matabaka mengine ya umma ule!

Firdausi anasema: "Fundi viatu mmoja akajitokeza na kujitolea kutoa kiasi kikubwa cha dhahabu na fedha ili kuzilipia gharama za vita baina ya Iran na Urumi. Wakati ule Anushirwan alikuwa mhitaji mno wa msaada wa fedha, kwa kuwa kiasi cha askari elfu thelathini wa Iran walikabiliwa na upungufu wa chakula na silaha. Kulikuwa na makelele miongoni mwa askari walioidhihirisha huzuni yao mbele ya

mfalme mwenyewe.

Anushirwan aliudhishwa na hali hii ya mambo na akatahadharika kuhusu mwishilizio wake. Mara moja akamwita waziri wake mwenye hekima aliyeitwa Buzurg Mehr atafute dawa ya hali ile na akamwamrisha aende upesi Mazandran akatafute fedha za kugharimia vita ile.

Hata hivyo, Buzurg Mehr akasema: "Hatari iko karibu sana, hivyo basi ni lazima kufanya jambo fulani liwezalo kutoa dawa ya hatari hii." Hapo ndipo Buzurg Mehr akapendekeza mkopo wa kitaifa. Ushauri huu ulipendwa na Anushirwan aliyeamrisha ya kwamba zichukuliwe hatua kuhusiana na jambo hili bila ya kuchelewa. Buzurg Mehr akawapeleka maafisa kwenye majiji na miji ya karibuni na wakawafahamisha matajiri wa sehemu hizo hali ile.

Fundi viatu akajitolea kutoa gharama zote za vita ile. Malipo aliyoyataka kutokana na huduma hii yalikuwa kwamba mwanawe wa pekee aliyependa sana elimu aruhusiwe kuipata. Buzurg Mehr alililifikiria ombi hili kuwa ni dogo sana likilinganishwa na zile fedha alizozitoa.

Aliharakisha kumwendea mfalme na kumfahamisha lile ombi la fundi viatu. Anushirwan alichukizwa, akamkemea waziri wake na akasema: "Unaniomba jambo la ajabu kiasi gani! Hili ni jambo lisilofaa hata kidogo, kwa sababu, atakapotoka nje ya mpango wa matabaka, mila ya mpango wa matabaka nchini humu itatetereka na madhara yatakayotokana na hali hiyo, yatakuwa makubwa mno kuliko ile dhahabu na fedha anayotaka kuitoa."

Firdausi anaielezea falsafa ya kidanganyifu ya Anushirwan kwa maneno ya yeye mfalme mwenyewe: "Mwana wa mfanyibiashara atakapokuwa katibu na vile vile akajipatia ustadi, hekima na ujuzi.

Basi, mwana wetu atakapokitwaa kiti cha enzi, atamhitaji katibu aliyejaaliwa bahati njema.
Kama mwana wa mtu ajishughulishaye na viatu atajipatia ustadi, utamwazima macho yenye uwezo wa kuona vizuri, pamoja na masikio.

Katika tukio hilo, hakuna kitakachomsalia mtu mwenye busara wa ukoo bora ila majuto na majonzi."

Hivyo pesa za fundi viatu yule zilirudishwa kwa amri ya "Mfalme Mwadilifu." Jambo hili lilimfanya yule fundi viatu asiyekuwa na msaada wowote kutokuwa na furaha hata kidogo na; kama ilivyo kawaida kwa watu wanaokandamizwa, alimlalamikia Allah Mwenye nguvu zote wakati wa usiku na akaifanya "kengele ya uadilifu wa Mungu ilie."

Kwa kauli ya Firdausi: "Yule mjumbe alirudi na pesa zile na yule fundi viatu akahuzunika sana kuhusiana na fedha zile.

Alihuzunishwa sana na maneno ya Mfalme na ulipoingia usiku aliipiga "kengele ya Mungu."[10]

Alipokuwa akizungumzia juu ya sababu za kuanguka, utovu wa utulivu na mvurugiko wa kipindi cha utawala wa Wasasani, mwandishi wa kitabu kiitwacho *Tarikh-i-Ijtima'i-Iran*; ambaye yeye mwenyewe

yu mmoja wa watangulizi wa wazalendo, anatupa picha ya haki ya elimu kuwa kitu kilichotengwa kwa ajili ya watu wa matabaka ya juu, kwa maneno haya: "Katika kipindi hiki elimu na mafunzo ya matawi ya kawaida ya elimu yalikuwa yakimilikiwa na watoto wa watu wa koo bora na viongozi wa dini, na karibuni watoto wote wengine wa Iran waliinyimwa." [11]

Kwa hakika mila hii ya kuuweka umma katika hali ya ujinga ilikuwa muhimu mno kwamba hawakupenda kuiacha kwa gharama yoyote ile. Hivyo basi, wengi wa Wairani walinyimwa haki ya elimu pamoja na haki nyingine, ili kwamba tamaa za kiusumbufu na zisizofaa za hawa watu wachache walioongozwa vibaya ziweze kutimizwa.

## Ushuhuda Wa Historia Juu Ya Wafalme Wa Kisasania

Wengi wa wafalme wa Kisasania walijitwalia sera ya ukali ya serikali na walitaka kuwatiisha watu kwa nguvu. Waliwatoza watu kodi kubwa mno na zenye kutaabisha.

Hivyo basi, watu wa Iran kwa kawaida hawakuridhika, lakini kwa kuchelea uhai wao hawakuthubutu kulitamka neno lolote lile la malalamiko. Halikuwezekana hilo, kiasi kwamba hata wasomi na watu wenye uzoefu hawakupewa utambuzi wo wote ule na baraza la Kisasania.

Watawala wa Kisasania walikuwa madikteta na waliozingatia mno matakwa yao kiasi kwamba hakuna mtu yeyote aliyeweza kutoa maoni yake juu ya jambo lo lote lile.

Ingawa mara nyingi historia hugeuzwa kupitia kwa watu washikao madaraka, hadithi zimesimuliwa kuhusu dhuluma na ukatili wa wadhalimu.

Khusro Pervez alikuwa yu mwenye moyo mgumu mno kiasi kwamba Tha'labi anaandika hivi kuhusiana naye: "Khusro aliarifiwa ya kwamba gavana fulani, aliamrishwa kuja kwenye baraza la mfalme lakini alikuwa ametoa udhuru. Mara moja mfalme huyo alitoa amri kwamba: "Kama ni vigumu kwake kuja mbele yetu kwa mwili wake wote, sisi tutatosheka na sehemu tu ya mwili huo, ili kwamba mambo yamuwie mepesi. Mwambie, mtu huyo ahusikaye akilete kichwa chake tu barazani kwangu."[12]

## Ghasia Katika Zama Za Wasasani

Tunapojifunza sehemu ya mwisho ya zama za Wasasani, jambo lisiloweza kupotea machoni petu ni utawala mbaya wa serikari, na kuwapo kwa utovu wa kanuni na fitina na ghasia kwenye utawala wa Wasasani.

Wana wa wafalme, watu wakuu na machifu wa jeshi walikuwa wakigombana. Kundi moja likimtawaza mwana mfalme mmoja na jingine likimwuzulu na kumchagua mwingine.

Waislamu wa Uarabuni walipoamua kuitwaa Iran, familia ya kifalme ya Wasasani ilikuwa nyonge mno na iliyojitumbukiza mno kwenye ugomvi. Katika kipindi cha miaka minne kilichoanzia kwenye mauaji ya

Khusro Pervez na kwenye kupanda kwenye kiti cha enzi kwa Sheroya hadi kwenye kutawazwa kwa mfalme wa Kisasania wa mwisho Yazd Gard, wafalme wengi waliitawala Iran.

Idadi yao imetajwa kuwa ni kuanzia sita hadi kumi na wanne. Hivyo basi, Serikali ya Iran ilipita kutoka mkono huu kwenda mwingine kwa kiasi cha mara kumi na nne katika kipindi cha miaka minne. Inaweza kufikiriwa vizuri, kuwa ni hali gani ya nchi hii iliyokuwa nayo wakati mapinduzi yaliyotokea humo mara kumi na nne katika kipindi cha miaka minne na kila mara mtu mmoja anauawa na mwingine anatawazwa badala yake.

Kila mwenye kuzishika hatamu za Serikali, huwaulia mbali wale wengine waliokitaka kiti cha enzi na alizifanya aina zote za ukatili ili kukipata cheo chake hicho. Baba aliimwua mwanawe, mwana alimwua babie na ndugu aliwamalizilia mbali nduguze.

Sheroya alimua baba yake, Khusro Pervez ili kukitwaa kiti cha enzi [13] na vile vile aliwaua wana arobaini wa Khusro Pervez (yaani nduguze). [14]

Shehr Baraz alimua kila mmoja ambaye hakuwa na uhakika naye kwamba labda angalikuwa hatari kwa kiti chake cha enzi au la. Hatimaye, wale wote waliopata kukikalia kiti cha enzi, wakiwa ni wanaume na wanawake, na wakiwa ni wazee au vijana, waliwaua akraba zao (yaani wale wana mfalme wa Kisasania) ili kwamba asiwepo abakiaye hai miongoni mwa wale watakaokitwaa kiti cha enzi.

Kwa kifupi ni kuwa, ghasia na utovu wa serikali vimeitwaa mielekeo hiyo katika zama za Wasasari kiasi kwamba watoto na wanawake walitawazwa kwenye kiti cha enzi, kisha wakauawa baada ya majuma machache, na wengine wakatawazwa badala yao.

Katika hali hii, ufalme wa Kisasania, ingawa ulikuwa na fahari na utukufu wake, ulikuwa ukielekea haraka haraka kwenye uchakavu wake, mgawanyiko na maangamizi.

## Hali Ya Mchafuko Ya Iran Ya Wasasani Katika Mtazamo Wa Kidini

Sababu kuu zaidi ya hali ya ghasia nchini Iran katika zama za Wasasani ilikuwa ni tofauti na hitilafu za maoni katika mambo ya dini.

Ardshir Baabkaan, akiwa yu mwasisi wa ukoo wa Kisasania, yeye mwenyewe alikuwa mwana wa Mubid (kasisi wa dini ya Majusi) na alikifikia kiti cha enzi kwa msaada wa watu wa kiroho wa dini ya Majusi, alizitumia njia zote katika kuibalighisha dini ya jadi zake nchini Iran.

Katika siku za Wasasani dini rasmi na maarufu ya Taifa la Wairani ilikuwa ni Umajusi na kwa kuwa Serikali ya Wasasani ilidumishwa kwa msaada wa makasisi, wakuu wa dini ya Kimajusi walipata kila msaada kutoka kwenye baraza la kifalme. Matokeo yake ni kwamba, wakuu wa dini ya Kimajusi walipata nguvu zaidi nchini Iran katika zama za Wasasani, kiasi kwamba waliifaidi nafasi ya tabaka lenye nguvu

zaidi nchini humo.

Daima watawala wa Kisasania walikuwa vibaraka tu wa makasisi na, kama ye yote miongoni mwa watawala hawa, hakuwatii watu wa kiroho, alipatwa na upinzani wao mkali na fedheha itokanayo na upinzani huo.

Hivyo basi, wafalme wa Kisasania, waliwazingatia mno wakuu wa dini kuliko watu wengine wote na kutokana na msaada walioupata makasisi hao kutoka kwa Wasasani, idadi yao iliongezeka siku baada ya siku. Wasasani, waliwatumia watu wa kiroho sana katika kuiimarisha dola yao. Walijenga mahekalu mengi ya ibada ya moto kwenye kila pembe na upenyo wa ile dola kuu ya Iran, na kila kwenye hekalu waliiweka humo idadi kubwa ya makasisi.

Inasemekana kwamba Khusro Pervez alijenga hekalu la moto na akawateua makasisi elfu kumi na mbili hekaluni humo kuimba tenzi na kusali. 15

Hivyo, dini ya Kimajusi ilikuwa ndio dini ya baraza la mfalme. Makasisi walijaribu kwa juhudi zao zote kuunyamazisha umma ulionyimwa na ulioteswa na kuijenga hali ya hewa ambayo watu wasiweze kuzihisi taabu zao.

Mwandishi wa kitabu kiitwacho "*Tarikh–i– Ijtima'i–i–Iran*" anaandika hivi: "....Wakishinikizwa na nguvu iliyotoka kwao (yaani hao makasisi), Wairani, walifanya juhudi za kujikomboa kutokana na taabu hizi. Kwa sababu hii, ikiwa ni kinyume na itikadi rasmi ya 'Mazdesti Zartushti' iliyokuwa dini ya serikali na baraza, na iliyoitwa '**Behdin**', dini mbili nyinginezo zilitokea miongoni mwa Wamajusi..."16

Hakika hili lilitokana na ukali na matendo makali ya watu wakuu na maka– sisi kwamba katika Iran ya Wasasani dini mbalimbali zilikuwa zikitokea, moja baada ya nyingine. Mazdak na kabla lake Mani, 17 walijaribu kuleta mabadiliko kwenye hali za kiroho na kidini za nchi ile, lakini juhudi zao hazikufaulu.

Ilikuwa katika mwaka wa 497 Masihiya hivi kwamba Mazdak alikuja kwenye umaarufu. Alitangaza kubatilishwa kwa umilikaji wenye mashar– ti, ubatilishaji wa ndoa ya wake wengi na udumishaji wa nyumba za wake na masuria wa mtu kuwa ndio msingi wa mpango huo wa mabadiliko. Mara tu, baada ya matabaka ya walionyimwa kuujua mpango wa Mazdak, walimzunguka na wakayaendesha mapinduzi makuu chini ya uongozi wake.

Shabaha pekee ya maasi na vyama hivi ilikuwa kwamba watu waweze kuzipata haki zilizo halali walizozipewa na Allah, Mwenye nguvu zote. Hatimaye ilimbidi Mazdak kupambana na uadui wa watu wa kiroho na upinzani wa jeshi, na matokeo ya jambo hili yalikuwa matatizo na maangamio kwa Iran.

Vile vile dini ya Kimajusi ilikuwa ishaupoteza ukweli wake katika siku za mwishoni za Wasasani. Moto ulikuwa umepewa utakatifu mwingi mno kiasi kwamba ilifikiriwa kuwa haramu kukifua chuma kilichochukua hali ya moto kwa sababu ya kubakia kwenye ujirani wake, na mingi ya msingi na itikadi za Kimajusi zilipewa sura ya ushirikina na visasili.

Katika kipindi hiki, ukweli wa dini hii ulikuwa umetoweka na nafasi yake kuchukuliwa na ibada fulani fulani zilizo duni, zisizo na maana na za kipuuzi. Kawaida zao zilikuwa daima zikikuzwa na makasisi ili kuikuza nguvu yao. Visasili na ushirikina wa kipuuzi vimepenyeza mno kwenye dini hii kiasi kwamba vimewafanya hata wale watu wa kiroho kuwa wagumu. Na hata miongoni mwa makasisi walikuwamo watu walioutambua udanganyifu wa ibada na itikadi za Kimajusi na walikuwa wakijitua mizigo ya ibada na itikadi hizi.

Kuanzia kwenye wakati wa Anushirwan kwenda mbele, njia ya mwangaza ilifunguka nchini Iran, na matokeo ya kupenyeza kwa elimu ya Kigiriki na Kihindi pamoja na kukutana kwa itikadi za Kimajusi na zile za Kikristo na za dini nyinginezo, mwanga ule kila mara ulikuwa ukizaa uangalifu wa watu wa Iran. Hivyo, zaidi ya vile ilivyopata kuwa kwenye wakati wowote ule mwingine, walijihisi kuhuzunishwa na ushirikina na dhana tupu zisizo na msingi za dini ya Kimajusi.

Mwishowe, kuoza kulikotokea kwenye jamii ya kiroho ya Kimajusi na ushirikina na ngano za kipuuzi zilizoivunja dini ya Kimajusi zikawa chanzo cha mwelekeo mwingine na mtawanyiko kwenye dini na maoni ya taifa la Wairani.

Kutokea kwa tofauti hizi, na kuwako kwa dini mbalimbali kulizaa moyo wa mashaka na kutoweza kuamua, kutembea akilini mwa watu wenye busara na kutokana na watu hao, pole pole moyo huo ulipenyeza akilini mwa watu kwamba umma wote uliipoteza kabisa dini na itikadi sahihi waliyokuwanayo hapo mwanzoni.

Hivyo basi, hali ya kutoishika dini na uzembe iliizunguka Iran. Barzuyah, mganga maarufu wa zama za Wasasani ameisawiri picha kamili ya mgeuko wa kiitikadi na hali iliyochafuka ya Iran ya Wasasani kwenye utangulizi wa kitabu chake kiitawacho ‘*Kalilah wa Damnah*’

## Vita Baina Ya Iran Na Urumi

Buzurq Mehr, aliyekuwa mtu hodari na aliyekuwa na cheo kikuu zaidi kwenye utawala wa Anushirwan, kwa mara nyingi sana aliiokoa Iran kutokana na hatari kubwa mno kutokana na nguvu ya sera yake ya kibusara na uzoefu. Hata hivyo, kwenye nyakati fulani fulani, watu wenye hila na wachongezi waliutia giza uhusiano wake na Anushirwan na baada ya watu hao kumchochea Mfalme kuchukua hatua dhidi yake, ikatolewa amri ya kufungwa kwake.

Wafitini hao hao waliitia sumu akili ya Anushirwan kuhusu Dola ya Kirumi na ikamchochea kuyakataa mapatano ya amani ya kudumu na kuwahujumu Warumi ili kuipanua mipaka ya nchi na kuyadhoofisha mashindano ya hatari yawezayo kutokea. Hatimaye ilianza vita na katika muda mfupi tu jeshi la Iran liliiteka Sham, likaichoma Antakia na kuiharibu Asia Ndogo.

Baada ya vita na umwagaji damu wa miaka ishirini, majeshi yote mawili yalizipoteza nguvu na nafasi zao za ushindi; na, baada ya kupata hasara kubwa sana, yalifanya mikataba ya amani mara mbili na

wakakubaliana kuidumisha mipaka yao ya awali, chini ya masharti ya kwamba serikali ya Kirumi itaitaka Serikali ya Iran kulipa dinari elfu ishirini kila mwaka.

Kadiri ya vita vya muda mrefu, na pia wale waliopigana kwenye maeneo ya mbali kutoka katikati ya nchi, yawezavyo kuleta madhara kwa uchumi na viwanda vya taifa, kunaweza kukisiwa vizuri sana. Tukifikiria uchumi wa zama zile, haikuwazekana kurekebisha upesiupesi athari za vita ndefu kiasi hicho. Vita hivi pamoja na shambulio ilitoa utangulizi wa kuanguka kabisa kwa serikali ya Iran. Madonda ya vita hivi yalikuwa bado hayjapona wakati ilipoanza vita vingine vya miaka saba. Baada ya Mfalme wa Kirumi aliyeitwa Tibrius, kukikalia kiti cha enzi, akiwa na nia ya kulipiza kisasi alifanya mashambulizi makali nchini Iran na akautishia uhuru wa nchi hiyo. Hali ya yale majeshi mawili ilikuwa bado haijaamulika, Anushirwan aliiaga dunia na mwanawe Khusro Pervez akakitwaa kiti cha enzi.

Katika mwaka 614 Masihiya, yeye naye, akizitegemea nyudhuru fulani fulani alianza upya kuwashambulia Warumi na matokeo ya shambulio la awali kabisa yaliiteka Sham, Palestina, na Afrika; wakaiteka nyara Yerusalemu, yakazichoma sehemu zao takatifu na kuiharibu kabisa miji mbali mbali. Baada ya kuimwaga damu ya Wakristo wapatao elfu tisini, vita hivyo vilikoma kwa faida kuuendea upande wa Iran. Wakati huo ulimwengu uliostaarabika wa siku zile ulipokuwa ukiungua kwenye moto wa vita na ukandamizaji, Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w) alipewa dhamana ya ujumbe wa Utume.

Huo ulikuwa ni mwaka 610 Masihiya. Aliwabalighishia watu ujumbe wenye kuhuisha wa Upweke wa Mungu na kuwaitia kwenye amani, ukweli, nidhamu na mibaraka.

Kushindwa kwa Warumi waliokuwa wakimwabudu Mungu mikononi mwa Wairani wenye kuabudu moto kulichukuliwa na watu wa Makkahh wenye kuabudu masanamu kuwa ni ndege njema na walifikiria kwamba, katika wakati wa karibu, wao nao wangaliweza kuwashinda wenye kumwabudu Mungu (yaani Waislamu). Hata hivyo, Waislamu walisikitishwa na taarifa hizi. Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w) aliusubiri ufunuo wa Allah na kisha ikafunuliwa aya ifuatayo: “Warumi wameshindwa na Wairani, kwenye nchi iliyo karibu (ya Sham na Palestina), nao baada ya kushindwa kwao, watashinda...”(*Al-Ruum*, 30:2-3). Utabiri huu uliofanywa na Qurani Tukufu ulitimia katika mwaka wa 627 Masihiya. Hercules alipoishambulia na kuichukua Naynava.

Washindani hawa wawili walikuwa wakipumua pumzi za mwisho maishani mwao na walikuwa wakipanga kupata askari wa kuzidishia nguvu majeshi yao. Hata hivyo, kutokana na mapenzi ya Allah iwe kwamba hizi nchi mbili ziangazwe na ibada ya Allah Aliye pekee, na roho zilizodhoofishwa za Wairani na Warumi ziweze kurudishiwa nguvu na upepo mwanana wenye kuhuisha wa Uislamu, haikuchukua muda mrefu kabla ya kuuawa Khusro Pervez na mwanawe Sheroyah, na huyo mwanawe naye alifariki dunia baada ya miezi nane tangu kufa kwa baba yake.

Katika kipindi hiki Iran ilipitia kwenye ghasia nyingi mno kiasi kwamba, baada ya Sheroyah walikuwapo watawala tisa waliotawala kwenye kipindi cha miaka minne (ambao miongoni mwao wanne walikuwa ni wanawake), hadi mwishowe, jeshi la kiis- lamu likaikomeshezea mbali hali hii ya mambo. Ugomvi huu,

ulioenea kwa zaidi ya miaka hamsini, kwa hakika ulikuwa wenye msaada mkubwa wa kutia moyo utekaji wa Waislamu.

1. Tarikh 'Ulumwa Adabiyat dar Iran Dr. Safa, uk. 3 – 4; Iran dar Zaman-i- Sasaniyan, Christensen, uk. 267.
2. Rejea: Payambar-i- Rehnuma, Juzuu I, uk. 42 – 43.
3. Payambar-i-Rehnuma, Juzuu 1, uk. 42 – 43.
4. Payambar-I-Rehnuma, Juzuu I, uk. 43; Kwenye kitabu kiitwacho 'Ganj-i- Daanish' Muhammad Taqi Khan Hakim, Mu 'tamadus Sultan', amelielezea zulia hilo 'Nigaristan' kwa kirefu zaidi alipokuwa akitafiti kuhusu baraza la Makhosro.
5. Sanii Mulukul Ardh wal Ambiya, uk. 4260.
6. Tarikh-i-Tabari, kama kilivyonukuliwa na Christonson, uk. 327.
7. Tarikh-i-Ijtima'i-i-Iran, Juzuu 2, uk. 24 – 26.
8. Limadha Khasir al-Aalam bi inhi-taatil Muslim, uk. 70-71.
9. Iran fi ahdith Sasani'in, uk. 424.
10. Firdausi ameisimulia hadithi hii mwenye kitabu chake Shahnamah kama tukio la utawala wa Anushirwan kuhusiana na vita baina ya Iran na Urumi (Shahnamah, Juzuu 6, uk. 257-260). Dr Sahib-al-Zamani ameichanganua hadithi hii mwenye kitabu chake kiitwacho 'Dibacha-i-bar Rehbari' (uk. 258-262) kwa jinsi ivutiayo mno. Vile vile tazama kitabu kiitwacho 'Guzarish Nama-i-Iran', cha bwana Mahali Quli Khan Hidayat. (uk. 232)
11. Tarikh-i- Ijtima'i – i- Iran, Juzuu 2, uk. 26.
12. Al-Uyun, uk. 136, Amali Saduq uk. 274 na Biharul Anwar, uk. 35.
13. Murujuz Zahab, Juzuu 1, uk. 281,
14. Tarikh-i- Ijtima'i-i-Iran, cha Sa'id Nafisi. Juzuu 2, uk. 15 – 19.
15. Tarikh-i-Tamaddun-i-Sasani, Juzuu 1, uk. 1.
16. Tarikh-i-Ijtima'i-i-Iran, Juzuu 2, uk. 20.
17. Dini ya Mani ilikuwa ni muungano wa Uzoroasta na Ukristo. Hivyo, Mani aliasisi dini mpya kwa kuichanganya dini ya kienyeji na ya kigeni.

# Sura Ya Nne: Jadi Wa Mtukufu Mtume (S.A.W.W)

## Nabii Ibrahm (A.S.), Bingwa Wa Imani Ya Mungu Mmoja.

Lengo la kutoa taarifa za maisha ya Nabii Ibrahim (a.s.) ni kuwajulisha wasomaji jadi zake Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w) kwa kuwa yeye Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alikuwa ni kizazi cha Nabii Isma'il (a.s.) aliyekuwa mwana wa Nabii Ibrahim (a.s.). Na kwa vile watu hawa waw- ili watukufu pamoja na halikadhalika na jadi wengine wengi watukufu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) wengi wana fungu kubwa katika hisoria ya Bara Arabu na Uislamu, ni bora kwamba taarifa fupi ya maisha yao itolewe hapa, kwa sababu matokeo ya historia ya Uislamu, kama zilivyo pete za mnyororo, yana uhusiano kamili na yale matukio yaliyotukia kwenye wakati ule ule wa kuanza kwa Uislamu pamoja na yale ambayo kwa kadiri fulani yalikuwa yakitokea kwenye sehemu za mbali kutoka yalipo.

Kwa mfano, ulinzi na msaada alioupata Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kutoka kwa Abdul-Muttalib, upendeleo alioupata na taabu alizozipata Abu Twalib (as) kwa ajili yake, ukuu wa familia ya Hashim na chanzo cha

uhasama wa Bani Umayyah (dhidi ya familia ya Hashim) vinafikiriwa kwamba ni matukio muhimu yanayounda msingi wa historia ya Uislamu. Ni kwa sababu hii kwamba sura moja ya historia ya Uislamu iwekwe kwa kuyajadili matukio haya.

Tunayakuta matukio yaliyo mashuhuri na yenye kuonekana dhahiri, ya maisha ya Nabii Ibrahim (a.s.). Ni vigumu kuzisahau juhudi zake katika kuiinua bendera ya Upweke wa Mungu na kuing'oa ibada ya masanamu na watu. Halikadhalika midahalo yake mikuu na ya adabu njema aliyoifanya baina yake na wenye kuziabudu nyota, iliyonukuliwa na Qur'ani Tukufu kwa lengo la kuwaelimisha na kuwaongoza watu, ni mafundisho matukufu zaidi juu ya itikadi ya upweke wa Mungu kwa ajili ya wenye kuutafuta ukweli.

## Kwa Nini Kuabudu Viumbe Kulitokea

Sababu iliyomfanya mwanadamu kuviabudu viumbe si yoyote nyingine ila ni ujinga ulioandamana na maamrisho ya maumbile (ambayo, ikiwa ni kanuni ya ujumla, hukiamini kisababisho cha kila tukio).

Kwa upande mmoja, mwanadamu anapokuwa yu mwenye kutawaliwa na maumbile alilazimika kukimbilia kwenye sehemu fulani fulani, kuifikiria mamlaka yenye kushinda na yenye nguvu itoshelezayo katika kuumba utaratibu huu usio kifani na kuzifikiri nakshi zenye kupendeza kwenye maumbo mbalimbali kuwa ni kazi ya kistadi ya mchoraji. Hata hivyo, kwa upande mwingine, kwa kuwa mwanaadamu anataka kuipita njia hii bila ya mwongozo wa Manabii, ambao ndio viongozi wa Mwenyezi Mungu, nao wame– teuliwa ili kuusalimisha ukamilifu wa hii safari ya kiroho ya mwanaadamu, alikimbilia kwenye viumbe visivyo na uhai pamoja na wanyama na wanadamu kabla ya kulifikia lengo lake sahihi (yaani Allah, Mungu wa Pekee) na kuipata njia yake kwa kuzichunguza dalili za maumbile na kukimbilia Kwake.
Hivyo basi, alivifikiria viumbe hivyo kuwa ndivyo yale malengo anayoyatafuta. Kwa sababu hiyo, wanachuoni, baada ya kuvisoma vitabu vya Mwenyezi Mungu na jinsi Mitume walivyowaita watu kwa Mungu na midahalo yao na watu hao, walikiri kwamba lengo la Mitume halikuwa kuwafanya watu waamini kuwako kwa Mwumba wa Ulimwengu. Kwa kweli, kazi yao halisi katika jamii ilikuwa kuwafanya watu kuwa huru kutokana na makucha ya ushirikina na ibada ya masanamu. Kwa usemi mwingine ni kuwa, wamekuja kuwaambia watu, "Enyi watu! Allah, Ambaye kuwako Kwake twakuamini sisi sote Yuko hivi na wala Hayuko vile; Yeye Yu Mmoja tu, wala si wawili. Msiwape viumbe nafasi ya Allah. Mkubalini Allah kuwa Yu Mmoja tu. Msimkubali mshirika yeyote au mwenzi wake."

Sentensi isemayo: "Hakuna Mungu ila Allah", hutoa ushuhuda uangazao juu ya yale tuliyoyasema hapo juu. Huo ndio mwanzo wa mahubiri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w). Maana ya sentensi hii ni kwamba, hakuna apasikaye kuabudiwa ila Allah, na kusema hivyo kwalazimu kwamba kuwako kwa huyo Mwumba ni ukweli ukubalikao, ili kwamba watu waweze kuitwa kwenye kuukubali "Upweke" na "Umoja" wake. Sentensi hii yaonyesha kwamba, machoni mwa mwanadamu wa zama zile, sehemu ya kwanza (yaani kwamba Ulimwengu unaye Allah) si jambo la kupingana. Tukiliachilia mbali jambo hili, kujifunza

hadithi za Qur'ani Tukufu na mazungumzo ya Mitume na watu, hulifafanua zaidi jambo hili. [1]

## Mahali Alipozaliwa Nabii Ibrahim (A.S.)

Mtetezi wa imani ya Mungu Mmoja alizaliwa katika mazingira yaliyozagaa giza la ibada ya masamu na ya wanadamu. Mwanadamu alionyesha unyenyekevu mbele ya masanamu aliyoyatengeneza kwa mikono yake mwenyewe na vilevile mbele ya nyota. Katika hali hizi, jambo lililoliinua daraja la Nabii Ibrahim (a.s.) na kuzivika taji juhudi zake kwa ushindi lilikuwa ni uvumilivu na ustahimilivu wake.

Mahali alipozaliwa yule mshika bendera wa imani ya Mungu Mmoja palikuwa ni Babeli (Babylon). Wanahistoria wamekuwa wakiifikiria sehemu hii kuwa ni moja ya maajabu saba ya ulimwengu na wameyarekodi masimulizi mengi kuhusu utukufu na ukuu wa ustaarabu wa nchi hii.

Mwanahistoria maarufu wa Kigiriki Herodote (aliyeishi kati ya mwake 484 – 425 kabla ya Masihi) aliandika hivi: "Babeli ilijengwa kwa umbo la pembemraba. Kila upande wake ulikuwa na urefu wa '*league*' 120 ('league' moja ni kiasi cha kilometa tano hivi) na kizingo chake kilikuwa '*league*' 480".[2] Vyovyote vile iwavyo maelezo haya yawezavyo kutiwa chumvi zaidi, yanaudihirisha ukweli usiokatalika (yanaposomwa pamoja na maandishi mengine).

Hata hivyo, siku hizi, miongoni mwa hayo mandhari na majengo marefu yenye kuvutia hakuna chochote kiwezacho kuonekana ila kichunguu cha udongo baina ya Mito Tigrisi na Furati, kilichofunikwa na kimya cha kifo. Wakati mwingine kimya hiki huvunjwa na wataalamu wa elimu ya nchi za mashariki (mustashirik) kupitia uchimbaji wanaoufanya ili kupata taarifa za ustaarabu wa Wababeli.
Nabii Ibrahim (a.s.) msanifu wa itikadi ya upweke wa Mungu, alizaliwa katika zama za utawala wa Namrud mwana wa Kan'an. Ingawa Namrud alikuwa mwenye kuabudu masanamu, vile vile alidai kuwa yu Mungu na akijinufaisha kutokana na ujinga wa umma wenye wepesi wa kuamini bila ya kuhitaji ushuhuda, alizitia itikadi zake akilini mwao. Yaweza kuonekana kwamba ni jambo lenye kushangaza kuwa mtu anaweza akawa mwenye kuabudu masanamu na pia adai kuwa yu mungu. Hata hivyo, Qur'ani Tukufu inatupa mfano wa itikadi hii. Nabii Musa (a.s.), mwana wa Imran alipoyatingisha madaraka ya Firauni kwa mantiki yake yenye nguvu na akaukanusha uongo wake kwenye mkutano wa hadhara, wale waliomwunga mkono Firauni walimwambia Firauni:

{وَقَالَ الْمَلَأُ مِنْ قَوْمِ فِرْعَوْنَ أَتَذَرُ مُوسَىٰ وَقَوْمَهُ لِيُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَيَذَرَكَ وَآلِهَتَكَ ۚ} 127

***"Kundi toka kaumu ya Firaun likasema: Je, utamwacha Musa na kaumu yake walete uharibifu katika nchi na kukuacha wewe na miungu yako..."* (*Al-Araaf, 7:127*).**

Inafahamika wazi kwamba Firauni alikuwa akidai kuwa yu mungu na alikuwa na kawaida ya kutangaza akisema: "Mimi ndimi mola wenu mkuu." Hata hivyo, aya hii yaonyesha kwamba, ijapokuwa Namrud alikuwa na itikadi na dai hilo, vile vile alikuwa akiyaabudu masanamu.

Ulinzi mkubwa zaidi aliojipatia Namrud ulikuwa ni kujipatia msaada wa wanajimu na wapiga ramli, watu waliokuwa wakifikiriwa kuwa ndio wenye hekima wa zama zile. Haitakuwa kosa kusema kwamba, unyenyekevu wao mbele ya Namrud uliimarisha njia ya Namrud kuyanyonya matabaka ya watu wenye kukandamizwa na wajinga. Zaidi ya hapo, baadhi ya jamaa zake Nabii Ibrahim (a.s). – kwa mfano Azar aliyeyatengeneza masanamu na ambaye pia alikuwa mjuzi wa unajimu) walikuwa miongoni mwa wafuasi wa Namrud. Jambo hili lenyewe lilikuwa kizuizi kwa Nabii Ibrahim (a.s.) kwa kuwa, zaidi ya kupambana na itikadi za ujumla, vile vile aliwajibika kuukabili upinzani wa ndugu zake mwenyewe.

Namrud alikuwa kazama kwenye bahari ya itikadi za kishirikina. Alikuwa amelitandaza zulia la kufanyia tafrija na kunywa pale wanajimu walipoipiga kengele ya kwanza ya hali ya hatari na kusema: "Serikali yako itaan– guka kupitia kwa mtu ambaye yu mwana wa ardhi hii." Hofu ya ndani ya Namrud iliamshwa na akasema: "Je, mtu huyo tayari kaishazaliwa au bado?" Wanajimu walimjibu ya kwamba alikuwa bado Hajazaliwa. Hapo Namrud akaamrisha wanawake watengwe na wanaume (kwenye usiku ambao, kutegemeana na matabiri na maamuzi ya wanajimu mimba ya mtu huyu aliye adui itabebwa). Hata hivyo ingawa lilitendeka hilo, wauaji wake waliwaua watoto wa kiume. Wakunga waliamrishwa kupeleka taarifa juu ya watoto waliozaliwa kwenye ofisi maalum.

Katika usiku huo huo mimba ya Nabii Ibrahim (a.s.) ilitunga. Mama yake akawa mjamzito na kama vile alivyokuwa mama wa Nabii Musa (a.s.), mwana wa Imran, aliificha habari ya ujauzito wake hadi mwishoni. Baada ya kujifungua alilikimbilia pango lililokuwa karibu na mji wake, ili kuyahami maisha ya mwanawe mpenzi. Alimwacha mwanawe yule pembeni mwa pango lile na kulitembelea katika nyakati za mchana au usiku, kwa kadiri hali ilivyomruhusu. Matokeo ya udhalimu huu ni kwamba, kwa kadiri muda ulivyopita, Namrud alijipatia amani ya kifikra, na akaamini ya kwamba amemchinja adui wa kiti chake cha enzi na utawala wake.

Nabii Ibrahim (a.s.) aliitumia miaka kumi na mitatu ya uhai wake kwenye pango lile lililokuwa na njia nyembamba ya kupitia na kisha mama yake akamtoa. Alipotokea mbele ya watu, wale waliomuunga mkono Namrud walidhania kwamba alikuwa mgeni nchini mle.

Hivyo mama yake akasema: "Huyu ni mwanangu. Alizaliwa kabla ya utabiri waliotabiri wanajimu."[3]

Nabii Ibrahim (a.s.) alipotoka mle pangoni aliimarisha itikadi yake asilia katika upweke wa Mungu kwa kuichunguza dunia na mbingu, kumetameta kwa nyota na ubichi wa miti. Aliishuhudia jamii ngeni ya ajabu na kushangaza.

Aliliona kundi la watu waliokuwa na tabia ya kipuuzi ya kuzielekeza nyuso zao kwenye nyota zimetametazo. Vile vile aliwaona baadhi ya watu ambao kiwango chao cha akili kilikuwa chini kuliko kile cha wengine. Walitengeneza masanamu kwa mikono yao na kisha wakayaabudu.

Kitu kilichokuwa kibaya zaidi miongoni mwa vitu hivi ni kwamba, mwanadamu, akijichukulia faida isiyo ya haki kutokana na ujinga na upuuzi wa watu, alidai kuwa yu mungu wao na akajitangaza kuwa yeye ndiye yule aliyevihuisha viumbe vyote na kuyaamuru matukio yote. Nabii Ibrahim (a.s.) alilazimika

kujitayarisha kupambana katika mistari ya mbele wa mapambano hayo matatu. Qur'ani Tukufu imeisimulia hadithi ya kampeni zake kwenye hii mistari ya mbele mitatu.

## Kampeni Ya Nabii Ibrahim Dhidi Ya Ibada Ya Masanamu

Giza la ibada ya masanamu limeenea katika nchi nzima ya Babel, na mahali alipozaliwa Nabii Ibrahim (a.s.): Miungu mingi ya kidunia na ya kimbinguni imeyanyima matabaka mbali mbali ya jamii uwezo wao wa kufikiri na ujuzi. Baadhi ya watu hawa waliifikiria miungu hiyo kuwa yenyewe inayo nguvu, ambapo wengine waliwafikiria kuwa ni wasila (njia) wa kuipatia radhi ya Mwenyezi Mungu.

## Siri Ya Ushirikina

Waarabu wa kabla ya Uislamu waliamini kwamba kila kiumbe na kila tukio halina budi kuwa na kisababisho maalum na kwamba Allah Aliye Mmoja tu hana nguvu za kuviumba vyote hivyo.

Hii ilitokana na ukweli wa kwamba kwenye zama zile, sayansi ilikuwa bado kugundua uhusiano uliopo baina ya viumbe na matukio mbali mbali. Matokeo yake ni kwamba watu wale walidhania kwamba viumbe vyote na matukio ya kimaumbile ni vitu tofauti na visivyohusiana. Kwa sababu hii walilazimika kumfikiria Mungu mwenye kujitegemea kwa kila tukio kama vile mvua na theluji, tetemeko la ardhi na kifo, njaa na upungufu, amani na utulivu, ukatili na umwagaji wa damu n.k. Hawakuuwazia ukweli uliopo kwamba ulimwengu mzima ni mmoja na sehemu zake zote zinafungama, na kila moja miongoni mwazo inayo athari kwa zile nyingine.

Akili isiyoelimika ya mwanadamu wa siku zile ilikuwa bado haijaitambua siri ya kumwabudu Allah Aliye Mmoja tu na haikutambua kwamba Allah, Anayeutawala ulimwengu wote Yu Mola mwenye nguvu zote na Mjuzi wa yote. Yeye Yu Muumba Aliye huru kutokana na kila aina ya unyonge na upungufu, Uwezo Wake, ukamilifu Wake, elimu Yake na hekima Yake havina kikomo.
Yu juu ya kila kitu kiwezacho kufikiriwa kuwa ndio Yeye. Hakuna ukamilifu Asiokuwa nao. Hakuna kitu kiwezekanacho Asichoweza kukiumba. Yeye ndiye Allah Aliye Mmoja tu, Mwenye uwezo wa kuviumba viumbe na matukio yote bila ya msaada na kuungwa mkono na mtu yeyote. Anaweza kuviumba viumbe na matukio mengine kwa jinsi ile ile Aliyoviumba hivi vilivyoko hivi sasa. Hivyo basi, kutegemeana na akili, kuwako kwa *wasila* wa mamlaka yawezayo kuwa kando na uhuru wa mapenzi ya Allah Asiye kifani ni jambo lisilokubalika.

Itikadi ya kwamba ulimwengu una waumba wawili, mmoja wao akiwa yu asili ya mema na nuru, na mwingine yu asili ya uovu na giza vile vile haikubaliki. Na itikadi kwamba kuna wasila wa watu fulani kama vile Mariamu na Isa kuhusiana na mambo ya uumbaji wa Ulimwengu, au kwamba utawala wa ulimwengu wa kimaada (huu uonekanao) umewekwa mwenye mamlaka ya mwanaadamu, ni udhihiriaho wa ushirikina na kuongezea chumvi. Mwenye kuuamini Upweke wa Allah ni yule ambaye, ukiwaachilia mbali Mitume na Mawalii, hukihifadhi cheo cha Mwumba wa huu ulimwengu na haihusishi kazi ya mmoja wao na mwingine.

Njia waliyoitumia Mitume katika kuwafunza na kuwaongoza watu ni ile ya mantiki, (kutumia hoja) na akili, kwa kuwa walihusika na akili za wanaadamu. Walitamani kuijenga serikali ipasikayo kujengwa chini ya msingi wa imani, elimu na uadilifu, na serikali ya namna hiyo haiwezi kujengwa kwa kutumia ugomvi, vita, na umwagaji wa damu. Hivyo basi, hatuna budi kutofautisha baina ya serikali ya Mitume na serikali ya Firaun na Namrud. Lengo la kundi la pili ni usalama wa utawala na serikali zao kwa kuzitumia njia zote ziwezekanazo, japo nchi zao zianguke baada ya kufariki kwao dunia.

Kwa upande mwingine, watu wa kimungu hupenda kuunda serikali itakayokuwa na njia katika maisha ya mtu sirini na katika hadhara, awe mtawala huyo yu mwenye nguvu au dhaifu katika wakati wowote ule maalum, au awe yu hai, au kaisha kufa. Hakika lengo hili haliwezi kufikiwa kwa kutumia nguvu au shinikizo.

Mwanzoni kabisa Nabii Ibrahim (a.s.) alifanya kampeni dhidi ya itikadi ya nduguze (yaani wenye kuabudu masanamu), ambao miongoni mwao ni Azar aliyekuwa na cheo kikuu zaidi. Alikuwa bado Hajapata ushindi kamili kwenye jambo hili alipolazimika tena kupigana kwenye nyanja nyingine ya mapambano. Kiwango cha fikara za hili kundi la pili kilikuwa juu kidogo na kilichoeleweka kuliko kile cha kundi la kwanza, kwa kuwa, kinyume na dini ya jamaa zake Nabii Ibrahim (a.s.), watu hawa wamevitupilia mbali viumbe duni na visivyo na faida vya kidunia na wakawa wanaziabudu nyota za mbinguni.

Nabii Ibrahm (a.s.) alipokuwa akifanya kampeni dhidi ya ibada ya nyota, alianza kwa maneno mepesi, ukweli mchache wa kifalsafia na kisayansi uliokuwa bado haujazingatiwa akilini mwa watu wa zama zile na hata siku hizi, hoja zake hizi zinawabumbuaza wanachuoni wenye utaalamu wa mantiki na midahalo. Zaidi ya hayo yote, vile vile Qur'ani Tukufu imezinukuu hoja za Nabii Ibrahim (a.s.) na mwandishi wa kitabu hiki anayo heshima kuziingiza tena hoja hizo kwenye kurasa hizi pamoja na maelezo mafupi.

Baada ya kutoka mle pangoni, Nabii Ibrahim (a.s.), ili aweze kuwaongoza watu aliukodolea macho usiku na kutazama mbinguni wakati wa kuchwa kwa jua na akabakia kuwa macho hadi lilipokuchwa jua tena katika siku ya pili. Katika kipindi hiki cha masaa ishirini na manne alihojiana na kuzungumza na makundi matatu na kuzikanusha itikadi zao kwa hoja zenye nguvu.

Giza la usiku liliingia na kuzificha dalili zote za uhai. Nyota angavu, 'Zuhura (Venus)' ilitokea kwenye pembe ya upeo wa macho.
Ili kuwaridhisha wenye kuabudu nyota ya Zuhura, Nabii Ibrahim (a.s.) alikubaliana nao na akajisingizia kuufuata msitari wao na akasema: "Huyu ndiye Mola wangu." Hata hivyo, ile nyota ilipozama na kutoweka kwenye pembe ya anga, akasema: "Siwezi kumkubali Mungu mwenye kuzama." Kwa hoja hii yenye nguvu, aliikana itikadi ya wanaoabudu Zuhura na kuuthibitisha uongo wa ibada yao hiyo.

Katika hatua nyingine macho yake yaliuangukia ungo angavu wa mwezi na kwa uangavu wake wenye kuvutia na uzuri. Ili kuwapendeza wenye kuuabudu mwezi, alikubali wazi wazi kuwa ni Mungu, lakini baadae aliipasua vipande vipande itikadi hii nayo kwa hoja zake zenye nguvu. Ilitokea kwamba, mkono

wenye nguvu wa Mungu uliufanya ule mwezi nao uzame kutoka kwenye upeo wa macho na mng'ao wake kutoweka nchini. Nabii Ibrahim (a.s.), pasi ya kuzidhuru hisia za wenye kuabudu mwezi, alisema huku akiwa na maono yenye ukweli: "Kama Mola wangu wa kweli hataniongoza, hakika nitapotea, kwa sababu Mungu huyu anazama kama vile zizamavyo nyota, nao wenyewe umo kwenye utaratibu maalum na mpangilio uliotengenezwa na mtu fulani, mwingine."

Giza la usiku lilikoma na jua likachomoza, na kukipasua kifua cha upeo wa macho na likaanza kuitawanya miali yake ya rangi ya dhahabu kwenye uso wa nchi. Wenye kuliabudu jua walizigeuzia nyuso zao kwa Mungu wao. Ili kuzitimiza kanuni za mdahalo, Nabii Ibrahim (a.s.) nae aliukubali Uungu wake. Hata hivyo, kuzama kwa jua lile kulithibitika utii kwenye utaratibu maalum wa ulimwengu na Nabii Ibrahim (a.s.) alikana waziwazi kupasika kwake kuabudiwa. (Taz. **Surah al-An'am**, 6:75 –79).

Hakuna shaka kuhusu ukweli uliopo kwamba pale alipokuwa akiishi mle pangoni, Nabii Ibrahim (a.s.), kupitia kwenye upendeleo usio kifani wa Mwenyezi Mungu alijipatia elimu juu ya Upweke wa Allah kutoka chemchemi ya Yule Asiyeonekana (Allah), elimu ambayo ni maalum kwa Mitume. Hata hivyo, baada ya kuzichunguza na kujifunza hizi sayari za angani aliipa elimu ile umbo la hoja. Hivyo basi ukiachilia mbali kule kuwaonyesha njia iliyonyooka wale watu waliopotea na kuwapatia mwongozo, ameacha hazina ya elimu yenye thamani isiyo kifani iwezayo kutumiwa na wale wautafutao ukweli.

## Ufafanuzi Wa Mantiki Ya Nabii Ibrahim (A.S.)

Nabii Ibrahim (a.s.) alitambua ya kwamba Allah Anautawala ulimwengu, lakini swali lilikuwa kwamba ni iwapo chanzo kile cha nguvu ni hizi sayari za mbinguni, au ni Yule Mwenye nguvu zote na aliye bora kuliko sayari hizi.

Baada ya kujifunza hali ya sayari hizi zizungukazo huko na huko aligundua ya kwamba sayari hizi zing'aazo na kutoa nuru zinawajibika kuchomoza, kuzama, kupunguka na kutoweka kwa mujibu wa utaratibu maalum na zinazunguka kwenye mihimili yao katika njia isiyo badilika, na jambo hili, lenyewe lathibitisha ya kwamba zinayatii utashi wa mtu fulani mwingine, na nguvu iliyo kuu na yenye uwezo zaidi inazidhibiti na kuzifanya zipite kwenye mzunguko maalum.

Hebu natulielezee jambo hili zaidi: Ulimwengu una "Uwezekano" na "Mahitaji." Viumbe mbali mbali na matukio ya kimaumbile katu hayako huru kutokana na kumhitaji (Muumba) Mwenye nguvu zote. Yanamhitaji Allah Mjuzi wa yote katika kila sekunde ya mchana na usiku – Allah Ambaye wakati wowote ule, hatakuwa msahaulifu wa mahitaji yao. Sasa, kuzihusu hizo sayari za mbinguni, zinakuwako na ni zenye faida katika wakati fulani na hutoweka na kutokuwa na faida kwenye wakati mwingine. Viumbe vya aina hiyo havina sifa za lazima katika kuwa miungu ya viumbe vingine na kuyatimiza mahitaji yao.

Nadharia hii inaweza kupendekezwa katika namna ya maelezo mbalimbali ya kinadharia na kifalsafia. Kwa mfano tunaweza kusema: Sayari hizi za angani ziko katika mwendo na zinasogea kwenye mihimili yao. Iwapo kama mwendo wao hauna hiari na uko kwenye shurutisho, basi ni lazima uwepo mkono

wenye nguvu wenye kuzitawala.

Na kama mwendo wao unategemeana na hiari yao, ni haki ionekane ni nini shabaha ya mwendo huu. Kama zinasogea ili zipate ukamilifu nazo ni kama vile ilivyo mbegu inayoinukia kutoka ardhini na kukua hadi ikawa mti na ukazaa matunda, jambo hili litalazimika kuwa na maana ya kwamba zinahitaji aina ya nguvu yenye huruma, yenye uwezo, yenye akili na iliyo huru itakayoutoa upungufu wao na kuzipa sifa ya ukamilifu.

Lakini, kama mwendo na mizunguko yao yaelekea kwenye unyonge, na kasoro, nazo ni kama mtu aliyeupita ujana wake na kaingia upande wa uzeeni wa umri wake, basi mwendo wao utakuwa ni mwelekeo wa kwenye upungufu na maangamio, na katu hautaafikiana na daraja ya Mungu Apasikaye kuutawala ulimwengu na vile vyote vilivyomo ndani yake.

## Mbinu Za Majadiliano Na Midahalo Waliyoitumia Mitume

Historia ya Mitume yaonyesha kwamba waliianza kazi ya kuitengeneza jamii kwanza kwa kuwaita jamaa zao kwenye njia ya kweli na kisha wakauendeleza ‘mwito’ huo hadi kwa watu wengine. Hivi ndivyo hasa alivyofanya Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w) mara tu baada ya kuteuliwa kwake kuifanya kazi ya Utume. Kwanza kabisa aliwaita watu wake mwenyewe kwenye Uislamu na akaujenga msingi wa ‘Ujumbe’ wake kwenye mabadiliko yao, kufuatana na amri ya Allah:

{وَأَنْذِرْ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ {214

***“Na uwaonye jamaa zako wa karibu zaidi.”*(*Surah al-Shu’araa, 26:214*).**

Nabii Ibrahim (a.s.) naye aliitumia njia hii na kwanza akayafanya mabadiliko ya watu wake. Azar alikuwa na cheo kikuu sana miongoni mwa ndugu zake, kwa sababu, ukiachilia mbali kwamba alikuwa msomi na msanii, vile vile alikuwa mnajimu mahiri. Katika baraza la mfalme Namrud, neno lake lilichukuliwa kuwa ni lenye nguvu na maamuzi yake ya kinajimu yalikubaliwa na wazee wote wa baraza kuwa ni sahihi.

Nabii Ibrahim (a.s.) alitambua ya kwamba kama angeliweza kumvutia Azar kwenye upande wake, angalikuwa ameikamata ngome yenye nguvu ya wenye kuyaabdudu masanamu. Hivyo basi, alimshauri kwa njia iliyo nzuri mno kwa kadiri alivyoweza, kutoviabudu viumbe visivyo na uhai. Hata hivyo, kutokana na sababu fulani fulani Azar hakuupokea ujumbe na ushauri wa mpwawe, Nabii Ibrahim (a.s.).

Hata hivyo, kwa kadiri tuhusikavyo hapa, jambo lililo muhimu zaidi katika hadithi hii ni ile njia ya kuitia (kwenye ujumbe wa Allah) na jinsi ya kuzungumza alikozungumza Nabii Ibrahim (a.s.) na Azar.

Ukizichunguza kwa undani na kwa uangalifu aya za Qur’ani Tukufu zilizoyanukuu mazungumzo haya huidhihirisha zaidi ile njia ya majadiliano na uitaji (wa kwenye njia ya Allah). Sasa hebu natuone ni njia gani aliyoitumia Nabii Ibrahim (a.s.) kumwitia Azar kwenye njia sahihi:

Alimwambia ami yake:

{إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ يَا أَبَتِ لِمَ تَعْبُدُ مَا لَا يَسْمَعُ وَلَا يُبْصِرُ وَلَا يُغْنِي عَنْكَ شَيْئًا {42

{يَا أَبَتِ إِنِّي قَدْ جَاءَنِي مِنَ الْعِلْمِ مَا لَمْ يَأْتِكَ فَاتَّبِعْنِي أَهْدِكَ صِرَاطًا سَوِيًّا {43

{يَا أَبَتِ لَا تَعْبُدِ الشَّيْطَانَ ۖ إِنَّ الشَّيْطَانَ كَانَ لِلرَّحْمَٰنِ عَصِيًّا {44

{يَا أَبَتِ إِنِّي أَخَافُ أَنْ يَمَسَّكَ عَذَابٌ مِنَ الرَّحْمَٰنِ فَتَكُونَ لِلشَّيْطَانِ وَلِيًّا {45

{قَالَ أَرَاغِبٌ أَنْتَ عَنْ آلِهَتِي يَا إِبْرَاهِيمُ ۖ لَئِنْ لَمْ تَنْتَهِ لَأَرْجُمَنَّكَ ۖ وَاهْجُرْنِي مَلِيًّا {46

{قَالَ سَلَامٌ عَلَيْكَ ۖ سَأَسْتَغْفِرُ لَكَ رَبِّي ۖ إِنَّهُ كَانَ بِي حَفِيًّا {47

***“Alipo mwambia baba yake: Ewe baba yangu! Kwa nini unamwabudu asiyesikia na asiyekufaa chochote? Ewe baba yangu! Bila shaka nimefunuliwa ukweli juu ya siri nyingi; hivyo basi, nifuate, ili nikuongozee kwenye njia iliyo sawa. Ewe baba yangu! Usimwabudu shetani, kwa kuwa yu mwasi kwa*** **(*****Allah*****)** ***Mola wa Rehema. Baba yangu! Hakika mimi ninahofia ya kwamba itakugusa adhabu kutoka kwa*** **(*****Allah*****)** ***Mwingi wa rehema na kwamba uwe rafiki wa shetani.” Akasema: Je, unaichukia miungu yangu, ewe Ibrahim? kama huachi lazima nitakupiga mawe na uniondokelee mbali kwa muda?*****(*****Ibrahim*****)** ***akasema; Amani iwe juu yako, nitakuombea msamaha kwa Mola wangu, kwani yeye ananihurumia sana.*** **(*****Surat Maryam; 19:42-47*****)**

Azar akiujibu mwito wa Nabii Ibrahim (a.s.) alisema: “Ewe Ibrahim! Unathubutu kuikanusha miungu yangu? Acha upuuzi (wako) huu, au sivyo utarujumiwa hadi ufe. Toka nyumbani mwangu upesi sana.”

Mnyoofu Ibrahim (a.s.) aliivumilia kauli hii mbaya ya Azar na kwa utulivu kamili, na akajibu: “Amani na iwe juu yako. Nitamwomba Mola wangu Akughufirie.”

Je, yawezekana kuwako jibu lifaalo zaidi na mazungumzo ya upole na yakubalikayo kuliko haya maneno ya Nabii Ibrahim (a.s.)?

# Je, Azar Alikuwa Ndiye Baba Yake Nabii Ibrahim (A.S.)?

Aya tulizozinukuu hapo juu pamoja na aya ya kumi na tano ya *Surah Tawbah* na aya ya kumi na nne ya *Surah al-Mumtahinah* zinaweza kutoa dhana ya kwamba Azar alihusiana na Nabii Ibrahim (a.s.) katika kiwango cha baba na Ibrahim (a.s.) naye amemwita, 'baba.' Hata hivyo wazo la kuwa Azar mwenye kuyaabudu masanamu yu baba yake Nabii Ibrahim (a.s.) haliafikiani na maoni yakubaliwayo na wanachuoni wote wa Kishi'ah, waitakidio kwamba jadi zake Mtukufu Mtume (s.a.w.w) pamoja na wale wa Mitume wengine walikuwa wachamungu walio uitakidi Upweke wa Allah. Mwanachuoni maarufu wa Kishi'ah, Sheikh Mufid katika kitabu chake kizuri sana,[4]ameichukulia dhana hii kuwa ni yenye kukubaliwa na wanachuoni wote wa Kishi'ah na idadi kubwa ya wanachuoni wa Kisunni pia wameafikiana nao katika kuitakidi hivyo. Hivyo basi, swali huibuka, nini maana halisi ya aya tulizozitaja na suala hili lawezaje kutatuliwa?

Wengi wa wafasiri wa Qur'ani Tukufu wanadai kwamba ingawa kwa kawaida neno "**Ab**" hutumia mwenye lugha ya kiarabu kwa maana ya 'baba', hii si maana pekee ya neno hilo, na katika kamusi ya kiarabu na katika istilahi za Qur'ani mara kwa mara neno hili limetumika kwa maana ya ami vile vile. Kwa mfano, kwenye aya ifuatayo neno '**Ab**' husimama kwa maana ya 'ami.'

أَمْ كُنْتُمْ شُهَدَاءَ إِذْ حَضَرَ يَعْقُوبَ الْمَوْتُ إِذْ قَالَ لِبَنِيهِ مَا تَعْبُدُونَ مِنْ بَعْدِي قَالُوا نَعْبُدُ إِلَٰهَكَ وَإِلَٰهَ آبَائِكَ إِبْرَاهِيمَ

وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ إِلَٰهًا وَاحِدًا وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ {133}

***"Je, mlikuwapo pale mauti yalipomfikia Ya'qub? Aliwaambia wanawe: "Je, mtamwabudu nani baada yangu?" Wakajibu wakasema: "Tutamwambudu Mola Wako na Mola wa baba*** (***Aba***) ***zako, Ibrahimu, Isma'il na Is'haka; Yeye ni Mola Mmoja tu. Nasi kwake tumenyenyekea."*** (***Surah al-Baqarah, 2:133***)

Hakuna shaka yoyote ile kuhusiana na ukweli uliopo kwamba Nabii Isma'il (a.s.) alikuwa ami yake Nabii Ya'qub (a.s.) na wala hakuwa baba yake, kwa sababu Nabii Ya'qub (a.s.) alikuwa mwana wa Nabii Isihaka (a.s.) aliyekuwa nduguye Nabii Isma'il (a.s.). Hata hivyo, ingawa ilikuwa hivi, wana wa Nabii Ya'qub (a.s.) wamemtaja kuwa yu baba wa Nabii Ya'qub (a.s.) yaani wamemwita '**Ab**' kama alivyo Nabii Ya'qub (a.s.). Kwa kuwa neno hili lina maana mbili upo uwezekano kwamba kwenye aya zizungumziazo juu ya Azar kuitwa kwenye njia iliyonyoka na Nabii Ibrahim (a.s.), zinaweza zikawa na maana ya 'ami', na ni hivyo hasa, kutegemeana na maoni ya pamoja yaliyotajwa na Sheikh Mufid. Na inawezekana kwamba Nabii Ibrahim (a.s.) alimwita mlezi wake kwa muda mrefu sana naye (Nabii Ibrahim a.s.) alimwangalia kana kwamba alikuwa baba yake hasa.

## Azar Katika Qur’ani Tukufu

Kwa lengo la kutaka kuona ushahidi wa Qur’ani Tukufu juu ya uhusiano baina ya Nabii Ibrahim (a.s.) na Azar tungalipenda kuukaribisha usikivu wa msomaji kwenye maelezo ya aya mbili:

Yakiwa ni matokeo ya juhudi za nguvu alizozifanya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Bara Arabu iliangazwa na nuru ya Uislamu. Wengi wa watu wake waliipokea dini hii kwa moyo mmoja na wakatambua ya kwamba ushirikina na uabudu masanamu vitaishilizia Motoni na mateso. Ingawa walifurahia kuwa katika dini ya kweli, walijihisi kuwa ni wenye huzuni kukumbuka kuwa baba zao na mama zao walikuwa wenye kuyaabudu masanamu.

Usikiaji wa aya zenye kuielezea hali mbaya watakayokuwa nayo wenye kuyaabudu masanamu katika Siku ya Kiyama, uliwawia mzito. Ili kuyaondoa mateso haya ya kifikara walimwomba Mtukufu Mtume (s.a.w.w) amwombe Allah maghufira juu ya jadi zao waliofia katika hali ya ukafiri, kama vile Nabii Ibrahim (a.s.) alivyomwombea Azar.

Hata hivyo, aya zifuatazo zilifunuliwa kulijibu ombi lao hilo:

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَنْ يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ وَلَوْ كَانُوا أُولِي قُرْبَىٰ مِنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُمْ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ
113}}

وَمَا كَانَ اسْتِغْفَارُ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ إِلَّا عَنْ مَوْعِدَةٍ وَعَدَهَا إِيَّاهُ فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ أَنَّهُ عَدُوٌّ لِلَّهِ تَبَرَّأَ مِنْهُ ۚ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَأَوَّاهٌ حَلِيمٌ
114}}

***“Haimpasi Nabii (Wetu Muhammad) na wale walioamini ya kwamba wawaombee maghfira washirikina, japo wawe ni karaba (zao) baada ya kuwabainikia ya kwamba wao wameichuma adhabu ya Moto (wa Jahanamu) uwakao. Wala haikuwa Ibrahim kumuombea msamaha baba yake kwa ajili tu ya kuitimiza miadi aliyomwahidi; Lakini ilipombainikia ya kwamba yeye alikuwa adui wa Allah alijiepusha naye; Hakika Ibrahim alikuwa mwenye huruma, mvumilivu.” (Surah Tawbah, 9:113-114)***

Ingeweza kuonekana kuwa na mwelekeo zaidi kwamba mazungumzo ya Nabii Ibrahim (as) na Azar, na yeye Nabii Ibrahim (a.s.) kumwahidi Azar kumwombea maghfira, jambo lililoishilizia kwenye mkatiko wa uhusiano na kukataana, yalitokea wakati Nabii Ibrahim (a.s.) alipokuwa mtoto – yaani wakati alipokuwa bado anaishi nchini Babeli na alikuwa bado Hajadhamiria kwenda Palestina, Misri na Hijaz.

Baada ya kuichunguza aya hii tunaweza kuamua ya kwamba, Azar alipong’ang’ania kwenye ukafiri na ibada yake ya masanamu, Nabii Ibrahim (a.s.), akiwa bado yu mtoto, alikata uhusiano wake naye na katu hakupata kumfikiria tena baada ya hapo.

Katika kipindi cha baadae cha uhai wake yaani pale alipokuwa mzee, Nabii Ibrahim (a.s.) baada ya kulitimiza jukumu lake kubwa (yaani ujenzi wa Al- Ka'ba) na kumleta mkewe na mwanawe kwenye jangwa kavu la Makkahh, aliwaombea watu kadhaa kutoka ndani ya moyo wake, wakiwemo wazazi wake, na akaomba dua yake itakabaliwe na Allah. Katika wakati ule aliomba hivi:

{رَبَّنَا اغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِلْمُؤْمِنِينَ يَوْمَ يَقُومُ الْحِسَابُ {41

***"Mola wangu! Unisamehe mimi na wazazi wangu na waumini katika Siku ya Kusimamishwa hesabu."*** (***Surat Ibrahim, 14:41***)

Aya hizi zadhihirisha ya kwamba sherehe ya dua hii ilifanyika baada ya kwisha ujenzi wa Al-Ka'ba wakati Nabii Ibrahim (a.s.) alipokuwa kwenye kipindi cha uzee wake. Kama baba yake aliyeionyesha huba na utii kwake kwenye aya hii na akamwombea ni yule yule Azar, ingalikuwa na maana ya kwamba Nabii Ibrahim (a.s.) hakujitenga naye kwenye kipindi chote cha uhai wake na kwenye nyakati fulani alimwombea, pia ambapo aya iliyofunuliwa kulijibu ombi la kizazi cha washirikina inaonyesha dhahiri kwamba baada ya kipindi fulani, alipokuwa bado yu mtoto, Nabii Ibrahim (a.s.) aliuvunja uhusiano wote na Azar na akajitenga naye, na kujitenga na kukana vina maana ya kukoma kuzungumza, kutokujaliana na kuacha kuombeana dua kwa ajili ya wokovu wa kila mmoja wao.

Aya hizi mbili zinaposomwa kwa pamoja, inadhihirika ya kwamba yule mtu ambaye Nabii Ibrahim (a.s.) alimchukia katika ujana wake na ambaye alikata mafungamano yote ya usikivu na kupendana alikuwa ni mtu mwingine kuliko yule aliyemkumbuka hadi kwenye kipindi cha uzee wake na akamwombea maghfira na wokovu.5

## Nabii Ibrahim (A.S.) Mvunja Masanamu

Muda wa sikukuu ulikaribia na watu wa Babeli walio wazembe wakautoka mji kwenda porini ili kuondoa na uchomvu wao na kuitia nguvu milango yao ya fahamu na kuzifanya kawaida za sikukuu hiyo. Hivyo mji ukawa hauna watu. Matendo yaliyotangulia ya Nabii Ibrahim (a.s.) na makemeo yake na lawama zake vimewafanya watu wa Babeli kuwa na hofu. Hivyo basi, walisisitiza kwamba Nabii Ibrahim (a.s.) aende pamoja nao na ashiriki kwenye sherehe za sikukuu hiyo.

Hata hivyo, azimio lao hilo liliangukia kwenye kipindi cha ugonjwa wa Nabii Ibrahim (a.s.). Hivyo basi, katika kulijibu wazo lao, alisema kwamba alikuwa mgonjwa na asingaliweza kushiriki kwenye sherehe za sikukuu hiyo.

Hakika hiyo ilikuwa siku ya furaha kwa mtu aitakidiye upweke wa Allah, pamoja na washirikina pia.

Kwa washirikina ilikuwa na maana ya kuisherehekea sikukuu ya zamani sana na walikwenda chini ya mlima na kwenye nchi yenye majani mabichi kuziendesha sherehe za sikukuu ile na kuzihuisha desturi

za jadi zao. Na kwa upande wa yule mtetezi wa Upweke wa Allah, vile vile ilikuwa ni siku adhimu ya sikukuu isiyo na kifani ambayo kwa muda mrefu alikuwa akitamani kuipata ili kwamba mji ule wautoke wapinzani na auvunjevunje mdhihiriko wa ukafiri na ushirikina.

Kundi la mwisho la watu likatoka mjini mle, na Nabii Ibrahim (a.s.) akau- fikiria wakati huu kuwa ndio ile fursa aliyokuwa akiitafuta, na akiwa moyoni kajawa na matumaini na imani kwa Allah aliliingia hekalu la masanamu.

Kwa mbali hivi aliviona vipande vya magogo vilivyochongwa na masanamu yasiyo na uhai. Akakifikiria kiasi kikubwa cha chakula ambacho wenye kuyaabudu masanamu hayo walikuwa wakikileta kwenye hekalu lao kikiwa ni sadaka ya kuitafutia baraka, na akaingia kukitafuta chakula kile. Alimega tonge la mkate, akalishika mkononi mwake na kuliashiria kwenye yale masanamu na kusema kwa dhihaka: “Kwa nini hamzili aina zote hizi za vyakula?” Ni dhahiri kwamba hawa miungu wa kubuniwa wa washirikina hawakuwa na uwezo wa kusogea japo kidogo tu, ukiachilia mbali kula kitu chochote kile.

Kimya cha mauti kilijaa kwenye ule ukumbi mkubwa wa hekalu la masanamu, kimya ambacho kiliweza kuvunjwa tu na mapigo makubwa ambayo Nabii Ibrahim (a.s.) alikuwa akiipa mikono, miguu na miili ya masanamu. Aliyavunja masanamu yote, hadi kikapatikana kichuguu kikubwa cha vipande vya miti na madini vilivyovunjika-vunjika na kupondwapondwa katikati ya hekalu lile. Hata hivyo alilisaza lile sanamu kubwa zaidi na akaliweka shoka begani mwake.

Nabii Ibrahim (a.s.) aliyatenda hayo kwa lengo maalum. Alijua kwamba wenye kuyaabudu masanamu watakaporudi kutoka kule porini wataielewa hali halisi na wataitumia hali iliyokuwapo kuwa ni ya kubunia tu na isiyo na ukweli kwa kuwa katu wasingesadiki ya kwamba mapigo hayo yaliyopigwa yale masanamu mengine yalifanywa na lile sanamu kubwa, lisilokuwa na uwezo hata kidogo wa kusogea au kukitenda chochote kile, na kwenye tukio lile, yeye (Nabii Ibrahim a.s.) ataitumia hali ile katika ‘mwito’ wake na kusema kwamba kwa mujibu wa imani yao wenyewe, iwapo lile sanamu halina japo uwezo kidogo tu basi yawezekanaje kwam- ba liwe Mola wa ulimwengu?

Jua liliingia kwenye upeo wa macho na likakoma kuangaza ulimwengu. Katika wakati ule, watu walianza kurudi mjini kwa makundi. Sasa ukaingia muda wa kuzitekeleza ibada za kuyaabudu masanamu, na makundi ya wenye kuyaabudu masanamu yakaanza kuingia hekaluni mle. Mandhari isiyotegemewa, iliyoidhihirisha huzuni na fedheha ya miungu yao, ilizivu- tia shauku zao wote. Kikaingia kimya cha kifo kwenye mazingira ya hekalu na kila mmoja wao akapandwa na ghadhabu. Hata hivyo, mmoja wao alikivunja kimya kile na akasema: “Ni nani aliyeutenda uharibifu huu?” Lawama za Nabii Ibrahimu (a.s.) za tangu kale juu ya masanamu yale na lawama zake za wazi wazi juu ya ibada ya masanamu ziliwafanya waamue kuwa ni yeye tu aliyeyafanya hayo. Hivyo basi lilikaa baraza la hukumu chini ya uongozi wa Namrud na kijana Ibrahim (a.s.) na mama yake waliletwa ili kuhukumiwa.

Mamie (Nabii Ibrahim a.s.) alishitakiwa kwa kosa la kuficha kuzaliwa kwa mtoto wake na kutotoa taarifa kwenye ofisi maalum ya serikali, ili mtoto yule aweze kuuawa.

Maama yule alilijibu shitaka hili hivi: “Niliona kwam- ba matokeo ya maamuzi ya serikali ya wakati ule (yaani kule kuwaua watoto wa kiume) jamii ya wanaadamu nchini humu inamalizika. Sikuiarifu ofisi ya serikali juu ya mwanangu, kwa sababu nilitaka kuona jinsi atakavyoendelea hapo baadae.

Kama ingebidi kuthibitisha kwake kuwa yu mtu yule yule ambaye watabiri (makasisi) wamemtabiri, ingelikuwepo sababu ya mimi kuwaarifu polisi ili waache kuimwaga damu ya watoto wengine. Na kama haijitokezi yeye kuwa ndiye mtu yule, basi nimemwokoa kijana wa nchi hii kutokana na kifo.” Hoja za mama yule ziliwatosheleza kabisa mahakimu.

Sasa Nabii Ibrahim (a.s.) akahojiwa. Akasema: “Hali ya mambo inaonye- sha kwamba lile sanamu kubwa ndilo lililoyapiga mapigo yote hayo na kama masanamu haya yana uwezo wa kusema ni bora mngaliliuliza.” Jibu hili lisiloeleweka vizuri, lililotiiwa madoa na dhihaka na dharau lilidhamiriwa kutumikia lengo jingine, na lengo lile lilikuwa kwamba Nabii Ibrahim alikuwa na uhakika kwamba watu wale watamjibu wakisema: “Ewe Ibrahim! Unatambua vema kwamba masanamu haya hayana uwezo wa kusema. Vile vile hayana hiari wala akili.”

Watakaposema hivyo, Nabii Ibrahim (a.s.) angaliweza kulitanabahisha baraza lile juu ya jambo moja la msingi. Kwa bahati ilitokea kama alivyotazamia Nabii Ibrahim (a.s.). Aliyazungumza yafuatayo kwa kurejea kauli ya watu wale iliyoushuhudia unyonge, fedheha na kutokuwa na uwezo kwa masanamu yale: “Kama masanamu haya yako vile muyaelezavyo, basi kwa nini mwayaabudu na kwa nini mwayaomba kukupeni haja zenu?”

Ujinga, ukaidi na kuiga mambo kwa njia ya upofu kulizitawala nyoyo na akili za mahakimu na mbele ya majibu ya Nabii Ibrahim (a.s.) yasiyokanika hawakupata njia nyingine ila kutoa hukumu itakayopatana na haja ya serikali ya zama zile. Hivyo basi, waliamua kwamba Nabii Ibrahim (a.s.) achomwe moto akiwa hai. Lundo kubwa la kuni lilichomwa na huyu mtetezi wa Upweke wa Allah alitupiliwa kwenye miali ya moto uwakao.

Hata hivyo, Allah Mwenye nguvu zote Alimnyooshea Nabii Ibrahim (a.s.) Mkono Wake wa Huruma na akamfanya sugu kutokana na madhara ya moto ule. Yeye (Allah) Aliigeuza ile hali ya jahannam ya bandia, iliyoten- genezwa na wanaadamu kuwa bustani ya kijani yenye kupendeza [6](Tazama *Surah al-Anbiya*; 21:51-70).

## Nukta Za Simulizi Hii Zenye Mafunzo

Ingawa Mayahudi wanadai kuwa ndio watangulizi wa msafara wa wale waaminio Upweke wa Allah, hadithi hii haikuwa maarufu miongoni mwao na haina nafasi kwenye Taurati yao ya siku hizi. Miongoni wa vitabu vya Mbinguni ni Qur’ani Tukufu tu iliyoisimulia hadithi hii. Hivyo basi, hapa chini tunayataja baadhi ya mafunzo ya hadithi hii ambayo kwa kweli hasa ndio mambo yenyewe hasa ambayo Qur’ani Tukufu inataka kuwafa- hamisha watu kwa kuzisimulia hadithi za Manabii mbali mbali.

Hadithi hii ni ushahidi wa dhahiri wa ujasiri na ushujaa usio kifani wa rafi– ki wa Allah (Nabii Ibrahim a.s.).

Nia yake katika kuyavunja masanamu na kuuvunjavunja mdhihiriko na njia ya ushirikina halikuwa jambo la kubakia kufichikana kwa watu wa Namrud kwa sababu kwa karipio na shutuma zake, tayari kaishadhihirisha kutopenda na chuki yake juu ya ibada ya masanamu wazi kabisa na alikuwa kila mara akisema wazi wazi na bila kificho: "Kama hamtayaacha mwenendo wenu uaibishao nitachukua uamuzi juu yao." Na siku ile watu walipokwenda porini, alisema waziwazi*:* "Haki ya Mungu! Bila shaka nitayapindua masanamu yenu mara tu muigeuzapo migongo yenu." (*Surah Anbiya*, 21:57).

Allama Majlisi ananakili hivi kutoka kwa Imam Sadiq (a.s.): "Harakati na kampeni ya mtu mmoja dhidi ya safu za makafiri, ambao idadi yao ilikithiri maelfu machache, ni ushahidi ulio hai wa ujasiri na uthabiti wa Nabii Ibrahim (a.s.), ambaye hakuwa na hofu yoyote akilini mwake katika njia ya kutukuza Jina la Allah na kuuimarisha msingi wa ibada ya Allah Aliye Mmoja tu."[7]

Wakati ambapo, yale mapigo (ya kuvunja masanamu) yaliyofanywa na Nabii Ibrahim (a.s.) yalikuwa dhahiri ni uasi wa silaha na mkali, lakini kama ionekanavyo kwenye mazungumzo yake na wale mahakimu, hakika harakati hii ilikuwa na hali ya kipropaganda, kwa sababu alifikiria kuwa njia ya mwisho katika kuziibua hekima na fikara za watu wale ni ile ya kuyavunja yale masanamu yote ila lile lililokuwa kubwa zaidi na kuliweka lile shoka begani mwake ili kwamba waweze kufanya uchunguzi zaidi juu ya sababu za tukio hili.

Na kwa kuwa mwishowe wangaliweza kuifikiria mandhari hii kuwa ni mzaha mtupu na katu wasingaliamini kwamba mapigo yale yalipigwa na lile sanamu kubwa, angalilitumia jambo hili katika kuyabalighisha maoni yake na kusema: "Kutokana na itikadi yenu wenyewe, hili sanamu kubwa halina uwezo hata kidogo, basi ni kwa nini mwaliabudu?"

Hii yaonyesha kwamba tangu mwanzoni kabisa Mitume wamekuwa wakizitumia hoja tu na midahalo ikiwa ndio silaha zao kali, ambazo daima zimekuwa zikitoa matokeo mema. Laa sivyo, basi ni nini faida ya kuyavunja masanamu machache ukilinganisha na hatari kwa maisha ambayo Nabii Ibrahim (a.s.) iliyomkabili? Ni muhimu kwamba tendo hili liwe na huduma kuu kwa kazi yake katika hoja zake kiasi cha kuweza kuyatoa mhanga maisha yake kwa ajili yake.

Nabii Ibrahim (a.s.) alitambua kwamba matokeo ya tendo hili ni kwisha kwa uhai wake. Hivyo basi, kama desturi angekuwa na wasiwasi au angejificha mahali fulani au kwa uchache kabisa angejilinda na mzaha na ubishi. Lakini hata hivyo, alikuwa na udhibiti kamili ya moyo wake na mishipa ya fahamu zake. Kwa mfano alipoliingia lile hekalu la masanamu aliliendea kila sanamu na kwa mzaha akalitaka lile chakula. Baada ya kukata tamaa alilivunjavunja na kulifanya kuwa kichuguu cha vipande vya mti vilivyovunjwavunjwa na akayachukulia yote hayo kuwa ni jambo la kawaida kabisa, kana kwamba hayatafuatiwa na kifo chake mwenyewe au kuhukumiwa.

Alipofika mbele ya baraza la hukumu alilijibu swali lao hivi: "Hakika (mtendaji) amelitenda hili, mkuu wao

ni huyu, basi waulizeni kama wanaweza kusema.” Ubishi wa aina hii mbele ya baraza lile uliweza kutegemewa tu kutoka kwa mtu aliyejitayarisha kwa hatima zozote zile ziwezazo kutokea na asiyeihisi hofu yoyote ile au kuchelea heshima na cheo cha wakuu wa baraza, moyoni mwake.

Na lenye kustaajabisha zaidi ni kule kuchunguza hali ya fikara za Nabii Ibrahim (a.s.) pale alipowekwa kwenye kombeo na akatambua kwa uhakika ya kwamba karibuni tu atajikuta katikati ya miali ya moto – moto ambao kuni zake zilikusanywa na watu wa Babeli ili kuitenda ibada takatifu ya dini, na ambao miali yake ilikuwa iki– waka kwa kupaa juu kwa nguvu mno kiasi kwamba hata kipanga hakithubutu kuruka kandokando au juu yake. Katika wakati ule ule, Malaika Jibrili a.s. alishuka kutoka mbinguni akidhihirisha kuwako tayari kwake kumpa (yeye Nabii Ibrahim a.s.) kila msaada, na akasema: “Hebu niambie kuhusu matamanio ya moyo wako.” Nabii Ibrahim (a.s.) alimjibu akisema: “Mimi ninayo tamaa. Hata hivyo, wewe hutaweza kuitambua tamaa yangu ila hutambuliwa na Mola wangu tu.[8] Jibu hili lauonyesha waziwazi utukufu na ukuu wa kiroho wa Nabii Ibrahim (a.s.).

Kwenye jumba kuu la kifalme lililokuwako maili chache kutoka ulipokuwapo ule moto, Namrud alingojea kwa shauku kuu na pasi na subira kuona kisasi kikilipizwa juu ya Nabii Ibrahim (a.s.) na alitaka kuiona jinsi miali ya moto ikimla. Ile kombeo ilitupwa kwa mrusho mmoja tu, mwili wa yule mtetezi wa Upweke wa Allah uliangukia kwenye moto. Hata hivyo, mapenzi ya Mola wa Nabii Ibrahim (a.s.) yanayopenya ndani yaliubadili ule moto wa bandia uliotengenezwa na watu na kuwa bustani katika hali iliyowashangaza mno watu kiasi kwamba Nimrud alimgeukia Azar kwa ghafla na pasi ya kujijua, na akasema: “Mola wa Ibrahim Anamchukulia kuwa ni kipenzi chake mno. [9]

Licha ya matukio yote haya, Nabii Ibrahim (a.s.) hakuweza kuihubiri itikadi yake kwa uhuru kamili. Hatimaye serikali ya zama zile, baada ya kushauriana iliamua kumfukuza nchini humo Nabii Ibrahim (a.s.). Kitendo hiki kiliifungua sura mpya maishani mwake na kikawa mwanzo wa safari yake ya kwenda Sham, Palestina, Misri na Hijaz.

## Ukurasa Mpya Katika Maisha Ya Nabii Ibrahim (A.S.)

Mahakama ya mjini Babeli ilimpiga marufuku Nabii Ibrahim (a.s.) kuishi nchini mle na akalazimishwa kuitoka sehemu ile aliyozaliwa na kwenda Misri na Palestina. Mfalme Amaliqa aliyekuwa akizitawala sehemu hizi alimpokea kwa mikono miwili na akampa zawadi nyingi, moja kati ya zawadi hizo ilikuwa ni mjakazi aliyekuwa akiitwa Hajjar.

Hadi wakati ule, mkewe Nabii Ibrahim (a.s.) Bibi ‘Sarah’ alikuwa Hajajaaliwa mwana na maendeleo hayo tuliyotaja hapo juu yaliziamsha hisia zake kwa upande wa mumewe mtukufu. Hivyo akamshauri Nabii Ibrahim (a.s.) amwoe Hajjar kwa kuwa yawezekana kwamba akajaaliwa mwana atakayekuwa chanzo cha faraja na furaha yao. Ndoa ile ilifanyika na baada ya muda, Bibi Hajjar alijifungua mwana aliyeitwa Isma’il. Haikuchukua muda mrefu, Bibi Sarah nae akashika ujauzito na akazaa mwana aliyepewa jina la Isihaka.[10]

Baada ya muda fulani kupita, akifanya kama alivyoamrishwa na Allah, alimchukua (Nabii) Isma'il (a.s.) na mama yake, Bibi Hajjar (a.s.) na akaelekea kusini (Makkah) na akawaweka mwenye bonde lisilofahamika. Bonde hili halikuwa likiishi watu na ni misafara ya watu tu iliyokuwa ikisafiri kutoka Sham kwenda Yemen au ikitoka Yemen kwenda Sham iliweza kukita mahema yao pale. Siku zote za mwaka zilizobakia sehemu hii ilibakia kuwa tupu na ilikuwa jangwa lenye joto kali tu, kama vile zilivyo sehemu nyingine za Uarabuni.

Makazi katika sehemu yenye kuogofya kama hii yalikuwa mtihani mkuu kwa mwanamke ambaye alikuwa amezitumia siku zake katika nchi ya Mfalme Amaliqa.

Joto la jangwa lenye kuunguza na pepo zenye joto lake kali mno viliiwakilisha mandhari ya kifo mbele ya macho yake. Nabii Ibrahim (a.s.) yeye mwenyewe pia alihuzunishwa na matukio haya. Alipokuwa akiishika hatamu ya mnyama wa kupanda kwa nia ya kumwabia kwa heri mkewe na mwanawe, rundo la machozi lilianza kumtiririka machoni mwake na akamwambia Hajjar: "Ewe Hajjar! Yote haya yametendeka kwa mujibu wa amri ya Allah Mwenye nguvu zote na amri Yake haiwezi kukaidiwa. Zitegemee baraka za Allah na uwe na uhakika ya kwamba hatatufedhehesha." Kisha alimwomba Allah kwa maneno yafuatayo na kwa dhamira halisi:

{رَبِّ اجْعَلْ هَٰذَا بَلَدًا آمِنًا وَارْزُقْ أَهْلَهُ مِنَ الثَّمَرَاتِ مَنْ آمَنَ مِنْهُمْ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۖ {126

***"Ewe Mola wangu! Ufanye mji huu (wa Makkahh) uwe na usalama na uwaruzuku watu wake matunda, wale miongoni mwao wanaomwamini Allah na Siku ya Mwisho..."***
***(Al-Baqarah, 2:126).***

Alipokuwa akikishuka kilima (cha Makkahh akienda zake) aligeuka na kutazama nyuma na akamwomba Allah kuwamiminia baraka Yake.

Ingawa, kwa kadiri ionekanavyo, safari hii ilikuwa ngumu mno na yenye usumbufu, lakini baadae ilidhihirika ya kwamba ilibeba matukio ya maana sana katika hatima yake, miongoni mwao ukiwamo ujenzi wa Al-Ka'ba tukufu iliyotoa msingi mkuu kwa ajili ya itikadi ya Upweke wa Allah, ukiipeperusha bendera ya ibada ya Allah Aliye Mmoja tu katika Bara Arabu na kuuweka msingi wa chama kikuu cha kidini ambacho baadae kitachukua sura yake halisi, yaani kile chama kikuu ambacho baadae kilifanya kazi nchini humu kupitia kwa mwishilizio wa Mitume (s.a.w.w.)

## Jinsi Chemchem Ya Zamzam Ilivyopatikana

Nabii Ibrahim (a.s.) aliichukua hatamu ya mnyama wake wa kupanda na akitokwa na machozi machoni mwake, aliiaga nchi ya Makkahh pamoja na Bibi Hajjar na mwanawe. Hata hivyo, baada ya muda mfupi chakula na maji alivyokuwanavyo yule mtoto na mamie vilimwishia na kifua cha Hajjar kilikauka. Hali ya mwanawe nayo ilianza kudhoofika. Mafuriko ya machozi yalitiririka machoni mwa yule mama

aliyehamishiwa mbali na yakayalowesha mapaja yake.

Katika hali hiyo ya kutojua afanye nini, aliamsha miguu, yake na akaenda hadi akakifika kilima cha Safa. Kutoka kilimani pale alikiona kioja cha mazigazi karibu na kilima cha Marwa na akayakimbilia. Hata hivyo, uchungu wa sura ya nchi yenye kuhadaa ulikatisha tamaa mno. Maombolezo na wasiwasi wa mwanawe mpenzi ulimfanya akimbie kwa ushupavu zaidi katika mielekeo yote. Hivyo alikimbia mara saba baina ya vilima vya Safa na Marwa ili kuyatafuta maji, lakini hatimaye aliyapoteza mategemeo yote na akamrudia mwanae.

Bila shaka katika wakati ule, mwanawe atakuwa kaishaifika hatua ya pumzi yake ya mwisho na atakuwa kaishaupoteza uwezo wa machozi au kulia zaidi. Hata hivyo, katika muda ule dua ya Nabii Ibrahim (a.s.) ilitakabaliwa. Mama yule mwenye taabu na aliyechoka aliyaona yale maji yaliyo safi yakiwa yameanza kububujika kutoka chini ya miguu ya Nabii Isma'il (a.s.).
Mama yule aliyekuwa akizitazama pumzi za mwisho za mwanawe na aliamini ya kwamba atafariki dunia baada ya muda mfupi tu, alijihisi kuwa yu mwenye furaha mno alipoyaona maji haya. Wote wawili, mama na mwana walikunywa hadi wakatosheka na mawingu ya kukata tamaa na kutokuwa na matumaini ambayo yaliweka kivuli kwenye maisha yao yaliondolewa na upepo mwanana wa baraka za Allah. [11]

Kupatikana kwa chemchem hii inayoitwa 'Zamzam', tangu siku ile, kuli– wafanya ndege wa angani kurukaruka juu yake na wakazitanda mbawa zao pana kama kifuniko juu ya vichwa vya mama mwenye huzuni na yule mwana. Watu wa kabila la 'Jarhani' waliokuwa wakiishi mbali kidogo kutoka kwenye bonde hili waliwaona wale ndege wakienda huko na huko na wakaamua ya kwamba yamepatikana maji katika eneo hilo. Waliwatuma watu wawili miongoni mwa watu wao kuithibitisha hali hiyo.

Baada ya kutembea huko na huko watu wale walikifikia kitovu kile cha baraka za Allah. Walipokaribia, walimwona mwanamke na mtoto mchanga wakiwa wamekaa kandoni mwa bwawa la maji. Walirudi kwa haraka na kuwataarifu machifu wao juu ya jambo hilo. Upesi sana watu wa kabila hili walikita mahema yao kuizunguka chemchem hii iliyobarikiwa na hivyo, Bibi Hajjar (a.s.) aliondolewa taabu na uchungu wa upweke uliokuwa ukimsumbua. Kukua na uchangamfu kamili wa Nabii Isma'il (a.s.) vilikuwa chanzo cha kufanya kwake maingiliano ya kindoa na kabila ya 'Jarhani' na hivyo akafaidika na msaada na jamii yao. Mara moja Nabii Isma'il (a.s.) alimwoa msichana wa kabila lile. Hivyo basi, kutokana na upande wa mama yao, kizazi chake kilihusiana na kabila lile.

## Wakutana Tena

Baada ya kumwacha mpenzi mwanawe na mkewe nchini Makkahh, chini ya amri ya Allah Mwenye nguvu zote, wakati fulani Nabii Ibrahim (a.s.) alifikiria kwenda kule kumwona mwanawe. Katika moja ya safari zake, ambayo labda ilikuwa ndiyo safari yake ya awali, alifika Makkahh na akaona ya kwamba mwanawe hakuwamo nyumbani mwake. Wakati ule Nabii Isma'il (a.s.) alikuwa kaishakua na kuwa mtu mzima na amemwoa msichana wa kabila la Jarham. Nabii Ibrahim (a.s.) alimwuliza mkewe Nabii Isma'il

(a.s.): "Yu wapi mumeo?" Akamjibu akisema: "Amekwenda kuwinda." Hapo alimuuliza kama anacho kitu chohote cha kula. Alimjibu kwamba hakuna kitu chochote.

Nabii Ibrahim (a.s.) alihuzunika mno kuuona utovu wa adabu na huruma wa mkaza mwanawe na akamwambia: "Isma'il atakaporudi nyumbani mpe salaam zangu na umwambie akibadili kizingiti cha nyumba yake." Baada ya hapo Nabii Ibrahim (a.s.) alirudi maskanini kwake.

Nabii Isma'il (a.s.) aliporudi aliisikia harufu ya baba yake na kutokana na maelezo ya mkewe alitambua ya kwamba yule mtu aliyeitembelea nyumba yake alikuwa ni baba yake, Nabii Ibrahim (a.s.), mwenyewe. Vile vile kutokana na ule ujumbe ulioachwa na baba yake alitambua ya kwamba alimtaka amtaliki mkewe wa wakati ule na amchague mwingine, kwa kuwa hakumfikiria yule mke wa wakati ule kuwa mwenzi afaaye maishani mwake.[12]

Pengine mtu anaweza akauliza ni kwa nini kwamba Nabii Ibrahim (a.s.) baada ya kuifanya safari ndefu kiasi kile asisubiri hadi mwanawe akarudi kutoka kule mawindoni na kwa nini alirudi Palestina bila ya kuonana naye?

Wanahistoria wanaelezea kwamba alirudi haraka kwa sababu alifunga ahadi na Bibi Sarah (Mkewe mkuu) kwamba asikae kule kwa muda mrefu na kurudi kwake upesi kulitokana na kuitunza ahadi ile. Vile vile baada ya safari hii aliamrishwa na Allah, Mwenye nguvu zote kufanya safari nyingine ya kwenda Makkahh, kwenda kuijenga Al-Ka'ba, pale na kuzivu- tia hapo nyoyo za wale wote wauaminio Upweke wa Allah.

Qur'ani Tukufu inathibitisha ya kwamba katika siku za mwishoni za uhai wa Nabii Ibrahim (a.s.) mji wa Makkahh ulikwishakua na kuwa jiji, kwa sababu, baada ya kulitimiza jukumu lake alimwamba Allah kwa maneno yafuatayo:

{وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَٰذَا الْبَلَدَ آمِنًا وَاجْنُبْنِي وَبَنِيَّ أَنْ نَعْبُدَ الْأَصْنَامَ {35

***"…. Mola wangu! Ujaalie mji huu (wa Makkah) uwe wa amani na uniepushe mimi na kizazi changu kutokana na kuyaabudu masanamu…" (Sura Ibrahim 14:35).***

Na wakati wa kuwasili kwake kwenye jangwa la Makkahh, aliomba akisema:

{رَبِّ اجْعَلْ هَٰذَا بَلَدًا آمِنًا وَارْزُقْ أَهْلَهُ مِنَ الثَّمَرَاتِ مَنْ آمَنَ {126

***"Mola wangu! Ufanye mji huu uwe wa usalama …" (Al-Baqarah, 2:126).***

Ili kuyamaliza majadiliano haya, inafaa kuzielezea hali za wakati wa ujenzi wa Al-Ka'ba na pia kuitoa historia yake fupi. Hata hivyo, ili tuweze kulifupisha lengo letu, hatuna budi kutoa hapa chini taarifa za

baadhi ya jadi zake Mtukufu Mtume (s.a.w.w) walio watukufu na walio maarufu katika historia.

## Qusayy Mwana Wa Kilaab

Yafuatayo hapa chini ni majina ya baba na jadi zake Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kwa utaratibu wa mwelekeo wa juu: Abdallah, Abdul-Muttalib, Hashim Abd-i-Manaaf, Qusayy, Kilaab, Marra, Ka'ab, Luayyi, Ghalib, Fahr, Malik, Nizar, Kinanah, Khuzaimah, Mudrikah, Ilyaas, Mudhar, Nazaar, Ma'ad na A'dnaan.[13]

Kizazi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w) hadi kwa Ma'ad mwana wa Adnaan ni kama ilivyoelezwa hapo juu. Hata hivyo kuna kutoafikiana kuhusu idadi na majina ya nasaba zake tangu kwa Adnaan hadi kwa Nabii Isma'il (a.s.) na kwa mujibu wa taarifa zilizonukuliwa na Ibn Abbas, kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) wakati nasaba yake ifikapo kwa Adnaan mtu na asiendeleze, kwa kuwa yeye Mtukufu Mtume (s.a.w.w) mwenyewe, kila alipoyataja majina ya jadi zake hakuendelea baada ya kufika kwa Adnaan, na akaamrisha kwamba watu wengine nao wasiyataje majina ya jadi zake wengine tangu hapo hadi kwa Nabii Isma'il (a.s.). Vile vile alisema kwamba kile kilichokuwa kikifahamika mno miongoni mwa Waarabu kuihusu sehemu ile ya jadi zake haikuwa sahihi.

Hivyo basi sisi nasi tumeitaja ile sehemu ya nasaba yake ambayo usahihi wake unakubalika, na maelezo marefu ya baadhi ya watu wahusikao. Watu tuliowataja hapo juu ni maarufu katika historia ya Uarabuni na historia ya Uhusiano na baadhi yao.

Hivyo basi, tunatoa hapa chini taarifa za maisha yao tangu kwa Qusayy hadi kwa baba mtukufu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w), Bwana Abdallah, na tutajizuia kuyataja matukio ya maishani mwa wale wengine wasio husika na mambo tunayoyazungumzia.[14]

Qusayy alikuwa jadi wa nne wa Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w), mama yake Bibi Fatimah aliolewa na Bwana Kilaab na akazaa wana wawili, Zuhrah na Qusayy. Yule wa pili alikuwa bado yu mtoto mdogo pale mumewe Bibi Fatimah alipofariki dunia. Baada ya hapo aliolewa na mume mwingine aliyeitwa Rabi'a na akafuatana naye kwenda Sham.

Qusayy alipata matunzo ya kiubaba kutoka kwa Bwana Rabi'a hadi kulipoibuka kutoafikiana baina yake na kabila la Bwana Rabia na matokeo yake yakawa kwamba wakamfukuza na kumtoa nje ya mipaka ya nchi yao. Mama yake alichukizwa na matendo aliyotendewa na akaamua kumrudisha Makkahh.

Mkono wa kudra ulimvutia Makkahh. Sifa zake njema zilizojificha zilimwezesha kuudumisha ukuu wake juu ya watu wa Makkah na hasa miongoni mwa watu wa kabila la Quraysh. Katika kitambo kifupi tu alijipatia ofisi kuu za serikali mle mjini Makkahh, na vilevile akawa mdhamini wa funguo za Al-Ka'ba na mtawala wa mji ule aliyekubalika. Matukio mengi makuu yanahusika na jina lake.

Miongoni mwao ilikuwa kwamba aliwahamasisha watu kujenga nyumba iitwayo 'Darun-Nadwah' pembezoni mwa Al-Ka'ba na hivyo akaasisi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya Waarabu ili kwamba

wakuu na machifu wao waweze kukaa pamoja kwenye jumba hili na kutatua matatizo yao. Bwana Qusayy alifariki dunia kwenye karne ya 5 Masihiya, na aliacha wana wawili, Abdur Daar na Abd Manaaf.

## Abd Manaaf

Alikuwa jadi wa tatu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w). Jina lake hasa lilikuwa Muahirah na jina lake la heshima lilikuwa Qamar al-Bat'ha (mwezi wa Bat'ha). Alikuwa mdogo kuliko Abdur Daar, lakini alijipatia heshima kuu miongoni mwa watu. Alikuwa mchamungu mno. Aliwaitia watu kwenye amali njema, akawatendea mema na alidumisha uhusiano mwema zaidi na karaba zake.

Ingawa alikwa na cheo cha juu zaidi kwenye jamii yake, katu hakupata kuwa mpinzani wa kaka yake Abdur Daar kuhusiana na suala la kuzishika ofisi kuu zihusianazo na Al-Ka'ba. Kufuatana na usia wa Qusay, utawala ulibakia mikononi mwa Abdur Daar, lakini ndugu hao walipofariki dunia wana wao walianza kugombea ofisi mbalimbali.

Baada ya ugomvi na kutoafikiana kwingi, hatimaye walipatanishwa na wakavigawa vyeo miongini mwao. Iliamuliwa kwamba udhamini wa Al-Ka'ba tukufu na uwenyekiti wa 'Darun Nadwah' vibakie mikononi mwa wana wa Abdur Daar na kazi ya kuwapatia mahujaji maji na kuwabu- rudisha ifanywe na wana wa Abd Manaaf. Mgawo huu wa ofisi ulikuwa ukitumika mwenye siku za kuanza kwa Uislamu. [15]

## Hashim

Alikuwa baba mkuu (au baba yake babu) wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w). Jina lake hasa ni Amr na jina lake la heshima lilikuwa 'Ala'. Yeye na Abd Shams walikuwa mapacha na ndugu zoa wawili wengine walikuwa ni Muttalib na Nawfal. Wanahistoria wamehadithia ya kwamba wakati wa kuzaliwa kwa Bwana Hashim na Abd Shams, kidole cha Hashim kiliun- gana na paji la uso la Abd Shams. Damu ilitoka mno pale walipotengan- ishwa na watu wakalichukulia jambo hili kuwa ni ndege mbaya.[16]

Mwanahistoria Bwana Halabi mwenye kitabu chake '*Siirah*' ameandika kwamba hii ndege mbaya ilijitokeza baadae, kwa sababu, baada ya kuanza kwa Uislamu, vita kali mno zilipiganwa baina ya Bani Abbas na Bani Umayyah waliodai kuwa kizazi chao kinatokana na Abd Shams.[17] Jambo hili laonyesha kwamba mwandishi wa *Siirah* hii ameyapuuza kabisa matukio ya kimsiba yaliyohusiana na kizazi cha Sayyidna Ali (as.) ingawa mchezo wa umwagaji wa damu walioutengeneza Bani Umayyah kwa kuimwaga damu takatifu ya dhuria wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) ni wenye ushahidi ung'aao wa kuwako kwa uadui baina ya hizi familia mbili. Hata hivyo, haijulikani ni kwanini mwandishi aliyetajwa alishindwa kuyataja matukio haya.

Moja ya mambo makhususi kuhusu dhuria wa Abd Manaaf ambayo yanaakisi kwenye makelele ya vita na kwenye maandishi ya Uarabuni ni kwamba walifia sehemu tofauti, yaani Hashim alifia nchini Ghaza, Abd Shams alifia Makkah, Nawfal alifia nchini Iraq na Muttalib alifia Yemen. Ili kuunakili mfano wa utu wema wa Hashim tunaweza kusema kwamba kila ulipoandama mwezi wa Dhul-Hajj (Mfungo tatu)

alikuwa akija kwenye Ka'aba tukufu akauegemea ukuta wake na kuhutubia kwa maneno yafuatayo:

"Enyi Waquraishi! Ninyi ni watu wenye busara na watukufu zaidi miongoni mwa Waarabu. Taifa lenu ni bora zaidi miongoni mwa mataifa yote, Mwenyezi Mungu amekupeni makazi kandoni mwa Nyumba Yake na amekupeni ubora kwa niaba yake juu ya dhuria wote wa Isma'il. Enyi ndugu zangu! Jihadharini! Mahujaji wa Nyumba ya Allah wanakujieni kwenye mwezi huu pamoja na wema mwingi mno. Wao ni wageni wa Allah na ni juu yenu kuwapokea. Wako watu wengi waliofukara miongoni mwao, watakaokuja kutoka sehemu za mbali. Ninaapa kwa Jina la Mola wa Nyumba hii kwamba kama ningalikuwa tajiri nitoshelezaye katika kuwaburudisha wageni wote wa Allah, nisingalikusisitizeni kutoa chakula.

Hata hivyo, hivi sasa mtatumia kila muwezacho kukitoa, na mlichochuma kwa njia ya halali. Ninakuapieni kwa jina la heshima la Nyumba hii kwamba hamtatumia kitu chochote kwa lengo hili, kile mlichokinyang'anya, au kutoa kwa njia ya kiunafiki au kwa kushurutishwa. Kama mtu yeyote yule havutiki kwenye kusaidia, yuko huru kutokukitu-mia kitu chochote kile." [18]

Kwa ajili ya nia na malengo, uongozi wa Hashim ulikuwa ni kwa ajili ya ustawi wa watu wa Makkahh nao ulikuwa na athari kubwa kwenye mategemeo ya hali za maisha yao. Kila ilipotokea njaa, wema wake haukuruhusu kwamba watu wapate taabu yoyote ile kwa tatizo hili. Moja ya hatua zake zilizojitokeza zaidi, alizozichukua kwa ajili ya maendeleo ya biashara ya watu wa Makkahh, ilikuwa ni kukamilishwa kwa mapatano na mtawala wa Ghassan.
Ni kutokana na mapatano haya kwamba mapatano mengine ya aina hiyo yalifanywa na kaka yake Abd Shams na Mfalme wa Ethiopia, na ndugu zake wengine wawili, Muttalib alifanya mapatano mengine na Mtawala wa Yemen, na Nawfal akafanya mapatano mengine na Mfalme wa Iran. Bidhaa ziliweza kubadilishwa kwa uhuru kabisa na nchi mbalimbali. Mapatano haya yalitatua matatizo mengi na yakaleta kuwako kwa idadi mjini Makkahh ambavyo vile vile vilikuwako kwenye zama za kuanza kwa Uislamu. Zaidi ya hapo, moja ya matendo yenye faida ya Hashim lilikuwa ni kuasisiwa kwa misafara ya Waquraishi kwen- da Sham kwenye nyakati za kiangazi na kwenda Yemen wakati wa kipup- we. Tendo liliendelea kwa muda mrefu hata baada ya kuanza kwa Uislamu.

## Umayyah Mwana Wa Abd Shams Aona Kijicho

Umayyah, mwana wa Abd Shams, aliona kijicho juu ya ukuu na heshima ya ami yake, Hashim, na akajitahidi kuwavutia watu kwake kwa kuwapa zawadi. Hata hivyo, ingawa alijitahidi kwa kadiri alivyoweza na akaweka pingamizi zake zote alizoweza, hakuweza kumvua Hashim cheo chake kile. Kinyume na hivyo, matusi yake na kumsingizia Hashim kulimzidishia Hashim heshima zaidi nyoyoni mwa watu.

Moto wa husuda uliendelea kuwaka moyoni mwa Umayyah. Mwishowe alimshinikiza ami yake kwamba wote wawili wamwendee mmoja wa wataalamu (wapiga bao) wa Uarabuni na yule tu atakayethibitishwa na mganga yule kuwa ndiye afaaye kwa utawala, azishike hatamu za utawala mikononi mwake.

Wema wa Hashim hakumruhusu kuingia mwenye mabishano na mwana wa kaka yake. Hata hivyo kwa kuwa Umayyah alikuwa akishinikiza mno, Hashim aliukubali mpango ule kwa masharti mawili:

Kwanza, kwamba yeyote yule atakayeshindwa kwenye jambo hilo atoe kafara ya ngamia mia moja wenye macho meusi wakati wa Hajj, na pili, kwamba akae nje ya mji wa Makkahh kwa kipindi cha miaka kumi.

Sasa ilitokea kwamba, mara tu baada ya mganga yule wa kiarabu (mpiga bao wa Asfaan) alipomwona Hashim, alianza kumsifu na akahukumu kwa kumpa haki. Hivyo basi Umayyah alilazimika kuutoka mji wa Makkahh na akakitumia kipindi cha miaka kumi nchini Sham[19]

Athari za huu uadui wa kurithi uliendelea kwa kipindi cha miaka 130 baada ya majilio ya Uislamu na ulifuatana na majinai ya mara kwa mara yasiyo na kifani kwenye historia ya mwanadamu. Hadithi tuliyoitaja hapo juu, ukiachilia mbali kule kuudhihirisha ukweli kuhusu jinsi uadui baina ya hizi koo mbili ulivyoanza, vilevile inaielezea sababu ya ushawishi walioufaidi Bani Umayyah mle nchini Sham, na inatambuliwa kwamba uhusiano wao wa tangu kale na watu wa Sham uliujenga msingi wa utawala wao kwenye eneo lile.

## Hashim Aoa

Salmah binti wa ‘Amr Khazraji alikuwa mwanamke mchamungu, aliyekuwa katalikiwa na mumewe na hakuwa tayari kuolewa tena.
Hashim alipokuwa akirudi kutoka Sham kwenye mmoja wa misafara yake alitua Yathirib (Madina) kwa siku chache hivi na akamchumbia Salmah. Salmah alivutiwa na utukufu, utajiri na tabia za Hashim, na kwa ushawishi aliokuwa nao miongoni mwa Waquraishi.

Salmah alikubali kuolewa na Hashim kwa masharti kwamba wakati wa kuzaa mtoto yeye Salmah awe miongoni mwa watu wake (yaani ajifungulie kwao). Kufuatana na sharti hili, Salmah aliutumia muda fulani mjini Makkahh pamoja na Hashim na muda wa kujifungua ulipokaribia alirudi Yathrib. Huko alijifungua mwana aliyeitwa Shibah, na baadae alifahamika kwa jina la Abdul-Muttalib. Wanahistoria wamezitaja sababu kadhaa zifuatazo zilizomfanya Shibah ajitwalie jina hili la heshima la Abdul-Muttalib:

Moja inasema kwamba wakati Hashim alipojihisi kuwa kifo chake kinamkaribia, alimwambia nduguye Muttalib: “Ewe ndugu yangu! Mtafute mtumwa wako Shibah.” Na kwa sababu Hashim (baba yake Shibah) amemwita mwanawe, “Mtumwa wa Muttalib” baadae alifahamika kwa jina hili la “Abdul-Muttalib” (yaani Mtumwa wa Muttalib).

Maelezo mengine ni haya: “Siku moja, mkazi mmoja wa Makkahh alipokuwa akipita kwenye mitaa ya mji wa Yathrib, aliwaona watoto wengi wakifanya mazoezi ya kufuma mishale. Mmoja wa watoto wale aliposhinda kwenye mchezo ule, mara moja alisema: “Mimi ni mwana wa chifu wa Bat’ha (Makkahh).” Yule mkazi wa Makkahh alijitokeza na akamuuliza yule kijana. Wewe ni nani?”

Yule kijana akajibu akasema: “Mimi ni Shibah mwana wa Hashim mwana wa Abd Manaaf.”

Yule mtu aliporejea Makkahh alimweleza Muttalib, nduguye Hashim na chifu wa Makkahh, habari zile. Huyu ami alimkumbuka yule mpwa wake na hivyo basi, alikwenda Yathrib. Sura ya yule mwana nduguye ilimkumbusha Muttalib sura ya nduguye na hapo machozi yakamchuruzika mashavuni mwake.

Wakabusiana kwa huba na hisia. Mama yake Shibah hakuwa tayari kutengana na mwanawe na akakataa asichukuliwe na kupelekwa Makkahh lakini kukataa kupinga kwake kuliimarisha zaidi dhamira ya Muttalib.

Hatimaye Muttalib alifaulu kulifikia lengo lake, na baada ya kuipata idhini ya mama yake mtoto, Shibah pamoja na yeye mwenyewe walimpanda mnyama na wakaenda Makkahh. Katika kipindi cha safari ile, joto kali la jua liliugeuza uso wa rangi ya fedha kuwa mweusi na vazi lake nalo lilichakaa na kupasuka.

Hivyo basi, kutokana na sababu hii, walipofika Makkahh, watu walifikiria kwamba yule kijana alikuwa mtumwa wa Muttalib. Walinong’onezana wakisema: “Kijana huyu (Shibah) ni mtumwa wa Muttalib.”Na ingawa Muttalib alisema mara kwa mara kwamba kijana yule alikuwa mpwa wake, ile fikara mbaya iliyokwisha kujenga mizizi akilini mwa watu iliendelea kuling’ang’ania wazo lile. Matokeo yake ni kuwa, yule mpwa wake Muttalib akafahamika kwa jina la Abdul-Muttalib (Mtumwa wa Muttalib).[20]

Vivyo maelezo mengine ni haya yafuatayo: “Abdul-Muttalib aliitwa hivyo, kwa sababu alilelewa na ami yake na lilikuwa ni jambo la kawaida miongoni mwa Waarabu kwamba kila mtu afugwapo na mtu mwingine aliitwa mtumwa wa mfadhili wake.

## Abdul-Muttalib

Abdul-Muttalib mwana wa Hashim, babu yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w), alikuwachifu wa Waquraish na mtu maarufu. Maisha yake ya kijamii, yote yalijaa sifa nzuri mno. Kwa vile matukio yote ya zama za uchifu wake vilevile yalihusiana na historia ya Uislamu, tunasimulia hapa chini baadhi ya matukio hayo:

Hakuna shaka yoyote kuhusu ukweli kwamba kwa vyovyote vile mtu awezavyo kuwa thabiti na imara, hatimaye huvutika kwa kiasi fulani na mazingira yake, na tabia na desturi za jamii huziathiri fikara zake. Hata hivyo katika nyakati fulani, baadhi ya watu huwa na utashi wa kimaumbile ya kuyakinza mambo yatawalayo mazingira yao kwa ujasiri na ushupavu, na kujiweka wenyewe na mazingira ya kutoathiriwa na maambukizo maovu.

Shujaa huyu wa mazungumzo yetu alikuwa kielelezo kamili cha wale watu ambao, kwenye maisha yao tunayaona mambo mengi yaliyo mema. Kama mtu ambaye, ingawa alitumia zaidi ya miaka themanini ya uhai wake miongoni mwa watu wenye kawaida ya kuyaabudu masanamu, ulevi, riba, uuaji wa watu, kwenye maisha yake yote asiiruhusu pombe kuigusa midomo yake na kuwazuia watu wasiue, wasinywe pombe, na wasifanye matendo maovu, na kuwazuia kuoa maharimu wao na kufanya tawafu wakiwa uchi, na kuwadhibiti kwenye mambo yahusuyo kiapo na ahadi mpaka kwenye pumzi ya mwisho ya uhai

wake, bila shaka mtu huyu atakuwa mmoja wa watu walio vigezo.

Wanaozaliwa mara chache mno kwenye jamii ya wanadamu. Kwa hakika ni muhimu kwamba yule mtu ambaye mwilini mwake imewekwa nuru ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) (aliye kiongozi mkuu zaidi wa wanadamu) awe msafi halisi na aliyeepukana kabisa na kila aina ya uchafu.

Kutokana na hadithi fupifupi na simulizi zenye mafunzo zisemekanazo kwamba zimesemwa na Abdul-Muttalib tunajifunza ya kwamba hata mle mwenye zile siku za mazingira ya ujinga, Abdul-Muttalib alihesabiwa miongoni mwa wale waliouitakidi upweke wa Allah na Siku ya Hukumu, na kila mara alikuwa akisema: "Mtu aliye mdhalimu huadhibiwa hapa ulimwenguni.

Hata hivyo, kama kwa bahati atakufa kabla ya kuadhibiwa vyakutosha, atapata mapatilizo kutokana na amali zake mwenye Siku ya Hukumu.21

Har'b mwana wa Umayyah alikuwa ndugu wa karibu wa Abdul-Muttalib. Vilevile alikuwa akifahamika kwamba yu mmoja wa watu watukufu mion- goni mwa Waquraishi. Myahudi mmoja alikuwa jirani wa Har'b. Siku moja Myahudi yule aliudhihirisha ukali wake dhidi ya Har'b kwenye moja ya bazaar (maduka) ya Tahamah na wakatoleana maneno makali. Tukio hili liliishilizia kwenye mauaji ya Myahudi yule kutokana na ushawishi wa Har'b.

Abdul-Muttalib alipolifahamu jambo hili alikata uhusiano wake na Har'b. Vilevile alijitahidi kupatikana malipo ya damu kutoka kwake na kuwapa wafiwa wa Myahudi yule. Hadithi hii fupi ni mfano wa shauku ya mtu huyu mnyoofu katika kuwasaidia wanyonge na katika kuutekeleza uadilifu.

## Kuchimbwa Upya Kwa Kisima Cha Zamzam

Tangu siku ile kilipopatikana kisima cha Zamzam watu wa kabila la Jarham waliishi kandokando mwake na walinufaika kutokana na maji ya kisima hiki kwenye kipindi kile cha miaka mingi walipokuwa wakiutawala mji wa Makkahh. Hata hivyo, ikiwa ni matokeo ya kuendelea kwa watu wa Makkahh kwenye biashara, utajiri wao, uzembe wao na utovu wa miiko katika matumizi ya maji, polepole kisima kile kilikauka.22

Maelezo mengine (kuhusiana na kisima hiki) yanasema hivi: "Watu wa kabila la Jarham walipotishiwa na kabila la Khaza'ah na wakalazimika kuyaacha makazi yao, chifu wao na mtu aliyekuwa maarufu aliyeitwa Mazaaz mwana wa 'Amr, alitambua kwamba karibuni atakoma kuwa mshika usukani wa mambo na adui wao ataishambulia nchi na serikali yake na kuiharibu kabisa.

Hivyo akaamrisha kwamba masanamu mawili ya paa yaliyofuliwa kwa dhababu na panga kadhaa za thamani, zilizoletwa kama zawadi kwenye Al-Ka'ba vitumbukizwe kisimani humo, na kisha kifukiwe kabisa ili kwamba maadui watakapokuja wasivitwae, na hapo baadae wao (Bani Jarham) watakapoitwaa tena nchi na utawala wao wenyewe waweze kuja kuutumia utajiri huo. Baada ya muda fulani kabila la Khaza'ah lilianza mashambulizi yao na kabila la Jarham pamoja na idadi kubwa ya dhuria wa Nabii

Isma'il (a.s.) walilazimika kuutoka mji wa Makkahh na wakaenda Yemen, na hakuna yeyote miongoni mwao aliyerudi Makkahh baada ya hapo.

Kuanzia muda ule na kuendelea kabila la Khaza'ah liliutawala mji wa Makkahh hadi walipotawala Waquraishi kwa kutawala Qusayy mwana wa Kilaab, baba mkuu wa babu yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w)- yaani baba yake babu wa Mtukufu Mtume s.a.w.w).

Baada ya muda fulani Abdul-Muttalib aliushika usukani wa mambo.Aliamua kukichimbua upya kile kisima cha Zamzam, lakini kwa bahati mbaya yeye hakuwa na uhakika wa mahali kilipokuwapo kisima kile. Baada ya kuchimba sana, alifaulu kukipata sehemu yake (halisi) na akaa- mua kuzichukua hatua za awali za kukichimba kisima kile akisaidiwa na mwanawe aliyeitwa Harith.

Kwa kawaida kwenye kila jamii mna kundi la wapinzani waliojaribu kuitafuta sababu moja au nyingine ili kuzuia utendaji wa kila amali ya uhakika. Hivyo basi, wapinzani wa Abdul-Muttalib, wakichelea kwamba heshima hii itamwendea yeye, walianza kumlaumu na wakisema: "Enyi wazee wa Waquraish! Kwa kuwa kisima hiki ni kumbukumbu ya jadi wetu Isma'il, nasi sote twahesabiwa kuwa tu dhuria wake, inafaa kwamba mtu- ruhusu sisi sote tushiriki kwenye kazi hii."

Kwa sababu fulani fulani Abdul-Muttalib hakukubaliana na wazo lao, kwa kuwa nia yake ilikuwa kukichimba kisima kile peke yake na kisha awaruhusu wote kuyatumia maji yale bila ya malipo. Vilevile alitaka kulichukua tena lile jukumu la kuwapatia maji mahujaji kwenye yale majira maalum ili kwamba kazi hii iweze kutendwa kwa utaratibu mwema chini ya uangalizi wake mwenyewe. Hata hivyo, jambo hili liliweza kuhakikishwa kwa kuishika kazi hii mikononi mwake, akiwa huru kabisa kutokana na wale wengine.

Jambo hili lilizaa mzozo mkali na mwishowe iliamuliwa ya kwamba wamuendee mtaalamu mmoja wa kiarabu (mpiga-bao) na uamuzi wake ufuatwe na watu wote. Hapo Abdul-Muttalib na wapinzani wake wakaianza safari. Walipita kwenye maeneo mengi ya nchi yaliyo kame. Wakiwa njiani mle, walikabiliwa na kiu kali, na ilikaribia kuwa na uhakika kwamba wataangamia.

Hivyo basi wakawa na hofu juu ya kifo na mazishi yao yatakayofuatia. Kwamba kila mtu ajichimbie kaburi, na atakapokufa mmoja wao, wale wengine wamzike. Na kama wataendelea kuyakosa maji na wote wakafa, wote watapata kuzikwa na kuokolewa kutokana na kuliwa na wanyama na ndege, ila yule atakayekuwa wa mwisho kufa.

Ushauri wa Abdul-Muttalib ulikubaliwa na watu wote na kila mmoja wao akaanza kujichimbia kaburi. Sasa wakawa wanakisubiri kifo kwa nyuso za huzuni na zilizopauka. Mara moja Abdul-Muttalib alipiga ukelele akisema: "Enyi watu! hiki kitakuwa kifo chenye kuaibisha na kufedhehesha. Ni bora kwamba sisi sote tutembee kwenye jangwa hili tukitafuta maji. Yumkini kwamba Allah akatuhurumia.[23]

Wote wakaanza kuwapanda wanyama wao na wakaanza kutwanyika. Hawakuwa na mategemeo sana ya kupata maji na wakaanza kutazamana kwa fadhaa. Hata hivyo, kwa bahati, waliyapata maji safi na

hivyo wakaokolewa kutokana na kifo kilichokuwa na uhakika wa kuwakumba. Kutoka hapo walirudi Makkahh na wakakubaliana kwa furaha na maoni ya Abdul-Muttalib kuhusiana na uchimbaji wa kisima kile, wakampa mamlaka kamili ya kuendelea na mradi wake ule.[24]

Abdul-Muttalib akaanza kukichimba kile kisima na mwanawe wa pekee wa wakati ule aliyeitwa Haarith na kichuguu cha mchanga kikajaa kandokando mwa sehemu ile. Kwa ghafla wakayagusa yale masanamu maw- ili ya paa yaliyofuliwa kwa dhahabu na zile panga kadhaa. Sasa Waquraish wakaamsha mzozo mwingine na wakadai fungu kwenye dafina zile. Hatimaye iliamuliwa kuumaliza mzozo ule kwa kupiga kura, kwa bahati yale masanamu mawili ya paa wa dhahabu yaliangukia kwenye fungu la Al-Ka'ba na zile panga ziliangukia kwenye fugu la Abdul-Muttalib, na Waquraishi wakaambulia patupu. Bwana Abdul-Muttalib mwenye fikara tukufu alizitumia zile panga katika kutengeneza lango la Al-Ka'ba na akawaweka wale paa ndani yake.

## Umadhubuti Wake Katika Kutimiza Ahadi

Baadhi ya sifa za Waarabu wa Zama za Jahilia zinastahili kusifiwa. Kwa mfano, walichukulia kuvunja ahadi kuwa ni tendo lenye kuchukiza mno. Kwenye nyakati fulani fulani waliishilizia masuala yao kwa maafikiano mazito na yenye udhia baina ya makabila ya kiarabu na wakayaheshimu maafikiano hayo hadi mwisho. Na kwenye matukio mengine waliweka nadhiri zichoshazo mno na zisizovumilika, lakini wakafanya juhudi zote katika kuzitimiza.

Alipokuwa akichimba Zamzam, Abdul-Muttalib alihisi kwamba kutokana na kutokuwa kwake na watoto wengi cheo chake kilikuwa dhaifu miongoni mwa Waquraishi kwa kiasi fulani. Hivyo basi aliamua kuweka nadhiri kwamba idadi ya wanawe itakapofikia kumi atamdhabihi mmoja wao mbele ya Al-Ka'ba. Hata hivyo, hakumweleza yeyote yule kuhusiana na kule kuiweka nadhiri hii.
Kwa kadiri muda ulivyopita idadi ya wanawe iliongezeka na kufikia kumi, na hivyo ule muda wa kuitimiza nadhiri ile ukafika. Kule kuiwazia tu azma hii kulikuwa mtihani mkubwa kwake. Hata hivyo, alichelea kubakia nyuma katika utekelezaji wa jukumu hili na kwa kufanya hivyo akawa mmoja wa wale walioshindwa katika kuzitimiza ahadi zao hivyo akaamua kuwaeleza wanawe jambo lile, na baada ya kuipata ridhaa yao, amchague mmoja wao kwa ajili ya lengo hilo kwa kupiga kura. [25]

Kule kupiga kura kulifanywa na kura ilimwangukia Abdullah (baba yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Mara moja Abdul-Muttalib aliukamata mkono wa Abdullah na kumwongozea kwenye madhabahu ya kudhabihia.

Waquraishi wanaume na wanawake walipopata habari za nadhiri ile na kule kupiga kura wakahuzunika mno. Mafuriko ya machozi yalitiririka mashavuni mwa watu. Mmoja wao alisikika akisema: "Oh! Ni bora kwamba wangaliniua mimi badala ya kijana huyu."

Machifu wa Waquraishi walikuwa wakisema: "Kama uhai wake ungaliweza kufidiwa kwa mali, tuko tayari kuutoa utajiri wetu wote mbele yake." Abdul-Muttalib hakufahamu afanye nini mbele ya hisia za watu

zivumazo.

Alijifikiria asije akawa mkosefu katika kumwasi Allah na kuivunja nadhiri yake. Ingawa aliyafikiria yote hayo, vile vile alikuwa akilifikiria suhulisho la tatizo hili. Mmoja wa wale waliokuwapo pale alisema: “Lipeleke tatizo hili kwa mmoja wa wataalamu wa kiarabu.

Inawezekana kwamba akaupendekeza ufumbuzi fulani.” Abdul-Muttalib na machifu wa kabila waliliafiki pendekezo lile na wakaondoka kuelekea Yathrib alikokiishi mtaala- mu yule. Yule mtaalamu aliomba aachwe kwa muda wa siku moja ndipo atoe jibu. Siku iliyofuatia watu wote walimwendea. Yule mtaalamu akauliza: “Ni dia gani mliyoiweka kwa mtu mmoja.” Wakamwambia kuwa ilikuwa ni ngamia kumi. Hapo yule mtaalamu akasema: “Hamna budi kupiga kura baina ya ngamia kumi na yule mtu mliyemchagua kudhabihi- wa. Kama kura ikimwangukia mtu yule basi ipandisheni idadi ya ngamia iwe mara dufu (yaani ishirini). Na kama kura ikimwanguka tena mtu yule basi ipandisheni idadi ya ngamia iwe mara tatu (yaani thelathini) na pigeni kura tena, na endaleeni kufanya hivyo hadi kura iwaangukie ngamia.

Ushauri uliotolewa na mtaalamu yule ulizituliza hisia za watu, kwa sababu iliwawia rahisi kuwadhabihi ngamia mia moja ikilinganishwa na kumwona kijana kama vile Abdullah akigaagaa kwenye damu. Alfajiri moja, baada ya kurejea kwao Makkahh, kazi ya kupiga kura ilifanywa kwa mara ya kumi, wakati idadi ya ngamia ilipopanda na kuwa mia moja, ile kura ikawaangukia wale ngamia. Wokovu na usalama wa Abdullah ulizaa kila hisia isiyo na kifani.

Hata hivyo, Abdul-Muttalib akasema: “Ni bora kwamba nipige kura tena ili niwe na uhakika kwamba Allah karidhika na kitendo changu hiki. Hivyo akaipiga kura ile mara tatu na kila mara kura iliwaangukia wale ngamia mia moja. Hivyo alishawishika na radhi ya Allah na akaamrisha kwamba ngamia mia miongoni mwa ngamia wake, wachinjwe kwenye siku ileile mbele ya Al-Ka’ba na asiwepo mwanaadamu wala mnyama atakayezuiwa kula nyama ya ngamia hao.[26]

## Machafuko Ya Mwaka Wa Ndovu

Tukio kuu litukiapo katika taifa, kiini cha sababu zake mara nyingi huwa za kidini, na mara chache huwa za kitaifa na kisiasa. Kwa kawaida huheshimiwa na umma, na kwa sababu hii huchukuliwa kuwa ndio mwanzo wa historia kwa ajili ya matukio ya siku za kale na zijazo. Kwa mfano, kazi ya Nabii Musa (a.s.) na kuhajiri kwa Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w) ni mwanzo wa historia kwa Wayahudi, Wakristo na Waislamu na wafuasi wa dini hizi huyahesabu matukio ya maisha yao wakirejea kwenye matukio haya.

Kwenye nyakati fulani fulani, baadhi ya mataifa ingawa wanayo historia ya kimsingi, vilevile huyachukulia baadhi ya matukio kuwa ndio mwanzo wa historia yao. Kama vile tuyaonavyo Mapinduzi Makuu ya Ufaransa na Mapinduzi ya Kikomunisti ya mwezi wa Oktoba 1917 katika Jamhuri ya Muungano ya Kisovieti ni mwanzo wa historia ya matukio mengi kwenye nchi za Magharibi. Mataifa yasiyostaarabika, yaliyonyimwa vyama vya kisiasa na kidini kama hivyo, kwa kawaida huyachukulia matukio yasiyo ya

kawaida kuwa ndio msingi wa histoia yao.

Kwa sababu hii, Waarabu wa Zama za ujinga, kutokana na kutokuwa kwao na ustaarabu ufaao, huyachukulia matukio yasiyofaa kama vile vita, matetemeko ya ardhi, njaa, na matukio mengine yasiyofaa kuwa ndio kipimo na asili ya historia yao.

Katika hali hii, tunaona katika kurasa za historia, idadi kadhaa ya vianzio vya historia ya Waarabu, cha mwisho miongoni mwao kilikuwa ni ghasia za Mwaka wa Ndovu, yaani yale mashambulio ya Abraha ili kuibomoa Al- Ka'ba, tukio ambalo baadae likawa mwanzo wa historia ya matukio mengineyo. Hapa chini tunatoa maelezo marefu na mchanganuo wa tukio hili lililo kuu, lililotokea katika mwaka 570 Masihiya, mwaka aliozaliwa Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.)

## Asili Ya Tukio Hili:

Tukio la 'Watu wa Ndovu' limetajwa kwa ufupi kwenye Qur'ani Tukufu na, baada ya kuisimulia hadithi hii, tutazitaja aya zilizofunuliwa kuhusiana na tukio hili. Wanahistoria wamekitaja chanzo cha tukio hili kama ifuatavyo:

"Baada ya Mfalme Zu Nuwaas wa Yemen kuimarisha mji mkuu wa serikali yake, akiwa kwenye moja ya safari zake alipitia mjini Yathrib (Madina). Wakati ule mji wa Yathrib ulikuwa na hadhi kubwa ya kidini. Kikundi cha Wayahudi kiliishi kwa wingi hapo na kujenga masinagogi kwenye sehemu mbalimbali za mji ule. Wayahudi wenye bahati njema (matajiri) walimkaribisha vizuri mno mfalme yule na wakamtaka awe Myahudi ili kwamba, wakiwa chini ya ulinzi wa serikali yake, wataweza kubakia salama kutokana na mashambulio ya Warumi Wakristo na Waarabu Waabuduo masanamu.

Juhudi zao kwenye jambo hili zilizaa matunda, Zu Nawaas aliifuata dini ya Kiyahudi na akafanya juhudi zote alizoziweza katika kuiendeleza dini ile. Watu wengi walimwelekea kwa kumwogopa. Baadhi yao waliadhibiwa kwa adhabu kali kwa kuwa kwao na maoni tofauti. Hata hivyo, watu wa Najran walioingia kwenye Ukristo muda fulani kabla ya hapo, hawakuwa tayari kwa gharama yoyote ile, kuiacha dini yao na kuyafuata mafundisho ya dini ya Wayahudi. Mfalme wa Yemen alichukizwa mno na uasi na dharau yao na akaja na jeshi kubwa kuwatiisha waasi. Amiri jeshi wa jeshi lile alipiga kambi karibuni na jiji la Najran akachim- ba handaki hapo, akawasha moto mkubwa kwenye handaki lile na kuwaogopesha wapinzani wake kwa kuwachoma.

Hata hivyo, watu mashujaa wa Najran, waliokuwa na itikadi yenye nguvu mno juu ya Ukristo, hawakutishika. Walikipenda kifo na kuchomwa moto kwa mikono miwili na miili yao ililiwa na miali ya moto." 27

Mwanahistoria mashuhuri wa Kiislam, Ibn Athir Jazari ameandika hivi: "Wakati ule ule mmoja wa wakazi wa Najran aliyeitwa Daws alikwenda upesi–upesi kwa Kaisari, Mtawala wa Kirumi, aliyekuwa mlinzi mkuu wa Ukristo wakati ule, na akamweleza tukio lile. Pia alimwomba yule Mfalme amwadhibu muuaji

yule aliyeizima taa ya mwongozi kule Najran na aidumishe kwa marefu zaidi ile nguzo ya Ukristo kwenye eneo lile iliyokuwa ikilegalega.

Yule mtawala wa Kirumi aliidhihirisha huzuni yake na huruma na akasema: “Kwa kuwa mji mkuu wa serikali yangu uko mbali mno kutoka nchini mwenu, ninamwandikia barua Negusi, Mfalme wa Ethiopia, alipize kisasi juu ya katili yule kwa ajili ya kuwaua watu wa Najran. Yule Mnajrani akaichukua ile barua ya Kaisari na akaipeleka Ethiopia upesi kwa kadiri alivyoweza. Alipofika kule alimwelezea Negus hadithi yote. Hisia za heshima za Mfalme wa Ethiopia ziliibuka. Alipeleka nchini Yemen jeshi lililo na zaidi ya askari sabini elfu likiwa chini ya amiri jeshi Mwafrika aliyeitwa Abraha Ashram. Jeshi hili la Waethiopia lenye uongozi mzuri na zana bora na za kutosha likaivuka bahari (ya Sham) na kupi- ga kambi kwenye pwani ya Yemen. Zu Nawaas alikamatwa kwa ghafla. Matendo yote haya yalidhihirisha kwamba hayatoshi na hakuna jibu lolote alilolipokea kuhusiana na barua aliyowaandikia machifu wa kikabila aki-waomba washiriki mwenye vita ile. Shambulio dogo tu lilitosha kuubomoa msingi wa serikali yake (Zu Nawaas) na ile nchi ya Yemen yenye watu wengi ikawa milki ya Serikali ya Ethiopia. Mfalme wa Ethiopia alimteua amiri jeshi wa jeshi lile, Abraha kuwa kaimu katika eneo lile.

Abraha alifurahi sana kwa kuwalipizia kisasi Wakristo wa Najran na kupata ushindi na akaanza kuishi maisha ya kiungwana. Ili ajipatie upendo zaidi mbele ya Mfalme wa Ethiopia alijenga kanisa la fahari mjini San’a lisilokuwa na kifani kwenye zama zile kwa utukufu wake kisha akamwandikia barua Negus akisema hivi: “Kwa kupatana na matakwa yako Jalali Mfalme ujenzi wa kanisa umetimia. Ninategemea kwamba nitaweza kuwafanya watu wa Yemen waache kwenda hija kwenye Al- Ka’ba, na nafasi yake itachukuliwa na kanisa hili.” Mambo yaliyomo kwenye barua ile yalipofahamika, yalitokea mambo yasiyofaa miongoni mwa makabila ya kiarabu. Hali hii ilikithiri mno kiasi kwamba usiku mmoja mwanamke wa kabila la Bani Afqam aliunajisi ua wa kanisa lile.

Kitendo hiki kilichoonyesha dharau kubwa, utwezo na uadui wa Waarabu kwa kanisa la Abraha, kuliishtua Serikali ya wakati ule. Zaidi ya hapo kwa kadiri Abraha alivyozidisha kulinakshi na kulipamba lile kanisa, ndivyo watu walivyozidi kujiambatanisha na Al-Ka’ba.

Matukio haya yalimfanya Abraha aape kwamba ataivunja Al-Ka’ba. Aliandaa jeshi kwa lengo hili, akawaweka ndovu wapiganao kwenye mstari wa mbele na akaamua kwenda kuivunja ile Nyumba ambayo msingi wake ulijengwa na yule mwasisi wa Upweke wa Allah, Nabii Ibrahim (a.s.).

Machifu wa Bara Arabu walitambua ya kwamba hali ile ilikuwa nyeti na ya hatari na wakawa na yakini kwamba uhuru na taifa la kiarabu binafsi ulikuwa unaelekea kwenye kuvunjika. Vile vile ushindi wa Abraha wa siku zilizopita uliwaweka mbali na uchukuaji wa maamuzi yenye maana.

Hata hivyo, machifu wa makabila yenye shauku walimkabili Abraha walipigana kwa ushujaa mkubwa. Kwa mfano, Zu Nafar, aliyekuwa mmoja wa watu wakuu wa Yemen aliwanasihi watu wake, kwa hotuba motomoto, kuihami nyumba takatifu (Al-Ka’ba). Hata hivyo, jeshi kubwa la Abraha lilizikata safu zao zilizoandaliwa upesi sana. Baada ya hapo, Nafil mwana wa Habib alifanya mapigano makubwa, lakini

watu wake nao walishindwa. Yeye mwenyewe alikamatwa na akamwomba msamaha Abraha. Abraha alikubali kulitimiza ombi lake kwa sharti la kwamba ayaongoze majeshi yake kuelekea Makkahh. Hivyo Nafil akawa mtumishi wake na akamwongoza hadi alipofika Taif.

Hapo alimpa kazi hiyo mmoja wa marafiki zake aliyeitwa Ayurgha! Huyu kiongozi mpya aliwaongoza hadi Mughmas – sehemu iliyokuwa karibu na Makkahh – na hapo jeshi la Abraha likapiga kambi. Kufuatana na desturi za kale, Abraha alimwamrisha mmoja wa maafisa wake kuwateka ngamia na wanyama wengine wa kufugwa wa Tahamah. Miongoni mwa ngamia waliotekwa, 200 walikuwa mali ya Abdul-Muttalib. Baadae Abraha alimwamrisha afisa wake mwingine aliyeitwa Hanatah kumpelekea chifu wa Waquraishi ujumbe wake.

Alimwambia Hanatah hivi: "Ninaweza kuiona hali halisi ya maangamizo ya Al-Ka'ba. Bila shaka kwenye hatua ya kwanza kabisa Waquraishi watapinga. Hata hivyo, ili kuthibitisha kwamba damu yao haimwagwi, huna budi kwenda Makkahh upesi sana. Huko ukaonane na chifu wa Waquraishi na umwambie kwamba lengo langu ni kuibomoa Al- Ka'ba na kama Waquraishi hawatapinga, watakuwa salama kutokana na usumbufu." Yule mjumbe aliyetumwa na Abraha alifika Makkahh na akaonana na makundi mbalimbali ya Waquraishi na wakalijadili jambo hilo kwenye sehemu mbalimbali. Alipoulizia juu ya chifu wa Waquraishi alipelekwa nyumbani kwa Abdul-Muttalib. Baada ya Abdul-Muttalib kuusikia ujumbe wa Abraha alisema hivi: "Sisi kamwe hatuelekei kwenye mapigano. Al-Ka'ba ni Nyumba ya Allah. Ni Nyumba aliyoiasisi Nabii Ibrahim (a.s.). Allah atafanya lolote lile Alionalo kuwa linafaa."

Vile vile yule afisa wa Abraha aliidhihirisha ridhaa yake kwa kuyasikia yale maneno ya chifu wa Waquraishi yaliyo laini na yenye maafikiano na yaliyoiashiria itikadi yake ya kiroho. Hivyo basi, alimwomba Abdul- Muttalib akubali kufuatana naye hadi kambini kwa Abraha.

## Abdul-Muttalib Aenda Kambini Kwa Abraha

Abdul-Muttalib alikwenda kambini kwa Abraha akifuatana na wanawe wachache. Busara, utukufu na heshima ya huyu kiongozi wa Waquraishi vilimfanya Abraha ampende na kumheshimu mno kiasi kwamba alishuka kwenye kiti chake cha enzi, akampa mkono Abdul-Muttalib na akamfanya aketi ubavuni kwake. Kisha, kwa heshima kuu akamwuliza Abdul- Muttalib, kupitia kwa mkalimani ni kitu gani kilichomleta pale na alihitaji nini. Akilijibu swali hili alisema: "Wale ngamia wa Tahamah, ambao pia walikuwa na ngamia wangu mia mbili, wametekwa na askari wako. Ningependa kukuomba uamrishe kwamba ngamia hao warejeshwe kwa wenyewe." Abraha alijibu hivi: "Uangavu wa wajihi wako wenye heshi- ma takatifu ulinifanya nikufikirie kuwa u mtu mkubwa sana. Hata hivyo, ombi ulililoliomba kwa ajili ya vitu vidogo mno kumeipunguza thamani yako machoni mwangu. Ukiuzingatia ukweli uliopo kwamba mimi nimekuja kuibomoa na kuiharibu Nyumba takatifu ya jadi zenu niliitege- mea kwamba utazungumzia juu ya Al-Ka'ba na kuniomba niache kulitimiza lengo langu hili ambalo litaupiga pigo kubwa uhuru wenu na maisha yenu ya kisiasa na kidini. Mimi sikutegemea kwamba utazungumzia juu ya vitu vichache vidogo na visivyo na thamani na kuom- ba kwa ajili hiyo."

Akiyajibu maneno ya Abraha, Abdul-Muttalib aliitam- ka sentensi ambayo, thamani na faida yake bado vimehifadhiwa. Alisema: "Mimi ndiye mwenye ngamia hao. Hii Nyumba nayo inaye Bwana wake mwenye kulikinga kila lenye kujipenyeza juu yake." Abraha aliposikia hivyo alitikisa kichwa chake na akasema kwa majivuno: "Hakuna yeyote aliye na nguvu zaidi ya kuweza kunizuia nisiitimize azma yangu." Kisha akaamrisha kwamba ile mali iliyonyakuliwa irudishwe kwa wenyewe."

## Waquraishi Wasubiri Kurejea Kwa Abdul-Muttalib

Waquraishi walikuwa wakisubiri kwa hamu kubwa kurejea kwa Abdul- Muttalib ili wayajue matokeo ya mazungumzo yake na Abraha. Hivyo basi, alipokutana na machifu wa Waquraishi aliwaambia: "Kimbieni upesi kwenye mabonde na kwenye vilima pamoja na wanyama wenu ili kwam- ba muwe salama kutokana na kila aina ya dhara." Baada ya hapo watu waliziacha nyumba zao upesi upesi na wakakimbilia vilimani. Wakati wa usiku vilima na mabonde yote yalivuma vilio vya watoto, maombolezo ya wanawake na milio ya wanyama.

Katikati ya usiku ule Abdul-Muttalib na Waquraishi wengine walikishuka kilele cha kilima na wakalifikia lango la Kaabah. Yeye (Abdul-Muttalib), huku machozi yakimchuruzika na moyo ukimuungua, aliishika nyororo ya lango la Al-Ka'ba mkononi mwake na akazisoma beti chache za shairi akizunguma na Allah swt. Alisema hivi: "Ee Allah! Sisi hatuitegemezi imani yetu kwa yeyote yule ila Wewe tu, katika kusalia salama kutokana na ufisadi na madhara yao.

Ee Mola! Wazuie dhidi ya Nyumba Yako takatifu. Adui wa Al-Ka'baa ni yeye yule aliye mshindani dhidi Yako.

Ee Mhifadhi! Wakatilie mbali mikono yao ili kwamba wasiinajisi Nyumba Yako.

Mimi ninayo haki juu ya mali yangu, hivyo basi, ninajitahidi kwa ajili ya usalama wake. Hata hivyo, usalama wa Nyumba Yako ni Jukumu Lako. Usiruhusu kuja kwa ile siku ambayo Msalaba utakuwa mshindi juu yake (Nyumba hii), na wakazi wa nchi zao wakajiingiza nchini Mwako na kuiteka."

Kisha akaiachia ile nyororo ya lango la Al-Ka'ba na akakimbilia kwenye kilele cha mlima ili aone maendeleo ya jambo lile.

Alfajiri na mapema Abraha na majeshi yake wakajitayarisha kuingia mjini Makkahh. Hata hivyo lilijitokeza kundi la ndege kwa ghafla kutoka upande wa baharini, wakivichukua vikokoto vidogo midomoni na mwenye makucha yao kivuli cha hawa ndege weusi kililifanya anga la juu ya kambi kuwa na giza na silaha zao ndogo zionekanazo kutokuwa na thamani zilizaa athari za ajabu. Ndege hawa wenye silaha za vikokoto hivyo walivimimina vikokoto hivyo kwa amri ya Allah juu ya jeshi la Abraha kwa jinsi ambayo vichwa vyao vilivunjikavunjika na nyama ya miili yao ilitolewa miilini mwao.

Kokoto moja ilimpiga Abraha kichwani, na kwa sababu hii hofu ilimshika na akaanza kutetemeka. Alikuwa na uhakika kwamba ghadhabu ya Allah imeshuka. Kisha akawatupia jicho askari wake na

akaona kwamba miili yao imeanguka chini kama majani ya miti. Hivyo basi, mara moja akawaamrisha wale waliosalimika kurudi Yemen na kwenda Sa'na kwa kuipitia ile njia waliyoijia. Jeshi lililosalia likaondoka kuelekea Sa'na kwa kuipitia ile njia waliyoijia. Jeshi lililosalia likaondoka kuelekea San'a laki-ni, lilipokuwa njiani, wengi wa askari wake waliangamia kutokana na majereha na hofu.
Hata Abraha mwenyewe alifika Sa'na akiwa kwenye hali mbaya mno kiasi kwamba nyama ya mwili wake ilipasukapasuka na alikufa kifo kibaya mno.

Tukio hili la kimauti na lisilo kifani limepata kutambulika ulimwenguni kote. Qur'ani Tukufu inaisimulia hadithi ya 'Watu wa Ndovu' kwa maneno haya:

{أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحَابِ الْفِيلِ {1

{أَلَمْ يَجْعَلْ كَيْدَهُمْ فِي تَضْلِيلٍ {2

{وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ {3

{تَرْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ مِنْ سِجِّيلٍ {4

{فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَأْكُولٍ {5

***"Je, hukuona jinsi Allah Alivyolitenda jeshi la Ndovu? Je, Hakuiharibu hila yao kwa kuwapeleka makundi ya mbayuwayu waliowavurumishia mawe ya udogo uliookwa, hivyo Akawafanya*** (***kuwa***) ***kama majani makavu*** (***yaliyoliwa na mifugo***)***"*** (***Suratul-Fiil, 105: 1-5***).

Yaliyosimuliwa kwenye kurasa hizi ni kiini cha historia ya Uislamu inay- olihusu jambo hili[28] kwenye Qur'ani Tukufu. Sasa tutayasoma maelezo yaliyotolewa na mfafanuzi mkuu wa Kimisri, Muhammad Abduh na wanachuoni maarufu, Dakta Haikal, aliyekuwa Waziri wa Elimu chini Misri.

## Mjadala Wa Kiakili Juu Ya Miujiza

Maendeleo ya mwanaadamu yashangazayo na yaliyopatikama hivi karibuni kwenye nyanja mbalimabli za sayansi za kimaumbile na kukoma kwa maisha na nyingi miongoni mwa nadharia tete (hypotheses) za kisayansi, kumeleta ghasia kwenye nchi za Kimagharibi. Ingawa maelezo juu ya mabadiliko haya yamesimamia kwenye mipito ya kisayansi na yalizun- gukia kwenye mhimili wa sayansi ya kimaumbile pekee (kwa mfano, makisio ya Ptolemy yalionekana kuwa si ya kweli) na hayakuwa na uhusiano wowote na itikadi za kidini, yalizaa matazamio mabaya (pessimism) miongoni mwa matabaka mbalimbali kuhusu

nadharia na itikadi zilizo salia.

Siri za haya matazamio mabaya imesimama kwenye ukweli uliopo kwamba, wanachuoni walipoona ya kwamba nadharia za zamani zilizokuwa zikitawala fikara za mwanaadamu na vyuo kwa karne nyingi sasa zimesimama kwenye msingi wa uongo, na mkono wa elimu wenye nguvu na uwezo mkuu wa majaribio, na zaidi ya hapo, haikuwapo taarifa yoyote kuzihusu sayari mbalimbali za angani na miendo yao midogomidogo na kuwa katikati kwa dunia, na vilevile kuhusu korija kadhaa za mafafanuzi; walijifikiria kwamba hakuna mtu ajuaye ya kama je, yale mafafanuzi yaliyosalia ya kidini na kisayansi yaweza nayo kuwa kama yale mengineyo? Jinsi hii ya fikara, pole pole ilizipanda mbegu za shaka akilini mwa wengi wa wanachuoni wa sayansi za kimaumbile na kwenye kipindi kifupi tu, shaka hii ilikua na kuenea kwenye maeneo yote ya sayansi za Ulaya za siku zile kama maradhi ya kuambukiza.

Aidha, 'Baraza Kuu la kuhukumia wazushi wa Dini' (Idara ya uchunguzi wa itikadi) na ukali wa wakuu wa Kanisa vilikuwa na fungu kamili katika uotaji, na zaidi ukuaji wa hali hii ya kutokuwa na matarajio mema, kwa sababu wanachuoni wa zama zile waliofaulu katika ugunduzi wa nadharia fulanifulani za kisayansi waliangamizwa na Kanisa kwa adhabu kali na mateso.
Na haina hajja kusema kwamba shinikizo na mateso haya hayana budi kwamba yalizaa matokeo mabaya na tangu kwenye siku hizo ilitabiriwa kwamba, kama katika wakati wowote ule wana vyuoni hawa wataipata nguvu na wakayafanya maendeleo yatoshelezayo kwenye uwanja wa kimaumbile, wataipa dini na uchamungu 'kwa heri' kutokana na sera mbaya ya Mapapa."

Kwa bahati mambo yakapata kuwa hivyo. Kwa kuwa elimu kuhusiana na mambo mbalimbali imekua na wanachuoni wamepenya zaidi na zaidi kwenye uhusiano baina ya viumbe, ilizifunua siri zilizofichikana kutoka kwa mwanadamu kwa karne nyingi, na wakapata elimu juu ya sababu za matukio mengi ya kimaumbile kama vile matetemeko ya ardhi na mvua, pamoja na sababu za magonjwa mbalimbali, hawakufaulu sana juu ya mambo ya kimungu. (Asili, ufufunuo, miujiza na matendo yasiyo ya kawaida ya Mtukufu Mtume s.a.w.w na kadhalika) na idadi ya wenye shaka na wenye kukanusha inayoongezeka siku hadi siku.

Majivuno na kiburi juu ya elimu yao waliyokuwa nayo baadhi ya wanachuoni akilini mwao, na shinikizo la mapapa na makasisi vimekuwa chanzo cha baadhi ya wanasayansi kuyatazama mambo yote ya kidini kwa dharau na kutojali. Hawakukubali tena kuwa majina ya Torati au Injili yatajwe. Kwa mujibu wa fikara zao, tukio la fimbo ya Nabii Musa (a.s.) na mkono wake ung'aao havina budi kuchukuliwa kuwa ni hadithi tu, na kupulizia kwa Nabii 'Isa' (a.s.) kulikohuisha wafu wengi kwa idhini ya Allah, vile vile kulikuwa hadithi ya kubuniwa tu.

Ilitokea hivyo kwa sababu kiburi juu ya maendeleo ya elimu ya kisayansi na kumbukumbu ya shinikizo waliloshinikizwa nalo hapo kale viliwafanya wajifikirie kwamba: "Yawezekanaje kwamba kinapokosekana kisababisho cha kawaida, kipande cha mti kijitwalie umbo la joka, au wafu waweze kufufuka kwa njia ya dua?" wanachuoni waliolewa na mafanikio katika uwanja wa sayansi walifikiria kwamba walishajipatia funguo ya nyanja zote za elimu na wameuelewa uhusiano baina ya viumbe vyote na matukio.

Ni kwa sababu hii kwamba hawakuona uhusiano, japo ulio mdogo tu, baina ya kipande cha mti kikavu na chatu, au baina ya dua na usikivu wa mtu kwa upande mmoja na kufufuka kwa wafu kwa upande mwingine. Hivyo basi, waliyaangalia mambo haya kwa shaka, na kusita sita au kuyakana kabisa.

## Mtindo Wa Fikara Za Baadhi Ya Wanachuoni

Siku hizi mtindo huu wa kufikiria, ukiwa na mabadiliko madogo, umechukuliwa na wanachuoni wa Kimisri. Wanachuoni hawa ambao kwa kweli wao ni kiungo baina ya vyuo vya elimu vya Mashariki na vile vya Magharibi na kwa miaka mingi na mapema kuliko yeyote yule wamekuwa wakihamisha elimu na mitindo ya fikara ya watu wa Magharibi na kuwapelekea wale wa Mashariki, na kwa kweli wanafikiriwa kuwa wao ni daraja ya elimu na uhusiano wa kielimu baina ya pande mbili za nchi hizi, zimekuwa na ushawishi zaidi kuliko mtu yeyote mwingine kwa mtindo huu wa fikara (kwa kweli zikiwa na matengenezo maalum) na wanafuata mtindo huu katika mambo ya kuelezea na uchambuzi wa matatizo ya kihistoria na kisayansi.

Baadhi yao wameichagua njia ambayo kwayo wanataka kuwaridhisha Waislamu waiaminio maana ya dhahiri ya Qur'ani Tukufu na hadith za dhahiri na pia kuzichukua fikara za wanasayansi, au kwa kutolitoa wazo lisiloweza kuelezeka katika mwanga wa kanuni za sayansi za kimaumbile.

Kwa upande mwingine wanaona kwamba Qur'ani Tukufu ina nyororo ya miujiza isiyokanika na Kitabu hiki ni hukumu ya mwisho kwa Waislamu, na chochote kile ikisemacho ni sahihi na ni chenye kuafikiana na ukweli, kwa upande mwingine, wanaona kwamba sayansi za kimaumbile na wenye kuiunga mkono elimu ya kidunia hawayatambui mambo haya ambayo kulingana na fikara zao (zinazong'ang'ania kwenye kisababisho cha asilia kwa kila tukio la kimaumbile) yako kwenye kutoafikiana na kanuni za kisayansi.

Matokeo ya mambo haya mawili, kwa mujibu wa itikadi zao, hakuna hata moja lenye kunyambulika, na sasa wameishika njia nyingine ambayo kwayo wanataka kuyaridhisha makundi yote mawili (lile la dini na lile la sayansi). Yaani wanaihami maana ya dhahiri ya Qur'ani Tukufu na hadithi zenye maana ya dhahiri na vilevile wasikiseme chochote kilicho dhidi ya sheria za kisayansi.

Kufuatana na lengo hili, wanajitahidi kuieleza miujiza na matendo yasiyo ya kawaida ya Mitume (a.s.) kulingana na vigezo vya sayansi ya kisasa na kuzieleza maana za miujiza kwa njia ambayo yaonekana kuwa ni matukio ya kawaida tu. Kwa njia hiyo wameihami heshima istahiliyo ya Qur'ani Tukufu na hadithi zenye maana ya dhahiri na vilevile wamejipa uhuru kutokana na kila aina ya matazamio ya matokeo mabaya na kutokukubalika kwa mafunzo yao. Tukitoa mfano wa jambo hili, tunatoa hapa chini maelezo aliyoyatoa Muhammad Abduh, mwanachuoni maarufu wa Kimisri kuhusu tukio la 'Watu wa Ndovu' lililotajwa kwenye Qur'ani Tukufu:

"Ni maradhi ya ndui na homa ya taifodi iliyosababishwa na vumbi lenye kokoto za mawe lililoenea miongoni mwa jeshi la Abraha kupitia wadudu kama vile mbu na inzi. Na maneno "mawe ya udongo

uliookwa” yana maana ya “udongo wenye kokoto za mawe” uliotawanyishwa na upepo kila mahali na hivyo basi, ukaganda kwenye miguu ya wadudu wale. Matokeo ya kukutana kwa wadudu wale na miili ya wanadamu, wadudu wa maradhi (germs) waliingia kwenye vinyweleo vya ngozi ya mwili wa mwanaadamu na kufanya madonda yenye maumivu makali na machafu yalitokeza humo. Na wadudu hawa ni askari wa Mwenyezi Mungu walio na nguvu nyingi waitwao ‘Microbes’ katika istilahi za kisayansi.”

Mwandishi mmoja wa kisasa akiyaunga mkono maoni aliyoyatoa mwanachuoni tuliyemtaja hapo kabla, anasema kwamba, neno ‘Tayr’ lililotumika mwenye Qur’ani Tukufu lina maana ya cho chote kile kiruka-cho na ni pamoja na mbu na inzi.

Kabla hatujafikiria kwa makini maneno ya hawa waandishi wawili tuliowataja tunafikiria kwamba ni muhimu kunukuu tena hapa chini zile aya zilizofunuliwa kuhusiana na wale ‘Watu wa Ndovu’. Allah, Mwenye nguvu zote anasema hivi kwenye sura al-Fiil:

{أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحَابِ الْفِيلِ {1

{أَلَمْ يَجْعَلْ كَيْدَهُمْ فِي تَضْلِيلٍ {2

{وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ {3

{تَرْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ مِنْ سِجِّيلٍ {4

{فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَأْكُولٍ {5

***“Je, hukuona jinsi Allah alivyolitendea Jeshi la Ndovu? Je hakuiharibu hila yao kwa kuwapelekea makundi ya mbayuwayu waliowavurumishia mawe ya udogo uliookwa, hivyo akawafanya** (**kuwa**) **kama majani makavu yaliyoliwa na mifugo.”*** (***Suratul-Fiil, 105: 1-5***)

Kutokana na maelezo haya aya hizi zinaonyesha kwamba watu wa Abraha walikumbwa na ghadhabu ya Allah na sababu ya kifo chao ilikuwa ni hizi kokoto za udongo wa kuoka ambazo hawa ndege walizichukua na kuzirujumu juu ya vichwa, nyuso na miili yao.

Kujifunza aya hizi kwa undani na moja moja kunatuongoza kwenye kuamini kwamba kifo cha watu hawa kilitokana na silaha hizi zisizo za kawaida zionekanazo kuwa si zenye thamani na dhaifu, za kokoto za udongo uliookwa, lakini kwa kweli zilikuwa zenye nguvu na zenye kuleta madhara makuu. Kwa sababu

hii, aya hizi za Allah haziwezi kutafsiriwa kwa maana zozote zile zipewazo, kwa njia ya maelezo yaliyo katika hali ya kutoafikiana na maneno yake ya dhahiri, na pale utolewapo uthibitisho ukubalianao na aya hizo, juu ya usahihi wa maelezo hayo.

## Mambo Muhimu Kuhusu Maelezo Tuliyoyatoa Juu

Vilevile maelezo tuliyoyatoa hapo juu hayawezi kulidhihirisha tukio lote kuwa ni la kawaida na vivyo katika hadithi hii, husalia baadhi ya mambo yawezayo tu kuelezwa kwa kutoa sababu zisizo za kawaida. Hivyo basi, japo tuchukulie kuwa vifo na maangamizo ya watu wale yalitokana na 'microbes' wa ndui na homa ya taifoidi, swali hubaikia ni kwa vipi na ni kwa njia gani ndege hawa walipata mwongozo na mafunzo hadi wakaelewa kwamba 'microbes' wa homa la ndui na taifoidi waishakaa mwenye hizi kokoto za udongo wa kuoka katika ule muda maalum, na badala ya kwenda kuitafuta riziki yao, walijikusanya pamoja wakizielekea zile kokoto za udongo wa kuoka na wakiwa wamezishika kwa midomo yao wakawarujumu watu wa Abraha kama vile jeshi lishambuliavyo adui wake? Katika hali hii je, tunaweza kulichukulia tukio hili lote kuwa ni la kawaida na la kimumbile tu? Kama tuko tayari kukubali kwamba mambo yote haya yalitokea kwa mujibu wa amri ya Allah na kwamba nguvu isiyo ya kawaida ilikuwa ikifanya kazi kwenye tukio hili, basi uko wapi umuhumu wetu wa kuifikiria sehemu tu ya tukio hili kuwa ndiyo ya kawaida na tukimbie kuzieleza sababu zake.

Wadudu wadogo mno waitwao 'microbes' walio maadui wa wanaadamu wote, hawana uhusiano na yeyote kutokana na hali hii, jambo hili laweza kuelezekaje kwamba wadudu hawa walishambulia jeshi la Abraha pekee na kuwaacha wakazi wa Makkahh? Vitabu vya historia tulivyonavyo hivi sasa vinakubaliana kwa pamoja kwamba hasara yote waliyoipata ni askari wa Abraha tu, na Waquraishi na Waarabu hawakupata dhara lolote japo lililo dogo tu ingawa homa ile ndui na taifodi ni maradhi yanayoambukiza na vitu mbalimbali vya kimaumbile huvisafirisha kutoka sehemu moja hadi nyingine na wakati mwingine hutokea kwamba huiangamiza nchi nzima. Katika hali hii, je, tukio tunalolizungumzia laweza kuchukuliwa kwamba ni jambo la kawaida?

Tofauti za kimaoni walizonazo wale wanaoyatoa maelezo haya, kuhusu aina hii ya 'microbes' yenyewe huidhoofisha dhana yao. Wakati mwingine wanasema kwamba walikuwa wadudu wa kipindupindu na mara kwa mara wanadai kwamba walikwa ni wale wa homa ya ndui na taifoidi, ambapo bado hatujapata taarifa yoyote iliyo sahihi na ya kutegemeka kuhusiana na kutoafikiana huku. Miongoni mwa wasimuliaji wa hadithi ni Akramah pekee, ambaye, yeye mwenyewe yu asili ya kutoafikiana miongoni mwa wanachuoni, ameufikiri uwezekano huu na miongoni mwa wanahistoria Ibn Athri, alipokuwa akiunukuu uwezekano huu kuwa ni kauli dhaifu, amekwenda moja kwa moja kuikanusha.[29]

Maelezo yastaajabishayo zaidi ni yale aliyoyatoa mwandishi wa kitabu kiitwacho '*Hayat-i-Muhammad*' (Dakta Haikal, aliyekuwa Waziri wa Elimu wa Misri), alipokuwa akiisimulia hadithi ya 'Watu wa Ndovu.' Ingawa jambo lililo machoni mwake ni ile aya isemayo: 'Tuliwapelekea makundi ya ndege', yeye, baada ya kuinukuu Sura ya al-Fiil, anasema hivi, kuhusiana na vifo vya jeshi la Abraha: "Pengine wadudu wa

kipindupindu walikuja na upepo kutoka kwenye upande wa baharini." Sasa kama upepo umeleta wadudu wa kipindupindu kwa nini wale ndege walikuwa wakirukaruka vichwani mwao?

Zaidi ya hapo, hao ndege walikuwa waki- wavurumishia hizo kokoto za udogo uliookwa: Sasa kokoto hizi za udon- go uliookwa zilikuwa na kazi gani kwenye vifo vyao? Hivyo basi hatuna budi kuiepuka njia hii ya kufikiria na pasipo haja yoyote tuieleze miujiza mikuu ya Mitume kwa njia hii. Kimsingi, hali ya dini kwenye mambo haya, mbele ya sayansi za kimaumbile, ambazo maeneo yao ni madogo katika uhusiano na mambo ya kimaumbile, ni maradufu. Hivyo basi, hatuna budi kutoiacha misingi ya dini iliyokwisha kudumishwa kwa kutaka kuwaridhisha watu wachache wenye elimu ndogo ya dini na wasio na taarifa juu ya mambo ya aina hii, na hasa pale tusipokuwa na lazima yoyote ya kufanya hivyo.

## Mambo Mawili Yaliyo Muhimu

Tungalipenda kuyataja mambo mawili yaliyo muhimu, hapa: Hakutakuwapo kutoafikiana kuhusu ukweli uliopo kwamba kwa maelezo tuliyoyataja hapo juu, hatudhamirii kuyasahihisha na kuyaeleza mambo ambayo watu huyahusisha na Mitume na viongozi wa kidini kwa njia ya uzushi na mambo yasiyoungwa mkono na ushahidi wowote ukubalikao, na ambayo kwa kawaida yana hali ya kiushirikina. Maana yetu ni kwamba, kutegemeana na uthibitisho ukubalikao, tulionao mkononi, Mitume wa Allah waliyatenda matendo yasiyo ya kawaida ili kuuthibitisha uhusiano wao na ulimwengu wa kiroho. Lengo letu ni kuzihami aina hizi za miujiza. Kamwe hatusemi kwamba muujiza hauhitaji kanuni ya kisababisho na matokeo. Tunaiheshimu kanuni hii kikamilifu na tunaamini kwamba matukio yote ya ulimwengu hapa yana visababisho na hakuna jambo lijitokezalo pasi na kisababisho. Hata hivyo, tunalolisema ni kwamba si muhimu kwamba visababisho vya miujiza ni lazima kuwa kwenye mkumbo wa visababisho vya kawaida na vya kimaada. Hivyo basi miujiza na matendo ya Mitume yasiyo ya kawaida yana visababisho ambavyo havikubaliani na visababisho vya kawaida vya kimaumbile na kila mtu si mtambuzi wa siri hizi.

## Baada Ya Kushindwa Kwa Abraha

Ghasia za 'Mwaka wa Ndovu,' kifo cha Abraha na maangamizi ya maadui wa Al-Ka'ba na Waquraishi, kuliwatukuza mno wakazi wa Makkahh na Al-Ka'ba machoni pa ulimwengu wa kiarabu. Sasa hakuna mtu aliyethubu- tu kufikiria kuwashambulia Waquraishi au kuwafanyia madhara yoyote au kuibomoa Nyumba ya Allah. Mawazo ya watu wote yalikuwa kwamba: "Allah, kwa ajili ya heshima ya Nyumba Yake na kwa ajili ya heshima na umaarufu wa Waquraishi, amemfanya adui yao wa jadi kugaagaa kwenye vumbi na damu. Kutokana na hukmu hii tukufu ya Mwenyezi Mungu, Waquraishi na Al-Ka'ba wamekuwa wenye kuheshimika mbele ya Watu." ni kwa mara chache mno walifikiria kwamba jambo hili limetokea kwa ajili tu ya ulinzi wa Al-Ka'ba, na kwamba umaarufu au udogo wa Waquraishi hauna lolote lihusianalo nalo. Jambo hili lathibitika na ukweli uliopo kwamba, machifu wa maadui wa zama zile waliwashambulia Waquraishi mara kadhaa lakini katu hawakukabiliwa na hali hii.

Ushindi na mafanikio haya, yaliyopatikana bila ya jasho lolote na bila ya hata tone moja la damu ya Waquraishi kumwagika, yalizaa fikara mpya akilini mwao na majivuno yao, kiburi na kutojali kwao vikazidi. Sasa wakaanza kuamini udhaifu wa watu wengine, kwa sababu walijifikiria kuwa wao ni kundi mashuhuri miongoni mwa Waarabu na wakafikiria kwamba wao peke yao ndio waliopasika na uangalizi wa yale masanamu mia tatu na sitini na kupata msaada wao.

Tangu siku ile walianza kufanya karamu kubwa za furaha zisizo na mwisho na anasa zisizokuwa na kikomo. Waligugumia kikombe baada ya kikombe cha tembo ya mitende na mara kwa mara walijitia kwenye ulevi wa pombe katika eneo la Al-Ka'ba, na kulingana na methali yao, 'walizitumia siku njema za maishani mwao.' kwenye ujirani na masanamu yaliyotengenezwa kwa mawe na miti yaliyowahusu makabila ya kiarabu.

Katika mikutano hiyo, kila aliyekuwa amesikia hadithi yoyote ile juu ya Wamanzariya wa Hirah na Waghassaniya wa Sham na makabila ya watu wa Yemeni aliwasimulia wenzie nao waliamini ya kwamba walikuwa wakiyapata maisha yao ya furaha kutokana na uangalizi wa masanamu yaliyowadhoofisha Waarabu wa kawaida wakilinganishwa nao, na wamewapa (wao Waquraishi) fadhila juu ya wengineo wote.

## Mipaka Ya Kimawazo Ya Waquraishi

Mungu aepushie mbali kwamba huyu kiumbe mwenye miguu miwili (mwanadamu) siku moja aweze kuja kupata upeo wa maisha ulio wazi na aweze yeye mwenyewe kujidhania kuwa ni wa tabaka la kufikirika kupendelewa zaidi. Ni katika siku hiyo ambapo kwamba atajitengea maisha na uhai kwa ajili yake mwenyewe tu, na atakuwa haamini kwamba viumbe wenzie nao wanayo haki yoyote angalau kidogo ya uhai na thamani.

Ili kuuthibitisha ukuu na ubora wao juu ya wengineo, Waquraishi walia- mua siku ile kwamba hawatawaheshimu hata kidogo watu wa 'Hil' (lile eneo linalofikia umbali wa ligi nne – takriban kama maili kumi na mbili hivi – kutoka kwenye Al-Ka'ba kwenye pande zote nne huitwa '*Haram*' na eneo lililo nje ya umbali huo huitwa '*Hil*'), kwa sababu, kulingana na maoni yao, watu wengine walikuwa wakitegemea Hifadhi yao, na wameona kwa macho yao kwamba wao (Waquraishi) walikuwa ndio walengwa wa upendeleo wa miungu wa Al-Ka'ba.

Tangu wakati ule na kuendelea, Waquraishi walianza kuwa wakali kwa watu wengine. Wakiendesha udikteta kamili, waliamua kwamba kila watu wa 'Hil' wajapo kuhiji, wasivitumie vyakula waviletavyo bali wajipatie chakula kutoka kwa watu wa 'Haram.' Vile vile waliamua ya kwamba wakati wa kufanya ibada ya Tawafu wasivae nguo yoyote ile ila vazi la kienyeji la watu wa Makkahh lenye sifa za kitaifa.

Kama mtu hakuweza kuikabili gharama ya vazi lile, basi ilimlazimu mtu yule kuhiji bila ya nguo yoyote. Ama kuhusu baadhi ya Waarabu wenye vyeo vikuu ambao hawakuukubali mpango huu iliamuliwa ya kwamba baada ya kufanya Tawafu, itawalazimu kuzivua nguo zao na kuzitupa na hakuna aliyeruhusiwa

kuzigusa nguo hizo. Hata hivyo, kuhusu wanawake katika hali zote zile waliwajibika kufanya Tawafu wakiwa uchi. Waliweza kuzifunika pande za vichwa vyao tu kwa kipande cha nguo na walitakiwa wavumishe beti maalum.

Baada ya tukio lihusianalo na Abraha, aliyekuwa Mkristo, hakuna Myahudi wala Mkristo aliyeruhusiwa kuingia mji wa Makkahh, ila pale awapo mfanyakazi wa Makkahh aliyekodiwa. Katika hali hiyo, vilevile ilikuwa wajibu juu yake kutotamka japo neno moja juu ya itikadi na dini yake.

Mambo yalifanyika kwamba Waquraishi wakaziacha baadhi ya ibada za Hajj zilizokuwa zikitekelezwa nje ya Nyumba Takatifu. Kwa mfano hawakuwa tayari kuitekeleza ibada ya kusimama huko Arafah (sehemu iliyo nje ya 'Haram' ambako Mahujaji wanatakiwa kukaa hapo hadi kuchwa kwa jua siku ya mwezi tisa Dhul-Hajj (mfunguo tatu).30

Na walifanya hivyo ingawa jadi zao (kizazi cha Nabii Isma'il a.s.) walikufikiria huko kukaa Arafah kuwa ni sehemu ya ibada ya Hajj na ule ubora wao wa dhahiri walionao Waquraishi ulitokana na Al-Ka'ba na hizi ibada, kwa sababu ni kutokana na jambo hilo kuliko wawajibisha watu kuja kwenye sehemu hii iliyo kame, kila mwaka. Na kama si kwa ajili ya hii Nyumba Takatifu tu, hakuna hata mtu mmoja ambaye angalielekea kwenye ziara ya sehemu hii japo mara moja tu maishani mwake mwote.

Kwa mtazamo wa mkokotoo wa kijamii, uovu na ubaguzi huu ni vitu visivyo zuilika. Hivyo basi, ililazimu kwamba mazingira ya Makkahh yajitose kwenye uovu na unajisi ili kwamba ulimwengu uwe tayari kwa mapinduzi ya awali na harakati zenye kupenyeza kila mahali.

Ufukara wote huu, sherehe, ulevi na kutokujizuia vilikuwa vikiyafanya mazingira yale kuwa tayari zaidi na zaidi kwa kuja kwa mtengenezaji mkuu wa ulimwengu huu, na sio kwamba haikuwapo sababu, pale Waraqah bin Nawfal yule mtaalamu wa Uarabuni, aliyeingia kwenye dini ya Ukristo katika siku za mwishoni mwa uhai wake, na akajipatia elimu ya maandiko ya Injili alipozungumzia juu ya Allah na Mitume na aliikabili ghadhabu ya Firauni wa Makkahh kwa jina la Abu Sufyan aliyekuwa akisema: "Sisi watu wa Makkahh si wahitaji wa Allah wala Mitume, kwa kuwa tunaifaidi rehema na upendeleo wa masanamu yetu."

## Bwana Abdallah – Baba Yake Mtukufu Mtume (S.A.W.W)

Wakati ule Abdul-Muttalib alipoununua uhai wa mwanawe kwa kuwadhabihi ngamia mia moja kwa jina la Allah, Bwana Abdullah hakuwa zaidi ya umri wa miaka ishirini na nne. Tukio hili, zaidi ya kuwa sababu iliyomfanya (Abdullah) kuwa maarufu miongoni mwa Waquraishi, vilevile lilimpatia daraja kuu na heshima kwenye familia yake, hasa machoni mwa Abdul-Muttalib.

Sababu yake ilikuwa ni kwamba mtu hupenda hasa kila kitu kithibitishacho kuwa ni chenye gharama kuu kwake, na ambacho amepata taabu kubwa katika kukipata. Kwa sababu hii, Abdallah alipata heshima kubwa mno miongoni mwa marafiki na ndugu zake.

Haihitajiki kusema hapa kwamba pale Abdallah alipokuwa akienda na baba yake kwenye madhabahu ya kudhabihia, alikabiliwa na hisia kali zenye kuipinga azma yake hiyo. Hisia za heshima kwa baba yake na kuzithamini taabu alizozipata kwa ajili yake zikaidhibiti nafsi yake yote, na kwa sababu hiyo, hakuwa na njia yoyote nyingine ila kuitii amri yake. Hata hivyo, kwa upande mwingine kama vile yalivyotaka mamlaka ya takdir kwamba lile ua la majira ya machipuko la maisha yake linyauke kama vile lifanyavyo la majira ya kabla ya baridi, wimbi la ghasia na machafuko liliibuka akilini mwake.

Vilevile Abdul-Muttalib alijikuta akifanya jitihada baina ya nguvu mbili za 'imani'na 'upendo' na bila shaka hali hii ilisababisha mlolongo wa wasiwasi mkali akilini mwao wote.

Hata hivyo, tatizo hili lilipotatuliwa kwa jinsi tuliyoieleza hapo juu, alifikiria kufanya marekebisho kwa ajili ya mihemuko hiyo michungu kwa kumuoza Abdullah kwa Amina haraka sana, na hivyo akayaunga maisha yake, yaliyokwisha kuifikia hatua yake ya kuchoka kabisa kwa uhusiano wa msingi kabisa wa maisha yake mtu.

Hivyo basi, alipokuwa akirudi kutoka kwenye madhabahu ya kudhabihia, Abdul-Muttalib, ambaye bado alikuwa ameushika mkono wa mwanawe, alikwenda moja kwa moja nyumbani kwa Wahab mwana wa Abd Manaf wa kabila la Zuhrah na akaitimiza ndoa ya Bwana Abdullah na binti yake Wahab, Amina, aliyekuwa maarufu kwa utakatifu na adabu. Kwenye mkutano huo huo, yeye (Abdul-Muttalib) mwenyewe alimuoa Dalalah binamu yake Amina, aliyemzaa Hamza, ami na hirimu lake Mtukufu Mtume (s.a.w.w).31

Mwanahistoria wa zama hizi, Abdul Wahaab (Profesa wa historia wa Chuo Kikuu cha Misri, aliyeandika maelezo yenye faida juu ya historia ya Ibn Athir) ameyachukulia maendeleo tuliyoyataja hapo juu kuwa ni jambo lisilo la kawaida na anaandika hivi: "Kitendo ch Abdul-Muttalib kwenda kule nyumbani kwa Wahab siku ileile, (fikara za watu zilipofikia kikomo cha juu zaidi na machozi ya furaha yalikuwa yakitiririka chini ya mashavu yao) na vile vile kwa lengo la kutaka kuwachumbia wasichana wawili – mmoja kwa ajili yake mwenyewe na mwingine kwa ajili ya mwanawe, Abdullah – hakuafikiani na vipimo vya kawaida. Jambo pekee lenye kuwafaa na kuwa stahili ilikuwa ni kujipumzisha, ili kwamba waweze kujitoa uchovu wa kiakili, na kisha wayashughulikie mambo mengine."32

Hata hivyo, tunaamini ya kwamba, kama mwanahistoria huyo tuliyemtaja hapo juu angelichunguza suala hili kwa njia tuliyolitazama sisi, ingalikuwa rahisi mno kwake kulithibitisha tendo lao hili. Abdul-Muttalib aliweka muda wa kukamilisha ndoa hii na kulingana na desturi za Waquraishi, muda uleule ulipofika sherehe za harusi zilifanyika nyumbani kwa Amina. Abdullah na Amina walikaa pamoja kwa muda fulani na kisha Abdullah alisafiri kwenda Sham kwa ajili ya kufanya biashara. Hata hivyo, alipokuwa akirejea alifariki dunia kama tutakavyoeleza kwa kirefu hapa chini.

## Kufariki Dunia Kwa Abdullah Mjini Yathrib

Kwa kufunga ndoa, Abdullah aliufungua ukurasa mpya maishani mwake na nyumba yake iliangazwa

kwa kuwa na mwenzi, ambaye ni Bibi Amina.

Baada ya muda fulani Bwana Abdullah aliondoka kwenda Sham kufanya biashara, akifuatana na msafara uliokuwa ukienda huko kutoka Makkahh. Kengele ya kuondokea iligongwa na ule msafara ukaishika njia yake, ukiyachukua mamia ya nyoyo pamoja nao. Wakati ule Aminah alikuwa mjamzito. Baada miezi michache msafara ule ulirudi Makkahh. Watu kad- haa walitoka nje ya mji kwenda kuwapokea ndugu zao.

Baba mzee wa Bwana Abdullah naye alikuwa pale akimsubiri mwanawe, na macho ya mkewe yenye kudadisi, yalikuwa yakimtafuata miongoni mwa msafara ule, lakini kwa bahati mbaya hakuonekana popote pale. Baada ya kuulizia waligundua ya kwamba Abdullah alipokuwa akirejea kutoka Sham alipatwa na maradhi mjini Yathrib na hivyo basi, alibakia huko akijipumzisha kwa nduguze. Aminah aliposikia hivyo, alihuzunika mno machozi yakamtiririka mashavuni mwake.
Abdul-Muttalib alimtuma mwanawe mkuu, Harith, aende Yathrib akamlete Abdullah. Harith alipofika Yathrib aliambiwa ya kwamba mwezi mmoja tu baada ya kuondoka kwa ule msafara, Abdullah alifariki dunia kutokana na maradhi yale yale ya awali. Harith aliporudi Makkahh, alimpasha habari Abdul-Muttalib pamoja na mjane wa Abdullah yale yaliyotokea. Mali aliyoiacha Bwana Abdullah ilikuwa ni ngamia watano, kundi la kondoo na mjakazi mmoja aliyeitwa Ummi Ayman ambaye baadae alimnyonyesha Mtukufu Mtume (s.a.w.w).

1. Lakini wao walikuwa na wazo lao kuhusu masanamu? Je, waliyafikiria kuwa yanapasika kuabudiwa na kuwa wasila pekee, au walifikiria kwamba wao nao walikuwa na nguvu kama Allah? Jambo hili liko nje ya mazungumzo yetu hivi sasa ingwa maoni ya awali ni thabiti na yenye kuthibitishwa.
2. Lakini wao walikuwa na wazo lao kuhusu masanamu? Je, waliyafikiria kuwa yanapasika kuabudiwa na kuwa wasila pekee, au walifikiria kwamba wao nao walikuwa na nguvu kama Allah? Jambo hili liko nje ya mazungumzo yetu hivi sasa ingwa maoni ya awali ni thabiti na yenye kuthibitishwa.
3. Tafsir-i-Burhan, Juzuu 1, uk. 535.
4. Awa'il al-Maqalat, uk. 12.
5. Majma'ul Bayan, Juzuu 3, uk. 319 na al-Mizan, Juzuu 7, uk. 170.
6. Ama kuhusu maelezo kamili ya sura hii na mambo yahusianayo na kuzaliwa kwa Nabii Ibrahim (a.s.) na kule kuyavunja kwake masanamu, rejea Tarikh-I- Kamil, Uk. 53-62 na Biharul Anwar, Juzuu 12, Uk. 41-55, kwa ajili ya kufupisha maneno hatukuzitaja asili zote za maelezo haya.
7. Biharul Anwar, Juzuu 5, uk. 130, chapa ya 'Company print.'
8. Al-Uyun, uk. 136, Amali Saduq, uk. 274 na Biharul Anwar, uk, 35.
9. Tafsir-i-Burhan, Juzuu 3, uk. 64.
10. Sa'dus Su'ud, uk. 41-42 na Biharul Anwar, Juzuu 12, uk. 118.
11. Tafsiri-I-Qummi, uk. 52; na Bihaarul Anwaar, Juzuu 12, uk. 100.
12. Biharul Anwar, Juzuu 2, uk. 112 kama kilivyonakiliwa kutoka Qassas-i- Anbiya.
13. Tarikh-i-Kaamil, Juzuu 2, uk. 1 na 21.
14. Maisha yao yamezungumziwa na Ibn Athir mwenye Tarikh-i-Kaamil, Juzuu 2, uk. 15-21.
15. Ni ukweli ukubalikao kwamba ofisi zilizohusiana na Al-Ka'ba hazikuwako ilipojengwa hiyo Al-Ka'ba, na zilianzishwa pole pole, kufuatana na mahitaji ya muda. Hadi ulipokuja Uislamu, ofisi hizi ziligawanywa katika sehemu nne: (1) Udhamini wa Al-Ka'ba na kuzishika funguo zake, (2) Kuwapatia maji mahujaji katika nyakati za Hajj, (3) Kuwapatia mahujaji chakula, (4) Uchifu wa watu wa Makkahh, ushika bendera na uamirijeshi wa jeshi.
16. Tarikh-i-Tabari, Juzuu 2, uk. 13.

17. Siirah-i-Halabi, Juzuu 2, uk. 5.

18. Siirahi-i-Halabi, Juzuu 1, uk. 6-7.

19. Tarikh-i-Kaamil, cha Ibn Athir, Juzuu 2, uk. 10.

20. Tarikh-i-Kaamil, Juzuu 2, uk. 6; Tarikh-i-Tabari, Juzuu, uk. 8-9; na Siirah-i-Halabi, Juzuu 1, uk.8

21. Siirah-i-Halabi, Juzuu 1, uk. 4.

22. Moja ya sababu ziiongozeayo jamii kwenye msiba ni kuweko kwa dhambi na uasherati miongoni mwa watu wake na haiyumkini kwamba vitendo viabishavyo vilete njaa na misiba mingineyo mwenye mkondo wao. Dhana hii, achilia mbali kuafikiana kwake na misingi ya kifalsafa, vile vile imetajwa kwa msisitizo mwenye Qur'ani tukufu na mwenye Ahadithi za kiislamu.

23. Hapa swali huibuka ni kwanini wale wengine hawakuja na wazo hili? Inawezekana kwamba wote walikwisha kuyapoteza matumaini ya kupata maji.

24. Tarikh-i-Ya'qubi, Juzuu 1, uk. 206; na Siirah-i-Ibn Hisham Juzuu 1, uk. 45

25. Tukio tulilolitaja hapo juu limesimuliwa na wanahistoria wengi na waandishi wa Siirah (maandiko ya habari za maisha ya mtu). Hadithi hii yastahili kuthamini- wa kwa sababu hii tu kwamba inauainisha ubora wa tabia na umadhubuti wa Abdul-Muttalib na unaeleza dhahiri jinsi alivyokuwa na shauku katika mambo ya dini yake na katika kuzitimiza ahadi zake.

26. Siirah-i-Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 153; na Bihaar, Juzuu 16, uk. 74 – 79.

27. Tarikh-i-Kaamil, Juzuu 1, uk. 253 na kuendelea.

28. Siirah -i-Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 43-62; Fadhaa'il Shazaan, uk. 52-64; Bihaarul Anwaar, Juzuu 15, uk. 146-155; na Tarikh-i- Kaamil, Juzuu 1, uk. 260-263.

29. Tarikh-i-Kaamil, Juzuu 1, uk. 263.

30. Tarikh-i-Kaamil, cha Ibn Athir, Juzuu 1, uk. 266.

31. Tarikh-i-Tabari, Juzuu 2, uk. 4, na Siirah-i-Halabi, Juzuu 1, uk. 54.

32. Tarikh-i-Ibn Athir, Juzuu 2, uk. 4 – sehemu ya maelezo ya chini ya ukurasa

# Sura Ya Tano: Kuzaliwa Kwa Mtukufu Mtume (S.A.W.W)

Wingu jeusi la ujinga lilifunika kabisa Rasi ya Uarabu. Matendo yachuk- izayo na haramu, kama vile kampeni ya umwagaji wa damu unyang'anyi ulioenea kote kote na uuaji wa watoto wachanga vimeyaharibu maadili mema yote, na kuiweka jamii ya kiarabu kwenye mwinamo. Umbali baina ya uhai na vifo vyao umekuwa mfupi mno. Katika wakati huu huu nyota ya alfajiri ya ustawi ikajitokeza na ile hali ya hewa ya giza iliangazwa kwa kheri ya kuzaliwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Hivyo basi, hatua ya awali ya kuelekea kwenye msingi wa ustaarabu na maendeleo na ustawi wa taifa lililokuwa nyuma ulifikiwa. Mara miali ya nuru hii iliangaza ulimwengu mzima na msingi wa elimu, hekima na ustaarabu ukawekwa.

Kila ukurasa wa maisha ya watu wakubwa unafaa kujifunza na kuchun- guza. Wakati mwingine nafsi ya mtu huwa kubwa na kuu sana kiasi kwam- ba awamu zote za maisha yake, hata uchangani na utotoni mwake huwa siri. Maisha ya watu mastadi, viongozi wa jamii na watangulizi wa msafara wa ustaarabu, kwa kawaida ni yenye kuvutia na yana awamu zilizo nyeti na za kustaajabisha. Tangu kwenye susu hadi

kaburini, maisha yao yamejaa siri. Tunasoma juu ya watu wakuu kwamba vipindi vya utotoni na ujanani mwao ni vyenye kuvutia na vya kimiujiza. Na kama tunaikubali alama hii kuhusiana na watu wakuu wa ulimwenguni hapa, kukikubali kitu kifananacho na hivyo kuhusiana na Mitume na mawalii huwa rahisi mno.

Taurat na Qur'ani vimeyaelezea maisha ya utotoni ya Nabii Musa (a.s.) kuwa ni siri kubwa, na kusema: "Mamia ya watoto wasio na hatia walikatwa vichwa kwa lengo la kwamba Nabii Musa (a.s.) asizaliwe. Hata hivyo, kwa kuwa Allah Alipenda kwamba Nabii Musa (a.s.) ajitokeze ulimwenguni, ilitokea kwamba sio tu kwamba maadui zake hawakuweza kumdhuru, lakini hata Firauni, adui yake mkuu, mwenyewe akawa mlezi na msaidizi wake; Qur'ani Tukufu inasema:

{إِذْ أَوْحَيْنَا إِلَىٰ أُمِّكَ مَا يُوحَىٰ {38

أَنِ اقْذِفِيهِ فِي التَّابُوتِ فَاقْذِفِيهِ فِي الْيَمِّ فَلْيُلْقِهِ الْيَمُّ بِالسَّاحِلِ يَأْخُذْهُ عَدُوٌّ لِي وَعَدُوٌّ لَهُ ۚ وَأَلْقَيْتُ عَلَيْكَ مَحَبَّةً مِنِّي
{وَلِتُصْنَعَ عَلَىٰ عَيْنِي {39

إِذْ تَمْشِي أُخْتُكَ فَتَقُولُ هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ مَنْ يَكْفُلُهُ ۖ فَرَجَعْنَاكَ إِلَىٰ أُمِّكَ كَيْ تَقَرَّ عَيْنُهَا وَلَا تَحْزَنَ ۚ وَقَتَلْتَ نَفْسًا فَنَجَّيْنَاكَ
{مِنَ الْغَمِّ وَفَتَنَّاكَ فُتُونًا ۚ فَلَبِثْتَ سِنِينَ فِي أَهْلِ مَدْيَنَ ثُمَّ جِئْتَ عَلَىٰ قَدَرٍ يَا مُوسَىٰ {40

***"Tulimfunulia mama yake Musa mapenzi yetu, ya kwamba: 'Mtie sandukuni mtoto wako kisha litie mtoni na mto*** (***utamchukua na***) ***utamtupa ufukoni kwa usalama, ili amchukue*** (***yule aliye***) ***adui Yangu na adui yake. Na ninakupa huba itokayo kwangu na ili ulelewe machoni pangu.' Dada yake Musa alikwenda nyumbani kwa Firauni na akasema: "Je, nikuletee*** (***mtu***) ***atakaye mlea?" Basi mama yake Musa aliajiriwa kumlea mtoto yule na hivyo mwanawe akarejeshwa kwake!"*** (***Surah Twaahaa, 20:38-40***)

Kipindi cha ujauzito, kuzaliwa na kulelewa kwa Nabii Isa (a.s.) kilikuwa chenye kustaajabisha zaidi ya kile cha Nabii Musa (a.s.).
Qur'ani Tukufu inakisimulia kipindi cha kukua kwa Nabii Isa, hivi:

{فَاتَّخَذَتْ مِنْ دُونِهِمْ حِجَابًا فَأَرْسَلْنَا إِلَيْهَا رُوحَنَا فَتَمَثَّلَ لَهَا بَشَرًا سَوِيًّا {17

{قَالَتْ إِنِّي أَعُوذُ بِالرَّحْمَٰنِ مِنْكَ إِنْ كُنْتَ تَقِيًّا {18

{قَالَ إِنَّمَا أَنَا رَسُولُ رَبِّكِ لِأَهَبَ لَكِ غُلَامًا زَكِيًّا {19

{قَالَتْ أَنَّىٰ يَكُونُ لِي غُلَامٌ وَلَمْ يَمْسَسْنِي بَشَرٌ وَلَمْ أَكُ بَغِيًّا {20

{قَالَ كَذَٰلِكِ قَالَ رَبُّكِ هُوَ عَلَيَّ هَيِّنٌ ۖ وَلِنَجْعَلَهُ آيَةً لِلنَّاسِ وَرَحْمَةً مِنَّا ۚ وَكَانَ أَمْرًا مَقْضِيًّا {21

{فَحَمَلَتْهُ فَانْتَبَذَتْ بِهِ مَكَانًا قَصِيًّا {22

{فَأَجَاءَهَا الْمَخَاضُ إِلَىٰ جِذْعِ النَّخْلَةِ قَالَتْ يَا لَيْتَنِي مِتُّ قَبْلَ هَٰذَا وَكُنْتُ نَسْيًا مَنْسِيًّا {23

{فَنَادَاهَا مِنْ تَحْتِهَا أَلَّا تَحْزَنِي قَدْ جَعَلَ رَبُّكِ تَحْتَكِ سَرِيًّا {24

{وَهُزِّي إِلَيْكِ بِجِذْعِ النَّخْلَةِ تُسَاقِطْ عَلَيْكِ رُطَبًا جَنِيًّا {25

{فَكُلِي وَاشْرَبِي وَقَرِّي عَيْنًا ۖ فَإِمَّا تَرَيِنَّ مِنَ الْبَشَرِ أَحَدًا فَقُولِي إِنِّي نَذَرْتُ لِلرَّحْمَٰنِ صَوْمًا فَلَنْ أُكَلِّمَ الْيَوْمَ إِنْسِيًّا {26

{فَأَتَتْ بِهِ قَوْمَهَا تَحْمِلُهُ ۖ قَالُوا يَا مَرْيَمُ لَقَدْ جِئْتِ شَيْئًا فَرِيًّا {27

{يَا أُخْتَ هَارُونَ مَا كَانَ أَبُوكِ امْرَأَ سَوْءٍ وَمَا كَانَتْ أُمُّكِ بَغِيًّا {28

{فَأَشَارَتْ إِلَيْهِ ۖ قَالُوا كَيْفَ نُكَلِّمُ مَنْ كَانَ فِي الْمَهْدِ صَبِيًّا {29

{قَالَ إِنِّي عَبْدُ اللَّهِ آتَانِيَ الْكِتَابَ وَجَعَلَنِي نَبِيًّا {30

***“……., Kisha Tukampelekea*** (***Mariamu***) ***Roho wetu*** (***yaani Malaika Mkuu Jibrili***) ***aliyejimithilisha kwake*** (***na***) ***mwanaume kamili*** (***katika maumbile***). ***Na*** (***Mariamu***) ***akasema: “Hakika mimi ninajikinga kwa Allah Mwingi wa rehema kutokana nawe*** (***basi niondokee***) ***ikiwa unamuogopa Mwenyezi Mungu”*** (***Yule Malaika***) ***akasema: “Hakika mimi ni mjumbe wa Mola wako*** (***niliyetumwa***) ***ili nikupe*** (***bishara ya***) ***mwana mtakatifu.” Mariamu akasema: “Ninawezaje kumpata mwana hali*** (***Mimi ni Bikira***) ***hajanigusa mwanaume yeyote*** (***yule***) ***wala mimi si mwasherati?” Yule malaika akasema: “Itakuwa hivyo, anasema Mola Wako: “Haya ni rahisi Kwangu, na ili kwamba Tumfanye***

***Ishara kwa wanadamu na rehema itokayo Kwetu na hilo ni jambo lililokwisha hukumiwa."***

***"Pale pale akatunga mimba na akajitenga na watu, akaenda kukaa kwenye sehemu ya mbali. Na alipopata uchungu wa kuzaa, alilala kwenye shina la mtende; akasema kwa sauti kuu: "Laiti ningalikufa kabla ya haya na nikawa kitu kilichosahauliwa kabisa." Mara (sauti ya mtoto ) ikamwita kutoka chini yake ikisema: "Usihuzunike, hakika Mola Wako amejaalia (kutiririka) kijito chini yako, na kama ukitikisa hili shina la mtende, litakudondoshea tende zilizo nzuri (na) mbivu.***

***Hivyo basi, ufurahi, ule na unywe na uburudishe macho, na kama ukimwona mtu yeyote umwambie: "Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa (Allah) Mwingi wa rehema ya kufunga saumu hivyo katu leo sitazungumza na mtu yeyote."***

***"Kisha akamleta (mtoto Isa) kwenye kaumu yake akimpakata; wakasema: "Ewe Maryam, hakika umeleta kioja! Ewe dada yake Harun! Baba yako hakuwa mtu mbaya, wala mama yako hakuwa mwasherati. Lakini (Maryam) akaashiria kwake (mtoto Isa); wakasema: "Tuzungumze na aliye (bado yu) mtoto wa kwenye mahdi (susu)? (Isa) akasema: "Hakika Mimi ni mja wa Allah; Amenipa kitabu (Injili) na Amenifanya Nabii."***
***(Surah Maryam, 19:17-30)***

Waumini wa Qur'ani Tukufu na Torati na wafuasi wa Nabii Isa (a.s.) watakapouthibitisha ukweli tulioutaja hapo juu unaohusu kuzaliwa kwa Mitume hao wawili, hawatakuwa na haja ya kuyastaajabia matukio yasiyo kifani yaliyofuatia kwenye heri za kuzaliwa kwa Mtukufu wa Uislamu (s.a.w.w.) na hawana hoja ya kuyachukulia kuwa ni jambo la kupurukusha.
Tumejifunza kutokana na vitabu vya historia na Hadithi kwamba wakati wa kuzaliwa kwake Mtume (s.a.w.w) kuta za Ikulu ya Makhosro zilikatika na baadhi ya minara ikaanguka. Moto wa hekalu la moto wa Uajemi ulizimika. Ziwa la Sawah lilikauka. Masanamu yaliyokuwamo mwenye Haramu ya Makkahh yaligeuka chini juu.

Nuru ilishuka kutoka mwilini mwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) ikielekea mbinguni na ikauangaza umbali wa ligi (au kilometa) nyingi kwenye njia yake. Anushirwan na Makasisi wa Kimajusi waliota ndoto itishayo mno.

Alipozaliwa Mtume (s.a.w.w) alikuwa tayari kaishatahiriwa na kitovu kilishakatwa. Alipofika hapa ulimwenguni alisema: "Allah Yu Mkubwa na sifa zote njema zamstahiki Yeye tu, Naye Yu mwenye kusifiwa mchana na usiku."

Maelezo yote haya yameelezwa kwenye taarifa za kihistoria zikubaliwazo na watu wote na kwenye vitabu vya hadith.[1] Na tukizirudia habari zihusianazo na Nabii Musa (a.s.) na Nabii Isa (a.s.)' ambazo tumezitaja hapo juu, hakuna haki ya kusita katika kuyakubali matukio haya.

## Mwaka, Mwezi Na Tarehe Ya Kuzaliwa Kwa Mtume Wa Uislamu (S.A.W.W)

Kwa kawaida waandishi wa Siirah/wasifu wa maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wanakubaliana kwamba Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) alizaliwa mnamo 'mwaka wa ndovu' mwaka wa 570 Masihiya. Kwa kuwa ni dhahiri kwamba alifariki dunia mnamo mwaka wa 632 Masihiya, alipokuwa na umri wa miaka 62–63, mwaka wa kuzaliwa kwake hauna budi kwamba ulikuwa ni 570 Masihiya.

Karibuni waandishi wa Hadithi na Historia wote wanakubaliana kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alizaliwa kwenye mwezi wa Rabi'ul Awwal (mfunguo sita) lakini wanatofautiana kuhusiana na tarehe ya kuzaliwa kwake. Inafahamika vema miongoni mwa waandishi wa Hadithi wa Kishi'ah kwamba alizaliwa baada ya kuchomoza kwa jua, mnamo siku ya Ijumaa, tarehe 17 ya Rabi'ul Awwal, ambapo wanachuoni wa Kisunni wanaitakidi kwamba kuzaliwa kwake kulitokea mnamo tarehe 12 ya mwezi ule, siku ya Jumatatu.[2]

## Ni Taarifa Ipi Sahihi Kati Ya Hizi Mbili?

Ni jambo la kusikitisha mno kwamba Waislamu hawana taarifa zikuba- likazo juu ya tarehe ya kuzaliwa na kufa kwa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w), na kusema kweli, juu ya wengi wa viongozi wa kidini, na kuhusiana na shaka hii, nyingi za sherehe za kuzaliwa kwao na kumbukumbu za vifo vyao, hazifanyiki katika mtazamo wa kihistoria.

Ingawa wanachuoni wa kiislamu wameyaandika matukio mbalimbali ya kihitoria ya kiislamu, kwa utaratibu mwema, haifahamiki ni kwa nini tarehe za kuzaliwa na kufa za wengi wa viongozi wa Kidini hazikuandikwa baada ya uchunguzi makini.

Hata hivyo, tatizo hili hutatuka kwa kiasi fulani. Kuhusiana na jambo hili, hebu na tuchukue mfano mmoja.

Kama utataka kuandika maisha ya mwanachuoni wa mji fulani na tufikirie kwamba mwanachuoni huyu ameacha watoto na karaba zake wengine kadhaa, utataka kuulizia juu ya maelezo marefu ya maisha yake kutoka kwa wageni au kutoka kwa marafiki zake na watu wamjuao, ingawa wapo watoto wake na watu wengineo wa familia yake, ambao kwa kawaida wao wanazo taarifa kamili za kina na ujuzi sahihi juu ya maisha yake? Ni dhahiri kwamba dhamira yako haitakuruhusu kufanya hivyo.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) aliondoka kutoka miongoni mwa watu na akaacha nyuma yake familia na watoto wake. Hawa jamaa zake Mtume (s.a.w.w) wanasema: "Kama Mjumbe wa Allah yu baba yetu mpendwa na sisi tumelelewa nyumbani mwake, na chini ya uongozi wake, tunasema kwamba kiongozi wa familia yetu alikuja ulimwenguni humu katika tare- he hii na aliondoka mnamo tarehe hiii." Je, katika hali hii, inaruhusiwa kwetu kuyabana maneno ya watoto wake na kuzitegemea taarifa za watu wengine?

## Sherehe Ya Kumpa Jina Mtukufu Mtume Wa Uislamu (S.A.W.W)

Siku ya saba iliwadia. Abdul-Muttalib alichinja kondoo ili kudhihirisha shukrani yake kwa Allah na watu walialikwa kwenye sherehe ile kuu, iliy- ohudhuriwa na wengi wa Waquraishi, alimpa mjukuu wake jina la 'Muhammad.' Alipoulizwa ni kwa nini alimpa mjukuu wake huyo jina hili kwani halikuwa maarufu miongoni mwa Waarabu, alijibu hivi:

"Nilipenda kwamba asifiwe huko mbinguni na hapa duniani." Mwanachuoni Hassan Thabit, akilizungumzia jambo hili anasema hivi: "Muumba Alilitoa jina la Mtukufu Mtume wake kutokana na jina Lake Mwenyewe. Kwa sababu hiyo, kwa vile Allah ni 'Mahamud' (mwenye kustahiki sifa) Mtume Wake naye yu 'Muhammad' (mwenye kusifiwa). Maneno yote mawili yame- tokaka na asili moja na yana maana moja."[3]

Ni dhahiri kwamba maongezi ya siri yalihusika katika uchaguzi wa jina hili, kwa sababu ingawa jina la 'Muhammad' lilifahamika vizuri miongoni mwa Waarabu kabla ya hapo, ni watu wachache mno waliopewa jina hili. Kufuatana na hesabu sahihi, walizozikusanya baadhi ya wanahistoria, ni watu kumi na sita tu waliopewa jina hili kabla ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).[4]

Si lazima kueleza hapa kwamba jinsi neno litumikavyo kwa uchache ndivyo nafasi ya kutoelewana juu yake itakavyokuwa ndogo. Kwa kuwa Vitabu vya Mbinguni vimetabiri kuja kwa Uislamu na jina, mambo, dalili za kiroho na kimwili za Mtume (s.a.w.w), ililazimu kwamba dalili zake ziwe za dhahiri mno kiasi kwamba suala la kukosea kokote kule lisijitokeze.

Moja ya dalili hizi ilikuwa ni lile jina la Mtume (s.a.w.w.) na ililazimu kwamba jina hili liwe na watu wachache tu kiasi kwamba isiwepo shaka yoyote juu ya kumtambua, hasa pale sifa na dalili zake zitakapoam- batana na jina hilo. Kwa njia hii, yule mtu ambaye kuja kwake kumetabiri- wa na Torati na Injili atambulike kwa urahisi.

Qur'ani imeyataja majina mawili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w).[5] Katika *Suratul-Muhammad* aya ya 2, *Suratul-Fat-ha* aya ya 29, na *Surah al-Ahzab* aya ya 40, ameitwa '**Muhammad**' na kwenye *Surah al-Saff* aya ya 6 ameitwa '**Ahmad**' sababu ya tofauti hii ni kwamba, kama ilivyoelezwa kwenye historia, mama yake Mtume (s.a.w.w) alimwita 'Ahmad' kabla ya babu yake kumpa jina la 'Muhammad'[6].

## Mtukufu Mtume (S.A.W.W) Wakati Akiwa Mtoto Mchanga

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alinyonyeshwa na mama yake kwa siku tatu tu! Baada ya hapo wanawake wawili walipata heshima ya kuwa mama zake Mtume (s.a.w.w) wa kumnyonyesha.

**Suwaybah:** Bibi huyu alikuwa mjakazi wa Abu Lahab. Bibi huyu alimnyonyesha Mtume kwa kipindi cha miezi minne na akabakia kuwa kilengwa cha kuthaminiwa na Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe, na vile vile mkewe mwema (bibi Khadija a.s) kwa kipindi chote cha uhai wake.

Hapo kabla, bibi huyu alimnyonyesha Bwama Hamza, ami yake Mtume (s.a.w.w.) pia. Baada ya Mtume (s.a.w.w.) kuianza kazi yake ya utume alidhamiria kumnunua bibi huyu na akamtumia mtu Abu Lahabi, lakini alikataa kumwuza. Hata hivyo, bibi huyu alipata msaada kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) na ali-porejea kutoka kwenye vita ya Khaybar, alipata taarifa za kifo cha bibi huyu na dalili za huzuni zilijidhihirisha usoni mwake. Aliulizia kuhusu mwanawe ili kwamba amfanyie lolote lililo jema kwake, lakini aliambiwa kwamba alifariki dunia mapema kabla ya mama yake.

**Halimah:** Bibi huyu alikuwa binti wa Abi Zuwayb na alitokana na kabila la Sa'ad bin Bakr bin Hawaazan. Bibi huyu alikuwa na watoto watatu, ambao ni Abdillah, Anisah na Shima. Huyu wa mwisho pia alimhudumia Mtume (s.a.w.w). Ilikuwa ni desturi ya familia tukufu miongoni mwa Waarabu kwamba waliwapeleka watoto wao kwa wanyonyeshaji. Kwa kawaida wanyonyeshaji hawa waliishi kwenye sehemu za nje ya mji ili kwamba watoto hao waweze kulelewa kwenye hewa safi ya jangwani na ili waweze kukaa wakiwa na nguvu na wenye afya.

Kwa bahati, wakati wakiishi huko jangwani, waliweza kuwa na kinga ya magonjwa ya kuambukiza ya mjini Makkah yaliyokuwa hatari kwa watoto wachanga, na vilevile walijifunza lugha ya kiarabu kwenye sehemu isiyoathiriwa na mageuzi mabaya. Wanyonyeshaji waliotokana na kabila la Bani Sa'ad walikuwa maarufu sehemu hii. Walikuja mjini Makkah nyakati maalum za mwaka na kila mmoja wao alichukua mtoto mchanga. Ilipopita miezi minne tangu kuzaliwa kwa Mtume (s.a.w.w) wanyonyeshaji wa kabila la Bani Sa'ad walikuja mjini Makkah. Katika mwaka ule walikuwa na njaa kali na hivyo basi, walihitaji sana msaada kutoka kwa wenye familia tukufu.

Huyu mtoto mchanga wa Kiquraishi (Mtume (s.a.w.w.) hakunyonya ziwa la myonyeshaji yeyote. Mwishowe alikuja Bibi Halima na yule mtoto akakubali. Wakati huu familia ya Abdul-Muttalib ilifurahi sana.[7] Abdul- Muttalib alimgeukia Bibi Halima na kumwuliza: "Wewe u wa kabila gani?" Akamjibu ya kwamba alikuwa wa kabila la Bani Sa'ad.

Kisha Abdul-Muttalib alimuliza jina lake na akamuambia kuwa anaitwa Halima. Abdul-Muttalib alifurahi sana alipolisikia jina lake na lile la kabila lake na akamjibu: "Vizuri sana! Tabia njema mbili na sifa njema mbili. Mojawapo ni furaha na ustawi na nyingine ni upole na subra.[8]

1. Tarikh-i Ya'qubi, Juzuu 2, uk. 5; Bihaarul Anmaar, Juz. 15, sura 3, uk. 231-248; na Siirah-I Halabi, Juz. 1,uk. 64.
2. Mwanachuoni, Bwana Miqrizi amezikusanya taarifa zote zihusuzo siku, mwezi na mwaka wa kuzaliwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w) kwenye kitabu chake kiitwacho al-Amta' (Ukurasa wa 3).
3. Siirah-i Halabi, Juzuu 1, uk. 93.
4. Mudrak Pesh, Juzuu 1, uk. 97.
5. Ama kuhusu maneno 'Twaha' na 'Yasin' baadhi ya wanachuoni wanaamini yakwamba ni 'Muqatta' (ufupisho) wa herufi za Qur'ani tukufu wala si majina ya Mtukufu Mtume (s.a.w).
6. Siirah-i-Halabi, Juzuu ya 1, uk. 93.
7. Bihaarul Anwaar, Juzuu 15, uk. 442.
8. Siirah-i-Halabi, Juzuu 1, uk, 106.

# Sura Ya Sita: Utotoni Mwa Mtukufu Mtume (S.A.W.W)

Historia inatuambia kwamba maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yule kiongozi mtukufu wa waislamu yalijaa wingi wa matukio ya ajabu tangu utotoni mwake hadi kwenye kipindi cha kupewa kazi ya Utume, na matendo yote haya yalikuwa na hali ya ukuu. Kwa ujumla matukio haya yalithibitisha ya kwamba maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hayakuwa ya kawaida.

Ama kuhusu maelezo ya matukio haya, waandishi wamegawanyika makundi mawili, watu wa kimaada na idadi ya mustashirik.

Wanachuo wakimaada (*materialist*) ambao huuangalia ulimwengu kwa mtazamo wa kimaada na huufikiria utaratibu wa maisha kuwa umo ndani ya kuta nne za maada na wanaoitakidi kwamba mambo yote ni ya kimaada na hutegemea visababisho vya kimaada, nao hawayapi matukio haya muhimu wowote na hata matukio haya yaungwe mkono na ushahidi wenye nguvu zaidi, hawayasikilizi. Sababu ya msimamo wao huu ni kwamba, kwa mujibu wa kanuni za maada kutokea kwa matukio ya aina hii ni jambo lisilowezekana.

Hivyo basi, wanapoyaona matukio hayo yakiwa yamehifadhiwa kwenye historia, wanayahukumu kwamba ni kizazi cha dhana, huba na kuabudu kwa wafuasi wa dini maalum.

Vile vile liko kundi la mustashirik (*orientalists*), ambao kwa dhahiri hujionyesha kuwa wao ni wenye kumwamini Mungu na wachamungu na huidhihirisha itikadi yao juu ya nguvu kuu, lakini kutokana na unyonge wa itikadi yao, kiburi chao juu ya elimu yao na shinikizo la maada katika mawazo yao, wanapoyachambua matukio, huzifuata kanuni za maada. Katika mazunumzo yao mara kwa mara huikuta sentensi hii: "Utume ni hali ya kuwa mwanaadamu mwenye kipaji. Mtume ni mwenye kipaji cha kijamii aiangazaye njia ya maisha ya wanadamu kwa fikra zake nzuri n.k..."

Mazungumzo ya aina hii hutokana na fikra za kimaada zenye kuchukulia kwamba dini zote ni matokeo ya fikara za mwanaadamu, ingawa wanachuoni wa mafundisho ya dini, wanapozungumzia utume wa ujumla, wamethibitisha kwamba utume ni zawadi itokayo kwa Mungu ambayo ni chanzo cha mfumo wa kiroho na uhusiano, na haipatikani faida japo iliyo ndogo mno kwa upande huu (yaani wa mitume) ila pale tu uwapo uenezaji (wa taarifa ) kutoka upande wa Mwenyezi Mungu.

Hata hivyo, mustashirik wa Kikiristo kwa huyaangalia mambo haya kwa mtazamo wa kiulimwengu, na wanataka kuyapima matukio yote kulingana na misingi ya kisayansi, iliyogundulika kwa kuzipitia njia za majaribio, huyalaumu matukio yote yenye hali ya kiroho na huukana ukweli wake.

## Wenye Kumuabudu Allah

Hawa ni wale watu walioamini kwamba sifa na muundo wa ulimwengu huu wa kidunia viko chini ya utawala wa ulimwengu mwingineo na nguvu nyingine (ulimwengu wa faragha na asili ya uhai), na kwamba ulimwengu huo ndio wenye madaraka ya utaratibu huu ulioko kwenye huu ulimwengu wa kimaada (kidunia) ambao si huru na si wenye kujitegemea, na kwamba hizi taratibu zake zilizomo humu na kanuni zake za kimaumbile na za kisayansi zinaendeshwa na ulimwengu mwingine ambao ni mapenzi ya Muumba yanayozunguka vitu vyote vilivyoko. Yeye (Muumba) ndiye aliyeumba maada (matter) na kuweka kanuni madhubuti miongoni mwa michanganyiko yake na akaisimamisha kwenye msingi wa nyororo ya misingi ya kimaumbile na kisayansi.

Pamoja na kuziamini kanuni za kisayansi, na kuyakubali maneno ya wanachuoni kwa moyo wote juu ya uhusiano wa kimaumbile wa kimaada kwa kiasi ambacho zimethibitishwa na sayansi. Vile vile watu wa kundi hili wanaamini ya kwamba hizi kanuni na misingi ya kisayansi na utarati- bu upendezao mno wa ulimwengu huu wa kimaada vimeungana na mpan- go mwingine, ambao sehemu zake zote huzunguka kutegemeana na mapenzi ya Asili kuu. Aidha, hawazichukulii hizi kanuni za kisayansi kuwa ni za kudumu na zisizoweza kubadilishwa na wanaamini kwamba nguvu iliyo hadhiri daima inaweza kuzibadili wakati wowote ule inapopenda, ili kuweza kulifikia lengo maalum. Inao uweza wa kufanya hivyo na (wala sio tu kwamba inao uwezo, bali) kwa hakika ishafanya hivyo kwenye nyakati nyingi kwa ajili ya kuyafikia malengo ya aina hiyo kwa kadri ilivyotaka.

Wanasema kwamba matendo ya kiroho na yenye kustaajabisha, ya Mitume, yasiyolandana na kanuni za kimaumbile yameundwa kwa kupitia njia hii. Watu hawa hawajiruhusu pasipo haki kukana au kutilia shaka yale wayaonayo kwenye Qur'ani Tukufu na kwenye Hadith na pia vitabu vya historia vikubaliwavyo na kutegemewa kwa sababu tu kwamba, haiafikiani na kipimo cha maumbile na kanuni za kisayansi. Sasa tunayataja matukio mawili yatokayo katika siri na maajabu ya maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yakihusuyo kipindi cha utotoni mwake na masimulizi haya yanapozingatiwa, haitakuwapo nafasi yoyote ya kutowezekana au shaka juu yao.

Wanahistoria wamemnukuu Bibi Halima akisema: “Nilipolitwaa jukumu la kumlea mtoto mchanga wa Aminah niliamua kumnyonyesha maziwa yangu kwenye mkutano uleule na mbele ya mama yake. Hivyo nika- muwekea kinywani mwake ziwa langu la kushoto lililokuwa na maziwa, lakini mtoto yuke alilielekea zaidi ziwa langu la kulia. Hata hivyo, sikupa- ta kuwa na maziwa kwenye ziwa langu la kulia tangu nimzae mwanangu wa kwanza. Kufanya kwake vile kulinifanya nimwekee ziwa la kulia lisilo na maziwa kinywani mwake, na mara tu alipoanza kunyonya, lilijaa maziwa na tukio hili liliwashangaza wale wote waliokuwapo pale.[1]

Vilevile Bibi huyu amesema: “Tangu siku ile nilipomchukua Muhammad na kwenda naye nyumbani kwangu, nilipata ustawi (wa kimaisha) zaidi na utajiri na mifugo yangu ilizidi.”[2]

Bila shaka kwenye mambo haya hukumu ya watu wenye itikadi ya kimaada na wafuasi wao hutofautiana

na ile ya wale wamuabuduo Allah, ingawa hakuna hata mmoja wao aliye yachunguza matukio haya, na ushuhuda pekee walio nao ni kauli ya yaya wake Mtume (s.a.w.w.).
Kwa kuwa wale wafuatao kanuni za kimaada hawawezi kuyaeleza matukio haya kwa njia ya kimaumbile, mara moja husema tu kwamba matukio haya ni sanaa ya dhana. Kama wakiwa na heshima zaidi husema kwamba Mtume wa Uislam hakuwa na haja ya miujiza ya aina hiyo.

Hakuna shaka yoyote juu ya ukweli uliopo kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuwa na haja ya miujiza hii, lakini kutokuhitaji kitu ni jambo lililo tofauti kabisa na hukumu ya ukweli au uongo wake.

Hata hivyo, mtu mcha Mungu, huvichukulia viumbe vya ulimwengu kuwa huzidiwa nguvu na kutiishwa na Mapenzi ya Muumba wa huu ulimwengu, na huamini ya kwamba ulimwengu wote, ikiwa ni pamoja na wale viumbe wadogo (yaani ile chembe ndogo sana *atoms*) na vitu vikubwa zaidi (yaani *Milkyway*, au kilimia)[3] huzunguka kufuatana na mpango na utawala wake (Muumba).

Baada ya kujifunza matukio haya na dalili zao zinazoyaunga mkono, huyatazama matukio yote haya kwa heshima ipasikayo, na japo asitosheke, hayakatai moja kwa moja.

Katika Qur'ani Tukufu tunaliona tukio lililo mfano wa haya linalomhusu Bibi Maryam (mama wa Nabii Isa (a.s.) ambaye kuhusiana naye, Qur'ani Tukufu inasema:

"Na muda wa Mariamu kumzaa mtoto ulipokaribia, alilala kwenye shina la mtende na (kwa sababu ya uchungu wa kuzaa, upweke na hofu ya kulaumiwa) alimwomba Allah kifo.
Wakati huu alisikia sauti ikisema:

{فَأَجَاءَهَا الْمَخَاضُ إِلَىٰ جِذْعِ النَّخْلَةِ قَالَتْ يَا لَيْتَنِي مِتُّ قَبْلَ هَٰذَا وَكُنْتُ نَسْيًا مَنْسِيًّا {23

{فَنَادَاهَا مِنْ تَحْتِهَا أَلَّا تَحْزَنِي قَدْ جَعَلَ رَبُّكِ تَحْتَكِ سَرِيًّا {24

{وَهُزِّي إِلَيْكِ بِجِذْعِ النَّخْلَةِ تُسَاقِطْ عَلَيْكِ رُطَبًا جَنِيًّا {25

***"Usihuzunike. Mola wako amekujaalia kijito kitiririkacho chini ya miguu yako na kama ukilitikisa hili shina la mtende (lililokauka), litakudondoshea nyongani mwako tende nzuri na mbivu. (Sura Maryam 19:23-25).***

Ingawa kuna tofauti kubwa baina ya Maryam na Halima kuhusiana na vyeo na uchamungu wao, lakini vile vile ipo tofauti baina ya watoto hao wawili (Mtume s.a.w.w. na Nabii Isa a.s). Na kama sifa na fadhila za kibinafsi za Bibi Mariam zilimfanya azistahili baraka za Allah, basi vile vile inawezekana kwamba cheo na daraja ambalo mtoto huyu (yaani Muhammad) atalipata hapo baadae vitamfanya yaya wake astahiki baraka za Allah.

Vile vile tunajifunza jambo jingine zaidi kuhusiana na Bibi Mariam kutoka kwenye Qur'ani Tukufu: "Utakatifu na uchamungu wake (Mariam) vimemkweza mno daraja kiasi kwamba kila Zakaria alipoingia sehemu yake ya ibada alikikuta chakula kitokacho mbinguni, na kila alipomuuliza kinakotoka chakula kile, alikuwa akijibu kwamba kinatoka kwa Allah." (**Surah Aali Imran, 3:35**).

Chini ya msingi huu hatuna haja ya kutia shaka kuhusu usahihi wa miujiza hii au kuifikiria kwamba ni mambo yasiyowezekana.

## Miaka Mitano Ya Jangwani

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) aliitumia miaka mitano akiwa miongoni mwa watu wa kabila la Banu Sa'ad na akawa mtu wa makamo yatoshelezayo. Mnamo kipindi hiki Bibi Halimah alimpeleka Mtume (s.a.w.w), kwa mama yake mara mbili au tatu hivi na mwishowe akamrudisha kabisa.

Mara ya kwanza Bibi Halima alimrudisha kwa mama yake kilipomalizika kipindi cha kunyonyeshwa. Hata hivyo, bibi Halima alisisitiza kwamba apewe tena mtoto yule. Sababu ya msisitizo wake ule ilikuwa kwamba mtoto huyu amekuwa chanzo cha baraka alizozipata, na sababu za mama mtoto (Bibi Amina) kulikubalia ombi la bibi Halima ilikuwa wakati ule maradhi ya kipindupindu yaliukumba mji wa Makkah.

Mara ya pili ilikuwa wakati kikundi cha makasisi wa Kihabeshi walipokuja Hijaz na kumwona Mtume Muhammad miongoni mwa watu wa kabila la Banu Sa'ad. Viongozi wale waliona kwamba ishara zote za Mtume atakayekuja baada ya Nabiii Isa (a.s.), kama zilivyotabiriwa kwenye vitabu vya mbinguni alikuwa nazo mtoto huyu. Hivyo basi, waliamua kumkama- ta kwa njia yoyote ile watakayoiweza, na kumpeleka Ethiopia, ili kwamba ile heshima ya kuwa naye Mtume yule iangukie nchini mwao.[4]

Jambo hili si lenye kutokuwezekana hata kidogo, kwa sababu kama ilivy- oelezwa kwa dhahiri katika Qur'ani Tukufu, ishara za Mtume wa Waislamu (s.a.w.w.) zimeelezwa katika Injili. Hivyo basi, ilikuwa sahihi kabisa kwamba wataalamu wa zama zile waliweza kumtambua mtu aliye na ishara zile. Kuhusiana na jambo hili, Qur'ani Tukufu inasema:

وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ يَا بَنِي إِسْرَائِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ التَّوْرَاةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي
{مِنْ بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدُ ۖ فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَٰذَا سِحْرٌ مُبِينٌ 6}

***"Na aliposema Isa bin Mariam: 'Enyi wana wa Israeli! Hakika mimi ni Rasuli wa Allah kwenu, nisadikishaye yaliyo mbele yangu katika Taurati na kumbashiria Mtume atakayekuja baada yangu jina lake ni Ahmad,' lakini alipowafikia (yule Mtume aliyebashiriwa na Isa) na bayana, wakasema: 'huu ni uchawi wa dhahiri'" (Sura al-Saff, 61:6)***

Vile vile ziko aya zionyeshazo kwamba ishara za Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) zilielezwa katika vitabu vya mbinguni na watu wa kale walikuwa wanatambua kuhusiana na ishara hizo.[5]

1. Biharul Anwar, Juzuu 15, uk. 345 kama kilivyonukuliwa kutoka 'Fazaa'ili Waaqidi'
2. Manaaqib-i-Ibn Shehr Ashub, Juzuu 1, uk. 24.
3. Milkway au kwa Kiswahili; kilimia ni nyota ndogo nyingi sana zilizo jikusanya pamoja kama wingu jeupe angani wakati wa usiku.
4. Siirah-i-Ibn Hashim, Juzuu 1, uk. 167.
5. Tazama Sura al-'Araaf, 7:157.

# Sura Ya Saba: Kujiunga Tena Na Familia Yake

Allah kamwekea kila mtu kazi maalum. Kama mtu kaumbwa ili aitafute elimu na hekima, mwingine atakuwa kabarikiwa uwezo wa kugundua vitu na wa tatu atakuwa kabarikiwa uwezo wa kazi na juhudi. Kama watu fulani wamejaaliwa uwezo wa kuzifanya kazi za serikali na siasa, wengine wamepewa kazi ya kufundisha na kuwafunza wenzao na kadhalika.

Viongozi wenye huruma, wenye shauku ya kuwapo kwa utaratibu mzuri na jamala katika mazingira yao, na wenye kupenda maendeleo ya mtu mmoja mmoja pamoja na ya jamii nzima, huutahini ujuzi na akili za mtu kabla ya kumpa kazi, na humpa tu ile kazi ilandanayo na welekevu wake.
Kama halikufanyika hili, jamii hupatwa na hasara mbili. Kwanza kabisa yule mtu ahusikaye hafanyi kile awezacho na huthibitika kuwa bure. Inasemekana kwamba: "Kila kwenye kichwa mna welekevu. Yu mwenye bahati yule autambuaye welekevu wake."

Mwalimu fulani alikuwa akimshauri mwanafunzi mvivu. Alikuwa akimweleza kuhusu uovu wa uvivu na hatima ya wale wasiojifunza, lakini wakayatumia maisha yao katika kuyatafuta mambo ya uvivu. Ghafla akaona kwamba yule mwanafunzi, alipokuwa akiyasikiliza yale maneno yake, alikuwa pia akichora picha mchangani kwa kipande cha mkaa na mawe.

Mara moja akatambua ya kwamba kijana yule hakuumbwa kwa ajili ya kusoma na kwamba mkono wa maumbile umemdhamiria kuwa mchoraji. Hivyo akawaita wazazi wa kijana yule na akawaambia; "Ingawa mtoto wenu yu mzembe na mzito katika masomo, anao welekevu mzuri katika uchoraji. Hivyo basi, itakuwa vema kama mtamtayarishia mafunzo ya uchoraji. Wazazi wa kijana yule waliukubali ushauri wa mwalimu yule. Hivyo yule mwanafunzi akaanza kujifunza sanaa ile na hatimaye akawa mchoraji mkuu wa zama zake.

Kipindi cha awali cha maisha ya mtoto huitoa nafasi nzuri zaidi kwa wazazi na walezi wao kuutahini mwelekeo wepesi na kupata ujuzi juu ya akili zao kutokana na matendo, tabia, fikara na uwezo. Jambo hili huwa hivyo kwa sababu fikra, matendo na maneno mazuri na ya upole ya mtoto na kioo cha hali ya baadae ya maisha yake na kama akipewa mwongozo bora kwa akili zake, ndivyo atakavyoweza kupata faida kubwa kutokana na wepesi wake wa kuyaelewa mambo.

Kujifunza jinsi na tabia za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) tangu utotoni mwake hadi pale ilipoanza kazi ya Utume huisawiri machoni mwetu picha ya msingi wa maisha yake na fikara zake tukufu, na uchunguzi wa historia ya utotoni mwake hutuonyesha uzuri wa maisha yake ya baadae. Zaidi ya hapo, historia fupi ya maisha yake, tangu awali hadi pale alipoteuliwa kuishika kazi ya Utume, alipojitangaza kuwa yu kiongozi wa jamii, hutupa taarifa za maisha yake ya baadae na hulidhihirisha lengo la kuumbwa kwake, na vile vile hutuarifu kama dai lake la utume na uongozi liliafikiana na matukio ya maisha yake au la.

Hutuarifu kama maisha yake ya miaka arobaini, na mwenendo, taratibu, kauli na mwongozo wa ushirikiano wake mrefu na watu waunga mkono Utume wake au la. Hivyo basi, tukilizingatia hili tunaweka mbele ya wasomaji wetu, sehemu ya maisha ya awali ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Mama wa kunyonya mwenye huruma, wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.), alimlea kwa muda wa miaka mitano na alifanya kila alichokiweza katika kumlea na kumhifadhi. Katika kipindi hiki Mtume alijifunza ufasaha wa lugha ya kiarabu, katika siku za baadae alijifaharisha mno katika lugha hii. Baadae bibi Halima alimleta Makkah na akakaa na mama yake mpenzi kwa kipindi fulani akiwa chini ya ulezi wa babu yake mwenye huruma. Mtoto huyu ndiye peke yake aliyekuwa ukumbusho wa Bwana Abdillah katika familia yake iliyofiwa.[1]

## Safari Ya Kwenda Yathrib

Tangu siku ile yule mkemwana mpya wa Bwana Abdul-Muttalib (yaani bibi Amina) ampoteze mumewe aliye bado yu kijana na mtukufu, alikuwa akiisubiri nafasi ya kwenda Yathrib kujionea kwa macho yake pale mahali alipolalia mumewe mpenzi na vile vile kuwaona ndugu zake mjini mle.
Mwishowe aliamua kwamba muda ufaao kwa safari hiyo umewadia na mwanawe mpenzi kaishakuwa vya kutosha, kiasi cha kuweza kufuatana naye. Walijitayarisha kwa safari ile na wakaondoka kwenda Yathrib wakifuatana na Ummi Aiman.

Kwa mtoto mdogo wa kiquraishi safari hii ilikuwa ngumu na ilimsababishia maumivu ya kiroho, kwa sababu, kwa mara yake ya kwanza aliiona nyumba aliyofia baba yake mpenzi pamoja na sehemu aliyozikwa, na kwa kawaida, hadi wakati ule, mama yake tayari alikuwa kaishamueleza mambo mengi kumhusu baba yake.

Maumivu ya huzuni yalikuwa bado yamo moyoni mwake ulipotokea msiba mwingine wa kumpiga wimbi jipya la huzuni na masikitiko, kwa sababu, alipokuwa njiani akirejea Makkah, alimpoteza mama yake alipokuwa mahali paitwapo Ab'wa.[2]

Tukio hili la bahati mbaya lilimfanya kijana Muhammad kuwa mpendwa zaidi machoni mwa watu wa familia, kama waridi pekee lililosalia kwenye bustani hii ya mauaridi na akawa mpenzi zaidi wa Abdul-Muttalib. Alimpenda zaidi kuliko wanawe na akampa upendeleo zaidi kuliko mtu yeyote yule mwingine.

Kandoni mwa Kaabah liliwekwa zulia kwa ajili ya mtawala wa Waquraishi (yaani Abdul-Muttalib).

Machifu wa Waquraishi pamoja na wanawe mwenyewe walikuwa wakikaa kwa mzunguko juu ya zulia lile. Hata hivyo, kila macho ya Abdul-Muttalib yalipoangukia kwenye huu ukumbusho wa Abdulah, aliamrisha wampishe ili kwamba apewe nafasi ya kumweka kijana Muhammad (s.a.w.w.) katika zulia lile3. Qur'ani Tukufu inakitaja kipindi cha uyatima wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika *Surah al-Dhuha* na inasema:

{أَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيمًا فَآوَىٰ} 6

***"Je, Hakukukuta ni yatima na akakupa mahali pa usalama?"* (*Suratal-Dhuha, 93:6*).**

Falsafa ya msingi wa hali ya watoto yatima wa Waquraishi haieleweki vizuri kwetu. Tunajua tu kwamba ngurumo ya mafuriko ya matukio huashiria lengo jema.

Kwa kulizingatia jambo hili, tunaweza kukisia ya kwamba Allah alipenda kwamba kabla huyu kiongozi wa wanaadamu kuzishika hatamu za mambo na kuanza uongozi wake, hana budi kulionja pigo na misiba, na kuonja mageuzi ya hali za maisha ili aweze kujijengea uvumilivu mkubwa na moyo wa ushupavu na kwa taabu hizo aweze kujitayarisha kwa ajili ya kupambana na maisha yake ya baadae yenye silsila ya matatizo na kunyimwa, pamoja na kutokuwa na makazi.

Allah alipenda kuwa Mtume (s.a.w.w.) asiwe na elimu ya kufunzwa na mwanadamu na asiwajibike na kumnyenyekea mtu yeyote.

Tangu katika siku za awali za uhai wake awe huru na mwenye kujitosheleza na ajipatie uwezo wa kuendelea na utukufu kama mtu aliyejiumba ili watu waweze kutambua ya kwamba, kwa upande wake ufunuo si ufunuo wa kibinaadamu na kwamba wazazi wake hawakuwa na lolote walilolifanya katika kuzirekebisha tabia zake, fikara zake na uangavu wa maisha yake ya baadae na ukuu wake na ubora wake vimetokana na msingi wa utukufu wake.

## Kufariki Dunia Kwa Bwana Abdul-Muttalib

Matukio ya kiulimwengu ya kuhuzunisha sana hujitokeza katika kipindi cha uhai wa mwanadamu, moja baada ya nyingine, kama mawimbi makubwa ya bahari na kuumiza nafsi ya mwanadamu.

Mawimbi ya huzuni kubwa yalikuwa bado yangali yakiukumba moyo wa Mtume wa Allah pale ilipombidi kupambana pia na msiba mwingine. Alikuwa bado hajaufikia umri wa miaka minane pale alipompoteza babu yake. Kifo cha Bwana Abdul-Muttalib kilikuwa na athari kubwa mno kwa Mtume (s.a.w.w.) kiasi kwamba aliendelea kulia hadi ukingoni mwa kaburi lake na katu hakupata kumsahau.

## Ulezi Wa Bwana Abu Twalib

Tutazungumzia juu ya sifa na ukuu wa Bwana Abu Twalib katika sura maalum ya kitabu hiki na kuuthibitisha Uislamu wake na itikadi yake juu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa thibitisho zikubaliwazo na wanachuoni wa kiislamu. Hata hivyo, kwa sasa itafaa tu kwamba tusimulie matukio yanayohusiana na malezi ya Mtume (s.a.w.w.) aliyoyapata kwa Bwana Abu Twalib.

Zilikuwepo sababu kadhaa zilizomfanya Bwana Abu Twalib alichukue jukumu na heshima ya kumlea Mtume (s.a.w.w.). Yeye na Bwana Abdullah, baba yake Mtume Muhammad (s.a.w.w.) walitokana na mama mmoja.[4]

Na vile vile Bwana Abu Twalib alifahamika mno kwa ukarimu na wema wake, kwa sababu hiyo Bwana Abdul-Muttalib alimteuwa kuushika ulezi wa mjukuu wake mpenzi. Huduma aliyoitoa kwa uwezo wake wote imehifadhiwa katika vitabu vya historia kwa maneno mazuri mno na hapo baadae itasimuliwa.

Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa na umri wa miaka kumi na mitano, alishiriki katika vita pamoja na ami yake. Kwa vile vita hivi vilipiganwa mnamo miezi ambayo vita vilipigwa marufuku, vita vile viliitwa 'Vita vya Fujjaar.' Maelezo marefu juu ya 'Vita vya Fujjaar' yametolewa katika vitabu vya Historia.

## Safari Ya Kwenda Sham

Ilikuwa ni desturi ya Waquraishi waliojishughulisha na biashara kwenda Sham mara moja kwa mwaka. Bwana Abu Twalib alidhamiria kushiriki katika safari ya Waquraishi mwaka ule. Ama kuhusu yule mpwa wake (yaani Mtume s.a.w.w) ambaye kwa kawaida hakumwacha japo kwa kita- mbo kidogo tu, aliamua kumwacha mjini

Makkahh na kuwateuwa watu wengine kumwangalia. Hata hivyo, msafara ulipokuwa tayari kuondoka, Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alitiririkwa na machozi na kuuhisi mtengano ule na mlezi wake. Uso wa Muhammad (s.a.w.w.) uliojawa na huzuni ulizipandisha mno hisia za Bwana Abu Twalib kiasi kwamba alijua kuwa yu alazimika kuzikabili taabu kuwa naye Muhammad mwenyewe katika safari ile.

Safari hii aliyoichukua Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili inachukuliwa kuwa ni moja ya safari zenye kupendwa mno alizozichukua kwa sababu katika safari hii alipitia Madian Bonde la Qura nchi ya Wathamudi na kuyaona mandhari yenye kupendeza ya sura ya nchi ya Sham.

Msafara ule ulikuwa bado haujawasili Sham pale lilipotokea tukio fulani ulipokuwa njiani, mahali paitwapo Basra, ambalo lilivuruga mpango wa safari ya Bwana Abu Twalib kwa kiasi fulani. Maelezo ya tukio hili ni haya yafuatayo:

Kwa miaka mingi mtawa mmoja aliyekuwa akiitwa Bahira alikuwa akijishughulisha katika kufanya ibada zake katika nyumba yake maalum ya utawa iliyokuwa pale Basra. Mtawa huyu alikuwa na elimu nyingi

juu ya Ukristo, na Wakristo wa sehemu ile walimtukuza mno. Wakati mwingine misafara ya kibiashara ilitua mahali pale na wasafiri fulani walimtembelea mtawa yule ili kuzipata baraka zake.

Kwa bahati Bahira alipata kukutana na ule msafara wa Waquraishi. Macho yake yalimwangalia yule mpwa wake Bwana Abu Twalib aliyemvutia mno. Mtazamo wake wa siri na wa makini ulidhihirisha siri iliyojificha moyoni mwake. Alimkodolea macho kwa kitambo fulani, na ghafla tu akakivunja kimya kile na kuuliza:

“Ni nani anayehusiana na kijana huyu miongoni mwenu?” Baadhi ya wale waliokuwepo pale walimtazama ami yake. Bwana Abu Twalib, akasema: “Huyo ni mpwa wangu.” Hapo Bahira akasema: “Kijana huyu ana maisha ya baadaye yaliyo matukufu. Huyu ndiye yule Mtume aliyeahidiwa, ambaye Utume, ushindi na utawala wake wa ulimwengu mzima vimetabiriwa katika vitabu vya Mbinguni na dalili nilizozisoma vitabuni zinamhusu yeye.

Ndiye yule Mtume ambaye jina lake na jina la baba yake na kuhusu familia yake nimevisoma katika vitabu vya kidini na ninaelewa atatokea wapi na vipi dini yake itakavyoenea hapa ulimwenguni. Hata hivyo, itakubidi kumficha kutoka machoni pa Wayahudi, kwa kuwa, kama wakiyajua mambo yahusianayo naye, watamuua”.[5]

Wengi wa wanahistoria wanasema kwamba yule mpwa wake Bwana Abu Twalib hakuendelea zaidi ya sehemu ile (Basra). Hata hivyo, haifahamiki wazi kama yule ami yake Muhammad alimrudisha Makkah pamoja na mtu mwingine (jambo hili laonekana kuwa lisilowezekana hata kidogo baada ya Bwana Abu Twalib kusikia kutoka kwa mtawa yule kwamba asijitenge hata kidogo na yule mpwa wake) au yeye mwenyewe alirejea naye mjini Makkah na kutoendelea na ile safari. Na wakati mwingine inasemekana kwamba alikwenda pamoja na Muhammad kule Sham huku akimlinda mno.

## Uongo Wa Mustashirik

Katika sura moja ya kitabu hiki tutaelezea makosa na mara kwa mara uongo na masingizio ya uonevu wa mustashirik hawa ili kwamba msingi wa taarifa zao ueleweke na vile vile iwe dhahiri kwa kiasi fulani wanavyojaribu kwa makusudi kuzichanganya akili za watu wepesi wa kuamini kila kitu. Mkutano wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na yule mtawa ni jambo la kawaida kabisa.

Hata hivyo, hivi sasa ni miaka mingi ishapita tangu kutokee tukio hilo. Mustashirik wamelifanya kuwa hoja na wanasisitiza kuthibitisha kwamba Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) katika safari yake hii alijifunza kutoka kwa Bahira yale mafundisho yake matukufu ambayo aliwafunza watu miaka ishirini na nne badaye, na ambayo yalichangamsha upya, kama kioevu cha maisha kwenye mwili uliokufa wa jamii ya mwanadamu wa zama zile.

Wanasema: “Kuhusu ukuu wa roho, utakatifu wa akili, akili yenye uwezo wa kushika mambo na fikara za ndani zaidi, ambayo maumbile yamemjaalia Muhammad kwa wingi, alijifunza kutoka kwa mtawa yule

hadithi za Mitume na za jamii zilizopita kama vile za Waadi na Wathamudi na vile vile alijipatia mengi ya mafundisho yake muhimu kutoka kwake katika mkutano huo huo."

Inaonesha wazi kwamba maoni tuliyoyatoa hapo juu si chochote ila ni ubunifu tu na kamwe haifikiani na matukio ya maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Vile vile haiungwi mkono ila inakataliwa kisayansi na vipimo vya kikawaida.

Zifuatazo hapa chini ni thibitisho za yale tuliyoyasema hapo juu: Wanahistoria kwa pamoja wanakubaliana kwamba Mtume Muhammad (s.a.w.w.) hakujua kusoma na kuandika. Aidha, wakati wa ile safari yake umri wake haukuzidi miaka kumi na miwili.

Sasa je, inawezekana kuamini kwamba kijana wa umri usiozidi miaka kumi na miwili, aweze kujifunza habari za Torati na Injili na baadae, akiwa na umri wa miaka arobaini, azipe sura za ufunuo na kuasisi dini mpya? Jambo hili ni kinyume na vipimo vya kawaida na, tukiizingatia kadiri ya uwezo wa binadamu, tunaweza kusema kwamba haiwezekani kiakili.

Kipindi cha safari hii kilikuwa kifupi mno kuweza kumwezesha Mtume Muhammad kujifunza japo sehemu ndogo ya Torati na Injili, kwa sababu msafara ule ulikuwa ni msafara wa kibiashara na haukuchukuwa zaidi ya miezi minne, hii ikiwa ni pamoja na kipindi cha kutua pale Basra. Sababu yake ni kwamba, Waquraishi walisafiri mara mbili katika kipindi cha mwaka mmoja, kwenda Yemen katika majira ya baridi na kwenda Sham katika majira ya kiangazi, na kufuatana na jambo hili haiwezekani kudhania kwamba kipindi cha safari ile tuizungumziayo ulizidi miezi mine.

Na vile vile haiwezekani hata kwa yule mtaalamu mkuu zaidi wa ulimwengu huu kuvijua vitabu hivi viwili vilivyo vikuu katika kipindi kifupi namna hiyo, achilia mbali kijana mdogo asiyejua kusoma na kuandika, hasa tukizingatia ya kwamba hakuwa na mtawa yule kwa kile kipindi chote cha miezi minne na mkutano huu ulifanyika katika kituo wakati wa misafara na haukuendelea zaidi ya masaa machache.

Historia inatupa ushuhuda ya kwamba Bwana Abu Twalib alitaka kumchukua mpwa wake na kwenda naye Sham, hivyo pale Basra hapakuwa lengo la msafara wao. Aidha, Basra palikuwa mahali fulani katika njia na katika nyakati fulani fulani misafara ilitua pale ili kupumzika. Katika tukio lile inawezekanaje kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akae pale na kujishighulisha katika kujifunza Taurati na injili.

Ni mamoja kama tukisema kwamba Abu Twalib alimchukua na kwenda naye Sham au kwamba alikomea hapo (Busra) na kurejea Makkah au alimrudisha mpwa wake Makkah pamoja na mtu fulani, vyovyote vile iwavyo, mwishilizo wa msafara na vile vile ule wa Bwana Abu Twalib haukuwa pale Basra, ili kwamba tukaweza kufikiria msafara ule kwamba uliweza kujishughulisha katika biashara zao na wakati ule ule Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akajishughulisha na masomo.

Kama mpwa wake Bwana Abu Twalib alijipatia mafunzo kutoka kwa mtawa yule, bila shaka jambo hilo lingalipata kutangazwa miongoni mwa Waquraishi na wote wangalilizungumzia wakati wa kurejea kwao.

Zaidi ya hapo, hata Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe asingaliweza kudai mbele ya watu wake kuwa alikuwa asiyejua kusoma na kuandika na kwamba hakupata masomo yeyote, wakati tunapoona kwamba Mtukufu Mtume kwa dai hili hili, na hakuna yeyote aliyemwambia: “Ewe Muhammad! Umejifunza kutoka kwa mtawa wa Basra pale ulipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili na ukajifunza habari hizi zenye kuangaza kutoka kwake.”

Kama inavyojulikana waabudu masanamu wa Makkah walimlaumu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa mambo mbalimbali na wakaisoma Qur’ani Tukufu kwa makini ili wapate sababu ya kumlaumia.

Walifanya hivyo mno kiasi kwamba, safari moja walipoona kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika nyakati fulani fulani alijishirikisha na mtumwa wa kikristo, kule Marmah, waliichukua fursa hiyo na kusema kwamba Muhammad alijifunza yale aliyokuwa akiyasema kutoka kwa yule mtumwa wa kikristo.

Qur’ani Tukufu inaitaja lawama yao hii kwa maneno haya:

{وَلَقَدْ نَعْلَمُ أَنَّهُمْ يَقُولُونَ إِنَّمَا يُعَلِّمُهُ بَشَرٌ ۗ لِسَانُ الَّذِي يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ أَعْجَمِيٌّ وَهَٰذَا لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُبِينٌ {103

***“Na bila shaka Tunajua ya kwamba*** (***makafiri***) ***wanasema: ‘Hakika yumo mtu anayemfundisha*** (***Muhammad haya***) ***lakini lugha ya yule wanayemdokeza*** (***yule mtumwa wa kikristo***) ***ni ya kigeni na hii ni lugha ya kiarabu*** (***fasaha na***) ***cha dhahiri.”***
(***Sura al-Nahl, 16:103***)

hata hivyo, kuhusu lawama hii, (yaani ya kwamba Mtukufu Mtume s.a.w.w alijifunza kwa Bahira) hakikupata kukataliwa na Qur’ani Tukufu wala Waquraishi wagomvi wenye kukanusha hawaifanyi kuwa hoja yao. Na jambo hili, lenyewe ni uthibitisho wa dhahiri wa ukweli uliopo ya kwamba lawama hii ni matokeo ya akili za mustashirik.

Hadithi za Mtume, zilizosimuliwa kwa kirefu katika Qur’ani Tukufu, zinatofautiana mno na zile zilizosimuliwa katika Tourati na Injili. Na mambo yanayohusishwa na Mitume hao yamesimuliwa katika hivi vitabu viwili kwa njia isiyo ya adabu na yenye kuchukiza mno kiasi kwamba hazipatani hata kidogo na vipimo vya kiakili.

Ulinganisho wa vitabu hivi viwili na Qur’ani Tukufu waonyesha kwamba maelezo ya Qur’ani Tukufu hayakuchukuliwa kutoka katika vitabu hivi. Na kama ikidhaminiwa kwamba Mtume Muhammad alizipata taarifa juu ya historia za mataifa kutokana na hizo Injili mbili, ingalilazimu kwamba maelezo yake nayo yachanganyike na maneno ya upotovu na (ngano za watu wa kale).

Kama yule mtawa aliyekuwa akiishi katika njia iendayo Sham alikuwa na elimu pana zaidi ya theolojia na dini kiasi cha kuweza kumwelimisha Mtume kama vile Muhammad (s.a.w.w.) kwa nini mtawa huyu hakujipatia utukufu? Na ni kwa nini hakuweza kumwelimisha yeyote mwingine ghairi ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) wakati alipokuwa akitembelewa mara kwa mara na watu wengi?

## Kuitupia Jicho Taurati Iliyopo Sasa

Kitabu hiki cha mbinguni! hakifungamani hata kidogo na mambo yahusuyo masimulizi juu ya Mitume. Hapa tutataja kwa kifupi tu baadhi ya matukio yahusianayo na jambo hili ili ieleweke dhahiri kwamba, kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angalipata habari zake hizi za Qur'ani Tukufu ziangazazo, kutoka kwa mtawa yule, kusingalikuwako sababu ya kwa nini lisipatikane humo katika Qur'ani japo jambo lililo dogo mno lenye kuchukiza katika yale aliyoyasema. Kwa mfano: Taurati inasema katika kitabu cha Mwanzo (sura ya 32, aya ya 2-30): "Usiku mmoja Mungu alipigana mieleka na Yakobo hadi alfajiri,"

Mungu alimdanganya Adamu kwa kumwambia kuwa kama akila tunda la mti fulani atakufa, ambapo ukweli ulikuwa kwamba kama akilila tunda la mti ule atatambua mema na mabaya kama Mungu. Na alipolila, aliupata utambuzi ule.[6]

Taurati inasimulia kwa jinsi hii kushuka kwa malaika wawili kuja kumtembelea Nabii Ibrahim (a.s.). Mungu alishuka na malaika wawili ili kujua kama taarifa alizokuwa akizipata juu ya watu zilikuwa sahihi au zina uongo, kwa sababu hii, Mungu alimtokea Ibrahim, naye akasema: "Acha nilete maji mkanawe miguu." Baada ya hapo Mungu na wale malaika wawili waliochoka wakapumzika na wakala chakula (Tazama Mwanzo, sura ya 18, aya ya 1-9).

Mpenzi msomaji! Tafadhali soma pia habari zilizosimuliwa katika Qur'ani Tukufu na kisha uamue kama inawezekana kusema: "Qur'ani Tukufu iliyosimulia kila jambo kwa jinsi iliyo tukufu mno inayatwaa masimulizi yenye kuwahusu Mitume kutoka kwenye Taurati hii?" Na kama imey- achukua kutoka kwenye Taurati kwa nini usiwepo upotovu ulioakisiwa katika masimulizi haya yaliyopigwa chuku ndani yake?

## Kuitupia Jicho Injili

Tutayataja hapa matukio matatu ya ukweli wa dhahiri juu ya Injili, ili kuonyesha kama kweli hii Injili ndio asili ya Qur'ani ya Waislamu au la:

## Nabii Isa (A.S) Aonyesha Muujiza

Nabii Isa (a.s.) alikwenda harusini pamoja na mama yake na wanafunzi wake. Ilitokea kwamba mvinyo ulimalizika pale harusini. Kwa muujiza aliyabadili mabalasi saba yaliyojaa maji na kuwa mvinyo (Mt. Yohana, Sura ya 2, aya ya 1-11).

Nabii Isa (a.s.) alichukua kikombe cha mvinyo ule, akawapa na akasema: "Kunyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu...." (Mathayo, 26:27).

Ndugu msomaji, hata hivyo mtaiona mantiki ya Qur'ani Tukufu juu ya kule kunywa mvinyo ambao kunapingwa kabisa na maoni tuliyoyaona hapo juu. Qur'ani tukufu inasema:

{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَامُ رِجْسٌ مِنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ} 90

***“Enyi mlioamini! Hakika pombe na kamari na masanamu na mishale ya kupigia ramli ni uchafu utokanao na kazi ya shetani; basi uam- baeni ili mpate kufaulu.”***
(***Sura al-Maida, 5:90***).

Katika mazingira haya je, tunaweza kusema kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alizipata taarifa za Qur’ani Tukufu kutoka kwa yule mtawa wa Basra?

Injili ya siku hizi inamueleza Nabii Isa (a.s.) kama mtu mkali asiyekuwa na huruma hata kidogo kwa mama yake (tazama Mathayo, sura ya 12; Marko sura ya 13; Luka, sura ya 83) ambapo Qur’ani Tukufu inamweleza kinyume kabisa na hivyo:

{وَبَرًّا بِوَالِدَتِي وَلَمْ يَجْعَلْنِي جَبَّارًا شَقِيًّا} 32

***“Na*** (***yeye Allah Ameniusia***) ***kumfanyia wema mama yangu, wala hakunifanya niwe jeuri*** (***wala***) ***muovu.”*** (***Surat Mariam, 19:32***).

Watu wasio na upendeleo, wanapoyalinganisha masimulizi na maamrisho ya Qur’ani Tukufu na Biblia wanaweza kuelewa ya kwamba Biblia haiwezi kuwa chanzo cha Qur’ani.

1. Siirah-I Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 167.
2. Siirah-i-Ibn Halabi, Juzuu 1, uk. 125
3. Siirah-i-Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 168
4. Siirah-i-Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 179.
5. Tarikh-i-Tabari, Juzuu 1, uk. 33; Siirah-i-Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 180-183.
6. Taurati imeeleza kwa kirefu hadithi ya Adamu na Hawa katika kitabu cha Mwanzo Sura ya 2 aya ya 3.

# Sura Ya Nane:Kipindi Cha Ujana

Ni lazima kiongozi wa jamii awe mvumilivu, mwenye subira, afya timam na nguvu, shujaa na jasiri, asiye na woga na shupavu, na ni lazima awe na moyo mkuu.

Je, yawezekanaje kwa watu waoga, wanyonge wenye fikara dhaifu na wavivu kuiongoza jamii katika kuzipitia njia zenye mambo mengi? Je, watawezaje kuuchukua msimamo maalum mbele ya maadui na kuuhami utu na ukuu wao kutokana na mashambulizi ya watu kwa ujumla?

Ukuu na utukufu wa moyo wa kiongozi na nguvu na uwezo wake wa kimwili na kiroho vina athari ya ajabu kwa wafuasi wake. Wakati Sayyidna Ali, Amirul Muuminina, alipomteuwa mmoja wa wafuasi wake

waaminifu kwa ajili ya ugavana wa Misri, aliwaandikia barua wale watu wa Misri walioathiriwa na wengi wao kutolewa nje ya nchi hiyo kutokana na udhalimu wa serikali iliyokuwa ikitawala nchini mle.

Katika barua ile alimsifu gavana wake mteuliwa kwa ushujaa wake na usafi wa moyo wake. Hapa chini tunanukuu mateuzi fulani – fulani kutoka kwenye barua ile ambayo ndani yake sifa halisi za mtawala zimeelezwa: "Ninakuleteeni mja wa Allah asiyelala katika siku za hofu na asiyeonyesha woga anapomkabili adui mwenye hatari. Kwa wale walio waovu yu mkali mno zaidi ya moto uunguzao. Yeye ni Maliki bin Harithi atokanaye na ukoo wa Mazhaj. Yasikilizeni maneno yake, kwa kuwa yeye ni mmoja wa panga za Allah usiokuwa butu na ambao dharuba yake haikosi kuitenda kazi yake barabara."[1]

## Nguvu Ya Kiroho Ya Mtukufu Mtume (S.A.W.W)

Mtukufu Mtume (s.a.w.w katika kipindi cha utoto na ujana wake dalili za nguvu, ushujaa, umadhubuti na uhodari zilionekana katika paji la uso wa kipenzi cha Waquraishi. Alipokuwa na umri wa miaka kumi na mitano alishiriki katika vita vilivyopiganwa na Waquraishi dhidi ya kabila la Hawaazan na ambavyo viliitwa 'vita vya Fujjar' katika vita vile, kazi yake ilikuwa ni kuikinga mishale iliyolengwa ami zake. Katika *Siirah-i-Ibn Hisham*[2] mwandishi anainukuu sentensi ifuatayo kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Niliikinga mishale mbali na ami zangu."

Kushiriki kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika vita hivi na vile vile katika umri mdogo kiasi hiki kunatujulisha juu ya ushujaa usio kifani wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na sasa tunaelewa ni kwa nini Imam Ali (a.s.), yule shujaa mkuu zaidi wa mashujaa Amirul Muuminina anasema: "Kila mambo yalipotuwia magumu (sisi askari wa kiislamu) katika mstari wa mbele wa vita tulikimbilia kwa Mtukufu Mtume wa Allah (s.a.w.w.) na hakuna yeyote miongoni mwetu aliyekuwa karibu zaidi na adui kuliko Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe."[3]

Tutaitaja misingi ya mafunzo ya kijeshi ya kiislamu katika sura ihusianayo na vita vya Waislamu dhidi ya washirikina, na tutajifunza jinsi ya kupigana kwao, ambako daima kuliichukua sura yake kufuatana na maagizo ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Na jambo hili lenyewe ni moja ya mijadala ivutiayo ya historia ya Uislam.

## Vita Vya Fujjaar (Vya Kidhalimu)

Maelezo kamili ya mambo haya yako nje ya lengo la kitabu hiki. Hata hivyo, hapa chini tunaeleza kwa kifupi tu sababu na matukio ya vita hivi ambavyo moja miongoni mwao alishiriki Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ili kwamba wasomaji wangu wapenzi msisalie msiojua lolote juu yake.

Waarabu wa zama za ujinga waliutumia mwaka mzima katika vita na utekaji nyara. Vivyo, kuendelea kwa hali hii ya mambo kuliyafuja maisha yao. Kutokana na jambo hili, hawakupigana katika miezi minne ya mwaka (ambao ni Rajab (mfungo kumi), Dhil Qa'ad (mfungo pili), Dhil-Hajj (mfungo tatu) na Muharram (mfungo nne) ili waweze kuyafungua masoko ya biashara zao katika miezi minne na

kujishughulisha na kazi na kujichumia na mahitaji ya maisha.[4]

Kutokana na maamuzi haya, masoko ya Ukaaz, Mujannah na Dhil–Majaaz yalishuhudia mikusanyiko mikubwa ya watu katika miezi hii minne na marafiki pamoja na maadui walijishughulisha bega kwa bega wakiwa pamoja katika kununua na kuuza pamoja na kujitukuza. Malenga wakuu wa Bara Arabu waliziimba tungo zao. Wayahudi, Wakristo na wenye kuabudu masanamu walizielezea itikadi zao za kidini mbele ya ulimwengu wa kiarabu bila ya woga wowote wa kupata madhara kutoka kwa wapinzani wao.

Hata hivyo, katika kipindi cha historia ya Uarabuni mapatano haya yalivunjwa mara nne, wakati baadhi ya makabila ya kiarabu yaliyojitia katika vita baina yao. Na kwa vile vita hivi vilipiganwa katika miezi ambayo mapigano yaliharimishwa, vinaitwa vita za Fujjar. Sasa tunatoa hapa chini mikhtasari wa vita hivi.

**FUJJAR YA KWANZA:** Makundi mawili yaliyokuwa yakipigana yalikuwa ni makabila ya Kananah na Hawaazan na chanzo cha vita hivi kimetajwa kuwa ni hiki: Mtu mmoja akiitwa Badr bin Ma'shar alijichagu– lia sehemu katika soko la Ukaaz na akawa anasoma beti za shairi la kujitukuza mbele ya watu kila siku.

Siku moja alisimama na upanga wake mkononi, na akasema: "Enyi watu! Mimi ndiye mwenye kuheshimiwa zaidi na kama mtu yeyote yule atapinga dai langu hili, atakatwa upanga." Wakati ule akasimama mtu mmoja na akampiga Badr dharuba ya upanga mguuni mwake na akaujeruhi. Kutokana na sababu hii haya makundi maw– ili yalikamatana; lakini yaliacha ugomvi kabla ya kuuawa kwa mtu yeyote yule.

**FUJJAR YA PILI:** Sababu ya vita hivi ilikuwa kwamba mwanamke mmoja wa kabila la Bani Aamir aliyekuwa mzuri sana aliyavutia macho ya kijana mwanaume aliyemwomba mwanamke yule amwonyeshe uso wake. Yule mwanamke alikataa kufanya hivyo, yule kijana aliyejawa na ashiki alikaa nyuma yake na akayafunga kwa kuyashona pamoja mapaja yake marefu kwa miiba ili kwamba atakapoamka, uso wake uweze kuonekana. Katika tukio hili, wote wawili waliyaita makabila yao. Yale makabila maw– ili yaliacha kupigana baada ya baadhi ya watu kuuawa.

**FUJJAR YA TATU:** Mtu wa kabila la Kananah alidaiwa na mtu mwingine wa kabila la Bani Aamir yule mdeni alikuwa akichelewa kulipa. Watu hawa walianza kugombana kutokana na sababu hii. Vita vya umwagaji damu vilitishia kuzuka baina ya hayo makabila mawili, lakini, kabla ya hali kuchafuka zaidi, jambo hili liliamuliwa kwa amani.

**FUJJAR YA NNE:** Hivi ndiyo vile vita alivyoshiriki Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe. Kuna maoni tofauti kuhusiana na umri wake wakati ule. Baadhi ya watu wanasema alikuwa na umri wa miaka kumi na minne au kumi na mitano, wakati wengine wameandika kuwa wakati ule alikuwa na umri wa miaka ishirini. Hata hivyo, kwa vile vita hivi viliendelea kwa kipindi cha miaka minne, inawezekana kwamba maelezo yote haya yanaweza kuwa sahihi.[5] Asili ya ugomvi huu imeelezwa kuwa ni hii: Mtu mmoja

aliyeitwa Nu'maan bin Manzar alikuwa na desturi ya kuandaa misafara, kila mwaka, na kupeleka bidhaa kule Ukaaz, ili kwamba ngozi, kamba na hariri viweze kuuzwa pale kwa kubadilishwa na bidhaa nyinginezo.

Mtu mmoja aliyeitwa Urwatur Rijaal, aliyetokana na kabila la Hawaazan alichukua jukumu la kuiongoza na kuuhami msafara ule. Hata hivyo mtu mmoja aliyeitwa Baraaz bin Qays, wa kabila la Kanana alipatwa sana mawazo kuhusiana na mtu wa kabila la Hawaazan kutokana na kumzidi. Alimwendea Nu'man bin Manzar na akamlalamikia kuhusu mpango ule lakini alikataliwa. Baraaz alichukizwa na akawa mwenye kijicho na kila mara alikuwa akisubiri apate nafasi ya kumshughulikia Urwatur Rijaal watakapokuwa njiani. Hatimaye alimuua mwenyewe nchi ya Bani Marrah na hivyo akaipaka mikono yake damu ya mtu wa kabila la Bani Hawaazir.

Katika siku hizo, kabila la Waquraishi na Kanaanah yalikuwa washirika na tukio hili lilitukia wakati Waarabu walipokuwa wakijishughulisha na biashara zao katika soko la Ukaaz, mtu mmoja aliwaarifu Waquraishi kuhusu yale yaliyotukia. Hivyo, makabila ya Waquraishi na Kinanah wakazikusanya bidhaa zao mara moja na wakakimbilia kwenye eneo lenye Haram (eneo lililo umbali wa ligi nne au kilometa kumi na tisa hivi, kuzunguuka mji wa Makkah linaitwa Haram. Na kupigana katika eneo hili kuliharimishwa miongoni mwa Waarabu). Makabila haya mawili yaliharakisha hivyo ili wawahi kabla Bani Hawaazin hawajalifahamu tukio lile. Hivyo, mtu mmoja wa kabila la Hawaazin aliwafuatia, kabla ya kuifikia mipaka ya Haramu yalianza mapigano baina ya hizo pande mbili. Hatimaye waliacha mapigano baada ya kuingia usiku.

Makabila ya Waquraishi na Kanaanah waliitumia nafasi hii kwa kutorokea kwenye Haram wakati wa giza, na hivyo wakasalimika kutokana na mashambulio ya maadui. Baada ya siku ile Waquraishi na washirikina wao walitoka kule kwenye Haramu na kati- ka nyakati fulani fulani walipigana na maadui. Katika siku fulani Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) nae alishiriki katika vita hivi pamoja na ami zake kama tulivyoeleza hapo juu. Hali hii ya mambo iliendelea kwa kipindi cha miaka minne. Hatimaye vita vilimalizika kwa kabila la Hawaazin kulipwa fidia ambao wamepoteza watu wengi, ikilinganishwa na lile la Waquraishi.[6]

## Mapatano Ya Vijana

Hapo kale yalikuwapo mapatano yaliyoitwa 'mapatano ya Fuzul' miongo- ni mwa watu wa kabila la Jarhami, na kazi ya mapatano haya ilikuwa kuzilinda haki za waliokandamizwa. Kwa mujibu wa mwana historia maarufu aliyeitwa Imaduddin Ibn Kathir, wanachama wa mapatano haya walikuwa Fazal bin Fazalah, Fazal bin Harith na Fazal bin Wadaa'ah.[7]

Yalikuwa ni kama yale mapatano yaliyofanyika miongoni mwa Waquraishi kadhaa baadae, yalikuwa tofauti na Hilful Fuzul, kutokana na malengo yake (ambayo ni kuzilinda haki za waliokandamizwa), vile vile mapatano haya yaliitwa 'mapatano ya Fuzul'

## Mtukufu Mtume (S.A.W.W) Alishiriki Katika Mapatano Haya

Miaka ishirini kabla ya kuanza kwa kazi ya Utume, mtu mmoja aliwasili Mjini Makkah katika mwezi wa Dhil Qaadah (mfunguo pili) akiwa na bidha kadhaa. Bidhaa hizi zilinunuliwa na Aas bin Waa'il, lakini akashindwa kuzilipia bei waliyo kubaliana. Yule mtu alimwona Mquraishi mmoja aliyekuwa ameketi karibu na Ka'aba. Alianza kulalamika kwa sauti kuu na vile vile akazisoma beti kadhaa zilizoibua watu wenye fikra za heshima. Bwana Zubayr bin Abdul-Muttalib alisimama na watu wengine nao walimwunga mkono. Walifanya mkutano nyumbani mwa Abdullah bin Jad'aan na wakafanya mapatano na wakala kiapo ya kwamba wataungana, na kwa kadiri ya uwezo wao, na katika hali yoyote iwayo, watamfanya mdhalimu aisalimishe haki ya mdhulumiwa kwao. Ulipomalizika utaratibu wa mapatano haya waliamka na kumwendea Aas bin Waa'il. Walizichukua zile bidhaa alizozinunua na akashindwa kuzilipia kisha wakazirudisha kwa mwenyewe.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alishiriki katika mapatano haya yaliyodumisha ustawi wa waliokandamizwa. Mtume (s.a.w.w.) amezungumzia juu ya ukuu wa mapatano haya na simulizi mbili juu ya jambo hili tunazinukuu hapa chini:

"Nyumbani mwa Abdullah bin Jad'aan niliyashuhudia mapatano hayo. Hata hivi sasa (yaani baada ya kuanza kwa kazi ya Utume), kama nikiitwa kwenye mapatano ya aina hiyo nitayakubali (yaani bado ningali mwaminifu juu ya mapatano yale niliyoyafanya)"

Ibn Hisham ananukuu ya kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akizungumzia hivi, kuhusu mapatano hayo: "Siko tayari kuyavunja map- atano yangu, japo nipewe zawadi yenye thawabu mno."

Mapatano ya Fuzul' yalikuwa imara mno na yalithibitishwa kwamba hata vizazi vya baadae vilijiona kwamba ni vyenye kuwajibika nayo.
Mfano wake ni tukio lililotokea katika Ugavana wa Walid bin 'Utbah bin Sufyani, mpwawe (mtoto wa ndugu yake) Muawiya ambaye aliteuliwa na yeye kama gavana wa Madina. Bwana wa Mashahidi, Imam, Husein bin Ali (a.s.) ambaye katu maishani mwake hakupata kuisalimu amri ya udhalimu aliwahi kutofautiana na Gavana huyu wa Madina kuhusu mambo ya fedha. Gavana huyu, daima aliitegemea nguvu ya jimboni mle na ile ya serikali kuu (ya Sham), na alikuwa na kawaida ya kuwatoza raia zake kodi kubwa zaidi ya ilivyostahili.

Ili kuuvunjilia mbali msingi wa madhalimu na kuwafahamisha watu haki zao za kupata utawala wa haki, Imam Huseni (a.s.) alimgeukia Gavana yule na kumwambia: "Naapa kwa jina la Allah, kila utakaponitoza kodi kubwa kuliko vile inavyostahiki, nitauweka mkono wangu katika upanga na nitasimama katika Masjidun-Nabi na nitawaitia watu katika mapatano yaliyofanywa na jadi zao."

Miongoni mwa wale waliokuwepo pale ni, Bwana Abdallah bin Zubair aliamka na kuirudia sentensi ile ya Imam (a.s.) na akaongeza kusema: "Sisi sote tutaamka na kuichukua haki yake au tuuawe katika njia hii." Pole pole mwito wa Imam Husein bin Ali uliyafikia masikio ya watu wenye fikara tukufu kama vile

Mansur bin Mukhramah na Abdur Rahman bin Uthman na wote wakauen- dea upesu upesi mlango mtakatifu wa Imam, wakisema: “Tuko hapa!” Matokeo yake yalikuwa kwamba yule Gavana, akichelea maasi ya watu aliacha kuwatoza watu kodi kubwa kuliko ilivyostahili.[8]

1. Nahju Balaghah, Juzuu 3, uk. 92.
2. Juzuu 1, uk. 186. anaitafsiri kwa namna ile ile tuliyoieleza.
3. Nahjul Balaghah, Juzuu 3, uk. 314.
4. Kutokana na aya ya 36 ya Surah al-Tawbah tunaweza kuona kwamba kuharimishwa kwa vita katika miezi hii minne kuna asili ya kidini na Waarabu hawakuyachupa maharamisho haya.
5. Tarikh-i-Kamil, Juzuu 1, uk. 358-359 na Siirah-i-Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 184.
6. Siirah'i-Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 184-187.
7. Al-Budaayah Wal-Nihaayah , Juzuu ya 2, uk. 292.
8. Siirah-i-Halabi, Juzuu 1, uk. 155-157.

# Sura Ya Tisa: Kutoka Kwenye Uchungaji Hadi Kwenye Biashara

Viongozi wa ki-Mungu hupewa majukumu muhimu na makubwa. Hilo ni jukumu liandamanalo na mashaka na ufukara, mateso na misiba, mauaji na kifo, n.k, kwa kifupi ni kwamba huandamana na kila aina ya mateso. Na kadiri lengo lao liwavyo kuu na tukufu zaidi ndivyo magumu yaandamanayo nalo yatakavyokuwa makali na mabaya zaidi.

Kuhusiana na jambo hili, ushujaa na uvumilivu, yaani kuwa na subira katika matatizo yote, masuto, kujeruhiwa na mateso, yote hayo ni masharti kwa ajili ya mafanikio ya kiongozi wa ki-Mungu, kwa sababu uvumilivu na subra ni sharti halisi katika hatua ya kampeni ya kulifikia lengo lao.

Katika historia na masimulizi yahusianayo na Mitume, tunayaona mambo yaliyo magumu kwetu (sisi watu wa kawaida) japo kwa kuweza kuyafikiria tu. Tunasoma habari za Nabii Nuhu (a.s.) kwamba alihubiri dini kwa kipin- di cha miaka 950! Na matokeo ya kampeni yake hiyo, na juhudi zilizoen- delezwa kiasi hicho, ni watu themanini na moja tu waliomwamini. Kwa maneno mengine ni kwamba kila kwenye kipindi cha miaka kumi na miwili aliweza kumleta mtu mmoja tu kwenye njia iliyonyooka.

Ubora wa uvumilivu na subira hukua mwilini mwa mwanadamu pole pole. Ni muhimu kwamba ayakabili matukio yasiyopendeza ili kwamba roho yake iyazoee matatizo na mateso kwa ukamilifu.

Kabla ya Mitume hawajalifikia daraja la Utume walikuwa wakiitumia sehemu ya maisha yao wakiwa ni wachungaji wa wanyama ili kwamba wautumie wakati fulani wa maisha yao wakiwa nyikani wakiyalisha makundi ya wanyama, na hivyo waweze kuwa na subira na wavumilivu kwa ajili ya elimu ya wanadamu na ili waweze kuichukulia hali ya kuyavu- milia magumu na matatizo yote kuwa ni jambo la kawaida tu.

Huwa hivyo kwa sababu mtu awezapo kuyavumilia magumu kuhusiana na mnyama ambaye kwa upande wa akili na busara, hawezi kulinganishwa na mwanaadamu, hana budi kulikubali jukumu la mwongozo wa watu waliopotea, wanao wawajibikia na kutayarishwa kwa ajili ya kumwitakidi Allah. Tuliyoyazungumzia hapo juu ni kwa mujibu wa Hadithi inayosema: "Allah Hakumtuma Mtume yeyote asiyefanywa kuwa mchungaji wa wanyama, ili kwamba aweze kujifunza jinsi ya kuwaongoza watu.[1]

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) naye alikitumia kipindi fulani cha maishani mwake katika kazi hii na karibuni waandishi wengi wa *siirah* (wasifu) wameinukuu sentensi ifuatayo kutoka kwake: "Mitume wote walikuwa wachungaji kwa kipindi fulani kabla ya kukifikia cheo cha Utume." Watu wakamwuliza Mtume (s.a.w.w.); "Je, wewe nawe umepata kuwa mchungaji?" akajibu: "Ndio, kwa kipindi fulani niliwachunga kondoo wa watu wa Makkahh kwenye eneo liitwalo Qarariit."

Hakuna shaka kwamba ilikuwa muhimu kwa mtu yule aliyelazimika kupi- gana na akina Abu Jahl na akina Abu Lahab na aliyetaka kuwatengeneza watu, kutoka kwenye hali ya kuwa watu waliofedheheshwa, ambao akili zao na hekima zao vilikuwa katika kiwango cha kulipigia goti kila jiwe na fimbo, (kuwatengeneza ili) kuwa kundi la wale wasiokubali kulifuata penzi la yeyote yule ila penzi la Allah tu, kwamba mtu huyu ajizoeze somo la uvumilivu na subira, kwa njia mbali mbali na kwa kipindi fulani kitoshelezacho.

Tunafikiria vilevile kwamba ilikuwepo sababu nyingine iliyomfanya Mtume (s.a.w.w.) aichague kazi ya uchungaji. Ilikuwa kwamba kule kuziona njia za maisha za kipumbavu za wale waliokuwa na mamlaka miongoni mwa Waqureishi na kule kuyadhihirisha kwao maovu, kulikuwa na uzito mkubwa akilini mwa mtu huyu aliye shujaa na muungwana, na aliye na hisia kuu za utukufu wa utu wema. Mbali na hili, kushindwa kwa jamii ya watu wa Makkah kumuabudu Mwenyezi Mungu na kule kuyazunguka kwao masanamu yasiyo na uhai kulikuwa jambo lenye kuchukiza kwa mtu mwenye hekima. Kwa sababu hizi, Mtume (s.a.w.w.) alijitenga na jamii ile na akaitumia sehemu ya maisha yake akiwa porini na katika miteremko ya milima iliyokuwa mbali na ile jamii iliyonajisika, ili kwam- ba, japo kwa kipindi fulani tu, aweze kutokuwa na mateso ya kiakili yaliyosababishwa na hali ya kuhuzunisha iliyokuwepo katika zama zile.

Kwa kulichunguza anga lipendezalo na mpangilio na maumbile ya nyota na kuifikiria miche ya porini, mtu mwenye fikra zilizoongezeka ataweza kujipatia mamia ya dalili za utaratibu wa Mwenyezi Mungu na kuimarisha itikadi ya kawaida juu ya upweke wa Allah kwa nguvu ya dalili za kisayansi. Ingawa kuna ukweli ya kwamba tangu wakati ule wa kuwepo kwao, nyoyo zao ziliangazwa na mwanga wa kurunzi ya upweke wa Alllah, na hawakujifikiria kuwa wako huru kutokana na haja ya kujifunza juu ya viumbe na Ulimwengu, na kwa njia hii waliweza kufikia daraja la juu zaidi la yakini na itikadi.

## Pendekezo La Bwana Abu Twalib

Hali mbaya ya kiuchumi ya mpwawe ilimlazimisha Bwana Abu Twalib, ambaye alikuwa mmoja wa machifu wa Makkahh na watu watukufu wa Waquraishi na alikuwa maarufu kwa ukarimu wake, ushujaa

wake, na daraja kuu la unyoofu wake, alipanga safari ya kikazi kwa ajili yake. Hivyo basi, alimwambia mpwa wake: “Khadija binti Khuwaylad yu mmoja wa matajiri wa Waquraidhi na shughuli zake za kibiashara zimeenea hadi Misri na Ethiopia. Bibi huyu anamtafuta mtu mwaminifu atakayelibeba jukumu la biashara yake, amfanyie kazi katika msafara wa biashara wa Waquraishi na kuzipeleka bidhaa zake Sham ili akaziuze huko. Ewe Muhammad! Itakuwa bora kiasi gani kama utakwenda kujitambulisha kwake!”[2]

Unyoofu na ubora wa kiroho wa Mtume (s.a.w.w.) havikumruhusu kumwendea Khadija moja kwa moja bila ya kufahamisha lolote, na bila ombi kutoka kwa Bibi huyu, na kutoa pendekezo kama hilo. Hivyo, alimjibu ami yake akasema: “Inawezekana kwamba yeye mwenyewe Bibi Khadija atanitumia mtu” Mtume (s.a.w.w.) aliyasema hayo kwa sababu alijua kwamba alikuwa maarufu miongoni mwa watu kama mtu mwaminifu. Na ilitokea hivyo.

Bibi Khadija alipata habari za mazungumzo yao, mara moja alimtuma mtu kwa Mtume (s.a.w.w.) akisema: “Jambo lililonivutia kwako ni ukweli wako, uaminifu wako na utu wema. Niko tayari kukupa maradufu ya kile niwapacho watu wengine na nitakupa watumwa wawili wafuatane nawe na ambao watakutii kwa hali yoyote ile iwayo.[3]

Mtume (s.a.w.w.) alimweleza ami yake habari hii, na yeye akasema: “Kazi hii uliyopewa ni chanzo cha mahitaji ya maisha yako aliyokuruzuku Allah.” Msafara wa Waquraishi uliokuwa na bidhaa za Bibi Khadija ukawa tayari kuondoka. Bibi Khadija alimpa huyu wakala wake ngamia mwenye hatua za taratibu, kiasi fulani cha chakula cha gharama na watumwa wawili, na kuwaamrisha watumwa wale kuwa wenye heshima mno kwa Mtume (s.a.w.w.) katika sehemu zote katu wasilikatae alitendalo, na kumtii kwa hali zote zile.

Hatimaye msafara ule ukafika kule ulikokuwa ukienda na wanamsafara wote walipata faida. Hata hivyo, faida aliyoipata Mtume, ilikuwa kubwa mno ukilinganisha na ile waliyoipata wale wengine na vile vile alinunua vitu kadhaa kwa ajili ya kuviuza katika Soko la Tahaamah.

Baada ya msafara ule kufanya safari iliyofanikiwa kule Sham ulirudi Makkahh. Katika safari hii Mtume (s.a.w.w.), alipitia tena katika nchi ya

Waadi na Wathamudi. Kimya cha kifo kilichokuwepo kwenye mazingira ya taifa lile asi kiliyaibua mazingatio yake zaidi na zaidi juu ya dunia nyinginezo. Zaidi ya hapo kumbukumbu za safari iliyotangulia pia zilihusishwa. Alizikumbuka siku alipoyapita majangwa hayo hayo akiwa pamoja na ami yake. Ule msafara wa Waquraishi ulifika karibu na Makkahh. Akizungumza na Mtume, Mtumwa mmoja kati ya wale wawili aliyeitwa Maysarah alisema: “Ingekuwa bora kama ungeliingia Makkahh kabla yetu na kumwarifu bibi Khadija juu ya mambo ya biashara na faida kubwa mno tuliyoipata mwaka huu.” Mtume (s.a.w.w.) aliingia Makkah wakati bibi Khadija alipokuwa ameketi kwenye chumba chake cha juu. Alishuka chini upesi upesi kumpokea na akaenda naye kule chumbani. Mtukufu mtume (s.a.w.w.) alimhadithia, kwa njia bora zaidi, mambo yaliyohusiana na bidhaa zile. Wakati huo Maysara naye

aliwasili.[4]

Yule mtumwa wa bibi Khadija (Maysara) alimsimulia yale yote aliyoyaona katika ule msafara bila ya kuongeza wala kupunguza na yale yote yaliy- outhibitisha ukuu na imani ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) mwaminifu, pia alimweleza Bibi huyu kwamba katika safari ile yule 'mwaminifu' alito- fautiana na mfanya biashara mmoja juu ya jambo fulani.

Yule mtu alimwambia kwamba atayakubali maneno yake iwapo ataapa kwa 'Lat' na 'Uzza', lakini yule 'mwaminifu' alimjibu akisema: "Nawachukulia Lat na Uzza, mnaowaabudu kuwa ni vitu vidogo zaidi na vyenye kutwezwa zaidi usoni pa nchi."[5]

Vile vile Maisara aliongeza kusema kwamba kule Basrah, yule 'mwaminifu' alikaa chini ya mti akipumzika. Wakati ule mtawa mmoja aliyekuwa katika nyumba yake ya utawa alibahatika kumwona. Alikuja na kumwuliza jina lake na kisha akasema: "Huyu mtu aliyekaa katika kivuli cha mti ndiye yule Nabii niliyesoma bishara nyingi katika Tawrati na Injili."[6]

## Bibi Khadija Mwanamke Wa Kwanza Wa Uislam

Hadi wakati ule, hali ya kifedha na kuichumi ya Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa bado haijawa nzuri na bado alikuwa akihitaji msaada wa kifedha kutoka kwa ami yake Abu Twalib. Mambo yake ya kibiashara yalionekana dhahiri kutokuwa imara kiasi cha kumwezesha kumchagua mke na kujenga familia.

Safari yake ya mwisho kwenda Sham, na safari hii nayo akiwa yu wakala na mwakilishi wa yule mwanamke tajiri na maarufu wa Waquraishi (Khadija) iliimarisha hali yake ya kifedha na kiuchumi kwa kadiri fulani. Ushujaa na uzoefu wake viliyavutia mapenzi ya Khadija na akadhihirisha kuwako kwake tayari kumlipa kitu fulani zaidi na juu ya ujira waliopatana.

Hata hivyo, Mtukufu Mtume alikubali kupokea ule ujira waliopatana hapo awali. Kisha alikwenda nyumbani kwa Abu Twalib na kumpa kiasi chote alichokipata. Ili aweze kumpatia ami yake msaada fulani.

Abu Twalib alikuwa akimsubiri kwa shauku mpwawe aliyekuwa ukumbusho wa baba yake (Abdul-Mutwalib) na nduguye Abdullah. Machozi yalimtiririka machoni mwake mara tu alipomwona. Hata hivyo, alifurahi mno kusikia juu ya shughuli zake za kibiashara na faida zake na alidhihirisha kuwako kwake tayari kumpa farasi wawili na ngamia wawili ili aweze kuendelea na biashara yake. Ama kuhusu ile fedha aliyoichuma katika ile safari na aliyompa ami yake, (Abu Twalib) aliamua kuitumia katika kuchagua mke kwa ajili ya mpwa wake.

Katika hali hii, Mtume (s.a.w.w.) aliamua kumchagua mchumba. Hata hivyo, swala lililoibuka ni vipi uchaguzi ule ulivyomwangukia Bibi Khadija ambaye hapo kabla yake alikataa posa za wanaume wa kiquraishi waliokuwa matajiri zaidi na wenye akili kama vile 'Uqbah bin Abi Mu'it Abu Jahl na Abu Sufyan.

Ni sababu zipi zilizowaleta hawa watu wawili waliokuwa tofauti kabisa kimaisha, na zilizojenga uhusiano huu mzuri huba na mvuto wa kiroho baina yao kiasi kwamba Bibi Khadija alimpa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) utajiri wake wote, naye akautumia utajiri wa Bibi huyu wote alioupata kutokana na biashara zake zilizoenea hadi Misri na Ethiopia, katika njia ya upweke wa Allah na katika kuutukuza ukweli.

Na ilikuwaje kwamba ile nyumba iliyojaa vitu vilivyotiwa njumu za pembe za ndovu na lulu na kupambwa kwa hariri ya Bara Hindi na mazulia ya nyuzi za dhahabu za Uajemi (Iran) hatimaye ikawa kimbilio la Waislamu?

Sababu za matukio haya hazina budi kuthibitishwa kutoka kwenye historia ya maisha ya Bibi Khadija. Hata hivyo, jambo lisilokamilika hapo ni kwamba huduma, kujitia na kujitolea kwa aina hii bila shaka kusingaliweza kuwa kwenye kudumu ila tu pale kuwapo na chanzo kilichothabiti, safi na cha kiroho.

Kurasa za historia zathibitisha ya kwamba ndoa hii ilikuwa ni matokeo ya itikadi ya Bibi Khadija mwenye ucha mungu, usafi, na wema, pia uamimifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kipenzi cha Waquraishi, na historia ya maisha ya Bibi Khadija na masimulizi juu map- ato yake yaliudhihirisha ukweli huu.

Kwa vile Bibi Khadija alikuwa mwanamke mnyofu na mchamungu alita- ka ampate mume mchamungu na mwema na ni kwa sababu hii kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema juu ya Bibi huyu hivi: “Khadija yu miongoni mwa wanawake wa peponi wenye kuheshimiwa” Na mwanamke wa kwanza kumwamini Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alikuwa ni bibi Khadija (a.s.).

Imam Ali (a.s.), Amiri wa waumini, katika moja ya khutba zake, alipokuwa akieleza hali ya Uislam ya siku za mwanzoni za Utume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) iliyokuwa ikisikitisha alisema: “Wakati huo haikuwako familia ya kiislamu ila familia aliyokuwamo Muhammad na mkewe Khadija, nami nilikuwa wa tatu wao.”

Mwanachuoni Ibni Athir anasema kwamba mfanya biashara mmoja aliyeitwa Afif alikuja msikitini Masjidul-Haraam na alishangazwa mno kuuona mkusanyiko mkubwa wa watu na ibada iliyokuwa ikiendeshwa na watu watatu. Aliona ya kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akisali pamoja na Bibi Khadija na Sayyidna Ali (a.s.).

Alipokuwa akirejea kutoka Masjidul-Haraam alikutana na Bwana Abbas, ami yake Mtume (s.a.w.w.). Alimweleza yale aliyoyaona na akauliza kuhusu ukweli wake. Bwana Abas akamwambia: “Kiongozi miongoni mwa watu hao anadai Utume na yule mwanamke yu mkewe Khadija na mtu wa tatu ni Ali, mpwa wangu.” Kisha akaongeza kusema; “Mimi simtambui mtu yeyote katika (huu) uso wa ardhi apasikaye kuwa mfuasi wa dini hii ila hawa watatu.”

Ni nje ya madhumuni ya kitabu hiki kueleza na kunukuu maelezo yaliy- opokelewa juu ya fadhila za Bibi Khadija. Hivyo basi, ingelikuwa bora kama tungelizieleza sababu zilizosabibisha tukio hili la kihistoria (yaani ile ndoa ya Mtume Muhammad s.a.w.w na Bibi Khadija).

## Sababu Za Dhati Na Za Siri Za Ndoa Hii

Walimwengu, walichunguza kila jambo kwa mtazamo wa kilimwengu, wanadhania kwamba, kwa vile Bibi Khadija alikuwa tajiri na mfanya biashara, alihitaji mno mtu mwaminifu kuhusiana na mambo yake ya kib- iashara, na hivyo basi, akaolewa na Muhammad.

Na kwa vile Muhammad naye alikitambua cheo chake kikuuu alikubali ombi lake, ingawa ilikuwapo hitilafu katika umri wao. Hata hivyo, historia inatueleza kwamba Bibi Khadija alishawishika kuolewa na Mtume Muhammad (s.a.w.w.) 'mtu mwaminifu' miongoni mwa Waquraishi kutokana na nyororo ya sababu za kiroho, na muungano huu haukuwa na sababu za kidunia. Ushahidi wenye kuunga mkono dai letu hili
ni huu ufuatao: Wakati Bibi Khadija alipomuuliza Maisara kuhusu matukio yaliyotokea katika safari ya Mtume (s.a.w.w.) alimweleza habari za miujiza aliyoiona kwake na vile vile yale aliyoyasikia kwa yule mtawa wa Sham.
Bibi Khadija alipandwa na fikara nyingi, zenye asili ya shauku yake katika mambo ya kiroho ya Mtume na akamwambia Maisara kwa hiari yake mwenyewe: "Maisara! Hiyo inatosha. Umeuzidisha kuvutiwa kwangu na Muhammad mara dufu! Hivyo nakuacha huru wewe na mkeo na pia ninakupa dirham mia mbili, farasi wawili na nguo ya thamani kuu!
Baadae alimweleza Waraqah bin Nawfal yale aliyoyasikia kwa Maisara, Nawfal alikuwa mtaalamu wa Bara Arabuni. Naufal akasema: "Mtu awaye na sifa hizi, atakuwa ndiye yule Nabii wa Uarabuni".[7]

Siku moja Bibi Khadija alikuwa ameketi nyumbani mwake akizungukwa na wajakazi na watumwa wake. Pia alikuwapo pale mmoja wa wanachuoni wa Kiyahudi. Kwa bahati Mtume (s.a.w.w.) alipata kupita pale na yule mwanachuoni wa kiyahudi akamwona. Mara moja akamwomba Bibi Khadija amshikilie Mtume Muhammad (s.a.w.w.) aahirishe kazi zake nyingine na ajiunge na kundi hilo lao, kwa kipindi kifupi hivi.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikubali ombi la yule Myahudi mwenye busara ambalo lilitegemezwa juu ya kuziona dalili za Utume kwake. Kisha Bibi Khadija alimgeukia yule Myahudi mwenye busara na kusema: "Ami zake watakapo tambua utafiti wako na uchunguzi wako wataudhihirisha upinzani wao, kwa sababu wanawachelea Wayahudi kuhusiana na mwana wa ndugu yao." Hapo mtaalamu wa kiyahudi akajibu hivi: "Je, yawezekanaje kwamba mtu yeyote yule amdhuru Muhammad, wakati mkono wa kudra umemlea kwa ajili ya Utume wa mwisho na kwa ajili ya mwongozo wa wanadamu?"

Bibi Khadija akasema: "Unasema kwamba atakishika cheo hiki kwa dalili gani?" Yule Myahudi mwenye busara akajibu: "Nimezisoma dalili za Mtume wa mwisho katika Torati. Dalili zake ni pamoja na mambo matatu; yaani wazazi wake watafariki dunia, babu yake na ami yake watamlea, na atachagua mke kutokana na mwanamke atakayekuwa Sayidati wa Waquraishi." Kisha akamuonesha kidole Bibi Khadija na akasema "Amebarikiwa (bibi) yule atakayepata heshima kuwa mwenzi wa maishani mwake!"[8]

Waraqa, ami yake Bibi Khadija, alikuwa mmoja wa watu wenye busara wa Uarabuni. Alikuwa na elimu kamili ya Biblia na kila mara alikuwa akisema: "Allah Atamwinua mtu fulani kutoka miongoni mwa

Waquraishi kwa ajili ya kuwaongoza wanadamu, naye atamwoa mmoja wa wanawake matajiri wa Waquraishi" Na kwa vile Bibi Khadija alikuwa mwanamke tajiri zaidi wa Waquraishi, alikuwa kila mara akimwambia Bibi huyu: "Itawadia siku ambayo utaolewa na mwanaume mtukufu zaidi hapa duniani!"

Usiku mmoja Bibi Khadija aliota kwamba jua lilikuwa likizunguuka juu ya mji wa Makkah na kisha likashuka pole pole na kutua nyumbani mwake. Alimsimulia Waraqah bin Nawfal ndoto yake ile naye Nawfal akaitafsiri ndoto ile hivi: "Utaolewa na mtu mkuu na atakuwa maarufu ulimwenguni kote."

Haya ndio matukio yaliyonukuliwa na baadhi ya wanahistoria na marehe– mu Allamah Majlis[9] na vile vile yameandikwa katika vitabu vingi vya historia. Matukio yote hayo yanapofikiriwa huzidhihirisha wazi wazi sababu za mwelekeo wa Bibi Khadija kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Mwelekeo huu ulikuwa hasa ni kutokana na itikadi ya Bibi huyu katika hali ya kiroho ya Mtume (s.a.w.w.) na kwamba yule 'mtu mwaminifu' alifaa zaidi kuliko wengineo, hakuna sababu yoyote nyingine katika kutokea kwa muungano huu.

## Mazingara Ya Posa Ya Bibi Khadija

Maelezo haya yanatosha kuthibitisha kwamba uchumba huu ulitoka upande wa Bibi Khadija mwenyewe; kiasi kwamba Ibn Hisham ananukuu[10] kwamba Bibi Khadija aliudhihirishia mwelekeo wake kwa hiari yake

na akasema: "Ewe binamu yangu! Kutokana na udugu uliopo baina yetu na ukuu wa heshima uliyonayo miongoni mwa watu wako na unyoofu, tabia njema na ukweli ulionao, ninaelekea kwako kwa moyo (wangu) wote ili unione." Yule 'mwaminifu' wa Waquraishi alijibu akisema: "Sina budi niwaarifu ami zangu jambo hili na jukumu hili halina budi kufanyika kwa ridhaa zao."

Wengi wa wanahistoria wanaamini ya kwamba Bibi Nafisa bint Alyah ndiye aliyelipeleka pendekezo la Bibi Khadija kule kwa Mtume (s.a.w.w.) la kutaka kuchumbiwa na Mtume (s.a.w.w.) kwa jinsi hii, Bibi Nafisah alisema:

"Ewe Muhammad! Kwa nini hukiangazi chumba cha usiku cha maishani mwako kwa nuru ya mke? Je, utakubali kama nikikualika kwenye urembo, utajiri, upole na heshima?" Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akajibu hivi: "Ni nini maana yako?" Hapo Bibi Nafisah akamtaja Bibi Khadija. Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Je, Khadija yuko tayari kwa jambo hilo wakati inapokuwapo tofauti kubwa baina ya hali ya maisha yangu na yake?" Bibi Nafisah akasema: "Ninayo mamlaka kwa niaba yake nami nitamfanya akubali, weka tarehe ya kulitimiza jambo hili ili kwamba walii wake (Amr bin Asad) akae pamoja nawe na jamaa zako na sherehe ya ndoa na tafrija viweze kufanyika.[11]

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alilizungumzia jambo hili na ami yake mheshimiwa (Abu Twalib). Ilifanyika tafrija kubwa iliyohudhuriwa na watu maarufu miongoni mwa Waquraishi. Jambo la kwanza kabisa Bwana Abu Talib alitoa hutuba, akiianza kwa kumhimidi Allah. Kuhusu yule mpwa wake, alimtambulisha

hivi: “Mpwa wangu Muhamamd bin Abdallah yu bora kuliko mtu yeyote wa kabila la Waquraishi atakayelin- ganishwa naye. Ingawa hana aina yoyote ile ya utajiri, hata hivyo mali ni kivuli kinachopita, na asili na nasaba ni vya kudumu.”12

Kwa kuwa Bwana Abu Twalib aliwataja Waquraishi na familia ya Hashim katika hotuba yake, Waraqah, ami yake Bibi Khadija aliijibu hotuba ile akasema: “Hakuna yeyote miongoni mwa Waquraishi aukanaye ubora wenu. Tunayo shauku ya kutaka kuikamata kamba ya utukufu wenu.” Hivyo sherehe ya ndoa hii ilifanyika na mahari ikaamuliwa kuwa ni dinar mia nne. Baadhi ya watu wanasema kwamba mahari ile ilikuwa ya ngamia ishirini.

**Umri wa Bibi Khadija:** Kwa kawaida inasemwa kwamba wakati wa kuolewa na Mtume (s.a.w.w.) Bibi Khadija alikuwa na Umri wa miaka arobaini na alizaliwa miaka kumi na mitano kabla ya ‘mwaka wa ndovu’ Hivyo baadhi ya waandishi wamesema kwamba umri wake mwenyewe wakati wa ile ndoa ulikuwa chini ya hapo. Kabla ya hapo aliolewa mara mbili. Majina ya waume zake yalikuwa ni Ais bin Abid na Abu Halah na wote wawili walikuwa wamefariki dunia.

1. Safinatul Bihar, chini ya neno ‘Nabi’
2. Bihaarul Anwaar, Juzuu 16, uk. 22.
3. Siirah Ibn Hisham, Juzuu 2, uk. 24.
4. Al- Kharaa’ij, uk. 186 na Bihaarul Anwaar, Juzuu 16, uk. 4.
5. Tabaaat-i-Kubra, uk..140.
6. Bihaarul Anwaar, Juzuu 15 uk. 18.
7. Siirah-i-Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 26.
8. Bihaarul-Anwaar, Juzuu 16, uk. 19.
9. Biharul-Anwaar, Juzuu 6, uk. 124
10. Siirah-i-Ibn Hisham. Juzuu 1, uk. 204.
11. Inafahamika vema kwamba Khuwaylid aliuawa katika vita vya Fujjar na kwa sababu hii ami yake aliidhinisha ndoa ile kwa niaba ya Bibi huyu. Hivyo basi, maoni yaliyotolewa na baadhi ya wanahistoria kwamba kwanza Khuwaylid hakukubali, lakini baadae alikubali kutokana na mwelekeo mkali wa Khadija, hayana msingi hata kidogo.
12. Manaaqib, Juzuu 1, uk 30 na Bihaarul-Anwaar, Juzuu 15, uk. 6.

# Sura Ya Kumi: Kuanzia Ndoa Hadi Utume

Kipindi cha maisha ya mwanadamu kilicho nyeti zaidi huanza pale anapopata makamu kiasi. Huwa hivyo kwa sababu hisia za kijinsia huufiikia ukamilifu wake, kila wakati tamaa za mwili huishawishi juhudi ya moyo kichwani mwake mtu, dhoruba ya ashki huitia giza hali ya hewa ya akili za mwanadamu, msingi wa kanuni za hisia za kimwili huwa thabiti zaidi na matokeo ya yote haya ni kwamba ile taa ya hekima hufifia. Katika kipindi cha mchana na usiku na mara kwa mara, kasiri kubwa la tamaa hujitwalia umbo thabiti machoni pa watu wazima.

Kama ikitokea kwa mtu fulani kuwa na utajiri pia katika kipindi kile, maisha huwa kitu cha hatari mno

kwake. Wakati hisia za kinyama na afya njema na bahati za kimaada na utajiri mwingi mno wa mtu vinapoungana, matokeo yake ni kwamba huujaza mpangilio wa maisha yake wingi wa matendo ya kiashki na amejawa na tamaa nyingi za kiashki bila ya kujali maisha ya baadae.

Kipindi hiki huitwa mpaka baina ya ustawi na upotovu, na mtu hufaulu kwa shida sana katika kujiamulia njia nyingine kwa ajili yake na katika kuchagua, kwa matumaini ya kujipatia tabia njema na fikara halisi, njia iwezayo kumsalimisha mtu kutokana na hatari zote.

Katika hali kama hiyo, huwa ni kazi ngumu mno kwa mtu kujihadharisha, na endapo mtu huyu hakulelewa na kuelimishwa vizuri katika mazingira ya kifamilia, basi mtu huyo hana budi kusubiri maanguko ya muundo wa maisha yake.

## Utu Uzima Wa Mtukufu Mtume (S.A.W.W)

Hakuna shaka yoyote ile kuhusu ukweli uliopo kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa shujaa, mwenye nguvu na afya njema, kwa sababu alilelewa kati- ka mazingira yasiyo na waa lolote, na wanafamilia wote wa ile familia alimozaliwa walikuwa na asili ya uhodari na ushujaa. Utajiri mkubwa wa Bibi Khadija alikuwa akiumiliki yeye vile vile na uwezo wote wa maisha mazuri ulikuwa mikononi mwake. Hata hivyo, lazima ifahamike ni kwa vipi alitumia mali hii ya kiulimwengu. Je, alijichagulia maisha ya anasa na je, alielekea kwenye kujitoshelezea matamanio yake, kama wafanyavyo vijana wengine? Au kwamba, ingawa alikuwa na njia na uwezo wote wa mali, alichagua mpangilio mwingine wa maisha yake ambao uliudhihirisha kikamilifu msingi wa maisha yake hisia halisi? Historia inashuhudia ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliyaongoza maisha yake kama watu mwenye busara na uzoefu walivyoishi. Daima alikuwa akiambaa ufisadi wa mali na uzembe na dalili za busara na tafakuri zilikuwa siku zote dhahiri usoni kwake. Ili kukaa mbali na ufisadi wa jamii aliutumia muda wake mwingi katika pango lililoko chini ya milima na kujifunza alama za uwezo wa Allah na kutafakari juu ya kuumbwa kwa ulimwengu.

## Hisia Za Utu Uzima Wake

Tukio moja lililotokea katika soko la Makkahh lilizijeruhi hisia za kiutu za Mtume (s.a.w.w.). Alimwona mtu akicheza kamari; kwa bahati mbaya mtu yule alimpoteza ngamia wake pamoja na nyumba yake kwa mchezo ule. Na si hayo tu, bali pia alijihatarisha na kuipoteza miaka kumi ya maishani mwake. Mtume (s.a.w.w.) alihuzunishwa mno na tukio hili kiasi kwamba hakukaa mjini Makkah siku ile. Hivyo basi, aliviendea vilima vya karibuni na hapo na kurudi mjini baada ya kupita sehemu ya usiku. Alihuzunishwa sana na kukiona kioja hiki cha kusikitisha na akafikiria sana na akashangazwa na utovu wa busara na hekima za watu hawa waliopotoka.
Kabla Bibi Khadija hajaolewa na Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) nyumba yake ilikuwa kitovu cha matimaini ya maskini. Na hata baada ya kuolewa kwake na Mtume (s.a.w.w.) hakuruhusu litokee japo badiliko lililo dogo mno katika hali ya nyumba yake au katika ukarimu wa utu wema wa mumewe.

Katika kipindi cha njaa na ukame, mama mlezi wa Mtume (s.a.w.w.), Bibi Halima alikuwa nyakati

nyingine akija kumsalimia mwanawe. Hapo, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na kawaida ya kutanda joho lake miguuni pa mama huyu akizikumbuka huruma zake na maisha ya kawaida aliyokuwa akiishi na Bibi huyu na kusikiliza yale aliyokuwa akisema. Wakati wa kuondoka kwake alimsaidia kwa kadiri ya uwezo wake.[1]

## Watoto Wake Watokanao Na Bibi Khadija

Kuzaliwa kwa mtoto huimarisha zaidi fungamano la ndoa na huyafanya maisha kuwa angavu na yenye kung'aa. Mkewe Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimzalia watoto sita. Wawili miongoni mwao walikuwa ni wanaume–mkubwa wao akiwa ni Qasim na mdogo ni Abdillah. Vile vile alizaa mabinti wanne, mwanahistoria ibn Hisham anaandika hivi:

"Binti wao mkubwa alikuwa ni Ruqayyah na wale watatu wengineo walikuwa ni Zainab, Ummi Kuluthum na Fatimah."[2] Wale watoto wa kiume walifari– ki dunia kabla ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kuanza kazi ya utume, lakini wale mabinti waliendelea kuishi."[3]

Kujizuia kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika matukio ya misiba kulikuwa kukijulikana sana. Hata hivyo, wakati wa vifo vya watoto wake wakati mwingine hisia za huzuni za moyoni mwake zilijidhihirisha machoni pake kwa njia ya kutiririkwa na machozi kwenye mashavu yake na jambo hili lilidhihirika mno wakati wa kifo cha Ibrahim ambaye mamake alikuwa ni Maria.

Wakati ule, moyo wake ulipokumbwa na huzuni, Mtume alikuwa akijishughulisha na kumhimidi Allah kwa ulimi wake. Alifanya hivyo sana kiasi kwamba mwarabu mmoja, kutokanana ujinga wake na utovu wa elimu juu ya misingi ya kanuni za Uislam, alipinga kulia kwa Mtume (s.a.w.w.). hata hivyo Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Kulia kwa aina hii ni neema."[4]

## Dhana Isiyo Na Msingi

Dakta Haikal ameandika hivi: "Hakuna ukanusho juu ya ukweli uliopo kwamba wakati wa kifo cha kila mmoja wa watoto wake Khadija aliiendea miungu (ya masanamu) na kuiuliza ni kwa nini miungu hiyo hikufurahishwa na kumbariki."

Kauli tuliyoinukuu hapo juu haiungwi mkono japo na ushahidi wa kihistoria ulio mdogo mno na si chochote ila ni dhana tupu.

Lengo lake ni kutoa dhana ya kwamba, kwa vile katika zama za Bibi huyu watu wote walikuwa wakiyaabudu masanamu, bila shaka Bibi Khadija naye alikuwa kama wao.

Hata hivyo, itikadi ya Kishi'ah ni kinyume na kauli hii na, kwa hivyo hali halisi nayo ni lazima iwe kama ile iaminiwayo na Mashi'ah. Sababu yake ni kwamba, bila shaka Mtume (s.a.w.w.) aliichukia ibada ya masanamu tangu utotoni mwake na hali hii aliidhihirisha wazi wazi katika msafara wake wa kwenda Sham. Kwa kuwa, alipopata kutofautiana na mfanyibiashara mmoja, kuhusiana na hesabu, na lile kundi

la pili likaapa kwa 'Laat' na 'Uzza'. Mtume (s.a.w.w) alisema: "Hivyo ndivyo vitu vibaya zaidi machoni mwangu!"

Katika hali hiyo, yawezaje kusemwa kwamba mwanamke kama Bibi Khadija, ambaye heshima na huba yake kwa mumewe haikuwa jambo la kutiliwa shaka, akimbilie kwenye masanamu (yaliyokuwa kitu kibaya zaidi machoni pa mumewe) wakati wa vifo vya wanawe. Aidha, sababu ya kuvutiwa kwake na Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na kule kujingiza kwake katika ndoa naye ni kuvutiwa kwake na tabia yake na mambo yake ya kiroho, kwa kuwa alisikia kwamba alikuwa ni Mtume wa mwisho. Katika hali hii, yawezekanaje kwamba aende na kuyalalamikia masanamu katika jambo hilo?" Tayari tulishawasimulia wasomaji wetu baadhi ya mazungumzo yake na Waraqa bin Nawfal (mnajimu wa kiarabu) pamoja na wanachuoni wengineo wa zama zile.

## Mwana Wa Kulea Wa Mtukufu Mtume (S.A.W.W)

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwita Zayd bin Haarith kuwa ni mwanawe kandoni mwa Jiwe Jeusi. Zayd alikuwa ni mtu aliyetekwa na maharamia wa kiarabu kutoka kwenye mipaka ya Sham na wakamwuza katika soko la Makkah na akanunuliwa na Hakim, jamaa yake Bibi Khadija. Hata hivyo haifahamiki dhahiri jinsi ilivyotokea baadaye hadi akanunuliwa na Bibi Khadija.

Mwandishi wa kitabu '*Hayaat Muhammd*' anasema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amepatwa mno na vifo vya wanawe, na ili ajiliwaze, alimwomba Khadija amnunue Zayd. Baadae Mtume (s.a.w.w.) alimpa uungwana na akamlea kama mwanawe hasa."

Hata hivyo, wengi wa waandishi wanasema kwamba wakati wa ndoa ya Bibi Khadija na Mtume Muhammad (s.a.w.w.), Hakim bin Hizaam alimpa shangazi yake (Khadija) huyu zayd. Kwa kuwa Zayd alikuwa kijana mwema na mwenye akili, Mtume alianza kumpenda na Bibi Khadija naye alimpa Mtume (s.a.w.w.) kijana huyu akiwa ni zawadi. Hata hivyo, mwishowe baba yake Zayd alitambua aliko mwanae (Zayd) baada ya kumtafuta kwa muda mrefu. Hapo Mtume (s.a.w.w.) alimruhusu Zayd arudi makwao na baba yake. Hata hivyo, kutokana na huba na upole wa Mtume (s.a.w.w.) juu yake, Zayd alipendelea kubakia na Mtume (s.a.w.w.). hii ndio sababu kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimpa uungwana, na kumchukua akiwa kama mwanawe hasa na akamwoza Zaynab, bint Jahsh.[5]

## Mwanzo Wa Tofauti Miongoni Mwa Wenye Kuabudu Masanamu

Kutokana na uteuzi wa Mtume (s.a.w.w.) kuishika kazi ya Utume, kulitokea kutofautiana kwingi miongoni mwa wakuraishi, ingawa msingi wa tofauti hizi ulijengeka zamani sana, na hata kabla ya uteuzi huu wa Mtume (s.a.w.w.), kiasi fulani watu wenye busara waliidhihirisha chuki yao na kutoipenda dini ya Waarabu.
Daima ilikuwako kauli katika kila pembe na ufa juu ya Nabii wa Uarabuni aliyekuwa akisubiriwa, ambaye atazihuisha ibada za Allah Aliye mmoja tu. Wayahudi walikuwa wakisema: "Kwa kuwa msingi wa dini yetu na ile ya yule Nabii wa Uarabuni ni moja, tutamfuata, na kwa msaada wa nguvu zake tutayavunja

masanamu na kulivunja jumba la ibada ya masanamu.

Ibn Hisham anasema katika *Sirah* yake:6 "Wayahudi walikuwa na kawaida ya kuwaogofya Waarabu waliokuwa wakiyaabudu masanamu wakasema kwamba wakati wa kudhihiri kwa Nabii wa Uarabuni ulikuwa ukikaribia upesi sana na atalibomoa jengo la ibada ya masanamu. Mbele ya

Waarabu, maneno haya yalitoa mandhari ya mapinduzi ya zama za ibada ya masanamu. Yalitoa mno picha hii kiasi kwamba kufuatana na mafunzo ya awali ya Wayahudi, baadhi ya makabila yatauitika mwito wa Mtume (s.a.w.w.) na kusilimu. Hivyo, kutokana na sababu fulani fulani tutakazozieleza baadae, Wayahudi waliendelea na ukafiri wao. Aya ifuatayo ya Qur'ani Tukufu inaizungumzia hali hii:

وَلَمَّا جَاءَهُمْ كِتَابٌ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ مُصَدِّقٌ لِمَا مَعَهُمْ وَكَانُوا مِنْ قَبْلُ يَسْتَفْتِحُونَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا فَلَمَّا جَاءَهُمْ مَا عَرَفُوا كَفَرُوا بِهِ ۚ فَلَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الْكَافِرِينَ {89}

***"Na kilipowajia kitabu** (**Qur'ani**) **kutoka kwa Allah kiyasadikishayo yale yaliyo pamoja nao** (**Torati**)**, na zamani walikuwa wakiomba ushindi dhidi ya makafiri; lakini yalipowafikia yale waliyoyajua waliyakana; basi laana ya Allah iko juu ya makafiri."*** (***Sura al- Baqarah, 2:89***)**.**

## Misingi Ya Ibada Ya Masanamu Yatikisika

Katika wakati wa sherehe ya moja ya sikukuu za Waquraishi lilitokea tukio la ajabu ambalo machoni pa watu waonao mbali, liliigonga kengele ya hatari ya kupinduliwa kwa utawala wa wenye kuabudu masanamu. Safari moja wakati wenye kuabudu sanamu walipolikusanyikia sanamu moja na walikuwa wakiyasugua mapaji ya uso ardhini mbele ya sanamu lile, wanne miongoni mwa watu wao maarufu waliokuwa mashuhuri kwa elimu na busara zao, walikikataa kitendo chao hicho na wakaendesha mjadala juu ya jambo hili katika sehemu ya faragha.

Moja ya jambo walilolijadili lilikuwa kwamba taifa lao limepotoka kutoka kwenye njia ya Ibrahim; na mawe waliyoyazunguuka watu hayasikii, wala kuona wala kuwatendea jema lolote wala dhara7 Watu hawa wanne walikuwa ni:

(1) Waraqah bin Nawfal, ambaye baada ya kusoma sana akawa Mkristo na akajipatia elimu pana juu ya Biblia,
(2) Abdallah bin Jahash aliyesilimu baada ya kuanza kwa Uislam na akahamia Ethiopia pamoja na Waislamu wengine,
(3) Uthman bin Huwayris aliyekwenda kwenye mahakama ya Kirumi na kuin- gia Ukristo,
(4) Zayd bin 'Amri bin Nafil, ambaye baada ya kujipatia elimu ya kutosha, alijichagulia dini ya Ibrahim.

## Unyonge Mwingine Wa Waquraishi

Wakati ule Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na umri usiozidi miaka thelathini na mitano, alipolazimika kuuona ugomvi mkubwa miongoni mwa Waquraishi ulioamuliwa kwa mkono wake Mtume (s.a.w.w.) wenye uwezo. Tukio lifuatalo laonesha jinsi Waquraishi walivyokuwa wakimheshimu na kumkubali kuwa yu mwaminifu na mkweli:

Mafuriko yenye kuogofya yalitiririka kutoka kwenye milima mirefu yakiielekea nyumba ya Allah, na kutokana nayo hakuna hata nyumba moja miongoni mwa nyumba za Makkahh hata ile Al-Ka'ba Tukufu Iliyosalimika kutokana na uharibifu ulioletwa na mafuriko hayo. Nyufa nyingi zilitokea katika kuta za Al-Ka'ba. Hivyo Waquraishi wakaamua kuijenga upya ile Al-Ka'ba lakini walichelea kuibomoa. Walid bin Mughayrah alikuwa mtu wa kwanza aliyechukua sululu mkononi mwake na akazibomoa nguzo mbili za Al-Ka'ba. Hapa akajihisi kuwa yu mwenye kuogopa mno na mwenye mashaka.

Watu wa Makkahh walikuwa wakisubiri kupatwa na msiba fulani, lakini walipoona kwamba Walid hakuipata ghadhabu ya masanamu, walipata matumaini ya kwamba kitendo chake kile kilipata kibali cha masanamu. Matokeo yake ni kwamba wote walijitia katika kazi ya kulibomoa lile jengo. Kwa bahati, katika siku ile ile, meli iliyotoka Misri iliyomilikiwa na mfanya biashara mmoja wa Kirumi ilipinduka kwenye bandari iliyopo karibu na Makkahh (Jiddah) kutokana na dhoruba kali. Waquraishi walipata taarifa za tukio hilo. Hivyo basi wakawapeleka watu Jiddah ili wakanunue mbao za meli ile kwa ajili ya ule ujenzi wa Al-Ka'ba. Ama huhusu kazi ya ujenzi walimwajiri mjenzi wa Kimisri aliyekuwa akikaa mle mjini Makkahh.

Kuta za Al-Ka'ba zilifikia urefu wa mwanadamu. Sasa ukafika wakati wa kuliweka lile Jiwe Jeusi kwenye sehemu yake. Katika hatua hii, ziliibuka tofauto miongoni mwa machifu wa makabila na kabila la Bani Abduddar na Bani Adi walifanya mapatano ya kwamba hawatamruhusu mtu yeyote mwingine kuifaidi heshima hii. Ili kuyaimarisha mapatano yao hayo, walikijaza damu chombo fulani na wakachovya mikono yao humo.

Kutokana na hali hii, ile kazi ya ujenzi ilisimama kwa kipindi cha siku tano. Jambo hili lilifika katika hali mbaya. Makundi mbali mbali ya Waquraishi yalikusanyika kwenye Masjid ul Haraam na likawapo tishio la kuzuka kwa ugomvi wa kumwaga damu.

Hata hivyo, hatimaye mzee mmoja mwenye kuheshimika kutoka miongoni mwa Waquraishi, aliyeitwa Abu Umayyah bin Mughyrah Makhzumi aliwakusanya machifu wa Kikuraishi na kuwaambia: "Mkubalini kuwa mpatanishi yule mtu atakayeingia (humu Masjidul Haraam) kupitia lango la Safa (kufuatana na baadhi ya vitabu vya historia ni Babus Salam)." Machifu wote waliukubali ushauri huu. Mara Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) akaingia Masjidul Haraam kupitia lango lile. Wote wakasema kwa pamoja: "Ni Muhammad, mtu mwaminifu. Tunakubali awe mpatanishi!"

Mtume (s.a.w.w.), ili kuumaliza ugomvi huu, aliwaomba walete shuka. Aliliweka lile Jiwe Jeusi katika ile

shuka kwa mikono yake na kisha akashauri kila mmoja wa wale machifu wanne wa Makkahh ashike pembe moja ya ile shuka. Lile Jiwe Jeusi lilipoletwa karibu na ile nguzo (ya kuwekea), Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akaliweka katika sehemu yake kwa mikono yake ya heri.

Kwa njia hii aliumaliza ugomvi ule wa Waquraishi uliokuwa ukingoni mwa kuzaa tukio la umwagaji wa damu.8

1. Siirah-i-Halabi, Juzuu 1, uk. 123.
2. Kuna tofauti kubwa kuhusu mabinti watatu wa Mtukufu Mtume, yaani Zainab, Ummu Kulthum na Ruqayyah.
3. Manaqib Ibn Shihr Ashub, Juzuu 1, uk. 140; Qurbul Asnad uk. 6-7; al- Khisaa'il, Juzuu 2, uk. 37; Bihaarul-Anwaar, Juzuu 22, uk. 151-152. baadhi ya wanahistoria wanasema kwamba wana wa kiume wa Mtume (s.a.w) walikuwa zaidi ya wawili (Tarikh-i-Tabari, Juzuu 2, uk. 35 na Bihaarul-Anwaar, Juzuu 22; uk. 166.
4. Amaali, Shaykhal-Mufid, uk. 247.
5. Al-Isaba, Juzuu 1, uk. 545; Usudul Ghabah, Juzuu 2, uk. 224.
6. Siirah-i-Ghabah, Juzuu 1, uk. 231
7. Siirah-i-Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 222-223.
8. Mtu mmoja aliyeitwa Habirah bin Wahab Makhzumi ameliandika tukio hili katika hali ya shairi katika wasifu aliouandika. Siirah-i-Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 213; Tarikh-i-Tabari, Juzuu 2; Furu'l Kafi, Juzuu 1, uk. 225; na Bihaar Anwaar, Juzuu 15, uk. 39-41. Inafaa kuona kwamba, wakati wa ujenzi wa Ka'bah, wale wote waliohusika wali- pashwa habari kama ifuatayo: "Katika ujenzi wa Al-Ka'ba tumieni mali mlizoji- patia kwa njia ya halali. Fedha mliyoichuma kwa njia isiyo sahihi au kwa rushwa au kwa dhuluma isitumike kwa lengo hili." Bila shaka fikara hii ndio hasa masim- bi ya mafundisho ya Mitume yaliyokuwa bado yamesalia miongoni mwa Waquraishi.

# Sura Ya Kumi Na Moja: Udhihiriko Wa Kwanza Wa Ukweli

Kwa kweli, kimsingi historia ya Uislamu huanzia kwenye ile siku ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipewa amri ya kuianza kazi ya Utume na kuleta mfululizo wa matukio katika mkondo wake. Siku ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipewa amri ya kulianza jukumu la kuwaongoza watu na maneno: "Wewe ni mjimbe wa Allah" yalikuwa yakigonga masikioni mwake, alilibeba jukumu lililo kuu lililobebwa na Mitume wote wa awali (a.s.). katika siku ile, sera ya yule 'mtu mkweli' wa Waquraishi ilifahamika vizuri na lengo lake likajidhihirisha zaidi. Kabla ya kulisikia tukio la kwanza la Utume wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ni muhimu kwamba tuyaeleze mambo muhimu mawili:

1. Umuhimu wa kuteuliwa kwa Mitume.

2. Mvuto wa Mitume katika kuitengeneza jamii.

## Umuhimu Wa Kuteuliwa Kwa Mitume

Allah Mwenyezi Amedukiza njia za maendeleo na ukamilifu katika maum- bile ya kila kiumbe na amekisheheneshа na nyenzo mbalimbali za msaada kwa ajili ya kupita katika njia iendayo kwenye ukamilifu. Hebu utupie jicho mche mdogo. Idadi kubwa ya visababisho hufanya kazi kwa ajili ya ukamilifu wake. Mizizi ya mche huu hufanya kazi kwa kadiri ya uwezo wake wote kuupatia chakula chake na kuupatia mahitaji yake yote na mishipa yake mbalimbali hutawanywa kwa kadiri ihitajikayo majimaji ya chakula miongoni mwa matawi na majani yake.

Hebu litizame umbo lake ni lenye kushangaza zaidi ya lile la miti mingine. Bakuli la ua huifanya kazi ya kuufunika uso wa chipukizi na kuyahami majani ya ua (petals) na rangi yake. Kadhalika sehemu nyingine za ua lile, ambazo zote zimeteuliwa kwa ajili ya kukilisha kiumbe chenye uhai na zinayatekeleza majukumu yao kwa njia iliyo bora zaidi kwa kadiri ya uwezo wao. Na kama ukienda hatua moja na kulitupia jicho umbo lishangazalo la ulimwengu wa wanyama utaona kwamba visababisho viwezeshavyo kuifikia mipaka ya ukamilifu viko pamoja nao.

Kama tukitaka kuelezea jambo hili kisayansi, tutasema kwamba ujuzi wa uhai, ambao ni baraka ya utendaji kazi wa maumbile, wamepewa viumbe wote. Qur'ani Tukufu imeueleza muongozo huu wa kweli kwa maneno haya:

**"Yeye (Allah) Ameumba kila kiumbe na akakifunza jinsi ya kuishi"**

Viumbe vyote, tangu kwenye chembe ndogo ya uhai (atom) hadi makundi makubwa ya nyota ya ulimwengu, vina fungu lao katika baraka hii. Allah baada ya kuchukua kipimo kamili ameionyesha njia ya ukamilifu na maendeleo yake ya polepole na ameainisha vipengele kwa ajili ya mafunzo na mabadiliko (*evolution*) ya kila kiumbe. Na huu ndio haswa 'mwongozo kwa ajili ya uwepo' ambao hutawala viumbe wote wa ulimwengu bila tofauti yoyote.

Hata hivyo, swali huibuka hapa kuhusu kama huu msukumo wa kimaum- bile juu ya kuwepo hutosheleza pia kwa kiumbe kile, ambao ndio bora kuliko vyote. Bila shaka sivyo hata kidogo. Sababu yake ni kwamba, ukiachilia mbali yale maisha ya kimaada, vile vile mwanadamu anayo maisha mengine ambayo ndio hasa msingi wa kuwepo kwake. Kama mwanadamu ataishi maisha ya kimaada tu na yasiyo na akili, kama jamii ya wanyama na ya miti, basi vile vipengele vya kimaada vingalitosha kwa mwendo wake, maendeleo na ukamilifu. Hata hivyo, kwa vile ametokea kuwa na maisha aina mbili, siri ya ustawi wake na utukufu umo katika ukamilifu wa maisha yote hayo.

Mtu wa kwanza wa kawaida ambaye aliishi kwenye mapango na kuwa na hali ya asili halisi, na ambaye katika silika yake ya kimaumbile hakuna upotovu hata kidogo uliotokea, mtu huyu hakuhitaji mafunzo makubwa kama yale ayahitajiyo mtu aliye staarabika.

Hata hivyo, mwanadamu anapoichukua hatua ya kwenda mbele na akayabadilisha maisha yake na

kuwa ya mkusanyiko mmoja, pia wazo la ushirikiano likajikita imara vizuri maishani mwake na kulitawala, basi kukengeuka ambako ni matokeo ya mgongano wa kijamii na mawasiliano hutokea katika nafsi yake, na tabia mbaya na fikara zisizo sahihi huichukua nafasi ya kiini cha fikara za asili na kuvuruga awiano na usawa wa jamii.

Mikengeuko hii humfanya Muumba wa huu ulimwengu alete waelimishaji wairekebishe jamii na kuyapunguza maovu ambayo ni matokeo ya wanadamu wanapoishi pamoja, ili kwamba, kutokana na taa ziangazazo na sheria za uadilifu, waweze kuongoza jamii kwenye njia iliyonyooka, ambayo huhakikisha ustawi wa watu wote wenye ustadi katika kila fani.

Haipingiki kwamba, kuishi kwa pamoja, licha ya kuwa kwake na faida, vile vile kunabeba maovu fulani na kunaleta mikengeuko mingi. Kwa sababu hii, Allah Mwenyezi, ameleta waalimu ili kwamba waweze kuipunguza mikengeuko na ukaidi, kwa kadiri iwezekanavyo, na kuliweka gurudumu la jamii katika njia sahihi kwa kuweka sheria za dhahiri.[1]

## Jukumu La Mitume Katika Kuitengeneza Jamii

Kwa kawaida inadhaniwa kwamba Mitume ni waalimu wa ki-Mungu ambao wanateuliwa ili kuwaelimisha watu. Watu hujifunzia kwenye shule za Mitume na njia zao za kijamii na tabia zao zimeelekezwa kwenye ukamilifu wa polepole kuelekea kwenye mwelekeo ulio sambamba na mafunzo ya wale viumbe waliobora zaidi. Ni kama kijana wa kiume aji- funzaye mambo mengi kwenye shule ya msingi, ya kati, chuo na chuo kikuu na anasogea siku hadi siku, ingawa katika siku ya kwanza hakuwa hata na picha japo ndogo ya mafunzo haya akilini mwake.

Hali kadhalika watu huipata elimu kutoka kwenye shule za Mitume, na sambamba na kuelimika kwao kutoka kwa Mitume, tabia zao na maisha yao ya kijamii hujipatia ukamilifu. Hata hivyo, tunaona kwamba Mitume ni waelekezaji wa watu. Kazi na jukumu lao ni kuwapa mazoezi na wala si kuwaelimisha, na kwamba msingi wa dini na sheria zao mkabala na mtazamo wao wa kimaumbile si kitu kipya au zawadi mpya. Na kama maumbile hayakukengeuka, na kama ujinga na tamaa ya mali haukuyakumba, yangetambua asili ya Sheria ya Mungu.

Hakika, yale tuliyoyasema hapo juu yametegemeana na kauli za viongozi wakuu wa Uislamu. Imam Ali, Amiri wa waumini (a.s.) amesema katika *Nahjul Balaghah* kuhusu lengo la Mitume hivi:"Yeye (Allah) amewateuwa Mitume kutoka miongoni mwa kizazi cha Adamu na akachukua ahadi kutoka kwao ya kuupeleka ufunuo kwa watu na kueneza ujumbe ambao wameaminishwa nao.

Amewapeleka ili wawaambie watu watimize ahadi yao ya kimaumbile na kukumbuka baraka walizozisahau. Aidha, kwa mafundisho yao, wao (Mitume) wawape watu onyo na kuwataka wazichimbue johari za hekima zao, kitu kilichosalia kwenye hali ya kufichikana katika hazina ya maumbile yao."[2]

## Mfano Wa Dhahir

Tunapodai kwamba kazi iliyofanywa na Mitume katika kuwafunza na kuwatengeneza watu ni sawa sawa na ile inayofanywa na mkulima wa bustani anayeulea mti, au tunaposema kwamba, kutokana na kuwaongoza watu na kufungua mtazamo wao wa kimaumbile, Mitume ni kama wataala- mu wa madini wanaochimba madini yenye thamani kutoka kwenye kiini cha milima, wala hatulisemi jambo lenye kupita kiasi (au kutia chumvi).

Jambo hili laweza kuelezwa hivi: Tangu katika hatua ya kwanza ya matengenezo ya kiini cha mmea, utakuwa na kila aina ya uwezo wa maendeleo ya kukua na kupevuka. Mara tu baada ya mmea huu kuanza kufanya kazi ya kuimarisha mizizi yake, kila aina ya utendaji wa mitambo ya madawa hewani na upatikanaji wa nuru na mabadiliko hutokea katika mmea mzima. Katika hatua hii, yule mkulima wa bustani anatakiwa afanye mambo mawili. Kwanza lazima afanye mambo muhimu yapatikane kwa ajili ya kuimarisha mizizi ili kwamba nguvu ya fichu ya mmea iweze kukua.

Pili, hana budi kuizuia mikengeuko, ili kwamba, kama nguvu ya ndani ya mmea ule ikichukua hatua inayozuia ustawi wake, hana budi kuikata. Hivyo basi, si kazi ya yule mkulima wa bustani kuufanya mmea ule ukue. Kinyume na hivyo, kazi yake ni kutoa na kuthibitisha kwamba zinapatikana hali zilizo muhimu ili kwamba ule mmea uweze kuufunua ukamilifu wake wa fichu.

Muumba wa huu ulimwengu alimuumba mwanadamu na akamjaalia nguvu nyingi na utashi wa kimaumbile. Ameurekebisha utashi wake (mwanadamu) wa kimaumbile kwa nuru ya upweke, na ibada ya Allah, pamoja na hisia za uadilifu, haki na upole na silika za kazi na juhudi. Mbegu hizi huanza kuota kwa kujiendesha zenyewe moyoni mwa mwanadamu. Hata hivyo, maisha yake ya kijamii huleta mkengeuko moyoni mwake. Silika ya kazi na juhudi hulitwalia umbo la choyo na tamaa ya mali, huba ya ustawi na maisha hujitokeza katika umbo la choyo na tamaa ya kuikuza hali yake, na ile nuru ya upweke wa Allah na ibada yake hujit- walia vazi la ibada ya miungu wa uongo.
Katika hali hii, Wajumbe wa Allah humpatia mwanadamu nuru ya ufunuo na mpango wenye hali sahihi za ukuaji na maendeleo, na kuurekebisha uasi wa silika.

Kama ulivyoona, Amiri wa Waumini (a.s.) amesema: “Mwanzoni mwa uumbaji (wa huu ulimwengu) Muumba alichukua ahadi inayoitwa ‘ahadi ya viumbe’ au ‘Angano la viumbe na maumbile.’ Ni nini lengo la ahadi hii ya viumbe? Lengo lake ni kwamba Allah Mwenyezi, baada ya kuwapa wanadamu mamia ya silika zenye faida na kwa kuchanganya na utashi wao, korija za tabia njema ziliichukua ahadi ya kimaumbile kutoka kwao kwamba watazifuata silika na tabia njema. Kwa mfano, kumpa kwake mwanadamu macho, kuna maana ya aina fulani ya kuichukua ahadi yake kwamba hatatumbukia kisimani.

Hali kadhalika, kule kumpa hisia za kumtambua Allah, na ile ya kutenda uadilifu n.k ina maana ya kupata ahadi yake ya kwamba atakuwa mchamungu na mwaminifu. Kazi ya Mitume ni kwamba wawashauri wanadamu wayatende mambo yao kwa mujibu wa ushuhuda wa uhai na kulipasua pazia la

bahati mbaya liwekwalo juu ya maumbile yake. Ni kutokana na sababu hii kwamba inasemekana ya kuwa msingi wa dini za kimbinguni unaundwa na mambo ya kimaumbile.

Unaweza kusema kwamba mwanadamu yu kama mlima wenye mawe ya thamani na chembe za dhahabu zilizojificha humo kama vile ambavyo wema, ujuzi, na maadili yamefichwa ndani ya maumbile ya mwadamu katika sura mbali mbali. Wakati Mitume na waaminio mizimu wanapouchunguza mlima wa moyo wetu kwa uangalifu sana wanaona kwamba umeungwa na idadi fulani ya sifa njema na fikara na hisia safi. Kisha wanaugeuza kwenye dharura ya maumbile kwa mafundisho na mipango yao. Wanaukumbusha maamrisho ya maumbile na dhamiri. Wanaulingania usikivu wa mwanadamu kwenye sifa njema za utu ulioji- ficha ndani mwake.

## 'Mwaminifu' Wa Waquraishi Akiwa Katika Mlima Hira

Mlima Hira uko Kaskazini mwa mji wa Makkahh na mtu anaweza kuki- fikia kilele chake katika muda wa nusu saa. Uso wa mlima huu una mabamba ya jiwe jeusi na hakuna dalili zozote za uhai zionekanazo mlimani humo. Katika sehemu yake ya kaskazini kuna pango liwezalo kufiki- wa na mwanadamu baada ya kuyapita mawe. Kimo chake ni kama kimo cha mwanadamu. Mwanga wa jua hupenya hadi kuifikia sehemu ya pango hili na sehemu yake iliyosalia daima huwa yenye giza.

Hata hivyo, pango hili lenyewe ni ushahidi wa matukio kama hayo ya kuhusu rafiki yake wa karibu kwamba hata katika siku hizi, watu huharak- isha kwenda huko kwa shauku kuu ili kuyasikia matukio haya kutokana na lugha yake ya kimya kimya na kukifikia kizingiti chake baada ya kuzipata taabu nyingi, na ili kuchunguza kutoka pango hili kuhusu taarifa za tukio la ufunuo, pamoja na kuhusu sehemu ya maisha ya yule mfadhili mkuu wa wanadamu. Na lile pango nalo linajibu kwa ile lugha yake ya kimya kimya; "Hii ndiyo maabadi (sehemu ya kuabudia) ya yule mheshimiwa wa Waquraishi.

Kabla ya kuianza kazi ya Utume alizitumia humu siku na mikesha mingi. Ameichagua sehemu hii iliyokuwa mbali na makelele, kwa ajili ya sala na ibada. Aliutumia mwezi mzima wa Ramadhani humu na kwenye nyakati nyinginezo alikimbilia katika sehemu hii kila mara.

Alifanya hivi mno kiasi kwamba mkewe mpenzi alijua kwamba asiporudi nyumbani atakuwa akijishughulisha na ibada kwenye mlima Hira. Na alipowatuma watu huko kwenda kumtazama walimkuta akitafakari na kusali kwenye sehemu hii."
Kabla ya kuianza kazi ya Utume alikuwa na kawaida ya kutafakari sana juu ya mambo mawili:

1. Alichunguza kwa makini mfumo wa maumbile na sayari zenye kung'aa, uwezo na usanii wa Allah katika maumbile ya kila kiumbe chenye uhai.

2. Kwa kufanya uchunguzi wa kina zaidi juu ya anga na nyota na kuvifikiria kwa busara viumbe vyote vya duniani, basi kila siku alikuwa akilikaribia karibu zaidi lile lengo lake.

Alitafakari juu ya jukumu zito ambalo alijua kwamba atalibeba. Pamoja na ubovu na uoza wa jamii ya

binadamu ya zama zile, hakuyafikiria mageuzi yake kuwa ni jambo lisilowezekana. Hata hivyo, utiliaji nguvu wa mpango wa kuitengeneza jamii nako hakukukosa matatizo na magumu yake. Hivyo basi, aliyatazama maisha yaliyochafuka ya watu wa Makkah na anasa za Waquraishi na akatafakari juu ya njia na jinsi ya ubadilishwaji wao.

Alishangazwa na watu kuabuduo masanamu yasiyo na uhai wala uwezo, na kuonyesha unyonge wao mbele yao na hapo dalili za kutokuwa na raha zilijidhihirisha usoni mwake. Hata hivyo, kwa vile alikuwa bado Hajaamrishwa kuielezea hali halisi, alijizuia kuielezea kwa watu wale.

## Kuanza Kwa Ufunuo

Malaika mmoja aliteuliwa na Allah kumsomea 'yule mwaminifu' wa Waquraishi aya chache ikiwa ni mwanzo na utangulizi wa kitabu cha mwongozo na ustawi, hivyo basi, ili kumpa 'mwaminifu' heshima kwa kumpa vazi la Utume. Malaika Mkuu Jibril mwenyewe na ile siku yenyewe ilikuwa ni ile siku ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kuteuliwa kuishika kazi ya Utume. Tutazungumzia juu ya lengo la siku ile hapo baadae.

Hakuna shaka juu ya ukweli uliopo kwamba kumkabili malaika kunahitaji matayarisho maalum. Mpaka pale tu moyo wa mtu uwapo mkuu na wenye nguvu hataweza kuvumilia kukutana na Malaika.

Yule 'Mwaminifu wa Waquraishi' amejipatia matayarisho kama hayo kwa njia ya sala ndefu, kutafakari sana na baraka za Allah, kama ilivyoelezwa na waandishi wengi wa Sirah, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), hata kabla ya kuteuliwa kuianza kazi ya Utume, aliota ndoto zilizokuwa za dhahiri kabisa kama mwanga wa mchana. Baada ya muda fulani masaa yaliyokuwa ya kupendeza sana kwake yalikuwa yale ambayo ndani yake alisali akiwa katika hali ya kujitenga.

Alizipitisha siku zake katika hali hiyo hadi katika siku maalumu, Malaika alimwekea ubao wa maandishi karibu naye na kusema: "Soma" Na Mtume (s.a.w.w.) kutokana na ukweli kwamba hakujua kusoma na kuandika, na hakujifunza kusoma na kuandika, alijibu ya kwamba hajui kusoma. yule malaika Mkuu akambana kwa nguvu[3] na kisha akamtaka asome. Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) alilirudisha jibu lilelile. Yule Malaika akambana tena kwa nguvu.
Kitendo hiki kilirudiwa mara tatu kwa ghafla alijihisi mwilini mwake kwamba anayaweza kuyasoma yale maandishi yake yaliyoko katika ule ubao ulioshikwa na yule Malaika. Hapo akazisoma aya zifuatazo ambazo kwa hakika huhesabiwa kuwa ni utangulizi wa kitabu cha ustawi wa mwanadamu.

{اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ {1

{خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ {2

{اقْرَأْ وَرَبُّكَ الْأَكْرَمُ} 3

{الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ} 4

{عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ} 5

***"Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba (kila kitu). Alimuumba mwanadamu kutokana na tone la damu! Soma na Mola wako ni Mkarimu. Ambaye Alimfunza mwanadanmu kuandika kwa kalamu yale asiyoyajua." (Surah al-Alaq, 96:1-5).***

Malaika Mkuu Jibril akaimaliza kazi yake na baada ya ule ufunuo, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) naye akashuka kwenye mlima ule wa Hira na akaenda akiielekea nyumba ya Bibi Khadija.[4]

Aya tulizozinukuu hapo juu zaonyesha waziwazi mpango wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa maneno machache, na kusema kwa dhahiri kwamba msingi wa dini yake unapatikana kwa kusoma na kujifunza na hekima na matumizi ya kalamu.

## Ulimwengu Kama Unavyoonekana Kwa Myakinifu

Maendeleo yanayoongezeka daima ya sayansi ya kawaida yamechukua kutoka kwa wanachuoni wengi ile nguvu ya kuingia ndani zaidi katika mambo ya kiroho yaliyo nje ya mipaka ya kalamu na sayansi ya kawaida na wamezizuia nuru zao. Wanadhania kwamba huu ulimwengu wa kimaada ndio ulimwengu pekee na chochote kile kisicho maada hakina faida yoyote. Kufuatana na maoni yao, chochote kile kisichoungana na kanuni za maada ni dhana tu na uongo.

Haina kupinga hapa kwamba wanasayansi hawa hawana ushahidi wowote juu ya kutokuwepo kwa ule ulimwengu mwingine ambao ndiko unakotoka ufunuo na msukumo. Yale wayasemayo tu ni haya: "Majaribio, maono na sayansi ya maumbile havituongozi kwenye jambo hili (yaani ule ulimwengu mwingine) na havitupi taarifa juu ya kuwako kwake. Kwa mfano, wanapokana kuwapo kwa roho itokayo, wanasema: "Kitu hicho hakionekani chini ya kisu cha uchambuzi wetu, na dalili za viumbe vya aina hii hazipatikani katika maabara yetu chini ya darubini na hivyo basi, kwa vile zana zetu za siku hizi hazituongozi kwenye vitu hivi si lazima kwamba viwe na uhai wa nje (ya huu wa duniani)."

Aina hii ya kufikiria ni pungufu, yenye ila na iliyochanganyika na upuuzi, ambayo 'kutokuwepo' kumeamuliwa au kuhesabiwa kuwa ni 'kutokuwa na ufahamu' na kwa vile zana walizonazo walimwengu hazifikishi kwenye hali halisi wanazoamini wale wanachuoni wamwaminio Allah, wao (wayakinifu) wanadhani kwamba zote hazina msingi.

Hakuna shaka juu ya ukweli kwamba wayakinifu hawajafaulu kuutambua ukweli wa yale wayasemayo

wanachuoni wa kidini kuhusu kuwako kwa Muumba, achilia mbali vitu vingine vya kimetafizikia.

Na inajitokeza kwamba kama hayo makundi makuu mawili (wanasayansi na wanadini) yakifanya midahalo katika hali ifaaayo, iliyo huru kutokana na chuki na kiburi, umbali baina ya uyakinifu na Dini utatoweka upesi sana na zile tofauti zilizowagawa wanachuoni katika makundi mawili zitatoweka.

Wale wamwabuduo Allah wametoa sababu kadhaa kuhusu kuwako kwa Allah Mwenyezi na wamethibitisha ya kwamba hizi hizi sayansi za kimaumbile zimewaongoza kwa yule Aliye mjuzi wa yote na huu utarati- bu wa ajabu unaozitawala sehemu za ndani na za nje za viumbe vyote, ndani yake mna uthibitisho wa kuwapo kwa Muumba. Vitu vyote hapa ulimwenguni, tangu lile kundi la nyota liitwalo 'Milky Way' hadi chembehai (atom), vinasogea kwa kufuatana na nyororo ya sheria zenye utaratibu maalum na katu haiwezekani maumbile yasiyoona wala kusikia yawe ndio chanzo na kidumisho cha utaratibu wa ajabu kiasi hiki. Na ni haja hii ya 'utaratibu mzuri wa ulimwengu' iliyo msingi wa korija za vitabu na majarida yachapishwayo na wanachuoni wa kiislamu.

Na kwa vile hoja hii ni yenye kueleweka na iwezayo kutumiwa na matabaka mbalimbali, mengi ya maandishi ya maumbile ya vitu vyote yametengenezwa na hoja hii na kila mtu aitegemea katika njia moja au nyngine. Ama kuhusu zile hoja nyinginezo zisizokuwa za maumbile ya vitu vyote, jambo hili limejadiliwa kwa kirefu kwenye vitabu vya Kifalsafa na vya elimu nyingi. Vitabu hivi vina hoja na maelezo juu ya roho yenye kutoka kwa viumbe vyenye uhai. Tungalipenda kuvirejea katika mistari ya maneno ifuatayo:

## 1. Dhana Ya Roho

Itikadi juu ya 'roho' ni moja ya masuala yaliyo magumu na yenye kutatanisha yaliyovutia mazingira ya wanachuoni. Wale wapendao kuliweka kila jambo katika uchambuzi, wamekana kuwako kwa roho na wanaimani ile roho yenye sifa za kimwili na kufanya kazi chini ya utawala wa sheria za umbile.

Kuwako kwa nafsi isiyo na mwili wa dhahiri ni moja ya masuala yaliyochunguzwa kwa makini na wale wamwabuduo Allah Mwenyezi na wanayaamini mambo ya kiroho na wametoa thibitisho nyingi juu ya kuwako kwa viumbe visivyo na miili ya umbo la kuonekana ambavyo kama mtu atajifunza katika hali ya hewa ifaayo, iliyoandamana na maarifa kamili, na misingi ya hoja za Kimungu, husimama katika uthibitisho kamili.

Na yote yale yasemwayo na wanachuoni wa Kimungu juu ya Malaika, roho, ufunuo na Wahyi yanategemea hoja za nguvu na za kusadikika.[5]

## 2. Usingizi Wa Kisumaku (Uhiponozi)

Inawezekana kwamba wale wanaotaka kukielewa kila kitu kwa njia ya majaribio ya kivitendo na wanaweza kurejea kwenye maandiko mengi yaliyoandikwa juu ya jambo hili la usingizi wa kisumaku – kuchukuliwa kwa kiinimacho- (*hypnotism*). Mmoja wa mwanzilishi wa tawi hili la elimu alikuwa ni daktari

wa Kijerumani aliyeitwa Mesmer. Ilikuwa ni karne mbili zilizopita alipoianzisha sanaa hii na kadiri muda unavyopita, maoni yake yanathibitishwa na wanachuoni. Aliwafunza baadhi ya watu kama hao kama walivyostahili kutegemeana na tabia na akili zao, wa kufanyiwa kiinimacho (kuwa kwenye hali inayofanana na kulala).

Alifanikiwa kuwabumbuaza, mbele ya wanachuoni wengi, watu walewale alioendeshea majaribio juu yao hapo awali. Alizitoa roho zao kutoka miilini mwao na kwa kuzipitia roho hizo alipata taarifa za matukio yaliyopita na yatakayotendeka baadae. Baada ya kupita karne mbili sanaa hii inapata ukamilifu wa polepole katika njia mbali mbali. Baada ya majaribio mengi, wanachuoni wameamua kama ifuatavyo:

Ukiachilia mbali ule uoni wa nje, mtu mwenye akili anao uoni wa ndani pia, na huu ni uoni ulio mpana zaidi ya ule wa nje.

Mtu awapo katika hali ya usingizi huwa akili zote mbili zaweza kusikia kutoka mbali, kuona kutoka nyuma ya pazia na kutoa taarifa kwa mukhtasari kuhusu matukio yajayo, matukio ambayo hayana dalili ya nje hata iliyo ndogo.

Kwa kutumia kanuni za usingizi huu wa kutengeneza inawezekana kutengeneza roho ya mtu kutoka mwilini mwake hadi kwamba roho hiyo ikaweza kuuona mwili mfu.

Ule utaratibu wa roho huwa na uhuru wa aina maalum.

Roho haikomi kuwako kutokana na kuoza na kutawanyika kwa sehemu mbali mbali za mwili.

Vile vile wanachuoni hawa wametoa uamuzi mwingine ufananao na huo. Hata kama tusiweze kuzikubali thibitisho hizo katika ukamilifu wao, mukhtasari wa majaribio haya yaliyoendeshwa katika kipindi cha karne mbili zilizopita na kushuhudiwa na wengi wa wataalamu wa nchi za Mashariki na za Magharibi; unathibitisha kuwako na ukweli na uhuru wa roho, na hilo ndilo lengo halisi la majadiliano haya. Wale wapendeleao wanaweza kuzisoma taarifa kamili za majadiliano haya katika vitabu vihusikavyo.

## 3. Msukumo Au Hisia Za Siri

Imani katika msukumo (wa akilini) ni msingi wa utume wa mitume yote na dini za kimbingu na huo (msukumo) umesimamia katika roho iliyotengwa yenye nguvu na uwezo wa kupokea elimu ya ki-Mungu iwe bila ya kuwapo mjumbe au kupitia kwa malaika. Wenye hekima wamesema hivi kuhusu msukumo: Msukumo una maana ya kwamba Allah Mwenyezi anawaonyesha njia halisi kwa mmoja wa aliowachagua na anampa maelekezo katika matawi mbali mbali ya elimu. Hata hivyo, jambo hili hufanyika kwa njia ya kimuujiza na isiyo ya kawaida.

## 4. Aina Za Wahyi

Kuhusiana na ukomo ulio na roho, inawasiliana na ulimwengu wa kiroho kwa njia mbali mbali. Hapa tunaandika maendeleo ya yale yaliyoelezwa juu ya jambo hili na yule kiongozi wa Uisilamu.[6]

Wakati mwingine mtu yule ahusikaye anapashwa habari za kweli za mbinguni kwa njia ya wahyi na kila njia ya msukumo na kila linalopendekezwa akilini mwake ni sawa na sayansi inayojishuhudia ambayo ndani yake hakuna shaka au wasiwasi unaoweza kuingizwa.

Anazisikia sentensi na maneno kutoka kwenye kitu chenye umbo la kuonekana (kama vile mlima au mti), kama vile tu Allah alivyozungumza na Nabii Musa (a.s.).

Hali halisi zinafunuliwa kwake wazi wazi katika namna ya ndoto.

Malaika anatumwa na Allah kufikisha amri maalum kwake. Qur'ani Tukufu ilifikishwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa njia hii, kama vile isemavyo wazi wazi katika *Surah al-Shu'ara*, 26; 192-195:

"**Ameiteremsha Roho (Jibril) mwaminifu juu ya moyo wako ili uwe miongoni mwa waonyaji kwa lugha ya kiarabu iliyo wazi-wazi.**"

## 5 Visasili

Ili kwamba vizazi vijavyo viweze kufahamu mambo ya watu wa ulimwenguni kote, waandishi pamoja na marafiki na washirika wa watu hao wameandika kwa kadri ya uwezo wao matukio ya maishani mwao. Wameandika kwa wingi mno kiasi kwamba ili kuyakamilisha maandishi yao vile vile wanajibebea magumu ya safari. Historia haimjui mtu yeyote ambaye matukio ya maisha yake yangepaswa kuwa yameandikwa kama yale ya Mtukufu Mtume wa Uislam (s.a.w.w.) na ambaye marafiki na wanafunzi wangepaswa kuwa wameandika kila jambo la maisha yake kwa kirefu zaidi.

Hali kadhalika mfungamano wetu umetusaidia katika kuyahifadhi kwa kirefu matukio na maelezo ya maisha ya yule Mtume Mashuhuri wa Uislamu na kumekuwa chanzo cha pambo la kitabu cha maisha yake. Ukiachilia mbali maadui wenye hekima vile vile jambo hili hufanywa na marafiki wajinga. Hivyo basi, ni muhimu kwa mtu aandikaye wasifu wa maisha ya mtu maarufu kwamba achukue tahadhari katika kuyachambua maisha yake na katu asividharau vipimo vikali vya kihistoria katika kuyapima matukio. Sasa tunazijia dalili za tukio la wahyi.

## 6. Dalili Za Wahyi

Nafsi adhimu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) iliangazwa na nuru ya wahyi (ufunuo). Alihifadhi moyoni mwake yale aliyoyasikia kutoka kwa Malaika (Jibriil). Baada ya tukio hili Malaika yule yule alizungumza naye hivi: "Ewe Muhammad! Wewe ni mjumbe wa Allah nami ni Jibriil!" Wakati mwingine inasemekana kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliyasikia maneno haya alipokuwa kishashuka kutoka kule mlimani Hira. Haya matukio mawili yalimwogofya na kumshtua kwa kiasi fulani. Sababu za hofu na mshtuko ni kutokana na jukumu kubwa alilopewa siku ile aliyoouona ukweli aliokuwa akiutafuta kwa muda mrefu.

Hata hivyo, mshtuko huu wa akili, kwa kiasi fulani ulikuwa ni wa kawaida na haukuwa kinyume na itikadi yake juu ya ukweli aliofikishiwa. Licha ya ukweli kwamba alikuwa na uhakika kwamba yale aliyoyapata

yalikuwa ni ujumbe wa Allah na yule aliyeyaleta alikuwa ni Jibriil, mshituko wake wote ulikuwa ni jambo la kawaida kwa kiasi fulani na halikuwa nje ya mpangilio.

Imekuwa hivyo kwa sababu kwa vyovyote vile nafsi ya mtu iwavyo na nguvu na kwa kadiri yoyote atakavyoweza kuhusiana na utaratibu wa ghaibu na ulimwengu wa kiroho, anapokabiliwa na Malaika kwa mara ya kwanza ambaye bado hajawahi kumwona kabla, na vile vile kwamba anamwona Malaika huyo kileleni mwa mlima, anawajibika kushikwa na mshtuko kama huu, na ndio maana mshituko huu ulitoweka baadae.

Mshituko wa akili na uchovu usio wa kawaida ulimfanya aende nyumbani kwa Bibi Khadijah. Alipoingia nyumba ile, mkewe mpenzi aliziona dalili za fikara nyingi na wasi wasi usoni mwake na akamwuliza kulikoni.
Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimsimulia Bibi Khadija yale yaliyotokea na vile vile akaiongezea ile sentensi isemayo "Nilijihisi kujiogopa mwenyewe."[7]

Bibi Khadija alimtazama kwa heshima, akamwombea na kumfariji kwa kuzitaja baadhi ya sifa zake njema. Miongoni mwa mambo mengine alisema: "Umpole kwa jamaa zako, unaonyesha ukarimu kwa wageni wako na huogopi kuzikabili taabu katika njia iliyonyooka. Allah Atakusaidia."

Kwa kuzitaja sifa hizi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), bila shaka Bibi Khadija alidhamiria kumfanya mwenye matumaini zaidi kuhusu mafanikio yake na kumtia moyo kwa ajili ya kufanikisha lengo lake alilotumwa kulitimiza. Ukweli huu unaweza kuthibitishwa vema kutokana na yale aliyoyasema Bibi huyu.

Kisha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alijihisi kuchoka. Hivyo, alimgeukia Bibi Khadija na akasema: "Nifunike." Bibi Khadija alimfunika na baada ya hapo upesi sana akapatwa na usingizi.

## 7. Bibi Khadija Aenda Kwa Waraqah Bin Nawfal

Tumekwisha mzungumzia Waraqah kwenye kurasa zilizopita na tumeeleza ya kwamba alikuwa mmoja wa wenye hekima wa Uarabuni. Ulikwishapita muda mrefu tangu auingie Ukristo baada ya kuisoma Injili na alikuwa ni mtu mwenye cheo kikuu katika jambo hilo. Alikuwa ni binamu yake Bibi Khadija. Mke mpenzi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), alimsimulia Waraqah aliyoyasikia kutoka kwa Mheshimiwa mumewe. Baada ya kuyasikiliza hayo, Waraqah alimjibu binamu yake akisema: "Binamu yako (yaani Mtume (s.a.w) yu mtu mkweli, na yale aliyokutana nayo ni mwanzo wa Utume na ameshukiwa na Jibriil........"[8]

Matukio tuliyoyataja hapo juu yamenukuliwa kutoka kwenye maelezo ya kihistoria. Haya ndio mambo yaliyosimuliwa na mfululizo wa waandishi na yanapatikana katika vitabu vyote vya historia. Hata hivyo, katika mfululizo wa masimulizi haya, tunayakuta mambo yasiyoafikiana na vile vipimo vihusuvyo Mitume tulivyonavyo. Zaidi ya hayo hayalandani na yale matukio ya maisha ya yule mtu maarufu tuliyokwisha kujifunza kufikia hapa. Na yale tutakayoyaweka mbele yako hivi sasa hayana budi kuchukuliwa kama ni sehemu ya habari za uongo za historia au lazima ifafanuliwe zaidi.

Tunashangazwa mno na maandishi ya Dakta Haikal, mwanachuoni maarufu wa Misri, ambaye ingawa alitoa dibaji ndefu katika utangulizi wa kitabu chake ambacho ndani yake alisema kwamba kikundi cha watu wametia uongo katika mawaidha ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kutokana na uadui au huba, yeye mwenyewe naye ameandika mambo yasiyo sahihi kabisa, ingawa baadhi ya wanachuoni wa Kishi'ah, kama vile marehemu Tabarsi, ametoa tahadhari yenye manufaa juu ya jambo hili.[9] Hapa tunazinukuu baadhi ya hizi hadithi za uongo (ingawa isingalikuwa muhimu kuzitaja kama wale marafiki wajinga au maadui wenye hila wasingaliziandika vitabuni mwao):

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipoingia nyumbani mwa Khadija alijifikiria kwamba inawezekana kwamba macho yake yalikosea au kwamba amekuwa mpiga bao!
Hata hivyo Khadija alimwondoshea wasiwasi wake kwa kusema kwamba alikuwa mwenye kuwasaidia yatima na mpole kwa jamaa zake! Hapo Mtukufu Mtume alimwangalia kwa shukurani mno na kumwomba amletee blanketi na amfunike.[10]

Tabari na wanahistoria wengine wameandika hivi: "Alipoyasikia maneno : "Wewe ni mjumbe wa Allah!" mwili wake mzima ulianza kutetemeka na akaamua kujitupa chini ya mlima. Hata hivyo, wakati ule yule Malaika ali- jidhihirisha na kumzuia asifanye hivyo.[11]

Baadaye Muhammad alikwenda kufanya ibada ya Tawafu kwenye Al- Ka'ba. Akiwa huko, alikutana na Waraqqah bin Nawfal, na akamsimulia habari zake. Waraqah akasema: "Naapa kwa jina la Allah! Wewe ni Mtume wa watu hawa na yule Malaika Mkuu aliyekuwa akimjia Musa, amekushukia. Baadhi ya watu wako watakataa kulikubali dai lako na watakufanyia madhara. Watakutoa mjini mwako na watakuwa vitani dhidi yako." Muhammad alijihisi kwamba aliyoyasema Waraqah yalikuwa sahihi[12]

## 8. Ukosevu Wa Msingi Wa Kauli Hizi

Tunahisi kwamba hadithi zote hizi ni sehemu ya mpango wa Waisraeli na zimebuniwa na Wayahudi na kuingizwa kwenye historia na Tafsir (maele- zo ya Qur'ani tukufu).

Kwanza, ili kuweza kuzipima kauli hizi, hatuna budi kuzitazama wasifu za mitume walioitangulia. Qur'ani tukufu imezitaja shughuli zao, na maelezo yao marefu yamepokewa juu ya matukio ya maisha yao. Hata hivyo, hatuoni matukio mabaya yafananayo na hayo katika maisha ya yeyote kati yao. Qur'ani tukufu imesimulia kwa ukamilifu habari za mwanzo wa Wahyi kwa Nabii Musa (a.s.) na imeeleza wazi wazi mambo yote ya tukio hili. Hata hivyo, haikutaja jambo kama vile woga, kutetemeka, na mshtuko wa akili yake kwamba, alipoisikia sauti, alijiwa na kutaka kujitupa chini ya mlima. Kwa kuwa amesikia sauti kutoka mtini kwenye jangwa wakati wa usiku wa giza nene na hapo akaarifiwa kuhusu uteuzi wake kuishika ofisi ya Utume.

Kama ilivyoelezwa na Qur'ani tukufu, Nabii Musa (a.s.) alikuwa mtulivu kabisa wakati ule. Na Allah Mwenyezi alimtaka aitupe fimbo yake na ali- fanya hivyo mara moja, hofu yake ilikuwa tu juu ya ile fimbo, iliyogeuka kuwa mnyama wa hatari. Je, yaweza kusemwa kwamba Nabii Musa (a.s.) alikuwa

mwenye amani na mtulivu wakati mkuu wa Mitume alikuwa ame- fadhaika sana alipoyasikia maneno ya Malaika, kiasi kwamba alitaka kuji- tupa chini ya kilele cha mlima? Je, lilikuwa ni jambo la hekima kusema hivyo?

Ni ukweli ukubalikao kwamba kwa kadiri nafsi ya mtu asivyokuwa tayari kwa hali yoyote kuzipokea siri za Mbinguni (yaani Utume) Mola, Mwingi wa rehema hamwinui mtu huyo kuishika kazi ya Utume, kwa sababu, lengo la kuwainua Mitume ni kwamba wawaongoze wanaadamu.

Mtu anawezaje kuwavutia watu wakati hisia za usalama wake na utulivu ni mchache mno kiasi kwamba anakuwa tayari kujiua kwa kuusikia Wahyi au unapokatika au kukoma. Wanachuoni wa 'Kalaam' (theolojia) wanakubaliana kwa pamoja kwamba Mtume anapaswa awe huru kutokana na vitu vyote vile viwavyo sababu ya watu kujitenga mbali naye. Katika hali hiyo je, tunaweza kuzikubali kauli hizi ambazo kwa vyovyote vile haziwezi kutumika kwa ajili ya kiongozi mkuu wa wanaadamu?

Pili, ilitokeaje kwamba kwa kuisikia sauti ya Mungu Nabii Musa alitosheka kabisa kwamba sauti ile ilitoka kwa Allah na mara moja alimwomba Allah kwamba ateuliwe Haruni ili awe mfuasi na msaidizi wake, kwa kuwa aliweza kuzungumza kwa ufasaha zaidi, lakini yule sayidi wa Mitume alisalia kuwa mwenye shaka kwa muda fulani hadi Waraqah alipoitoa shaka na kutokuwa na uamuzi huko kutoka akilini mwake?

Tatu, ni ukweli ukubalikao kwamba Waraqah alikuwa mkristo. Hata hivyo, alipotaka kuuondoa mshituko ule wa akili na kusitasita kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitaja jina la Nabii Musa mwana wa Imrani tu; "Hiyo ndio kazi ile ile aliyoteuliwa Musa mwana wa Imrani kuishika." [13]

Je, jambo hili peke yake halithibitishi kwamba mkono wa wasimulizi wa kiisraeli umekuwa kazini na kwamba wameibuni hadithi hii bila ya kuzingatia dini ya shujaa wake (Waraqah).

Tukiyaachilia mbali yote hayo inaweza kusemwa kwamba mambo hayaafikiani hata kidogo na ukuu na ubora wa Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) tunaoutambua. Mwandishi wa kitabu '*Hayat-i-Muhammad*' alitambua kwa kadiri fulani kuhusu kuzushwa kwa hadithi hizi. Hivyo basi, kwa sababu hii, wakati mwingine ameyanukuu mambo tuliyoyataja hapo juu kwa kutanguliza maneno: 'kama isemekanavyo'

Marehemu Allamah Tabarsi, mwanachuoni mkuu wa Kishi'ah amefanya uadilifu katika mambo haya katika Tafsiri yake. [14]

Kwa maelezo zaidi, basi rejea yaweza kufanywa kwenye kitabu kile.

1. Jambo hili laweza kueleweka vizuri zaidi kutokana na aya ifuatayo ya Qur'ani tukufu:-"Watu wote walikuwa taifa moja; hivyo Allah akawainulia Manabii ili wawe wabashiri na waonyaji, na pamoja nao akateremsha kitabu na ukweli ili kihukumu baina ya watu katika yale waliyohitilafiana;....(Surah al- Baqarah, 2:213).
2. Nahjul Balaghah, Hotuba 1.
3. Baadhi ya wachambuzi hawaafiki wazo hili la Mtukufu Mtume kubanwa kwa nguvu na Jibril, hivyo wanaona kipengele kama hicho ni chumvi iliy- oongezwa na wanukuu wa historia. Kwani kiakili ni vigumu sana siku ya kwanza ya masomo mwalimu mwenye hekima kumfanyia kitendo kama hicho mwanafun- zi asiyejua kitu, ambaye yeye mwalimu ajua fika

kwamba hajui chochote. Ukweli ni kwamba mawazo kama haya yahitaji uchambuzi wa ndani zaidi kimantiki na kihistoria. Na Allah ndiye Ajuaye – Mhariri.

4. Siirah Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 236, na Sahih Bukhari, Juzuu 1, uk. 3.

5. Maelezo kamili juu ya hoja hizi yanaweza kupatikana katika vitabu vya fal- safa chini ya kichwa cha habari cha: 'Majadiliano juu ya jambo hili kwenye kitabu: A'sfaar' cha Sadrul Muta'allihin.'

6. Bihaarul Anwaar, Juzuu 18, uk. 193, 194,255 na 256.

7. Tarikh-i-Tabari, Juzuu 2, uk. 205; Tarikh-i-Kamil Ibn Athir Juzuu 2, uk. 31.

8. Inapasa kufahamika kuwa aliyekwenda kwa Waraqah si Mtukufu Mtume bali ni Khadija, na hii hailazimu kuwa naye Mtume alikwenda kuthibitisha utume wake kwake. Pia dhahiri ni kuwa Khadija hakwenda kwa Waraqa ili kutaka kuthibitisha utume wa Mtume (s.a.w.w.), bali alikwenda kwa lengo la kumpa habari juu ya hali halisi iliyompata mumewe – Mhariri.

9. Majma'ul Bayaan, Juzuu 10, uk. 384.

10. Tabaqaat-Ibn Sa'ad, Juzuu ya 1, uk. 289; Hayaati Muhammad, Juzuu 1, uk. 195.

11. Tarikh-i-Tabari, Juzuu 2, uk. 205.

12. Tafsir-i-Tabari, Juzuu 30, uk. 161, tafsiri ya Surah al- Alaq; na Siirah-i-Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 238.

13. Siirah Ibn Hishamu, Juzuu 1, uk. 238. marehemu Allamah Majlis amenukuu katika kitabu Biharul Anwaar, Juzuu 18, uk. 228 na isa kutoka kwenye kitabu Bihaarul Anwaar, Juzuu 18, uk. 228, na Isa kutoka kwenye Sahih Bukhari na Siirah-i- ibn Hisham ambamo majadiliano haya yametegemezwa.

14. Majma'ul Bayaan, Juzuu 1, uk. 384.

# Sura Ya Kumi Na Mbili: Wahyi Wa Kwanza

## Tarehe Ya Kwanza Kwa Kazi Ya Utume

Kama vile ilivyo tarehe ya kuzaliwa na kufa kwake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), tarehe ya kuanza kwake kazi ya utume nayo haifahamiki kwa mtazamo wa kihistoria, karibuni wanachuoni wote wa Kishi'ah wanasema kwamba alipokea ujumbe wake wa kwanza mnamo tarehe 27 Rajab na alianza kazi yake ya Utume katika siku hiyo hiyo. Hata hivyo, wanachuoni wa Kissuni kwa kawaida hudai kwamba aliteuliwa kuishika kazi hii katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Kwa vile Mashi'a wanadai kuwa ni wafuasi wa dhuria wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) huzichukulia taarifa zao kuwa ni za kweli, na zenye kukata shauri. Kutokana na 'Hadithi Thaqalayn' wamezikubali taarifa za kizazi cha dhuria wa Mtukufu Mtume kuhusiana na tarehe ya uteuzi huu wa kazi ya Utume na kuwa ndiyo sahihi.

Dhuria wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wamesema: "Chifu wa familia (yetu) aliteuliwa kuishika kazi ya utume tarehe 27 ya mwezi wa Rajab."Kufuatana na jambo hili, Mashi'a hawatilii shaka yoyote kuhusiana na usahihi wa tarehe hii.

Kitu kiwezacho kuchukuliwa kuwa ndio msingi wa maoni mengine ni ile kauli ya Qur'ani tukufu, ambayo ndani yake imeelezwa kwamba aya za Qur'ani zilifunuliwa katika mwezi wa Ramadhani.

Na kwa vile siku ya kuanza kwa kazi ya Utume ni ile siku ya kuanza kufunuliwa Qur'ani tukufu, tunaweza kusema kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliteuliwa kuianza kazi ya Utume katika mwezi ule ule wa Ramadhani. Aya za Qur'ani tukufu zitajazo kwamba ilifunuliwa katika mwezi wa Ramadhani ni hizi:

{شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنْزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ}185

***"Mwezi wa Ramadhani ndio** (**mwezi**) **ambao ilifunuliwa Qur'ani......."*** (***Suratul-Baqarah 2:185***).

{وَالْكِتَابِ الْمُبِينِ} 2

{إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةٍ مُبَارَكَةٍ ۚ إِنَّا كُنَّا مُنْذِرِينَ} 3

***"Naapa kwa Kitabu kitukufu kwamba tumeifunua** (**hii Qur'ani** ) **kati- ka usiku uliobarikiwa.....*** (***Surah al-Dukhaan, 44:2-3***).

Na huu ni ule usiku wa Qadr (utukufu) uliotajwa katika *Surat al-Qadr* (aya ya 1) ambayo ndani yake mmesemwa ya kwamba: **"Tumeifunua Qur'anim katika usiku wa cheo.**"

## Jibu La Wanachuoni Wa Kishi'ah

Wanahadithi wa Kishi'ah na wafasiri wa Qur'ani tukufu wametoa majibu na maelezo mbali mbali kuhusiana na hoja hii; baadhi ya hoja hizo tunazitaja hapa chini.

### Jibu La Kwanza

Aya tulizozitaja hapo juu zaonyesha kwamba Qur'ani tukufu ilifunuliwa katika usiku mmoja uliobarikiwa wa mwezi mtukufu wa Ramadhani unaoitwa 'Usiku wa Cheo' lakini hapatajwi mahala pa kufunuliwa kwake na vile vile hawaashirii kwamba zilifunuliwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika usiku huo huo.

Inawezekana kwamba zilikuwepo funuo mbali mbali za Qur'ani, na masimulizi mengi ya Kishi'ah na Kisunni yanauthibitisha uwezekano huu. Mmoja wa funuo hizi ni ufunuo wa pole-pole wa Qur'ani tukufu kwa Mtume (s.a.w.w.), na mwingine ni ufunuzi wake wa visehemu sehemu kutoka kwenye '*Lauhul Mahfudh*'[1] kwenda '*Baytul Ma'amur'*[2] hivyo basi, hakuna kosa lolote kwa aya chache za *Surat al-Alaq* kufunuliwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika tarehe 27 ya Rajab na Qur'ani yote katika hali ya kitu chote kizima, ikafunuliwa katika mwezi wa Ramadhani kutoka mahali palipotajwa na Qur'ani tukufu kuwa ni *'Lauhul Mahfudh'* kwenda kwenye sehemu nyingine iitwayo *'Baytul Ma'amur'.*

Maoni haya yanathibitishwa na aya hiyo hiyo ya *Surah al-Dukhaan* isemayo: *"Tunaapa kwa Kitabu kitukufu kwamba Tumeifunua* (*hii Qur'ani*) *katika usiku uliobarikiwa....."* kutokana na aya hii ni dhahiri

kwamba (kutegemeana na uzito wa vijina (pronoun) virudivyo kwenye neno 'Kitabu' ) vilifunuliwa katika hali ya ukamilifu wake kwenye usiku mtukufu (ulioangukia katika mwezi wa Ramadhani) na ni sahihi tu kwamba ufunuo huu kuwa ni mwingine ghairi ya ule ufunuo uliofanyika katika wakati wa kuteuliwa kwake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuishika kazi ya Utume kwa sababu, wakati ule ni aya chache tu zilizofunuliwa.

Kifupi ni kwamba Qur'ani ilifunuliwa katika mwezi wa Ramadhani katika 'usiku wa cheo' haiwezi kuwa uthibitisho wa ukweli kwamba ndio siku ya uteuzi wa Mtume (s.a.w.w.) kuishika kazi ya Utume ambayo katika siku hiyo aya chache tu zilifunuliwa, nako kulitokea katika mwezi ule ule, kwa sababu aya tulizozitaja hapo juu zaonyesha kwamba Kitabu kizima (Qur'ani Tukufu) kilifunuliwa katika mwezi ule ule ambapo, katika siku za uteuzi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuishika kazi ya utume ni aya tano au sita tu zilizofunuliwa. Hivyo basi, hizo madhehebu mbili, wanapozieleza maana za aya tulizozitaja hapo juu katika masimulizi yao, wanasema kwamba Qur'ani nzima iliteremshwa kutoka 'Lauhul Mahfudh' kwenda 'Baytul Ma'amur' katika usiku ule. Wanachuoni wa Kishi'ah na Kisunni wameyanukuu maelezo tuliyoyataja na hasa Profesa Muhamad Abdul Azim Zarqaani wa chuo kikuu cha Al-Azhr' amezitaja kwa kirefu ndani ya kitabu chake.[3]

## Jibu La Pili

Jibu lililokamili zaidi, lililopata kutolewa na wanachuoni, ni hili la pili. Mwanachuoni Mkuu Tabatabai ameeleza kwa kirefu katika kitabu chake chenye thamani[4] na kiini chake tunakitoa hapa chini. Shabaha halisi na ya hakika ya Qur'ani tukufu kusema kwamba:

'Tumeifunua (hii Qur'ani ) katika mwezi wa Ramadhani' ni kwamba ili- funuliwa katika mwezi ule kwa sababu, zaidi ya kufunuliwa kidogo kidogo hii Qur'ani ina ukweli ambao ndani yake Allah Mwenyezi Alimwarifu Mtume (s.a.w.w.) katika usiku maalumu wa mwezi wa Ramadhani.

Kwa kuwa Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na elimu ya kitabu kitakatifu chote alielekezwa kutoharakisha katika kuyabalighisha yaliyokuwa humo na kwamba asubiri hadi aipokee amri juu ya ubalighisho wake kwa watu kwa pole pole. Qur'ani tukufu inasema: **"Usiharakishe kuzibalighisha habari za Qur'ani hadi upate amri kuhusiana na jambo hili kwa njia ya Wahyi."**

Jibu hili laonyesha kwamba Qur'ani tukufu ilikuwako katika hali ya ujumla wake uliofunuliwa katika ukamilifu wake katika wakati mmoja wa mwezi wa Ramadhani na vile vile ina kuwako kwake kwa utaratibu wa polepole kulikoanzia tangu katika siku ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuteuliwa kuishika kazi ya Utume hadi mwishoni mwa uhai wake.

## Jibu La Tatu

Kama tulivyoeleza kwa mukhtasari kuhusu aina mbali mbali za ufunuo, kwa hakika una hatua mbali mbali. Hatua ya kwanza ni ile ya ndoto. Hatua ya pili ni ile ya siri na sauti za mbinguni zinazosikika pasi na kumkabili Malaika. Na hatua ya mwisho ni ile ya Mtume kumwona Malaika na kuyasikia maneno ya

Allah kutoka kwake na kujifunza kupitia kwake juu ya hali halisi za dunia nyinginezo.

Kwa kuwa roho ya mwanaadamu haina nguvu ihitajikayo kuzihimili hatua mbali mbali za wahyi katika wakati wa kwanza, ni muhimu kwamba uwezo wa kuzihimili ukue polepole, tunaweza kusema kwamba: Katika siku ile ya kuteuliwa kwake kuishika kazi ya utume (tarehe 27 ya Rajab) na kwa kipindi fulani baada ya hapo, alikuwa akizisikia zile sauti za mbin- guni tu zilizomwarifu ya kwamba alikuwa ni Mjumbe na Mtume wa Allah na haikuwapo aya yoyote iliyofunuliwa katika kipindi kile. Na wakati mwingine baadaye polepole ufunuo wa Qur'ani tukufu ulianza katika mwezi wa Ramadhani.

Kwa kauli hii tuna maana ya kwamba kuteuliwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuishika kazi ya utume katika mwezi wa Rajab hakuhusiani na kufunuliwa kwa Qur'ani tukufu katika mwezi ule. Kutokana na jambo hili, hakuna Haja ya kuwapo hitilafu kati yake na kule kufunuliwa kwa Qur'ani tukufu katika mwezi wa Ramadhani na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuteuliwa kuishika kazi ya Utume katika mwezi wa Rajab.

Ingawa yale tuliyoyasema hapo juu hayaafikiani na maandiko ya vitabu vingi (kwa sababu wengi wa wanahistoria wamesema dhahiri kwamba aya za *Surat al-Alaq* zilifunuliwa katika siku ile ile ya uteuzi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuishika kazi ya Utume), mpaka tupate masimulizi yanayotueleza kwamba katika siku ile ya uteuzi wa Mtume kuishika kazi aliisikia sauti ya siri na isiyosema lolote kuhusu ufunuzi wa Qur'ani tukufu au aya zake. Wanalieleza jambo hili kwa kusema kwamba katika siku ile

Mtume alimwona Malaika aliyemwambia: "Ewe Muhammad! Wewe ni Mjumbe wa Allah." Na kwenye baadhi ya masimulizi ni kule kuisikia sauti tu kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) tu kulikotajwa na hakuna lolote lililosemwa kuhusu kumwona kwake Malaika.[5]

## Itikadi Ya Mtukufu Mtume (S.A.W.W) Kabla Ya Kuianza Kazi Ya Utume

Kwa kipindi kirefu suala la dini ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kabla ya kuianza kazi ya Utume limekuwa jambo la kujadiliwa baina ya wanachuoni wa Kishi'ah na Kisunni. Wameibua maswali yafuatayo na kutoa jibu kwa kila moja kati yao:

Je, Mtume (s.a.w.w.) aliifuata dini yoyote ile kabla ya kuteuliwa kuianza kazi ya Utume?

Kuchukulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa mfuasi wa dini, je dini hiyo ilikuwa ni dini yake mwenyewe.

Kama alikuwa mfuasi wa dini yoyote ile, je, dini hii ilikuwa dini iliyofunuliwa kwake pekee na alifuata kwa pekee au alihesabiwa kuwa mmoja wa wafuasi wa dini ile?

Kama alitenda kazi katika dini ile peke yake au akiwa yu mfuasi, ni Mtume wa kale yupi aliyekuwa na dini ile?

Haya ndio maswali manne ayaonayo mtu katika vitabu mbali mbali vya Siira (maisha ya Mtukufu Mtume s.a.w.w.), historia, na tafsiri za Qur'ani tukufu.

Hata hivyo, je, ni muhimu kwamba hatuna budi tutoe majibu halisi ya maswali haya? Je, kimsingi ni muhimu tuvisome vitabu mbali mbali vya historia, tafsiri za Qur'ani tukufu na maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kukusanya majibu yahitajikayo?

Tunaona kwamba mijadala juu ya mambo haya si muhimu hata kidogo.[6] Badala yake kilicho muhimu ni kwamba, hatuna budi kuthibitisha kwamba kabla ya uteuzi wake wa kuishika kazi ua Utume, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwitakidi na kumwabudu Allah Aliye Mmoja tu na alikuwa mchamungu na mnyoofu.

Jambo hili laweza kuthibitishwa kwa njia mbili zifuatazo:

Kwanza, kwa kuchunguza ile miaka yake arobaini ya kabla ya Uteuzi wake wa kuishika kazi ya Utume, na Pili, kwa kuyachunguza kwa makini yale yaliyosemwa na viongozi wa Uislamu kulihusu jambo hili:

Tukitoa mukhtasari wa maisha yake ya miaka arobaini, yalikuwa ni maisha ya wastani na unyoofu, uaminifu na ukweli, haki na uadilifu, wema na huruma kwa waliokandamizwa na masikini na chuki juu ya masanamu na wenye kuyaabudu. Alikuwanazo tabia hizi kwa wingi mno kiasi kwamba, safari moja alipokuwa akienda Sham katika biashara na mtu mmoja aliyekuwa akifanya naye mapatano, aliapa kwa majina ya masanamu, yeye akasema: "Vitu vichukizavyo mno vyenye kupandisha ghadhabu yangu ni hawa 'Laat' na 'Manaat' anaojiapiza kwao."

Mbali na hayo alikuwa akisali mfululizo katika pango la Hira katika mwezi wa Ramadhani na kufanya Hijja katika siku za Hajj, na tena kama asemavyo Imam wetu wa sita, yeye (Mtukufu Mtume s.a.w.w) alifanya Hajj kwa siri mara kumi na kwa mujibu wa wasimulizi wengine alifanya hivyo mara ishirini. Na kama tujuavyo ibada zote za Hajj ni utekelezaji wa ibada ambayo Nabii Ibrahim (a.s.) aliwaita watu na akata- ka kwamba kwa njia hii, wale wenye kumwamini Allah wa Pekee, wakusanyike katika sehemu moja maalum katika kipindi maalum.

Hali kadhalika, daima Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akimkumbuka Allah alipokuwa akila chakula na aliacha kula nyama ya wanyama waliochinjwa kwa njia isiyo halali, kwa kila mara alikuwa akishitushwa na kuyaona mandhari machafu, ulevi, na kucheza kamari, alivichukia mno vitu hivi kiasi kwamba wakati mwingine alikuwa akikikimbilia milimani na kurudi nyumbani baada ya kupita sehemu fulani ya usiku. Sasa, linalohitajika na fikara zetu ni hili:

Je, inawezekana kutia shaka juu ya itikadi ya mtu aliyepitisha maisha yake katika hali tuliyoitaja hapo juu na asiyekuwa na udhaifu japo ulio mdogo zaidi tangu mwanzoni mwa maisha yake, na aliyeipitisha sehemu ya maisha yake katika vilima na katika sehemu ya kujitenga ili atafakari juu ya maajabu yapendezayo ya ulimwengu huu. Tunamchukulia mtu wa kawaida kuwa mcha Mungu, mwenye kuwajibika na mwenye haki, kama tukiona moja ya kumi ya sifa hizi kwake, je tuzungumze nini juu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)?

Njia ya pili ya kuipata hali halisi ni uchunguzi wa nyaraka na masimulizi yaliyotufikia kutoka kwa viongozi wa Uislamu. Moja kati ya hayo ni masimulizi ya Imam Ali (a.s.), chifu wa itikadi ya Upweke wa Allah, katika 'Khutba-i Qaasi'ah': "Tangu wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipoacha kunyonya, Allah Mwenyezi alimshirikisha Malaika mtukufu zaidi pamoja naye ili aweze kumwonyesha njia ya unyoofu na wema wakati wa mchana na usiku.[7]

## Ulinganisho Baina Ya Mtume Muhammad (S.A.W.W) Na Nabii Isa (A.S).

Hakuna shaka juu ya ukweli kwamba Mtume wa Uislam (s.a.w.w.) anazo fadhila juu ya Mitume wote wa kabla yake. Na imeelezwa dhahiri katika Qur'ani tukufu juu ya baadhi ya Mitume kwamba waliinuliwa hadi kwenye daraja la Utume tangu utotoni mwao na vile vile walipelekewa vitabu. Kwa mfano, Qur'ani tukufu inasema juu ya Nabii Yahya (a.s.) hivi:

{يَا يَحْيَىٰ خُذِ الْكِتَابَ بِقُوَّةٍ ۖ وَآتَيْنَاهُ الْحُكْمَ صَبِيًّا {12

***"Kwa Yahya Tulisema: 'Kishikilie Kitabu kwa nguvu, na tukampa hekima, rehema na usafi tangu yungali mtoto."*** (***Surat Mariam, 19:12.***)

Wakati Nabii Isa (a.s.) alipokuwa bado yu mtoto mchanga wazee wa Bani Israiil walimshikilia mama yake awajulishe wamjue baba wa mtoto yule.

Bibi Mariam aliashiria kwenye kitanda cha mtoto yule ili kwamba watu wale walipate jibu la swali lao kutoka kwa yule mtoto mwenyewe. Nabii Isa (a.s.) aliwajibu kwa maneno haya kwa ufasaha mkuu na uthabiti:

{قَالَ إِنِّي عَبْدُ اللَّهِ آتَانِيَ الْكِتَابَ وَجَعَلَنِي نَبِيًّا {30

{وَجَعَلَنِي مُبَارَكًا أَيْنَ مَا كُنْتُ وَأَوْصَانِي بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ مَا دُمْتُ حَيًّا {31

***"....Hakika mimi ni mja wa Allah; amenipa Injili na amenifanya Nabii, na amenifanya mbarikiwa, popote niwapo, na ameniusia Sala na Zaka maadamu ningali hai."*** (***Surat Mariam, 19:30-31***).

Mwana wa Mariam anatufafanulia juu ya misingi na kanuni za dini yake tangu katika wakati wa utotoni mwake na anatangaza ya kwamba anaifuata kanuni ya ibada ya Allah Aliye Mmoja tu.

Sasa tunazivuta fikara zako kushuhudia na kukuuliza: "Wakati Nabii Yahya (a.s.) na Nabi Isa (a.s.) ni waumini wa kweli na wanazitangaza kweli za maumbile, je, tunaweza kusema kwamba huyu kiongozi

wa wanaadamu asiye na kifani na aliye mtukufu zaidi miongoni mwa wanaadamu hakuiona itikadi isiyo kifani hadi alipofikia umri wa miaka arobaini, ingawa hata katika muda wa ufunuo katika lile pango la Hira tayari alikuwa akijishughulisha na kutafakari?"

1. Tazama: "Tafsirul Mizaan" cha Allamah Muhammad Husayn Tabatabai.
2. Tazama: "Tafsirul Mizaan" cha Allamah Muhammad Husayn Tabatabai.
3. Manaahilul 'Irfaan fi'Ulumil Qur'ani, Juzuu 1, uk. 37.
4. Al-Mizaan, Juzuu 2, uk. 14-16.
5. Bihaarul Anwaar, Juzuu 18, uk. 184, 190 na 103.
6. Bihaarul Anwaar, Juzuu 18, uk. 271- 281.
7. Nahjul Balaghah, Juzuu 2, uk. 182

# Sura Ya Kumi Na Tatu :Ni Nani Waliokuwa Watu Wa Kwanza Kusilimu?

## Maendeleo Ya Uislamu

Maendeleo ya Uislam na kupenyeza kwake ndani ya watu tofauti tofauti kulifanyika polepole. Kwa mujibu wa maneno ya Qur'ani tukufu watu hao waliowatangulia wengine wote katika kusilimu na kuuhubiri Uislamu wanaitwa '*As-Saabiqun*' (watangulizi) na katika siku za mwanzoni mwa Uislamu heshima hii ya ziada ilikuwa kipimo cha usafi na ubora na hata miongoni mwa watu hawa, mtu amtanguliaye mwingine alipewa cheo cha heshima. Hivyo basi, hatuna budi kuzirejea taarifa zikubalikazo na kuamua, bila ya upendeleo kuhusu ni nani waliokuwa wa kwanza miongoni mwa wanaume na wanawake waliosilimu.

## Wa Kwanza Miongoni Mwa Mwanamke Kusilimu Alikuwa Ni Bibi Khadijah

Ni ukweli wa kihistoria ukubalikao kwamba miongoni mwa wanawake Bibi Khadija alikuwa wa kwanza kusilimu na hakuna riwaya zipinganazo juu ya jambo hili. Hapa tunataja muhtasaroi wa maandishi ya kihistotia yaliyo muhimu na yenye nguvu yaliyonukuliwa na wanahistoria kutoka kwa mmoja wa wakeze Mtume (s.a.w.w.)

Bibi Aisha asema hivi: "Kila mara nilikuwa nikisikitishwa na kutokiona kipindi cha Khadija, nilishangazwa na huruma na huba aliyoionyesha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwake, kwa sababu mumewe mpenzi alikuwa akimkumbuka zaidi kuliko mtu yeyoye mwingine na kama akimchinja kondoo aliwatafuta marafiki wa Khadija na kuwapelekea fungu la nyama ile. Siku moja Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akitoka nje ya

nyumba, alimkumbuka Khadija na kumsifu. Hatimaye nilishindwa kujizuia na nikasema kwa ujasiri kabisa: “Yeye hakuwa chochote zaidi ya kuwa bibi kizee na Allah amekupa mwanawake aliye bora.”

“.... Maneno yangu yalikuwa na athari mbaya kwa Mtukufu Mtume wa Allah(s.a.w.w.). Dalili za kuchukia na ghadhabu zilitokea katika paji la uso wake, na akasema: Si hivyo hata kidogo ..... sijajipatia mwanamke bora. Aliuamini Utume wangu wakati watu wote walipokuwa wamezama katika ukafiri na ibada ya miungu mingi.

Aliuweka utajiri wake mikononi mwan- gu wakati wa kwenye mazingira tahinifu. Kutokana na naye, Allah ameni- pa kizazi, ambacho sikukipata kutoka kwa yeyote yule mwingine”.[1]

Ushahidi mwingine juu ya Bibi Khadija kuwa mwanamke wa kwanza hapa ulimwenguni kusilimu ni lile tukio la kuanza kufunuliwa Qur’ani tukufu, kwa sababu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliposhuka kutoka kule pango la Hira na kumsimulia mkewe tukio hili, mara moja aliyathibitisha maneno ya mumewe na akamfariji. Zaidi ya hapo, alikuwa amesikia kutoka kwa watabiri na wapiga ramli wa Uarabuni juu ya Utume wa mumewe na ilikuwa ni kutokana na uaminifu na unyoofu wa huyu kijana wa Kibani Hashim kwamba alikubali kuolewa naye.

## Wa Kwanza Kusilimu Miongoni Mwa Wanaume Alikuwa Ni Ali (A.S)

**K**aribuni wanahistoria wote wa Kishi’ah na Kisunni wanakubaliana kwamba mwanaume wa kwanza kusilimu alikuwa ni Sayyidna Ali (a.s.). Na dhidi ya kauli hii maarufu vile vile inawezekana kupata kauli za nadra katika historia. Wasimuliaji wao wamechagua kuzungumza kinyume na hivyo. Kwa mfano, inasemekana kwamba mwanaume wa kwanza kusilimu alikuwa ni bwana Zay’d bin Harith au bwana Abu Bakr. Hata hivyo, nyingi ya hoja zinatoa ushahidi dhidi ya kauli hizi mbili. Baadhi ya hoja hizo ni hizi.

### Ushahidi Wa Kwanza

Tangu katika siku za utotoni Sayyidna Ali (a.s.) alilelewa nyumbani kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) naye Mtume alijitahidi kwa nguvu zake zote kumwelimisha kama vile afanyavyo baba mwenye huruma. Wengi wa waandishi wa wasifu husema kwa kukubaliana kwamba: “Kabla ya uteuzi wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kushika kazi ya Utume ulitokea ukame mkali sana mjini Makkah.
Bwana Abu Twalib, ami yake Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na familia kubwa ya kutunza, alikuwa chifu wa Waquraishi, na kipato chake hakikuweza kulandana na matumizi yake naye hakuwa tajiri kama alivyokuwa nduguye Abbas. Hali ya kifedha ya Bwana Abu Twalib ilimhimiza Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kulijadili jambo hili na bwana Abbas na wakaamua kuwachukua baadhi ya watoto wa Abu Twalib majumbani mwao ili waweze kuupunguza mzigo wake na kumsaidia katika kupata mahitajio yake. Matokeo ya mashauriano haya ni kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimchukua Sayyidna Ali (a.s.) na bwana Abbas alimchukua Bwana Ja’far chini ya ulezi wake.”[2]

Katika hali hiyo, tunaweza kusema kwamba, Sayyidna Ali (a.s.) alipokwenda nyumbani kwa Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na umri usiopungua miaka minane au kumi. Sababu ya kudhania hivyo ni kwamba, shabaha ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kumchukua Sayyidna Ali (a.s.) nyumbani kwake na kumweka chini ya utunzaji wake ilikuwa ni kupunguza mzigo wa chifu wa Makkah (Bwana Abu Twalib), na zaidi ya ukweli uliopo ni kwamba kutengana na wazazi wake mtoto aliye chini ya umri wa miaka nane au kumi ni jambo gumu; vile vile isingaliweza kutoa athari zipendezazo katika hali ya maisha ya Bwana Abu Twalib.

Hivyo basi, ni muhimu kwetu sisi kudhani kwamba umri wa Sayyidna Ali (a.s.) wakati ule ulikuwa katika hali ya kutoa athari zipendezazo kwa maisha yake anapochukuliwa kutoka kwa baba yake Bwana Abu Twalib. Katika hali hii, mtu awezaje kusema kwamba watu wasio wa nyumba ile, kama vile Bwana Zayd bin Harith na wegineo walijifungamanisha na siri za wahyi, ambapo binamu yake Mtume (s.a.w.w.), aliyekuwa karibu zaidi naye kuliko watu wote na daima alikuwa pamoja naye, akasalia katika hali ya kutozifahamu?

Lengo la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kumlea Sayyidna Ali (a.s.) lilikuwa kumfidia Bwana Abu Twalib kwa kadri fulani kwa huduma alizozitoa na kwa kadiri Mtume alivyopasika, hakikuapo chochote kilicho kuwa bora zaidi kwake kuliko kumwongoza mwanaadamu.

Kwa kuyazingatia mambo yote haya, mtu awezaje kusema kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alim–nyima binamu yake baraka hizi ingawa ukweli uliopo ni kwamba, yeye (Sayyidna Ali (a.s.) alikuwa mtu mwenye ujuzi mwingi na mwenye akili yenye elimu nyingi? Ingalikuwa bora kama tunajifunza juu ya jambo hili kutoka midomoni mwa Sayyidna Ali mwenyewe.

Katika hotuba yake iitwayo '*Qasi'ah*' alikieleza cheo na heshima yake mbele ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Mnaifahamu heshima aliyonipa Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na ujamaa wetu na itibari (nilivyokuwa nayo mbele yake).

Wakati wa utoto wangu alinilea chini ya malezi yake na kunikumbatia. Alinikumbatia kitandani mwake na nilikuwa na kawaida ya kuinusa harufu yake nzuri. Nilimfuata kama vile ndama wa ngamia amfuatavyo mama yake.

Kila siku aliinua (alionyesha ) dalili ya utu wema na kuniamrisha niifuate. Alikuwa akisali huko Hira kila mwaka (kabla ya uteuzi wake wa kushika kazi ya Utume) nami nilikuwa nikienda kumwangalia huko, ambapo hakuna yeyote aliyemwona.

Wakati ule Uislamu ulikuwa bado haujaifika nyumba yoyote ila ile ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Khadija, nami nilikuwa wa tatu wao. Nilikuwa nikiiona nuru ya wahyi na utume na kuinusa harufu nzuri ya Utume."[3]

## Ushahidi Wa Pili

Alipokuwa akiyasimulia maisha ya Afif Kandi, wanachuoni Ibn Hajjar (katika kitabu chake '*Al-Isabah*' Ibn

Abdul Bir (katika *Isti'ab*) na wanachuoni wengine wengi wa historia wamemnukuu (Afif Kandi) akisema kwamba: "Safari moja katika zama za ujinga nilikwenda Makkah. Mwenyeji wangu alikuwa ni Abbas mwana wa Abdul Mutwalib na sote tulifika kwenye mipaka ya Al-Ka'ba Tukufu.

Mara kwa ghafla nilimwona mtu mmoja akiwa kasimama kandoni mwa Al-Ka'ba. Kisha akaja kijana mwamaume na akasimama kuliani mwake. Mara baada ya hapo nilimwona mwanamke akija na kusimama nyuma yao. Nilimwona yule kijana na yule mwanamke wakifanya Rukuu na Sijida wakimwiga yule mwanaume. Mandhari hii isiyo na kifani ilinifanya nimwulize Abbas kuhusiana nayo.

Alisema: "Yule mwanaume ni Muhammad mwana wa Adullah na yule kijana ni binamu yake na yule mwanamke aliyesimama nyuma yao ni mkewe Muhammad." Kisha akaendelea kusema: "Yule mpwa wangu anasema kwamba ipo siku atakapozitawala hazina za 'Kisra' na 'Kaisari.' Ninaapa kuwa jina la Allah, hakuna mfuasi wa dini hii katika uso wa hii ardhi ila hawa watu watatu tu." Kisha yule msimuliaji anasema: "Ningalipenda kwamba ningalikuwa wanne wao!"

Kwa vile masimulizi haya hayamhusu Sayyidna Ali (a.s.) moja kwa moja hata watu hao washindwao kusimulia wema wake wameyanukuu. Miongoni mwa wana hadithi ni Bukhari pekee aliyefikiria kuihesabu kuwa ni 'dhaifu', lakini msimamo wake juu ya kizazi cha Mtume (s.a.w.w.) unafahamika vizuri mno. Msomaji anaweza kuyasoma masimulizi tuliyoy- ataja hapo juu kwa kirefu katika vitabu tulivyovitaja hapa chini.[4]

## Ushahidi Wa Tatu

Katika hotuba na maelezo ya Sayyidna Ali (a.s.) mara nyingi tunaziona sentensi zifuatazo na nyingine zifananazo na hizi:

"Mimi ni mja wa Allah na nduguye Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na ni mkweli aliye mkuu zaidi, na hakuna yeyote awezaye kuitamka sentensi hii baada yangu ila yule mtu aliye mwongo. Nilisali pamoja na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kipindi cha miaka saba[5]kabla ya mtu yeyote mwingine kufanya hivyo."

Mwandishi wa *Al-Ghadir* (Juzuu 3, uk. 222) amewanukuu waandishi wa masimulizi haya kutoka kwenye vitabu vya Ahadith na historia nasi twahitaji kuyanukuu masimulizi haya japo kwa mukhtasari tu.

## Ushahidi Wa Nne

Ahadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na mfuatano wa mashahidi wa maelezo mbali mbali yamenukuliwa kuhusiana na jambo hili.

"Mtu wa kwanza atakayekutana nami kwenye chemchemi ya 'Kauthar' na mtu wa kwanza kusilimu ni Ali mwana wa Abu Twalib."

Vile vile unaweza kusoma kuhusu wanachuoni walioziandika Ahadithi hizi katika juzuu ya tatu ya *Al-Ghadir*, ukurasa wa 320. ushahidi wa sehemu zote mbili umefikia hatua ya mfululizo na mtu

anapojifunza Ahadithi hizi bila ya upendeleo wowote anakuwa na uhakika juu ya Sayyidna Ali (a.s.) kuwa wa mbele zaidi miongoni mwa waumini.

Hivyo basi, mtu huyo hat– apendelea zile kauli nyingine mbili ambazo ni chache kuhusiana na kusimuliwa kwao. Idadi ya wenye kuiunga mkono kauli ya awali (yaani ile isemayo kwamba Sayyidna Ali (a.s.) alikuwa wa awali kusilimu) yenye masahaba wakuu wa Mtume (s.a.w.w.) na wanafunzi wa masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) ni zaidi ya sitini.

Idadi hii ni kubwa mno kiasi mwanachuoni Tabari[6] aliyeliacha jambo hili wazi na akajitosheleza na kuinakili kauli hii tu, anasema kwamba Ibn Sa'id alimwuliza baba yake:

"Je, Abu Bakr alikuwa mtu wa kwanza kusilimu?" baba yake akamjibu akasema: "La! Kabla ya kusilimu kwake zaidi ya watu hamsini walikuwa wamekwisha izunguuka njia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Hata hivyo, Uislamu wake ulikuwa bora kuliko Uislamu wa wengine."

## Majadiliano Ya Ma'mun Na Is'haaq

Mwanachuoni Ibn Abd Rabbih amelinukuu tukio la kuvutia katika kitabu chake '*Aqdul Farid*' liwezalo kuelezwa kwa muhtasari hivi: Mamun aliandaa mkutano wa mdahalo, na yule mwanachuoni mashuhuri, Is'haq alichukua nafasi ya mbele zaidi katika mdahalo huo.

Ilipoanzishwa mada ya Sayyidna Ali (a.s.) kuwatangulia wengine katika kusilimu ikasemwa kuwa Ali alikuwa yu mtoto tu lakini Abu Bakr alikuwa mtu mzima (wakati aliposilimu. Hivyo itikadi yake ina bora kuliko ile ya Ali).

Mara moja Ma'mun akaingilia na kusema: "Je, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwita Ali kwenye Uislamu wakati wa utoto wake, au itikadi yake ilitokana na msukumo wa Mungu? Kamwe mtu hawezi kusema kwamba itikadi yake ilitokana na msukumo, kwa sababu tukimwachilia mbali Ali, hata itikadi ya Mtume haikuwa ya msukumo ila ilikuwa matokeo ya mwongozo na ujumbe ulioletwa na Jibriil kutoka kwa Allah.

Hivyo basi, Mtume (s.a.w.w.) alipomwita kwenye Uislamu, alifanya hivyo kwa hiari yake au aliamrishwa na Allah kulilenda hilo? Hatuwezi kudhania Mtume (s.a.w.w.) ajitie au amtie mtu mwingine kwenye magumu na majukumu bila ya amri ya Allah.

Hivyo basi, hakuna ujira wowote ila kwamba tuseme kuwa mwito wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) unaungwa mkono na amri ya Mungu. Na je, Mola Mjuzi wa yote anaweza kumwamrisha Mtume wake kumwita kijana asiye na welekevu (ambaye 'kuwa na itikadi' au 'kutokuwa na itikadi' vyote ni mamoja) kusilimu? Hakika kitendo cha aina hiyo hakiwezekani kwa Allah, Mwenye hekima, Mjuzi wa yote.

"Hivyo basi, hatuna budi kulimaliza jambo hili kwa kusema kwamba itikadi ya Ali ilikuwa itikadi ya kweli na thabiti isiyokuwa duni hata kidogo inapolinganishwa na itikadi ya wengineo na ni Ali bin Abi Twalib ambaye aya za Qur'ani tukufu zifuatazo zilimstahili zaidi:

{أُولَٰئِكَ الْمُقَرَّبُونَ {11

{فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ {12

{ثُلَّةٌ مِنَ الْأَوَّلِينَ {13

***"Hao ndio watakaokaribishwa. Katika Bustani zenye neema. Fungu kubwa katika wa mwanzo."*** (***Surat al-Waaqi'a, 56: 11-13***)

1. Bihaarul Anwaar, Juzuu 16, uk. 8.
2. Siirah Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 246.
3. Nahju Balaghah, Juzuu 2, uk. 182.
4. Tarikh-i Tabari, Juzuu 2, uk.211; Tarikh-i Kamil, Juzuu 2, uk. 31-38; na Aa'laamul wara, uk. 25.
5. Katika baadhi ya masimulizi kipindi kimetajwa kuwa ni miaka mitano na kwa mujibu wa dalili nyingi inaweza kusemwa kwamba sehemu ya kipindi hiki kiliki- tangulia kipindi cha kazi ya Utume.
6. Tarikh-i Tabari, Juzuu 1, uk. 215. 225

# Sura Ya Kumi Na Nne:Kukoma Kwa Ufunuo

Roho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) iliangazwa na nuru ya wahyi na aliendelea kutafakari na kuwaza juu ya jukumu lisilo kifani ambalo Mola Mwenyezi amempa akisema:

{يَا أَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ {1

{قُمْ فَأَنْذِرْ {2

{وَرَبَّكَ فَكَبِّرْ {3

***"Ewe uliyejitanda shuka yako! Simama na uonye*** (***watu***)***. Na Mola wako umtukuze."*** (***Surat al-Muddath'thir 74:1-3***)***.***

Vile vile alitegemea kuupata ujumbe mwingine kutoka kwa Mola wake, ili kwamba kwa kuzisikia aya hizi na maneno ya Allah, akili yake iweze kuangazwa zaidi na maamuzi na dhamira yake viweze kuwa thabiti zaidi. Hata hivyo zilipita siku na miezi, lakini yule Malaika wa Allah aliyekutana naye mle kwenye pango

la Hira hakutokea tena na ile sauti isiyonekana iliyoifunulia roho yake haikusikika tena! Hatuifahamu sababu yake.

Yawezekana kwamba sababu ya kukoma kwa ule ufunuo ilikuwa kumpumzisha Mtume (s.a.w.w.), kwa sababu historia inasema kwamba daima ufunuo huandamani na shinikizo la kiroho lisilo la kawaida, hasa katika siku za awali za uteuzi wa Mtume kuishika kazi ya Utume, kwa sababu hadi katika muda ule, bado roho yake haijauzoea uoni wa kisiri wa kiasi kile. Tarehe ya kukoma kwa ule ufunuo pia nayo haifahamiki vizuri, lakini baada ya kuvisoma vitabu vya historian na Ahadithi tunaweza kuamua kwamba huu ufunuo ulikatwa kabla ya ubalighisho wa watu wote na hasa kule kuwabaghilishia ndugu wa karibu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Ilikuwa ni katika muda ambao Mtume (s.a.w.w.) bado Hajayapanua mahubiri yake hadi kuwafikia watu wote na kule kuwasiliana na watu binafsi kulikuwa bado hakujadumishwa. Hata hivyo, kama ilivyonukuliwa na marehemu Allamah Majlis[1] kutoka kwenye kitabu '*Manaaqib*' cha Ibn Shahr Aarhub, muda wa kukoma kwa ufunuo kulikuwa ni baada ya kuyapanua mahubiri yake hadi Mtume (s.a.w.w.) kuwahubiria Uislamu nduguze wa karibu. Hivyo basi, tunaweza kusema kwamba tukio hili lilitokea katika mwaka wa nne tangu Mtume (s.a.w.w.) kuteuliwa kuishika kazi ya Utume, kwa kuwa kule kuwahubiria Uislamu nduguze kulifanyika baada ya miaka mitatu tangu kuanza kwa Utume wake.

Wako baadhi ya wanahistoria wenye maoni tofauti[2] kuhusiana na jambo hili, ambayo hayakubaliani na ukweli uliothibiti wa waandishi wa wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na mkewe mpenzi wanasema: "Pale ulipokatwa mkondo wa ufunuo, mchafuko wa akili na shaka iliyomkumba Mtume (s.a.w.w.) wakati wa kuanza kwa kazi ya utume ulifufuka upya, mkewe nae akapatwa na mshtuko na akamwambia: "Nadhania kwamba Allah amekata mawasiliano yake na wewe."
Baada ya kuyasikia maneno hayo alirejea kule kwenye sehemu yake ya siku zote (Mlima Hira). Wakati ule ule ufunuo wa mbinguni ulikuja mara mbili na kuzungumza naye kwa maneno ya aya zifuatazo:

{وَالضُّحَىٰ} 1

{وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ} 2

{مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلَىٰ} 3

{وَلَلْآخِرَةُ خَيْرٌ لَكَ مِنَ الْأُولَىٰ} 4

{وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ} 5

{أَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيمًا فَآوَىٰ} 6

{وَوَجَدَكَ ضَالًّا فَهَدَىٰ} 7

{وَوَجَدَكَ عَائِلًا فَأَغْنَىٰ} 8

{فَأَمَّا الْيَتِيمَ فَلَا تَقْهَرْ} 9

{وَأَمَّا السَّائِلَ فَلَا تَنْهَرْ} 10

{وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ} 11

***"Naapa kwa mng'ao wa mchana na kwa usiku unapotia giza. Hakukuacha Mola wako, wala hakukukasirikia. Bila shaka mwisho ni bora zaidi kwako kuliko mwanzo. Na Mola wako hivi karibuni ataku- pa na utaridhika. Je, hakukuta ukiwa u yatima na akakuhifadhi? Na akakukuta ukihangaika Naye akakuongoza? Na akakukuta*** (***ukiwa***) ***masikini naye akakutajirisha? Basi usimkemee yatima, wala usimkaripie mwenye kuomba. Na neema ya Mola wako itangaze."*** (***Surat Adh-Dhuha, 93:1-11***)***.***

Kufunuliwa kwa aya hizi kulimpa furaha isiyo kifani na akatambua kwam- ba chochote kile kisemwacho na watu juu yake, hakikuwa na msingi wowote.

## Maoni Yetu Juu Ya Jambo Hili

Hatuwezi kuyakubali masimulizi haya katika ukamilifu wake. Maisha ya Bibi Khadija na mazungumzo yake na mumewe pamoja na ukumbuko wake bado vimehifadhiwa katika historia. Ni huyu huyu Bibi Khadija aliyefanya kazi kwa juhudi zake zote katika siku za awali za ufunuo katika kuuondoa mshituko wa mumewe. Basi vipi sasa anaweza kuwa chanzo cha mshituko wake, wakati bado angali akiziona tabia na utu wema wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na alijua ya kwamba Allah, anayemwamini, alikuwa mwadilifu na mnyofu. Ndiyo! Tukiyaachilia mbali yoye haya, vipi aweza kujenga akilini mwake, mashaka ya ajabu juu ya Allah na Mtume wake?

Licha ya haya yote wanachuoni wameeleza katika vitabu vyao vya '*Kalaam*' (theolojia) kwamba: "Baada ya kujipatia nyororo ya tabia njema zaidi zenye kumwainisha aliyenazo kutokana na wengineo, cheo cha Utume anakipewa mtu yule mwenye tabia bora zaidi na sifa maarufu, na kwa kadiri Mtume akosavyo

kuwa na idadi fulani ua hizi tabia maarufu, na hazitimizi masharti maalumu, cheo hiki hakipewi kamwe.

Juu ya sifa zote hizi ni utakaso, amani ya kiakili, itikadi, na kumtawakali Allah, na kwa sababu Mtume anakuwanazo sifa hizi, fikara zake haziwezi kupotoka." Wanachuoni wamesema: "Maendeleo ya polepole ya Mtume huanzia tangu utotoni mwake na pole pole elimu yake huifikia hatua ya ukamilifu. Haipiti akilini mwake shaka juu ya vitu avionavyo au avisikiavyo, japo iliyo ndogo kabisa. Zaidi ya hapo, maelezo ya mtu yeyote yule hayajengi shaka yoyote akilini mwa mtu mwenye cheo hiki."

Aya za Qur'ani tukufu tulizozinukuu hapo juu, na hasa ile aya isemayo: "**Hakukuacha Mola wako, wala hakukukasirikia.**"
Inaonyesha tu kwamba mtu fulani alimwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) maneno haya, lakini hayaonyeshi ni nani aliyeyasema na kama yalikuwa na athari gani nafsini mwake. Hata hivyo baadhi ya wafasiri (wa Qur'ani tukufu) wanasema kwamba maneno haya yalitamkwa na washirikina, na kutokana na uwezekano huu, aya zote hizi haziwezi kuhusiana na kuanza kwa ufunuo, kwa sababu hakuna yeyote miongoni mwao aliyeujua mwanzo wa Utume pamoja na kushuka kwa ufunuo ila Khadija na Ali, ili kwamba aweze kutoa lawama zake. Jambo hili lilikuwa hivi kiasi kwamba kama tutakavyoeleza baadae, ukweli wa Utume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) haukufahamiwa na washirika kwa kipindi fulani cha miaka mitatu kamili na alikuwa Hajaamrishwa kuutangaza Utume wake kwa watu wote, hadi ilipofunuliwa aya isemayo:

{فَاصْدَعْ بِمَا تُؤْمَرُ وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ {94

"**Basi yatangaze yale uliyoamrishwa,.....**" (***Surat al-Hijri,*** **15:94**).

Hivyo basi, hadithi ya kukoma kwa ufunuo ina ushuhuda wa kihistoria na haina ushuhuda wa Qur'ani, na huo nao hauna sura ya kupinga bali una tabia tulioieleza mwanzoni mwa sura hii.

## Mtukufu Mtume (S.A.W.W) Aliyaanza Mageuzi Kuanzia Kwenye Mzunguko Mdogo

Watu wenye hekima na viongozi wa jamii huzungumzia juu ya mipango mikubwa mikubwa, lakini huzianza kazi zao kwenye eneo dogo, na mara tu baada ya kupata ushindi mara moja hufanya juhudi ya kuzipanua kazi zao na hulipanua eneo la kutendea kazi kulingana na ushindi wao, na kujitahidi katika maendeleo ya pole pole.

Mwenye hekima mmoja[3] alimuuliza mmoja wa viongozi wa moja ya Mataifa makubwa ya siku hizi: "Ni ipi siri ya mafanikio yako kwenye mambo ya jamii?" Kiongozi yule alijibu akisema: "Njia ya fikara za watu wa Magharibi kama sie ni tofauti na zile zenu za watu wa Mashariki.

Daima tunaianza kazi kwa mpango mpana na uliofikiriwa vizuri lakini tunaianza kutoka kwenye sehemu ndogo na tunajaribu kuipanua baada ya kupata ushindi.

Na kama kwenye wakati ule tutagundua kuwa mpango ule si sahihi huiacha mara moja na kuanza kazi nyingine. Kwa upande mwingine, ninyi watu wa Mashariki hujitia kwenye kazi kwa mpango mpana na kuianza kazi hiyo kwenye sehemu kubwa na kuuweka mpango mzima kwenye vitendo, wote mara moja.

Na wakati wa kuitenda mkipatwa na tatizo, hamna njia yoyote ya kugeukia kulia ila kupata hasara kubwa. Zaidi ya hapo, ari yenu imekuwa katika hali ya kwamba daima mnafanya haraka na papara na daima mnataka kuyavuna mazao yenu siku ile ile ya kwanza. Mnatamani kuyapata matokeo ya mwisho katika siku za awali, na jambo hili lenyewe ni njia ya hatari sana ya fikara za kijamii ambayo hum– fanya mwanaadamu kuishia kwenye mvutano wa ajabu.

Tunafikiria kwamba njia hii ya fikara haihusiani ama na Mashariki au Magharibi. Daima watu wazima na wenye hekima na elimu huyafikia malengo yao kwa njia hii.
Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) vilevile aliyatenda mambo kwa mujibu wa kanuni hii ikubalikayo na aliibaghilisha dini yake kwa kipindi cha miaka mitatu kamili bila ya kufanya papara. Aliwafikishia dini wale aliowaona kuwa wanastahili na walioko tayari kwa mujibu wa mtazamo wa fikara na uwezo.

Ingawa lengo lake lilikuwa kuijenga jamii kubwa na iliyoenea kote duniani ili kwamba aweze kuwaleta watu wote chini ya athari ya bendera moja (bendera ya Upweke wa Allah) lakini kwenye kipindi hiki cha miaka mitatu, katu hakukimbilia kwenye ubalighisho kwa watu wote.

Alifanya mawasiliano maalumu tu na watu fulani fulani na kuwalingania kwenye dini yake watu wale aliowaona kuwa wanastahili, wanafaa na walio tayari kuipokea dini yake. Hatimae ni kwamba, kwenye kipindi hiki cha miaka mitatu alifaulu kuwaongoza watu wachache tu.

Katika kipindi hiki cha miaka mitatu machifu wa Waquraishi walikuwa wameleweshwa na utunzaji wa Ka'aba. Wakati Firauni wa Makkah (Abu Sufyani) na genge lake walipopata kuitambua asili ya wito na dai lake, walionyesha tabasamu la dhihaka midomoni mwao na wakaambiana: “Mwale wa mwito wake nao utakufa kama mwito wa Waraqah na Umayyah (waliouingia Ukristo kama matokeo ya kujifunza kwao Taurati na Injili na wakajifanya kuuhubiri Ukristo kwenye mikusanyiko ya Waarabu) na hautapita muda mrefu kabla yeye naye kujiunga na msafara wa wale waliosahaulika.”

Katika kipindi hiki cha miaka mitatu machifu wa Waquraishi hawakuchukua fursa yoyote na Mtukufu Mtume japo iliyo ndogo kabisa lakini daima walimheshimu. Yeye nae hakuwalaumu masanamu na miungu wao wazi wazi kwenye kipindi hiki bali akajishughulisha na kudumisha mawasiliano maalumu na watu wenye uoni wa dhahiri.

Hata hivyo, Waquraishi nao waliamka tangu mwenye ile hatua ya awali wakati ulipofanywa ule mwito maalumu kwa ndugu wa karibu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na ule mwito wa jumla kwa watu wote, na shutuma zake kwa masanamu na vitendo visivyo vya kiutu na tabia za Waquraishi vilianza

kuzungumziwa.

Katika siku ile walitambua kwamba ilikuwako tofauti kubwa sana baina ya mwito wake na ile ya Waraqah na Umayyah. Hivyo basi ulianza upinzani na ushindani wa siri na wa dhahiri. Mwanzoni kabisa alivunja kimya chake mbele ya nduguze na baada ya hapo akautoa mwito wake kwa watu wote.

Hakuna shaka yoyote juu ya ukweli uliopo kwamba matengenezo yenye mizizi iliyozama ndani zaidi, yenye kuathiri maneno yote ya maisha ya mwanaadamu na kumbadili mwelekeo wa jamii, hasa huhitaji nguvu mbili imara – nguvu ya kauli na nguvu ya ulinzi.

Nguvu ya kauli ili kwamba mzungumzaji aweze kuelezea kweli fulani fulani kwa jinsi ivutiayo na aweze kuwavutia watu wote na aweze kuwafikishia watu mawazo yake mwenyewe au zile fikara apokeazo kutoka kwenye ulimwengu wa ufunuo.

Nguvu ya ulinzi ili kwamba itokeapo hatari aweze kuandaa safu ya ulinzi dhidi ya maadui wavamiao. Unapokosekana uwezo huu, mwali wa mwito wake, huzimika pale mwanzoni kabisa.

Nguvu ya kauli ya Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa kamilifu ajabu na hakuna ukanusho wa ukweli kwamba alikuwa mzungumzaji mwenye mvuto aliyeweza kuieleza dini yake kwa ufasaha mkubwa.
Hata hivyo, kwenye siku za awali za mwito wake, hakuwa na ile nguvu ya pili, kwa sababu, kwenye hiki kipindi cha miaka mitatu, aliweza kuwasilimisha kiasi cha watu arobaini tu na ni dhahiri kwamba kipindi kidogo kiasi hiki kisingeweza kuchukua kazi ya ulinzi wake.

Hivyo basi, ili kuweza kujipatia safu ya ulinzi na ili kutayarisha kiini cha msingi, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwalingania nduguze wa karibu zaidi kwenye dini yake kabla ya kufanya ulinganiaji wa jumla.

Kwa njia hii aliuondoa unyonge wa ile nguvu ya pili na aliweza kujenga ngome muhimu dhidi ya hatari yoyote ile iliyoweza kutokea. Kwa uchechefu mwito huu ulikuwa wenye faida kwa maana ya kwamba japo nduguze wasingalivutika na dini yake wangalisimama kumlinda kutokana na athari za kidugu na kikabila, hadi ulipowadia wakati ambapo mwito wake ulipowavutia baadhi ya machifu wa taifa hili na kulifanya kundi jingine kumwelekea.

Vile vile aliamini kwamba ule msingi wa mageuzi umesimamia kwenye mageuzi ya mwilini mwa mtu binafsi. Mpaka mtu aweze kuwazuia watoto na ndugu zake kutokana na matendo maovu, vinginevyo mwito aufik- ishao mtu huyu kwa watu wengine hauwezi kuwa na athari zozote, kwa sababu kwenye tukio kama hilo, wapinzani wanaojitumbukiza kwenye lawama, watamuonyesha tabia ya nguduze mwenyewe.

Kutokana na wazo hili, Allah anamwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu kuwaita nduguze kwa maneno haya: “**Na uwaonye jamaa zako wa karibu zaidi**.” (***Surah al-Shua’raa*, 26:214**) ambapo kuhusu ule mwito wa watu wote, Anasema: “**Basi yatangaze yale uliyoamrishwa na ujitenge na washirikina, Nasi tutakuhami dhidi ya maadui**.” (***Surah al- Hijr,* 15:94**)

## Jinsi Ya Kuwalingania Jamaa Wa Karibu

Njia aliyoitumia Mtukufu Mtume (s.a.w) katika kuwalingania jamaa zake wa karibu ilikuwa yenye kuvutia sana, na siri ya njia hii ya mwaliko huwa wazi kabisa baadae pale hali halisi inapodhihirika.

Karibuni wafasiri na wanahistoria wote, wakiitafsiri aya isemayo: "**Na uwaonye jamaa zako wa karibuni zaidi**" Wanaandika kwamba Allah Mwenyezi alimwamrisha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) awaite jamaa zake wa karibu kabisa kwenye dini yake. Baada ya kuchukua tahadhari muhimu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimuagiza Ali bin Abi Twalib, ambaye wakati ule umri wake haukuzidi miaka kumi na mitano, kutayarisha mlo na kutayarisha maziwa pia kwenye mlo huo. Baada ya matayarisho hayo kukamilika, alialika wazee arobaini na watano kutoka miongoni mwa Bani Hashimu na vile vile aliamua kwenye tukio lile kuifichua ile siri iliyofichika.

Hata hivyo, kwa bahati mbaya ule mlo ulipomalizika, mmoja wa ami zake (Abu Lahabi), kabla Mtume (s.a.w.w.) Hajazungumza, alimtangulia kwa kusema mambo yasiyo na msingi na kuifanya hali ya hewa kutofaa kwa kubalighisha kazi ya utume.

Hivyo basi, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliona kuwa inafaa kuliahirisha jambo hilo hadi siku ijayo. Siku iliyofuatia alian- daa tena karamu. Baada ya mlo kwisha aliwageukia wazee wa familia yake na akayaanza mazungumzo yake kwa kumhimidi Allah na kuuhubiri Upweke Wake. Baada ya hapo alisema: "Hakika, kiongozo wa jamii katu hawadanganyi watu wake.
Ninaapa kwa jina la Allah, ambaye hakuna Mungu badala Yake, kwamba nimetumwa na Yeye kama Mjumbe Wake, hususan kwenu ninyi na kwa jumla kwa watu wote wa ulimwenguni humu.

'Ndio! Enyi ndugu zangu! Mtafariki dunia kana kwamba mnalala na baada ya hapo mtarudishwa kwenye uhai tena na mtapokea malipo kufuatana na matendo yenu. Malipo haya ni pepo ya Allah ya milele (kwa wale waliokuwa wema) na Moto wake wa milele (kwa wale waovu)."

Kisha aliongezea kusema: "Hakuna mwanaadamu aliyepata kuwaletea watu wake kilicho chema zaidi ya kile nilichokuleteeni. Nimekuleteeni mibaraka ya ulimwengu huu na ule wa Akhera. Mola wangu ameniamrisha nikuitieni Kwake. Ni nani miongoni mwenu atakayeniunga mkono ili kwamba awe ndugu yangu?" Hotuba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ilipofi- ka hapa, kilitawala kimya kamili juu ya mkutano wote na kila mmoja wa wale waliokuwapo pale alikuwa akifikiria juu ya ukuu wa lengo lile na hatima yake mwenyewe hapo baadae.

Mara kwa ghafla, Sayyidna Ali (a.s.) ambaye wakati ule alikuwa kijana wa umri wa miaka kumi na mitano, alivunja kimya kilichokuwa kimetawala mkutanoni pale. Alisimama na kusema kwa sauti ya nguvu: "Ewe Mtume wa Allah! Mimi niko tayari kukuunga mkono!" Mtume (s.a.w.w.) alimwamrisha akae. Akarudia maneneo tuliyoyetaja hapo juu mara tatu lakini hakuna yeyote aliyejibu ila yule kijana wa umri wa miaka kumi na mitano, ambaye alikuwa akitoa jibu lilelile.

Hapo Mtume (s.a.w.w.) aliwageukia jamaa zake na kusema: “Enyi watu! Kijana huyu ni ndugu yangu, wasii wangu na mrithi wangu miongoni mwenu. Yasikilizeni ayase– mayo na mfuateni.” Alipofikia hatua hii mkutano ulimalizika na wale waliokuwapo pale wal– imgeukia Bwana Abu Twalib kwa nyuso za tabasamu na kusema: “Muhammad amekutaka umfuate mwanao na kuzitii amri zake na amemtangaza kuwa mkuu wako.”[4]

Kilichoandikwa hapo juu ni kiini cha maelezo marefu yaliyonukuliwa na wafasiri na wanahistoria wengi kwa maneno tofauti tofauti ila Ibni Taymiyah mwenye maoni maalumu juu ya watu wa familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), hakuna yeyote aliyetia shaka juu ya usahihi wa Hadith hii na wote wameichukulia kuwa ni ukweli wa kihistoria usiokanika.

## Uhalifu Na Kuvunja Uaminifu

Upotoshaji na kutafsiri vibaya mambo na kuzificha hali halisi ni jambo la dhahiri la uhalifu na kuvunja uaminifu; na wakati wa mkondo wa historia ya kiislamu limekuwapo kundi la waandishi wenye upendeleo walioifanya njia hii na kupunguza thamani ya maandiko yao kutokana na masingizio. Hata hivyo, mkondo wa historia na maendeleo ya elimu umewafichua. Ufuatao hapa chini ni mfano wa masingizio ya aina hii:

Kama ninyi wasomaji wetu mlivyoona, Muhammad bin Jarir Tabari (aliyefariki mnamo mwaka wa 310 Hijiriya) amelisimulia tukio la mwaliko wa jamaa wa karibu zaidi kwa kirefu kwenye kitabu chake cha historia. Hata hivyo, kwenye tafsiri yake,[5] alipokuwa akiitafsiri aya isemayo: “Na uwaonye jamaa zako walio wa karibu zaidi.”

Anataja maneno aliyoyataja kwenye kitabu chake cha historia pamoja na maelezo na wanachuoni waliosimulia tukio hili, lakini anapoifikia sentensi isemayo “Ali yu ndugu yangu, wasii wangu na mrithi wangu.” Anaibadili sentensi hii na kusema “Ali yu ndugu yangu na kadhalika.” Na hakuna shaka na ukweli uliopo kwamba kuyaacha maneno: “wasii wangu na mrithi wangu” na kuweka maneno “na kadhalika” kuwa mbadala wao si chochote ila ni kuvunja uaminifu.

Hakutosheka na hilo tu lakini vile vile ameibadili sentensi ambayo yeye Mtume (s.a.w.w.) aliitamka kumhusu Sayyidna Ali (a.s.) (Huyu ni ndugu yangu na ni wasii wangu na mrithi wangu) na vile vile ameyatumia maneno yale yale “na kadhalika.”

Mwanahistoria hana budi kuwa huru na asiye na upendeleo katika kusimulia mambo na hana budi kuandika kile alichokichunguza na kukiona kuwa ni sahihi, kwa ushujaa usio kifani na uadilifu. Naweza kusema kwamba katu kilichofanya Tabari ayaache maneno haya mawili na kuweka mbadala wa maneno mawili ni ile chuki wake wa Kidini, kwa sababu hakumfikiria Sayyidna Ali (a.s.) kuwa makamu na mrithi wa mara moja wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Na kwa kuwa haya maneno mawili huonyesha dhahiri kwamba Sayyidna Ali (a.s.) alikuwa Wasii na

mrithi wa mara moja, Tabari anaona kuwa ni muhimu kuuhami msimamo wake wa kidini pia, alipokuwa akifafanua juu ya tukio la ufunuo wa aya hii.

Ibn Kathir Shaami, aliyefariki dunia kwenye mwaka wa 732 Hijiriya nae ameipita njia hii kwenye kitabu chake cha historia[6] aliyoipita Tabari kwenye siku za mwanzoni kwenye Tafsir yake. Hatuwezi kumsamehe Ibn Kathir kwa vyovyote vile, kwa sababu, *Tarikh-i Tabari* yenyewe ndio msingi wa Kitabu chake cha historia naye wazi wazi ameirejea *Tarikh Tabari* katika kuipanga sehemu hii ya kitabu chake, lakini ingawa alifanya hivi ameshindwa kulinukuu jambo hili kutoka kwenye kitabu cha historia tulichokitaja hapo, na kinyume na tegemeo letu amelitaja tukio hili kwa mujiubu wa *Tafsiri Tabari*.

Na tunauona uasi uliofanywa na Daktari Haykal, aliyekuwa Waziri wa Elimu wa Misri na mwandishi wa kitabu kiitwacho: "*Hayaat-i Muhammad*" aliyeifungua njia kwa ajili ya kizazi kipya kuuendea upotoshaji wa ukweli. Kidogo inashangaza kwamba inapokuwa kwamba kwenye dibaji ya kitabu chake ameyatumia maneno makali sana kwa wataalamu wa nchi za Mashatiki na kuwalaumu kwa upotoshaji wa mambo na uzushi, yeye mwenyewe analitenda kosa hili hili, kisha anaendelea mbele kidogo kwa sababu:

Kwanza: Kwenye toleo lake la kwanza la kitabu tulichokitaja, analinukuu tukio hili kwa njia ya pande mbili muhimu, yeye anaiandika sentensi moja tu (nayo ni Mtukufu Mtume s.a.w.w aliwageukia wazee na akasema:

Ni nani miongoni mwenu atakayeniunga mkono kwenye kazi hii ili awe ndugu yangu, wasii wangu na mrithi wangu?) lakini akaiacha kabisa ile sentensi nyingine ambayo Mtume (s.a.w.w.) alizungumzia Sayyidna Ali (a.s.) akiueleza uungaji mkono wake, na katu hakutaja kwamba Mtume (s.a.w.w.) alizungumzia akisema: "Enyi watu! Kijana huyu yu ndugu yangu, wasii wangu na mrithi wangu."

Pili: Kwenye toleo la pili na la tatu aliendelea mbele hatua moja na akaziacha sentensi zote mbili kutoka kwenye zile sentensi mbili na hivyo akapiga pigo lisilo lengeka kwenye msimamo wake yeye mwenyewe pamoja na ule wa kitabu chake.

## Utume Na Uimam Vimeungana

Kuutangaza urithi (Imamati) wa Sayyidna Ali (a.s.) siku za awali za utume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kunaonyesha kwamba nafasi hizi mbili hazikutengana, na wakati Mtume wa Allah alipotangazwa mbele ya watu mrithi wake naye aliteuliwa na kutambulishwa kwa watu siku ile ile, na jambo hili lenyewe laonyesha kwamba Utume na Uimamu vimeungwa na hakuna umbali baina yao.

Kwa dhahiri shahiri kabisa tukio hili lathibitisha uhodari na ushujaa wa kiroho wa Imam Ali (a.s.), Amiri wa Waumini. Hii ni kwa sababu, kwenye mkutano ambao watu wenye uzoefu na wazee walizama kwenye tafakari na mshangao, yeye alitamka uungaji mkono wake na utii kwa uthabiti halisi na akaudhihirisha uadui wake kwa maadui wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pasi na kuipita njia ya wanasiasa wanaojijali wenyewe. Ingawa wakati ule alikuwa kijana mdoga zaidi miongoni mwa wale waliokuwapo

pale, kwa kadiri umri ulivyohusika, lakini ushirikiano wake na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kipindi kirefu kwenye siku zilizopita, ulikuwa umeitayarisha akili yake kwa kupokea hali halisi ambazo wazee wa taifa lile walisitasita kuzikubali.

Abu Ja'far Askari amezungumza kwa ufasaha zaidi juu ya tukio hili. Wasomaji wanaweza kulirejea jambo hili lenyewe ndani ya *Sharh-i Nahjul Balagha*.[7]

1. Bihaarul Anwaar, Juzuu 18, uk. 197.
2. Tarikh-I Tabari, Juzu 1, uk. 48-52.
3. Mmoja wa wafalme wa ukoo wa Qajaar alipotembelea London.
4. Tarikh-i-Tabari, Juzuu 2, uk. 62-63; Tarikh-i Kamili, Juzuu 2, uk. 40-41; Musnad Ahmad bin Hanbal, Juzuu 1, uk. 111; na Sharh-i Nahjul Balaghah ya Ibn Abal Hadid, Juzuu 13, uk. 210-22.
5. Tafsir-i Tabari, Juzuu 19, uk. 74.
6. Al-Bidayah wan Nihaya, Juzuu 3, uk. 40.
7. Sharh-i Nahjul Balaghah, cha Ibn Abil Hadid (toleo la Misri) Juzu 13, kuanzia ukurasa 215 na kuendelea.

# Sura Ya Kumi Na Tano

## Kuwalingania Watu Wote

Ilikuwa imekwishapita miaka mitatu tangu kuanza kwa kazi ya Utume. Baada ya kuwaitia jamaa zake wa karibu zaidi kwenye Uislamu, Mtume (s.a.w.w.) aliamua kufanya mwito kwa watu wote.

Kwenye hiki kipindi cha miaka mitatu, amewaongoza baadhi ya watu kwenye Uislamu kwa mawasiliano maalum, lakini wakati huu aliwaita watu wote kwenye dini ya kumwabudu Allah, Aliye Mmoja wa Pekee. Siku moja alisimama kwenye mwamba mrefu na akasema kwa sauti kuu: "Yaa Sabah'aah!"[1]

Mwito wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ulipata mazingatio. Baadhi ya watu waliotokana na familia tofauti za Waquraishi walimkimbilia. Kisha aliwageukia wale waliokusanyika pale na kusema:

"Enyi watu! Je, mtaniamini kama nikikuambieni ya kwamba maadui zenu wako kwenye upande wa pili wa kilima hiki (safa) na wanadhamiria kuyashambulia maisha na mali zenu?" Wote wakamjibu wakasema: "Katu hatujasikia jambo lolote la uongo kutoka kwako maishani mwetu mwote." Kisha Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Enyi Waquraishi! Jiepusheni kutokana na Moto. Sina chochote niwezacho kukutendeeni mbele ya Allah. Ninakuonyeni dhidi ya mateso makali!" Kisha akaongeza kusema: "Nafasi yangu ni kama ile ya mlinzi, amwonaye adui kwa mbali na upesi upesi akawakimbilia watu wake kwa ajili ya usalama wao na kuwaonya dhidi ya hatari inayowakabilia kwa kusema: "Yaa Sabah'aah kwa njia fulani malumu."
Sentensi hizi zanaashiria msingi wa mwito wake na dini. Kwa kadiri fulani Waquraishi walikuwa wakiitambua dini yake hii, lakini maneno haya yalijenga hofu nyoyoni mwao kiasi kwamba mmoja wa

viongozi wa ukafiri (Abu Lahabi) alikivunja kimya cha watu wale na akasema: “Ole wako! Hivi umetuita kwa ajili ya jambo hili?” Kisha wale watu wakatawanyika.

## Wajibu Wa Imani Na Uvumilivu

Siri ya ushindi wa kila mtu imelalia kwenye mambo mawili: La kwanza, ni imani juu ya lengo lake mtu, na la pili, ni umadhubuti na juhudi kwenye njia ya kulifikia kwake lengo hili. Imani ni kichocheo cha ndani ambacho mchana na usiku hakina budi kumsukumiza mtu kwenye kuyafikia malengo yake, kwa sababu anaamini kwa dhati kwamba ustawi wake, ubora, kuneemeka kwake na mwisho mwema vinashirikiana nayo.

Na kuhusiana na shauku ambayo mwanaadamu anakuwa nayo mwenyewe, kila anapoikuza imani na matumaini yake, basi kwa utaratibu ule ule nguvu ya imani yake humwongoza na kumshauri kuyashinda magumu yote na kumweka mbali na shaka yoyote ile, ingawa ukweli uliopo ni kwamba, ustawi wake waweza kutegemeana na kulifikia lengo maalumu. Kwa mfano, mgonjwa ajuaye kwamba tiba yake na ustawi wake vinategemea kunywa dawa iwashayo, atainywa kwa urahisi, na mzamiaji aaminiye kwamba kuna lulu chini ya wimbi la bahari, basi hujitupa ndani ya kinywa cha wimbi bila ya kujali; na kuibuka baada ya kulifikia lengo lake.

Hata hivyo, iwapo yule mgonjwa au mzamiaji wana mashaka juu ya kuyafikia malengo yao, au hawaamini hata kidogo faida ya kazi yao, hawatachukua hatua yoyote kwenye mwelekeo ule, au japo wafanye, watakabiliwa na matatizo na machungu. Hivyo basi, ni ile nguvu ya imani hasana mategemeo vinavyotatua matatizo yote.

Hata hivyo, hakuna shaka yoyote juu ya ukweli uliopo kwamba mtu kuyafikia malengo yake kunaandamana na matatizo na vikwazo. Hivyo basi, ni muhimu kwetu kupambana dhidi ya vizuizi na kwa nguvu zetu zote kufanya juhudi ihitajikayo juu ya jambo lile, ili kwamba vikwazo vyote viweze kuondoka. Tangu kale imekuwa ikisemekana kwamba popote pale liwapo ua (lengo lenye tunzo) vile vile pana mwiba (tatizo) pamoja nalo. Hivyo basi, ua lile ni lazima lichumwe katika hali ambayo ule mwiba hautaichoma mikono au miguu ya mchumaji.

Qur’ani tukufu imelitaja jambo hili (kwamba siri ya ushindi imo mwenye imani juu ya lengo na uvumilivu wa mtu katika kulifikia lengo lile) katika sentensi fupi na imesema; **“Hakika wale wanaosema: ‘Mola wetu ni Allah’ kisha wakaendelea kuushika unyofu.....” (*Surah al-Fussilat*, 41:30).**

Yaani wale wamwaminio Allah na kuliamini lengo maalumu na kisha wakaonyesha uimara, na uhodari, bila shaka watalifikia lengo lao na watasaidiwa na Malaika.

## Uthabiti Na Ustahimilivu Wa Mtukufu Mtume (S.A.W.W.)

Kama matokeo ya mawasiliano maalumu ya Mtume (s.a.w.w.) kabla ya ‘kuhubiri Uislamu kwa watu

wote’ na juhudi zake zisizolegea baada ya hapo, timu iliyoteuliwa na aminifu iliundwa dhidi ya nguvu za ukafiri na ibada ya masanamu. Waislamu waliosilimu kwa siri kabla ya ‘ulingano kwa watu wote’ walipata uzoefu na wale walioitika mwito wa Mtume (s.a.w.w.) baada ya kulingania huko, na ikagonga kengele ya hatari kwenye mikusanyiko yote ya ukafiri na ushirikina.
Hakuna shaka kwamba ilikuwa rahisi kwa Waquraishi waliokuwa na nguvu na silaha za kutosha kukisagasaga chama hiki kinachoanza, lakini sababu ya hofu yao ilikuwa kwam– ba wanachama wa chama hiki kipya hawakuwa wa familia moja, bali watu wa familia mbali mbali nao wamesilimu. Hivyo, haikuwa rahisi kwa Waquraishi kuchukua hatua za uamuzi.

Machifu wa Kikuraishi, baada ya kushauriana waliamua kuubomoa msingi wa imani hii na yule mwanzilishi wa hii dini mpya kwa njia mbali mbali. Waliamua kulifikia lengo hili kwa kumwendea kwenye nyakati mbali mbali na vitu vya kuvutia na wakati mwingine kumwendea na kumpa ahadi mbali mbali na mara kwa mara kutumia vitisho na kumtesa. Kwa kipindi cha miaka kumi Waquraishi walifanya hivyo na hatimaye waliamua kumwua Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Hivyo basi, ili kumwokoa, Allah alimwamrisha Mtume (s.a.w.w.) kuutoka mji wa Makkah.

Katika kipindi hicho kilichokwisha elezewa, chifu wa Bani Hashimu alikuwa ni Bwana Abu Twalib. Alikuwa ni mtu aliyekuwa na tabia ya kiungwana na moyo wa ukarimu, na nyumba yake ilikuwa kimbilio la masikini na yatima. Mbali na kuwa chifu wa Makkah na kuzishika kazi fulani fulani zihusianazo na Ka’aba tukufu, pia alikuwa na cheo kikuu kwenye jamii ya Waarabu na kwa kuwa alikuwa mlezi wa Mtume (s.a.w.w.) baada ya kufariki dunia kwa Bwana Abdul–Muttalib, hivyo machifu wengine wa Waquraishi walimwendea kwa kikundi[2] na kumwambia hivi:

“Ewe Abu Twalib! Mpwa wako anawatukana miungu wetu, anaisema vibaya dini yetu, anazicheka fikara na itikadi zetu na anawachukulia jadi zetu kuwa walipotoka. Mwambie aachane nasi au umweke mikononi mwetu na ujizuie kumpa msaada.”[3]

Mzee wa Waquraishi na kiongozi wa ukoo wa Bani Hashim aliwajibu kwa namna ya busara na kwa sauti laini, na matokeo yake waliyaacha matendo yao hayo. Hata hivyo, Uislamu ulikuwa ukipenya na kuenea siku hadi siku na upeo wa hisia za kiroho za dini ya Mtume (s.a.w.w.) na maneno ya kuvutia na ya ufasaha ya kile Kitabu cha Mbinguni (Qur’ani tukufu) vilikuwa vikuipa msaada. Mtume (s.a.w) aliiwasilisha dini yake mbele ya watu hasa miezi ambayo vita iliharimishwa, wakati idadi kubwa ya mahu– jaji walipokusanyika mjini Makkah. Hotuba zake zenye ufasaha wa lugha na utamu na itikadi zake zenye kuvutia viliwavutia watu wengi.

Wakati huo huo, yule Firauni nae alitambua ya kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amepata umaarufu miongoni mwa makabila yote na amejipatia wafuasi wengi miongoni mwa makabila ya kiarabu yaishiyo mijini na mabedui. Hivyo mara moja wakaamua kumwendea kwa mara nyingine tena yule msaidizi pekee wa Mtume (Abu Talib) kumfanya atambue zile hatari ambazo zimeukumba uhuru wa watu wa Makkah na dini yao kutokana na ulinganiaji na kupanuka kwa Uislam. Hivyo wakamwendea tena kwa pamoja, na wakiyarejea maombi yao ya awali, walimwambia:

“Ewe Abu Twalib! Wewe ni mtu bora zaidi miongoni mwetu katika utukufu na umri, hata hivyo tulikujia hapo kabla na kukuomba umzuie mpwa wako asihubiri hii dini yake mpya, lakini hukuyasikiliza maneno yetu. Sasa hali imekuwa isiyovumilika kwa upande wetu. Hatuwezi kuvumilia zaidi kwamba mtu fulani awatusi miungu wetu na atudhanie kuwa tu wapumbavu na wajinga. Ni muhimu kwako kumzuia kutokana na matendo yote haya, na ambapo ikishindikana tutapigana dhidi yake pamoja na dhidi yako wewe, ambaye ndio msaidizi wake, ili kwamba wajibu wa kila kundi uweze kuwa dhahiri na moja ya makundi haya mawili liangamizwe.”
Bwana Abu Twalib, msaidizi na mlinzi mkuu wa Mtume (s.a.w.w.), kutokana na utambuzi wake na hekima zake kamilifu, alitambua kwamba ilikuwa inafaa kuonyesha uvumilivu kwa watu wale ambao heshima yao yote ya uhai wao ilikuwa ikikabiliwa na hatari.

Hivyo akatwaa msimamo wa amani na akawaahidi kwamba atazifikisha hisia zao machifu wale kwa mpwa wake. Bila shaka jibu hili kimsingi lilitolewa kwa lengo la kuuzima moto wa hasira zao ili kwamba hapo baadae njia ifaayo ya kulitatua tatizo hili iweze kufuatwa. Hivyo basi, baada ya kuondoka kwa machifu wale aliwasiliana na mpwa wake na kumfikishia ujumbe wao, na kwa bahati, ili kuitahini itikadi yake katika lengo lake, alitaka jibu kutoka kwake.

Hata hivyo, alipokuwa akijibu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliitamka sentensi moja inayofikiriwa kuwa moja ya mistari ya historia ivutiayo na ya thamani mno. Haya ndio maelezo ya jibu lake: “Ami yangu mpenzi! Ninaapa kwa jina la Allah kwamba japo waniwekee jua kwenye mkono wangu wa kulia na mwezi kwenye mkono wangu wa kushoto (yaani japo wanipe utawala wa ulimwengu mzima) sitaacha kuitangaza dini yangu na kulitafuta lengo langu, na nitaziendeleza juhudi zangu hadi nizishinde taabu hizi na kulifikia lengo langu la mwisho au niutoe uhai wangu kwa ajili yake”.

Bada ya kusema hivyo macho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yalijiwa na machozi kutokana na huba na shauku ya kulifikia lengo lake na akasimama akaenda zake. Kauli yake yenye kupenya na kuvutia ilitoa hisia za ajabu moyoni mwa yule chifu wa Makkah kiasi kwamba, ingawa zilikuwapo hatari zote zile zilizomwelekea, alimwita yule mpwa wake arudi na alipofika alimwambia: “Ninaapa kwa jina la Allah! Sitaacha kukusaidia na unaweza kuendelea vizuri katika kulifikia lengo lako hadi mwis- honi mwake.”[4]

## Waquraishi Wamwendea Bwana Abu Twalib Kwa Mara Ya Tatu

Kule kuendelea kwa Uislamu kwa kila siku kuliwasumbua mno Waquraishi na walikuwa na juhudi za kupata ufumbuzi wa tatizo hili. Wakakusanyika na wakawa na maoni ya kwamba msaada wa Bwana Abu Twalib unawezekana kwamba ni kutokana na ukweli kwamba alimtwaa Mtume (s.a.w.w.) kama mwanawe na kama ilikuwa ndio hivyo, ingewezekana kwamba wangeweza kumpelekea kijana mwenye sura nzuri na kumtaka amtwae kama mwanawe.

Hivyo basi walimwendea na kijana aliyeitwa ‘Ammaarah bin Walid bin Mughayrah’ aliyependeza mno miongoni mwa vijana wa Makkah, na wakimwendea Bwana Abu Twalib kwa mara ya tatu, walianza kulalamika na kumhofisha kwa maneno haya: “Ewe Abu Twalib! Mwana wa Walid ni kijana mshairi na

vile vile yu mwenye sura ya kupendeza mno na mwenye akili. Tuko tayari kukupa kijana huyu ili umtwae kama mwanao na uache kumsaidia mpwa wako!" Abu Twalib aliposikia hivyo alichomwa sana moyoni, na akawakemea kwa sauti kuu na uso wenye hasira, akisema: "Mnanifanyia udhalimu mkubwa sana! Mnanitaka nikuleleeni mwana wenu nami nikupeni mwanangu kipenzi ili mkamwuue. Ninaapa kwa jina la Allah kwamba haitakuwa hivyo." Hapo akasimama Mut'am bin Adi na akasema: "Pendekezo walilotoa Waquraishi ni la sawasawa kabisa, lakini wewe hutaikubali." Bwana Abu Twalib akajibu akasema: "Hamjakuwa waadilifu na nina uhakika kwamba mnataka kunifidhehesha na kuwachochea Waquraishi wapigane dhidi yangu. Hata hivyo, mko huru kutenda lile mlitakalo!"

## Waquraishi Wajaribu Kumvutia Mtukufu Mtume (S.A.W.W)

Waquraishi walikuwa na uhakika kwamba isingaliwezekana kumfanya Bwana Abu Twalib aukubali ushauri wao na, ingawa hajaeleza dhahiri kuwa yu mwislamu, bado alikuwa na imani kuu kwa mpwa wake na alimpenda sana. Hivyo wakaamua kujizuia kutoingia kwenye mazungum- zo yeyote naye. Hata hivyo, waliifikiria njia nyingine nayo ilikuwa kwamba wamtamanishe Mtume Muhammad kwa kumpa cheo, utajiri zawadi na mwanamke mrembo, ili kwamba ayaache mahubiri yake. Hivyo, wakaenda nyumbani kwa Bwana Abu Twalib kwa kikundi wakati ambapo yule mpwa wake alikuwa ameketi pamoja nae. Msemaji wa kikundi kile alipokuwa akiyafungua mazungumzo alisema: "Ewe Abu Twalib! Muhammad amezitawanya safu zetu zilizokuwa zimeungana na amesababisha mfarakano baina yetu. Amezicheka akili zetu na ametudhihaki sisi na masanamu yetu. Kama anashawishiwa kafanya hivi na umask- ini na ufukara wake, tuko tayari kumpa utajiri mkubwa sana. Kama anataka cheo, tuko tayari kumkubali awe mtawala wetu na tutamsikiliza. Na kama yu mgonjwa na anahitaji matibabu, tutamleta mganga mzoefu kumtibu...."

Bwana Abu Twalib aliugeuzia uso wake kwa Mtume (s.a.w.w.) na akasema: "Wazee wa kabila lako wamekuja na wanaomba kwamba uache kuwashutumu masanamu ili kwamba wao nao wakuache." Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimjibu ami yake akisema: "Sitaki kitu chochote kutoka kwao. Ama kuhusu vitu hivi vinne wanavyovitoa, basi wao nawalipokee neno moja kutoka kwangu ili kwamba, chini ya msaada wake, waweze kuwatawala Waarabu na kuwafanya wasio Waarabu kuwa wafuasi wao." Alipoifikia hatua hii alisimama Abu Jahal na kusema: "Tuko tayari kukusikiliza mara kumi." Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Neno langu pekee ni kwamba muukubali Upweke wa Mola."

Maneno ya Mtume (s.a.w.w.) yaliyokuwa hayategemewi yalikuwa kama maji baridi yaliyomiminwa kwenye birika la moto. Wote wakazongwa na fadhaha kali iliyoandamana na uchungu na kukata tamaa kiasi kwamba pale pale wote kwa pamoja, bila ya kuhiari wakasema: "Tuiache miungu mia tatu na sitini na tumwabudu Allah, mmoja tu!?"

Waquraishi walitoka nyumbani mle hali nyuso zao na macho yao yakiwa yanaungua kwa ghadhabu na walikuwa wakiifikiria njia ya kulifikia lengo lao. Kwenye aya za Qur'ani tukufu zifuatazo tukio hili hasa limeelezwa:[5]

{وَعَجِبُوا أَنْ جَاءَهُمْ مُنْذِرٌ مِنْهُمْ ۖ وَقَالَ الْكَافِرُونَ هَٰذَا سَاحِرٌ كَذَّابٌ} 4

{أَجَعَلَ الْآلِهَةَ إِلَٰهًا وَاحِدًا ۖ إِنَّ هَٰذَا لَشَيْءٌ عُجَابٌ} 5

{وَانْطَلَقَ الْمَلَأُ مِنْهُمْ أَنِ امْشُوا وَاصْبِرُوا عَلَىٰ آلِهَتِكُمْ ۖ إِنَّ هَٰذَا لَشَيْءٌ يُرَادُ} 6

{مَا سَمِعْنَا بِهَٰذَا فِي الْمِلَّةِ الْآخِرَةِ إِنْ هَٰذَا إِلَّا اخْتِلَاقٌ} 7

***"Na makafiri wanastaajabu kwamba amewafikia Mtume kutoka miongoni mwao; makafiri wanasema: 'Huyu ni mchawi, mwongo.' Je, anawashutumu miungu wote wengine isipokuwa mmoja tu? Hakika hili ni jambo la ajabu. Kikundi cha machifu wa makafiri wakaondoka kwenye mkutano na Mtume wakiambiana: 'Twendeni. Dumuni kwenye ibada ya miungu wenu. Mtu huyu anataka kukutawaleni. Sisi hatukuyasikia haya kwenye dini iliyopita. Si chochote haya ila ni uzushi."*** (***Surah Sad, 38: 4 – 7***).

## Mfano Wa Mateso Na Maonevu Ya Waquraishi

Moja ya vipindi vya majonzi mengi vya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kilianza siku ile alipoamua kukivunja kimya na wazee wa Waquraishi wakapoteza matumaini yote ya yeye kuvikubali vile vitu walivyotaka kumpa, kutokana na maneno yake maarufu:

"Ninaapa kwa jina la Allah! Japo muniwekee jua kwenye mkono wangu wa kulia na mwezi kwenye mkono wangu wa kushoto ili kwamba niyaache mahubiri yangu, sitapumzika hadi Allah aifanye dini yangu ishinde au niyatoe maisha yangu kwa ajili yake!" Hadi kwenye muda ule Waquraishi walikuwa, wakati wa makabiliano yote naye, waliihifadhi heshima yake, lakini walipoona kwamba zawadi zao za upatanisho zimeshindikana, walilazimika kuibadili njia ya fikara zao na kuuzuia Uislamu kuenea kwa gharama zote na kuzi– tumia njia zote kwa lengo hili. Hivyo basi, baraza la Waquraishi liliamua kwa pamoja kutumia dhihaka, mateso na vitisho ili kumzuia Mtume (s.a.w.w.) kutokana na kulitekeleza lengo lake.

Ni dhahiri kwamba mwana mageuzi, mwenye shauku ya kuwaongoza watu wa ulimwengu wote hana budi kuzingatia subira na uvumilivu mbele ya usumbufu, mateso, mashambulizi ya kiuwoga na mapigo ya kimwili na kiakili, ili kwamba kidogo kidogo aweze kuyashinda matatizo, na hii ndiyo iliyokuwa sera ya wana mageuzi wengine vilevile. Hapa chini tunatoa taarifa za baadhi ya maonevu na mateso ya Waquraishi ili kwamba kiwango cha subira na uvumilivu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) viweze kudhihirika.

Mbali na kipengele cha kiakili na kiroho (imani, uthabiti na uvumilivu) kilichomsaidia Mtume (s.a.w.w.) kwa ndani, vile vile alikuwa na kipengele cha nje kilichomhakikishia usalama na msaada kwa ajili yake, na hicho kilikuwa kule kuungwa mkono na Bani Hashim na Bwana Abu Twalib akiwa kiongozi wao, kwa sababu Bwana Abu Twalib alipotambua kwamba Waquraishi wamechukua uamuzi wa mwisho na usiobadilika wa kumtesa mpwa wake, aliwakusanya watu wote wa ukoo wa Bani Hashim na kuwaomba wamlinde Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Baadhi yao walijitolea kumsaidia na kumlinda kwa ajili ya imani yao na wengine walikubali kufanya hivyo kwa sababu ya ujamaa.

Kutokana nao ni watu watatu tu (Abu Lahabi na wengine wawili ambao majina yao tutayataja hapo baadae), pamoja na maadui wengine wa Mtume (s.a.w.w.) waliojizuia kuyakubali maamuzi yake. Hata hivyo, ingawa yalikuwapo hayo, hizi hatua za kiulinzi hazikuweza kumhami dhidi ya baadhi ya matokeo yasiy- opendeza na kila maadui walipomwona akiwa peke yake, hawakuacha kumtendea kila aina ya madhara. Huu ni mfano wa maonevu aliyopatiwa Mtume (s.a.w.w.) na Waquraushi.

Siku moja Abu Jahl alimwona Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenye kilima cha Safa na akamtusi na kumhuzunisha. Mtume (s.a.w.w.) hakuzungumza naye hata kidogo na akaenda nyumbani kwake. Vile vile Abu Jahl alik- wenda kujiunga na Waquraishi waliokuwa wamekusanyika kandoni mwa Ka'aba. Bwana Hamza aliyekuwa ami na ndugu wa kunyonya wa Mtume (s.a.w.w.), nae alirudi siku ile ile kutoka kwenye uwindaji na alikuwa amechukua upinde wake begani mwake. Ilikuwa ni desturi yake kwamba baada ya kurudi mjini Makkah na kabla ya kuwaona watoto na ndugu zake, alikwenda kwenye Ka'aba na kufanya Tawafu na kisha ndipo ayaendee makundi mbali mbali ya Waquraishi waliokusanyika kandoni mwa Ka'aba na kusalimiana nao.

Katika siku ile baada ya kuzifanya ibada hizi, alikwenda nyumbani kwake. Kwa bahati mjakazi wa Abdullah Jad'aan, aliyelishuhudia tukio tulilolita- ja hapo juu, alimjia na kumwambia: "Ewe Abu Ammarah (jina la kiukoo la Hamzah)!
Natamani kwamba ungekuwapo hapa dakika chache kabla na ukawa umeliona tukio nililoliona! Hapo ungalifahamu jinsi Abu Jahl alivy- omtusi na kumwonea mpwa wako." Maneno ya yule mjakazi yalijenga hisia ngeni akilini mwa Bwana Hamza na akaamua kulipiza kisasi cha kutusiwa kwa mpwa wake kwa Abu Jahl, kabla Hajafanya jambo lolote lile. Hivyo basi, alirudi na akamwona Abu Jahl akiwa amekaa miongoni mwa kundi la Waquraishi.

Bila ya kuzungumza na yeyote yule, aliuinua upinde wake wa kuwindia na kuupiga kichwani mwa Abu Lahab na fuvu lake la kichwa likajeruhiwa. Kisha akamwambia: "Unamtusi yeye (Mtume s.a.w.w) na hali mimi nimeipokea dini yake nami ninaipita njia ile ile anayoifuata. Kama una nguvu yoyote ile, basi toka tupigane!"

Hapo kikundi cha watu wa ukoo wa Bani Makhzuni wakasimama ili kumwunga mkono Abu Jahl, hata hivyo, kwa kuwa yeye alikuwa mtu mjanja na mwana diplomasia, aliepusha kila aina ya ugomvi na kujihami na akasema: "Nilimkosea Muhammad, nae Hamza anayo haki ya kutokuwa na raha juu ya jambo hili."[6]

Ukweli huu wa kihistoria uliokubalika unaonyesha kwamba Bwana Hamza, ambaye baadaye alikuwa mmoja wa maamiri jeshi wa Uislamu wakuu, alikuwa mtu mwenye ushawishi na shujaa. Alifanya kila aliloliweza katika kumhami na kumlinda Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na kukiimarisha kikundi cha Waislamu. Kama asemavyo Ibn Athir, 7

Waquraishi waliuona Uislamu wa Hamza kuwa ni moja ya vipengele vikubwa zaidi kwa maendeleo na nguvu ya Waislamu na hivyo basi, walikimbilia mipango mingineyo tutakayoieleza baadae.

Wanahistoria wa Kisunni, kama vile Ibn Kathir Shaami wanasisitiza kwamba: "Athari za Uislamu wa Abu Bakr na Ummar hazikuwa ndogo zinapolinganishwa na athari za kusilimu kwa Hamza, na Uislamu wa hawa makhalifa wawili wakuu ulikujakuwa njia ya utukufu, nguvu na uhuru wa Waislamu.8

Hakika hakuna shaka yoyote juu ya ukweli kwamba kila mtu alichangia katika nguvu na kuenea kwa Uislamu, lakini, licha ya hilo, katu haiwezi kusemwa kwamba athari za Uislamu wa hawa makhalifa wawili zilikuwa sawa na athari za Uislamu wa Hamza.

Sababu ya uamuzi huu ni kwamba, Bwana Hamza alikuwa mtu ambaye aliposikia kwamba mzee wa Waquraishi amemtusi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikwenda kumuuliza yule mkosefu bila ya kumtaarifu mtu yeyote juu ya azma yake ile na akalipiza kisasi vikali mno dhidi yake. Na hakuna aliyethubutu kusimama na kumpinga au kupigana naye.

Kwa upande mwingine, Ibn Hisham, mwandishi mkuu wa wasifu wa Mtume wa Uislamu, alisimulia tukio moja lihusianalo na Bwana Abu Bakr lionyeshalo kwamba alipojiunga na kundi la Waislamu hakuwa na nguvu iliyohitajika katika kujihami yeye mwenyewe au Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).9 Maelezo kamili juu ya tukio hilo tunayatoa hapa chini:

"Siku moja Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipita karibu na kundi la Waquraishi. Mara watu wale walimzingira na kila mmoja wao akaanza kuyarudia, kwa njia ya dhihaka, yale maneno yake aliyokuwa akiyasema juu ya masanamu na Siku ya Hukumu na kusema: "Je, unasema hivi?" Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwajibu akisema: 'Ndio, mimi ndimi nisemaye hivi.'

Kwa kuwa Waquraishi waliona kwamba hayuko mtu yeyote wa kumhami Mtume (s.a.w.w.) waliamua kumuua. Hivyo, mtu mmoja alijitokeza na kuyakamata mapindo ya vazi lake. Ilitokea kwamba Bwana Abu Bakr ali- tokea kuwapo pale ubavuni pa Mtume (s.a.w.w.). Akiwa kajawa na machozi machoni, alisimama ili amsaidie Mtume (s.a.w.w.), na akasema: "Je, ni sahihi kwamba mumuue mtu auaminiye Upweke wa Allah?" Baadae (kwa sababu fulani fulani) watu wale waliacha kumtendea maovu Mtume (s.a.w.w.) na akaondoka akaenda zake, na Bwana Abu Bakr akaen- da nyumbani kwake akiwa kajeruhiwa kichwani."

Ingawa tukio hili laweza kuwa ushahidi wa huba na shauku ya Khalifa huyu kwa Mtume (s.a.w.w.), kwanza kabisani ushahidi madhubuti wa udhaifu na woga wake. Linaonyesha kwamba wakati ule hakuwa na nguvu au cheo cha kijamii kitambulikanacho. Na kwa vile hatua ya kivitendo ya Waquraishi

dhidi ya Mtume (s.a.w.w.) ingaliweza kufuatiwa na matokeo maovu dhidi yake, walimwacha yeye na wakayaelekeza makali ya kitendo chao kwa yule mfuasi wake na wakamvunja kichwa chake.

Kama ukiliweka lile tukio la Bwana Hamza lidhihirishalo ujasiri na ushujaa wake sam- bamba na tukio hili mojawapo kati ya matukio, unaweza kuamua vizuri sana kwamba ni Uislamu wa yupi uliokuwa na athari kubwa zaidi kwenye siku za awali za Uislamu juu ya heshima, nguvu na hofu ya makafiri.

Hivi karibuni utasoma habari za Uislamu wa Umar. Uislamu wake nao, ukiwa ni kama ule wa rafiki yake wa tangu kale, haukuimarisha nguvu ya ulinzi wa Waislamu. Lakini kwa Aas bin Waai'l, iliwezekana kwamba damu ya khalifa (Umar) ingeliweza kumwagwa kwenye ile ile siku aliyosilimu, kwa kuwa yeye (Aas bin Waai'l ) alikuja na kulihutubia lile kundi lililotaka kumuua Umar kwa maneno haya: "Mwataka nini kwa mtu aliyejitwalia itikadi kwa ajili yake mwenyewe? Je, mwadhania kwamba ukoo wa Adi utamtoa kwa urahisi? Sentensi hii yaonyesha kwamba ni hofu juu ya ukoo wake iliyowafanya watu wengine kumbakisha hai na ulinzi kutoka kwenye koo za wale watokanao nazo ilikuwa jambo la kawaida na la desturi na haikuwako tofauti yoyote kuhusiana na jambo hili, baina ya wa hali ya juu na wa hali ya chini.

Ndio, Kituo cha ulinzi wa Waislamu kilikuwa ni nyumba ya Bani Hashim na mzigo mzito wa jukumu hili, ulikalia bega la Bwana Abu Twalib na familia yake, kwa sababu, kuhusiana na watu wengine waliojiunga na Waislamu hawakuwa na nguvu iliyohitajika japo kwa kujihami wao wenyewe, na hivyo basi, suala la Uislamu wao kuwa chanzo cha heshima na utukufu wa Waislamu halikuibuka.

## Abu Jahl Amvizia Mtume (S.A.W.W)

Kuendelea kwa Uislamu kulikozidi daima kulikuwa kumewafanya Waquraishi wahangaike. Kila siku walifikiwa na taarifa ihusuyo mwelekeo (wa kwenye Uislamu) wa mtu mmoja au mwingine wa kabila lao. Hivyo basi, kutokana na hali hiyo, hasira yao ilikuwa inawaka moto! Siku moja, yule Firauni wa Makkah, Abu Jahl, alisema kwenye mkutano wa Waquraishi: "Enyi Waquraishi! Mnaweza kuona jinsi Muhammad anavyoifikiria dini yetu kuwa ni haina thamani na anaikashifu dini ya jadi zetu na miungu yao, na anatuita wajinga.
Ninaapa kwa jina la Allah kwamba kesho nitamvizia na nitaliweka jiwe kando yangu; na Muhammad atakaposujudu nitamtwanga na jiwe lile kichwani mwake." Siku iliyofuata, alifika Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenye Masjidul Haraam ili asali, na akasimama baina ya '*Rukni Yamaani*' na *Hajjarul-Aswad* (Jiwe Jeusi). Kikundi cha Waquraishi waliokuwa wakiitambua ile nia ya Abu Jahl walikuwa wakisubiri kuona kama atafaulu kwenye kampeni yake au la. Mtume (s.a.w.w.) akaenda sijida na yule adui yake mzee akajitokeza kutoka kwenye maoteo yake na akamwendea.

Hata hivyo, haikuchukua muda mrefu kabla Hajapigwa na hofu na akarejea kwa wale Waquraishi wenzie huku akitetemeka na kufadhaika na uso wake ukiwa umejaa wasi wasi. Wote wakakimbilia mbele na kuuliza: "Ewe Abu Hakim! Ni kitu gani kilichotokea?" akajibu kwa sauti dhaifu mno iliyoisaliti hofu yake na mchafuko wa akili: "Machoni mwangu yalitokea mandhari nisiyowahi kuyaona kabla yake maishani

mwangu. Ilikuwa ni kwa sababu hii ambapo kwamba niliuacha mpango wangu."

Hivyo basi, bila shaka nguvu isiyoonekana ilitokea kwa amri ya Allah na kujenga kitisho kilichomhami Mtumufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) kutokana na madhara ya maadui kwa mujibu wa ahadi ya Allah isemayo: "**Sisi Tutakuhami kutokana na madhara ya wale wafanyao dhihaka.**"

Matukio mengi ya mateso ya Waquraishi dhidi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yameandikwa kwenye kurasa za historia. Ibn Athar amekusanya sura nzima juu ya somo hili na ameyataja majina ya maadui wakatili wa Mtume (s.a.w.w.) walioishi mjini Makkah na ukatili walioutenda.[10]

Lolote lile tulilolisema hapo juu ni mfano tu. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alijiona kuwa kila siku alikuwa akikabiliwa na mateso mapya. Kwa mfano, siku moja Uqbah bin Abi Mu'it alimona Mtume (s.a.w.w.) akifanya

'Tawaf' na akamtusi. Alimfunga kilemba chake shingoni mwake na akamkokotea nje ya Masjid. Watu fulani wakamwokoa Mtume (s.a.w.w.) kutoka mikononi mwa Uqbah kwa kuwaogopa Bani Hashim.[11]

Mateso na maonevu aliyopatishwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na ami yake Abu Lahab na mkewe Ummi Jamil hayakuwa na kifani. Alitokea kuwa jirani wao wa mlango wa pili. Hawakujizuia kumtupia kila aina ya uchafu, na siku moja walimtupia matumbo ya kondoo kichwani mwake. Hatimaye Bwana Hamza, akiwa na lengo la kulipiza kisasi akambandika Abu Lahab matumbo yale kichwani.

## Mateso Ya Waquraishi Dhidi Ya Waislamu

Katika siku za mwanzoni za kazi ya utume, kuendelea kwa Uislamu kulikuwa na matokeo ya visababisho kadhaa, kimoja miongoni mwao kilikuwa ni uthabiti wa Mtume (s.a.w.w.) na masahaba na wafuasi wake. Mifano ya subira na ustahimilivu wa huyu kiongozi wa Waislamu umeelezwa, ambapo uvumilivu na ustahimilivu wa Waislamu waliokuwa wakiishi mjini Makkah (makao makuu ya ushirikina na ibada ya masanamu) unastahili kuzingatiwa. Maelezo ya kujitoa muhanga na uthabiti wao yatatolewa kwenye sura ihusuyo matukio ya baada ya Hijrah (kuhamia madina).

Kwa wakati huu tutalieleza matukio mabaya yahusianayo na maisha ya baadhi ya wafuasi wa mwanzoni kabisa wa Mtume (s.a.w.w.) waliokuwa wakiishi kwenye mazigira ya Makkah yasiyokuwa na hifadhi.

## Bilal Mu-Ethiopia:

Wazazi wa Bwana Bilal walikuwa miongoni mwa watu walioletwa Bara Arabuni kutoka Ethiopia wakiwa ni mateka. Yeye mwenyewe (ambaye baadaye alikuwa muadhini wa Mtukufu Mtume s.a.w.w.) alikuwa mtumwa wa Umayyah bin Khalaf. Umayyah alikuwa mmoja wa maadui wa kuu wa yule kiongozi mkuu wa Waislamu. Kwa vile nduguze Mtume (s.a.w.w.) walilishika jukumu la ulinzi wake, Umayya kwa lengo la kulipiza kisasi, alikuwa akimtesa hadharani yule mtumwa wake ambaye alisilimu karibuni tu. Akimlaza uchi kwenye mchanga ulio na joto kwenye siku za joto kali zaidi, akimwekea jiwe kubwa na lililo na joto

kali kifuani mwake na kumsemesha kwa maneno haya:

“Sitakuachia mpaka ufe kwenye hali hii au uikane dini ya Muhammad, na uwaabudu ‘Laat’ na ‘Uzza!”

Licha ya mateso yote hayo, Bwana Bilal alimjibu Umayyah kwa maneno mawili tu yatokanayo na itikadi yake thabiti; alimwambia: “Ahad! Ahad! (yaani Allah yu Mmoja tu nami katu sitarejea kwenye dini ya ushirikina na masanamu).

Watu waliushangaa sana uthabiti wa huyu mtumwa mweusi aliyekuwa mateka wa mikononi mwa mtu aliyekuwa na moyo mgumu. Watu hawa walishangazwa mno kiasi kwamba Waraqah bin Nawfal yule mwanachuoni mkristo wa kiarabu, alilizwa mno na hali ya Bilal na akamwambia Umayyah: “Ninaapa kwa jina la Allah! Kama ukimwua kwa njia hii, nitalifanya kaburi lake kuwa sehemu takatifu lipasalo kutembele- wa na mahujaji!” [12]

Wakati mwingine Umayyah alimtendea Bwana Bilal mambo makali zaidi. Aliifunga kamba shingoni mwa Bwana Bilal na kuwapa watoto kamba ile wamkokote mitaani! [13]

Umayyah na mwanawe walitekwa kwenye vita vya Badr, vita vya kwanza vya Uislam. Baadhi ya Waislamu hawakupendelea kuuawa kwa Umayyah, lakini Bwana Bilal akasema: “Huyu ni kiongozi wa ukafiri na hivyo ni laz- ima auawe!” Kwa kushikilia kwake, baba na mwana walilipwa kwa ajili ya maovu na wakauawa.

## Kujitoa Muhanga Kwa Ammar Na Wazazi Wake

Ammar na wazazi wake walikuwa miongoni mwa Waislamu wa awali kabisa. Walisilimu wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipoichagua nyumba ya Arqam bin Abil Arqam kuwa makao ya kulingania Uislam. Wakati wenye kuyaabudu masanamu walipotambua kusilimu kwa Ammar na wazazi wake hawakuacha kuwatesa na kuwaonea. Ibn Athir[14] anasema: “Wenye kuyaabudu masanamu waliwalazimisha watu hawa watatu kuzitoka nyumba zao kwenye mazingira ya joto kali na kuutumia muda wao kwenye upepo mkali na wenye joto kali wa jangwani. Mateso haya yalirudiwa kwa mara nyingi mno kiasi kwamba, Yaasir alifariki dunia kutokana na taabu alizozipata. Siku moja Sumayyah; mjane wa Yaasir aligombana na Abu Jahl kutokana na jambo hili. Mtu huyu mwenye moyo mgumu na katili alimchoma mkuki moyoni mwake na akamwua na yeye pia.
Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikasirishwa mno na maonevu waliyoten- dewa watu hawa. Siku moja aliwaona wakiteswa. Aliwageuzia uso huku akilia na machozi yakimbubujika machoni mwake, na akasema: “Enyi familia ya Yaasir! Kuweni na subira, kwa kuwa nafasi yenu iko Peponi.”

Baada ya kifo cha Yaasir na mkewe, wenye kuabudu masanamu walimwadhibu na kumtesa Ammar kama walivyomwadhibu Bilal. Ili kuyaokoa maisha yake, hakuwa na njia yoyote nyingine iliyomsalia ila kuukana Uislamu, lakini upesi sana akatubia na akakimbilia kwa Mtukufu

Mtume (s.a.w.w.) kwa moyo uliokuwa ukimdunda. Akamsimulia Mtume (s.a.w.w.) tukio lile, na Mtume

(s.a.w.w.) akamwuliza: “Je, kulitokea kule- galega kokote katika imani yako ya ndani?” akajibu; “Moyo wangu umuejaa imani tele.” Hapo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Usihofu hata kidogo akilini mwako na endelea kuificha itikadi yako ili uweze kujiokoa kutokana na madhara yao.” Aya ifuatayo ya Qur’ani tukufu ilifunuliwa kuhusiana na itikadi ya Ammar: 15

{مَنْ كَفَرَ بِاللَّهِ مِنْ بَعْدِ إِيمَانِهِ إِلَّا مَنْ أُكْرِهَ وَقَلْبُهُ مُطْمَئِنٌّ بِالْإِيمَانِ{106

*“(**Atapata adhabu kali mno yule**) **anayemkataa Allah baada ya imani yake, ila yule aliyeshurutishwa hali moyo wake ni imara katika imani yake,……’** (**Surah Nahl, 16:106**).*

Inasemekana kwamba Abu Jahl aliamua kuibana familia ya Yaasir aliyetokana na tabaka la watu wasiokuwa na hifadhi hata kidogo wa mjini Makkah.

Hivyo basi akaamrisha kwamba ukokwe moto na utayarishwe mjeledi wa ngozi. Baada ya hapo Yaasir, Sumayyah na Ammaar walikokotewa kwenye sehemu iliyochaguliwa na wakaadhibiwa kwa kuchomwa na ncha ya upanga na miali ya moto na kutandikwa kwa mjeledi. Maonevu haya yalirudiwa mara nyingi kiasi kwamba Yaasir na Summayah wakafariki dunia, lakini hawakuweza kuiacha sifa ya Mtume (s.a.w.w.) hadi muda wao wa mwisho.

Waquraishi walioishuhudia mandhari hii ya kimsiba na la kuhunisha, ingawa walikuwa na umoja katika kuushinda Uislamu, walimsaidia Ammar ambaye wakati ule alikuwa kakumbwa na majeraha na huzuni mpaka akaachiliwa kutoka makuchani mwa Abu Jahl ili apate nafasi ya kuwazika wazazi wake.

## Abdullah Bin Mas’ud

Waislamu waliosilimu kwa siri walikuwa wakiambiana kwamba bado Waquraishi hawajaisoma Qur’ani tukufu na ingefaa kama mmoja wao angalikwenda kwenye Masjidul-Haraam na kuzisoma baadhi ya baadhi ya aya za Kitabu Kitakatifu kwa sauti kuu. Abdullah bin Mas’ud alionyesha kuwa alikuwa tayari kufanya vile. Alikwenda Masjid wakati Waquraishi walipokuwa wamesimama kando kando mwa Al-Ka’ba na akazisoma aya zifuatazo kwa sauti kuu na tamu:

{الرَّحْمَٰنُ {1

{عَلَّمَ الْقُرْآنَ {2

*“Mwingi wa rehema. Amefundisha Qur’ani ……….”* ( ***Surah al- Rahman, 55:1-2***)
Aya zenye utamu za Sura hii ziliwagonga Waquraishi kwa hofu ya ajabu. Na ili kuzizuia athari za huu mwito wa mbinguni, uliokuwa ukiyafikia masikio yao kupitia kwa mtu yule asiyekuwa na ulinzi,

wakasimama wote na kumpiga hadi damu ikaanza kutiririka kutoka mwilini mwake mwote na akarejea kwa wale wafuasi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika hali ya kuhuzunisha. Hata hivyo, walifurahi kwamba hatimaye ile sauti yenye kuhuisha imeyafikia masikio ya maadui.[16]

Yale tuliyoyazungumza hapo juu yalikuwa ni kwa njia ya mfano, vinginevyo, idadi ya wafuasi wa dhati wa Uislamu waliojitoa mhanga waliovumilia shida kali kupita kiasi kwenye siku za awali za Ujumbe wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na wakaonyesha uthabiti wao katika njia ya kulifikia lengo lao ni kubwa sana. Hata hivyo tutaacha kuyataja majina yao na matukio ya maishani mwao kwa sababu za ufupisho wa mambo.

## Maadui Wakali Mno Wa Mtukufu Mtume (S.A.W.W)

Utambuzi wa baadhi ya maadui wa Mtume (s.a.w.w.) ni jambo muhimu kuhusiana na baadhi ya matukio ya Uislamu ya baada ya kuhajiria Madina, na hapa chini tunatoa majina na maelezo yao kwa ufupi:

**Abu Lahab:** Yeye alikuwa jirani wa Mtume (s.a.w.w.). Hakuiachilia nafasi hata moja katika kumpinga na kumtesa yeye na Waislamu.

**As'wad bin Abd Yaghus:** Alikuwa mchekeshaji. Alipowaona Waislamu wasio na msaada na maskini aliwadhihaki na kusema: "Hawa watu waliokumbwa na umasikini wanajifikiria kuwa wao ni wafalme wa ulimwengu na wanadhani kwamba hivi karibuni watapata kiti cha enzi na taji la Mfalme wa Iran." Hata hivyo kifo hakikumruhusu kuona kwa macho yake jinsi Waislamu walivyojipatia nchi, viti vya enzi na mataji ya Kaisari na Kisra.

**Walid bin Mughayrah:** Alikuwa mzee wa Kikuraishi aliyekuwa na utajiri mwingi. Tutayasimulia mazungumzo yake na Mtume (s.a.w.w.) kwenye sura ifuatayo.

**Umayyah na Ubay wana wa Khalaf:** Siku moja Ubay alimletea Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mifupa ya watu waliokufa na kumwuliza: "Je, huyo Allah wako anaweza kuihuisha mifupa hii?" Pale pale lilikuja jibu kutoka kwenye chanzo cha ufunuo:

{قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ 79}

***"Sema: "Ataihuisha huyohuyo Aliyeiumba hapo awali. Na Yeye ni Mjuzi wa kila** (**namna ya**)**kuumba."**(**Surat Yaasin: 36:79**)*

**Abul Hakam bin Hisham:** Waislamu walikuwa wakimwita Abu Jahl (baba wa ujinga) kutokana na uadui na ukaidi wake dhidi ya Uislamu. Yeye nae aliuawa kwenye vita vya Badr.

**Aas bin Waa'il:** Alikuwa ni baba yake Amr bin Al-Aas. Yeye ndiye aliyempa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) jina la utani la *'Abtar'* (asiye na kizazi).

**Uqbah bin Abi Mu'it:** [17]Alikuwa mmoja wa maadui wa Uislamu waliokuwa wakiogofya sana na katu hakuipoteza nafasi ya kumtendea madhara Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Waislamu.
Vile vile lilikuwapo kundi jingine la maadui wa Uislamu ikiwa ni pamoja na Abu Sufyani na wengineo. Wanahistoria wameandika taarifa zao kwa kirefu na kwa ajili ya kufupisha mambo, tutaacha kuwanukuu hapa.

## Umar Ibn Khattab Asilimu

Kusilimu kwa kila mtu miongoni mwa Waislamu wa awali kulikuwa ni athari ya kisababisho kimoja au kingine na wakati mwingine tukio dogo sana liliwezakuwa sababu ya kusilimu kwa mtu au kikundi. Kishawishi cha kusilimu kwa khalifa wa pili ni chenye kuvutia. Ingawa kwa msimamo wa utaratibu wa yalivyotokea matukio ingalikuwa bora kuliandika tukio hili baada ya kuelezea tukio la Waislamu kuhamia huko Ethiopia, lakini, tunaona kwamba inafaa kulieleza hapa, kama tulivyowaeleza baadhi ya wafuasi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Ibn Hisham[18] anasema: "Kutoka kwenye familia ya Khattab (baba yake Umar) ni binti yake Fatimah na mumewe Sa'id bin Zayd tu waliosilimu. Kwa kuwa katika siku za awali za Uislamu, uhusiano wa Umar na Waislamu ulikuwa wa uadui mkubwa na alifikiriwa kwamba yu mmoja wa maadui wakaidi zaidi wa Mtume (s.a.w.w.), hivyo dada yake na mumewe siku zote waliificha itikadi yao asiifahamu. Licha ya hivyo, Khubaab bin Art alikuwa akija nyumbani kwao kwenye masaa waliyoafikiana na kuwafundisha Qur'ani tukufu.

Hali ya kuchanganyikiwa ya watu wa Makkah ilimfanya Umar kuwa na hisia kali, kwa kuwa aliona kwamba mifarakano na michafuko ilitawala miongoni mwao na zile siku angavu za Waquraishi zimebadilika na kuwa usiku wa giza.

Hivyo Umar aliamua kwenda kuukatilia mbali mzizi wa fitina na mgawanyiko kwa kumwua Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Ili kulifikia lengo hili, alikuwa akitafuta sehemu anakopatikana Mtume (s.a.w.w.).Aliarifiwa ya kwamba alikuwa kwenye nyumba iliyokuwako kandoni mwa bazaar ya Safa, na watu arobaini kama vile Hamza, Abu Bakr, Ali n.k. wamelichukua jukumu la kumlinda na kumhami.

Na'im Ibn Abdullah aliyekuwa mmoja wa marafiki wa karibu zaidi wa Umar anasema: "Nilimwona Umar akiwa amebeba upanga wake. Nilimwuliza kuhusu lengo alilokuwa akiliendea. Alijibu hivi: "Ninakwenda kumtafuta Muhammad aliyejenga mfarakano miongoni mwa Waquraishi. Ameicheka hekima na akili zao, kuitangaza dini yao kuwa haina thamani na kuwatweza miungu wao. Nakwenda kumuua."

Na'im anasema: Nilimwambia "Umedanganyika. Je, wadhania kwamba dhuria wa Abd Munaf wataubakisha uhai wako? Kama wewe ni mtu upendaye amani, basi huna budi kuitengeneza kwanza nyumba yako. Dada yako Fatimah na mumewe wamesilimu na wanaifuata dini ya Muhammad."

Maneno ya Na'im yalisababisha dhoruba ya ghadhabu akilini mwa Umar. Matokeo yake ni kwamba

aliuachilia mbali ule mpango wake wa awali na akaenda nyumbani kwa shemeji yake. Alipofika karibu na nyumba ile, alisikia uvumi wa mtu fulani aliyekuwa akiisoma Qur’ani tukufu kwa sauti ivutiayo. Namna Umar alivyofika kwa nyumbani kwa dada yake ilikuwa kiasi kwamba dada yake yule na mumewe pia walitambua kwamba alikuwa karibuni kuingia.
Hivyo, walimficha yule mwalimu wao wa Qur’ani tukufu nyuma ya nyumba yao ili aweze kubakia kujificha machoni pa Umar. Pia Fatimah alilificha lile karatasi lililoandikwa aya za Qur’ani tukufu.

Bila ya salamu au maamkuzi kwa wenye nyumba wale, Umar akasema: “Uvumi ule niliousikia ulikuwa ni wa nini?’ Wakamjibu; “Hatukusikia kitu chochote.” Umar akasema: “Nimesikia kwamba mumesilimu na kuifuata dini ya Muhammad!” Aliitamka sentensi hii kwa ghadhabu kali na kuanza kumshambulia shemeji yake. Hapo dada yake akasimama ili kumhami mumewe.

Umar akamshambulia yeye pia na akakijeruhi kichwa chake vibaya mno kwa ncha ya upanga wake. Fatimah akiwa hajiwezi pale, akiwa anachuruzika damu kichwani mwake, alisema kwa hamasa kubwa ya imani: “Ndio. Tumesilimu na tunamwamini Allah na Mtukufu Mtume wake. Fanya vyovyote utakavyo.”

Hali ya kuhuzunisha ya dada huyo, aliyekuwa akisimama kandoni mwa kaka yake huku uso na macho yake yakiwa yametapakaa damu na akizungumza naye, vilimfanya Umar atetemeke, na hatimaye alijutia kitendo chake kile. Hivyo basi, akasisitiza kwamba wamwonyeshe lile karatasi ili kwamba ayatafakari maneno ya Muhammad. Dada yake akichelea asije akalipasua, alimtaka aapie kwamba hatafanya hivyo, na yeye aliahidi pia na kuthibitisha kwa kiapo kuwa atalirudisha karatasi lile baada ya kulisoma. Kisha Umar akalishika karatasi lile mkononi mwake. Aya chache za Qur’ani tukufu zilikuwa zimeandikwa mle. Hapa chini tunaiandika tafsiri yake:

1} طه{

2} مَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لِتَشْقَىٰ{

3} إِلَّا تَذْكِرَةً لِمَنْ يَخْشَىٰ{

4} تَنْزِيلًا مِمَّنْ خَلَقَ الْأَرْضَ وَالسَّمَاوَاتِ الْعُلَى{

5} الرَّحْمَٰنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَىٰ{

6} لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَمَا تَحْتَ الثَّرَىٰ{

7} وَإِنْ تَجْهَرْ بِالْقَوْلِ فَإِنَّهُ يَعْلَمُ السِّرَّ وَأَخْفَى{

***“Twaa Haa. Hatukukuteremshia Qur’ani ili upate mashaka. Bali iwe mawaidha kwa wenye kunyenyekea. Ni ufunuo utokao kwa Yule Aliyeiumba ardhi na mbingu zilizoinuka juu. Mwingi wa rehema ametawala juu ya Arshi. Ni Vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini na vilivyomo baina yao na vilivyomo chini ya udongo. Na kama ukinena kwa kauli kubwa (au ukinong’ona), basi hakika Yeye anajua yaliyo siri na yaliyofichikana zaidi.” (Surah Twaa Haa, 20:1-7).***

Aya hizi zenye ufasaha wa lugha na maneno yaliyowazi na thabiti zilimvutia mno Umar. Yule mtu aliyekuwa adui katili wa Qur’ani tukufu na Uislamu dakika chache zilizopita, aliamua kuzibadili fikira zake. Aliiendea ile nyumba ambayo kabla ya hapo alisikia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) angaliweza kupatikana humo na akabisha mlangoni. Mmoja wa wafuasi wake Mtume (s.a.w.w.) alichungulia kupitia kwenye tundu la mlango na kumwona Umar akiwa amesimama na upanga mkononi mwake akisubiri mlango ufunguliwe. Mara moja akarudi na kumtaarifu Mtume (s.a.w.w.) hali ile, Bwana Hamza mwana wa Abdul-Muttalib akasema:

“Mwache aingie. Kama kaja kwa nia njema tutamkaribisha, lakini kama malengo yake si mema, tutamwua.” Usimamaji wa Umar mbele ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) uliwahakikishia heri na uso wake mng’avu na kuionyesha kwake huzuni na aibu kuliyashuhudilia malengo yake hasa.
Hatimaye akasilimu mikononi mwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mbele ya wafuasi wake na hivyo akajiunga na safu za Waislamu.19

1. Badala ya kugonga kengele ya hali ya hatari, Waarabu waliyatumia maneno haya na kwa kawaida wakaanzisha taarifa zenye kutahadharisha pamoja nayo.
2. Ibn Hisham ameyataja majina na maelezo ya watu hawa mwenye ‘Siirah’ yake.
3. Siirah Ibn Hisham, Juzuu 10, uk. 265.
4. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 265-266.
5. Tarikh-i Tabari, Juzuu 2, uk. 66 na 67; Siirah-ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 295 na 296.
6. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 313 na Tarikh-i Tabari, Juzuu 2, uk. 72.
7. Tarikh-i Kamil, Juzuu 2, uk. 59.
8. Al-Bidaayah wan Nihaayah, Juzuu 3, uk. 26.
9. Siirah, Juzuu 1, uk. 311, Tabari amelinukuu tukio zima kwenye Ta’rikh yake, Juzuu 2, uk. 72. isipokuwa kwamba kichwa cha khalifa kilijeruhiwa.
10. Tarikh-i Kamil, Juzuu 2, uk. 47.
11. Bihaarul Anwaar, Juzuu 18, uk. 204.
12. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 328.
13. Tabaqaat-i Ibn Sa’ad, Juzuu 1, uk. 233.
14. Tarikh-i Kamil, Juzuu 2, uk. 45.
15. Siirah-i Hisham, Juzuu 1, uk. 320.
16. Siirahi Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 324.
17. Tarikhi Kamil, Juzuu 2, uk. 47-51; Usudul Ghabah; Al-Asabah; Al-Ist’iaab n.k
18. Siirahi Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 365.
19. Ibn Hisham ametoa masimulizi mengine ya kusilimu kwa Umar (Juzuu 1, uk. 368).

# Sura Ya Kumi Na Sita: Uamuzi Wa Waquraishi Juu Ya Qur'ani Tukufu

Mjadala ambao hasa ni juu ya kiini cha mujiza, na hali ya kimuujiza ya Qur'ani tukufu uko nje ya nafasi ya kitabu hiki. Hata hivyo mijadala ya kihistoria inatuambia kwamba hiki Kitabu cha mbinguni kilikuwa silaha kuu na kali zaidi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Ilikuwa hivyo kiasi kwamba washairi mahiri na duru za kuarudhi na kutunga na kuhutubia zilikanganywa na kushangazwa na ufasaha, utamu wa sauti na mvuto wa maneno yake, sentensi na mistari ya tenzi zake, na wote walikiri kwamba Qur'ani tukufu ya Muhammad iko kwenye kiwango cha juu zaidi cha ufasaha wa lugha na uwazi na ustadi wake juu ya maneno na jinsi yake ya kuelezea mambo haikuwa na kifani.

Kuchoma kwake moyoni, kupenya kwake, upeo wa furaha na mvuto wa Qur'ani tukufu vilikuwa kwenye hali ya kwamba hata wale maadui wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walio wakali zaidi walitetemeka nafsini mwao walipozisikia baadhi ya aya zake zikisomwa, na wakati mwingine walikuwa wakifurahishwa mno kiasi kwamba kwa kiasi cha muda hivi hawakuweza kusogea kutoka pale walipokuwa kutokana na kubutwaa. Hapa chini tunatoa mifano juu ya jambo hili.

## Uamuzi Wa Walid

Walid alikuwa mmoja wa mahakimu wa Uarabuni. Matatizo mengi ya Waarabu yalitatuliwa kupitia kwake. Alikuwa na utajiri mwingi mno. Kikundi cha Waquraishi kilimwendea ili wapate ufambuzi wa tatizo la kupenya kwa Uislamu kwenye nyumba zote na wakamweleza jambo hili na wakamwomba awape maoni yake juu ya Qur'ani ya Muhammad. Walimwuliza: "Je, Qur'ani ya Muhammad ni uchawi au kupiga bao au ni hotuba au ni ufasaha wa kusema alioutayarisha?" Yule mtaalamu wa Uarabuni aliomba apewe muda ili kwamba aweze kuyaeleza maoni yake baada ya kuisikiliza Qur'ani tukufu. Kisha aliamka kutoka kwenye maskani yake akaenda kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Alikaa pamoja nae kwenye *Hajar-i Isma'il* na akasema: "Hebu nisomee chochote kile kutokana na ushairi wako."

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimjibu akisema: "Ninachokisema mimi si ushairi. Sivyo, bali ni neno la Allah alilo- literemsha kwa ajili ya mwongozo wenu." Kisha Walid akasisitiza kwam- ba Mtume (s.a.w.w.) amsomee Qur'ani. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akam- somea aya kumi na tatu za kwanza za **Surah al-Fussilat** na alipoifikia Aya hii: "Na kama wakikengeuka, sema: 'Nakuhadharisheni na adhabu iliyowakamata Waadi na Wathamudi."(***Surah al-Fussilat***, **41:13**).

Walid alitetemeka vikali mwilini mwake. Nywele zake zote zikasimama mwilini mwake na akaamka akiwa mwenye hali ya kushangaa na akarudi nyumbani kwake. Hakutoka nje ya nyumba yake kwa siku nyingi, kiasi kwamba Waquraishi wakaanza kumdhihaki na kusema: "Walid ameiacha dini ya jadi zake na kuichukua dini ya Muhammad.[1]

Tabari anasema: "Ilipofunuliwa *Surah al-Ghaafir* kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), aliisoma kwa sauti ya kuvutia mno ili kuzifikisha aya za Allah kwa watu. Kwa bahati wakati ule Walid alikuwa ameketi karibu naye na alizisikia aya hizi lakini hakuzingatia.

{تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ} 2

{غَافِرِ الذَّنْبِ وَقَابِلِ التَّوْبِ شَدِيدِ الْعِقَابِ ذِي الطَّوْلِ ۖ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۖ إِلَيْهِ الْمَصِيرُ} 3

{مَا يُجَادِلُ فِي آيَاتِ اللَّهِ إِلَّا الَّذِينَ كَفَرُوا فَلَا يَغْرُرْكَ تَقَلُّبُهُمْ فِي الْبِلَادِ} 4

***"Hiki Kitabu kimefunuliwa na Allah, Mwenye nguvu. Mjuzi Mwenye kuzighufiria dhambi na mwenye kuzikubalia toba, mkali wa kuad- hibu, Mola wa ukarimu. Hakuna apasaye kuabudiwa ila yeye (tu); vyote vitarejeshwa kwake. Hakuna abishanaye juu ya ufunuo wa Allah ila wale waliokufuru. Yasikughuri matendo yao nchini.........."***
**(*Surah al-Ghaafir, 40:2-4*).**

Aya hizi zilimvutia mno yule mtaalamu wa Uarabuni. Bani Makhzumi walipomkusanyikia alitoa uamuzi wake juu ya Qur'ani tukufu kwa maneno haya: "Leo nimesikia kutoka kwa Muhammad maneno yasiyotokana na aina ya maneno ya mwanaadamu na jinni. Ni yenye sauti tamu na yana uzuri maalumu. Matawi yake yamejaa matunda na mizizi yake imejaa mibaraka tele. Ni maneno yaliyojitokeza kwa dhahiri na hakuna maneno yoyote mengine yaliyojitokeza zaidi ya haya."

Alizitamka sentensi hizi na kisha akaenda zake na Waquraishi walifikiri kwamba ameanza kuiamini dini ya Muhammad.[2]

Kutegemeana na kauli ya mwanachuoni mkuu[3] huu ulikuwa ndio utuku- zo na usifiwaji wa awali kabisa wa Qur'ani uliotolewa na mwanadamu, na uchunguzi makini wa maneno haya; huifanya hali ya kimuujiza ya Qur'ani tukufu mkabala na ujinga wa kiarabu kuwa dhahiri kabisa. Na inadhihirika kwamba sababu ya Qur'ani kuwa muujiza machoni pao ilikuwa ni ule mzamo wake usio na kifani, mvuto, uzuri na utamu wa sauti, kwa sababu hawakupata utamu na uzuri kwenye kitu chochote kingine ila Qur'ani tukufu.

## Mfano Mwingine

Utbah bin Rabiyyah alikuwa mmoja wa wazee wa Kiquraishi. Wakati ule Bwana Hamza aliposilimu baraza lote la Quraishi liliingiwa na huzuni na masikitiko na machifu wao walihofia kwamba dini ya kiislamu itazidi kuenea zaidi. Katika hatua hiyo Utbah akasema: "Nitamwendea Muhammad na kuweka ahadi kadhaa kwake. Inawezekana akaikubali mojawapo ya hizo na kuiacha dini hii mpya." Wale

machifu walikubaliana na maoni yake. Hivyo akaamka na akaishika njia kumwendea Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambaye wakati ule alikuwa amekaa kule Masjid. Alimpa ahadi za utajiri, utawala, na matibabu kwa maneno ya upole. Alipokoma kuzungumza, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akamwambia: "Je, hayo ndiyo yote yale uliyotaka kusema?" akajibu "Ndio!" hapo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Hebu zisikilize aya hizi, kwani hili ndilo jibu la hayo yote uliyoyasema":

1} حم}

2} تَنْزِيلٌ مِنَ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ}

3} كِتَابٌ فُصِّلَتْ آيَاتُهُ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ}

4} بَشِيرًا وَنَذِيرًا فَأَعْرَضَ أَكْثَرُهُمْ فَهُمْ لَا يَسْمَعُونَ}

***"Haa Miim. (Huu ni) Uteremsho utokao kwa Mwingi wa rehema, Rahimu. Ni Kitabu ambacho aya zake zimefafanuliwa wazi wazi, ni Qur'ani yenye uwazi kwa watu wanaojua. Itoayo habari njema na ionyayo, lakini wengi wao wamekengeuka hivyo hawasikii." (Surah Haa Miin, 41:1-4).***

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alizisoma aya fulani fulani za Sura hii. Alipoifikia aya ya thelathini na saba ya Sura hii akafanya *'Sajdah.'* Baada ya hapo alimgeukia 'Utbah na kumwambia: "Ewe Abu Walid! Je, umeusikia Ujumbe wa Allah?" Kwa kiasi fulani 'Utbah alikuwa amebumbuazwa na lile Neno la Allah. Alikuwa ameweka mikono yake nyuma ya kichwa chake, kikawa kimeegea hapo, aliendelea kuukodolea macho uso wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kipindi kirefu, kana kwamba alikuwa amenyang'anywa uwezo wake wa kunena.

Kisha aliamka na kwenda kwenye sehemu waliokusanyika Waquraishi. Kutokana na hali yake na uso wake machifu wa Waquraishi walitambua kwamba alikuwa amevutiwa na maneno ya Muhammad na amerudi katika hali ya fedheha iliyoandamana na mhangaiko wa akilini. Wote walikuwa wakitazama kwa shauku kamili wauone uso wa 'Utbah.

Wote wakamwuuliza: "Kumetokea nini?" akajibu: "Ninaapa kwa jina la Allah nimesikia kutoka kwa Muhammad nisiyopata kuyasikia kutoka kwa mtu yeyote. Ninaapa kwa jina la Allah! Maneno hayo si ushairi wala uchawi wala upiga ramli. Ninafikiria kwamba ingalifaa tumwache aendelee kuihubiri dini yake miongoni mwa makabila mbali mbali. Kama akifaulu na kujipatia nchi na milki, tutalichukulia jambo hilo kuwa ni fahari kwa ajili yenu na ninyi nanyi mtanufaika kutokana na nayo. Na kama akishindwa, watu wengine watamwua na ninyi vile vile mtapata sahala."

Waquraishi wakamdhihaki 'Utbah kwa kauli na maoni yake yale na wakasema kwamba amepumbazwa na maneno ya Muhammad.4

Hii ni mifano miwili ya maoni ya wazungumzaji wakuu wenye ufasaha wa lugha wa Zama za Ujinga na mifano mingine vile vile inapatikana.

## Makri Ya Ajabu Ya Waqurishi

Siku moja baada ya jua kuzama, machifu wa Waquraishi kama vile 'Utbah, Shaybah, Abu Sufyan, Nazar bin Harith, Abul Bakhtari, Walid bin Mughayrah, Abu Jahal, Aas bin Waai'l n.k. walikusanyika kandoni mwa Ka'bah na wakaamua kumwita Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kujadiliana nae moja kwa moja kuhusu jambo lile. Hivyo basi, wakamtuma mtu mmoja kwenda kumtaka Mtume ashiriki kwenye mkutano ule. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipoarifiwa jambo lile alitoka upesi upesi na kujiunga na mkutano wao, akitegemea kuwaongoza kwenye njia iliyonyooka.

Yalianza mazungumzo kutoka pande zote na Waquraishi wakarudia kuzieleza huzuni zao. Wakalalamika kwamba mfarakano na ugomvi vimejitokeza miongoni mwa Quraishi, na wakonyesha kuwa kwao tayari kwa kafara lolote lile. Mwishoni walimwomba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ombi lililoelezwa kwenye aya zifuatazo:-

{وَقَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْأَرْضِ يَنْبُوعًا {90

{أَوْ تَكُونَ لَكَ جَنَّةٌ مِنْ نَخِيلٍ وَعِنَبٍ فَتُفَجِّرَ الْأَنْهَارَ خِلَالَهَا تَفْجِيرًا {91

{أَوْ تُسْقِطَ السَّمَاءَ كَمَا زَعَمْتَ عَلَيْنَا كِسَفًا أَوْ تَأْتِيَ بِاللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ قَبِيلًا {92

{أَوْ يَكُونَ لَكَ بَيْتٌ مِنْ زُخْرُفٍ أَوْ تَرْقَىٰ فِي السَّمَاءِ وَلَنْ نُؤْمِنَ لِرُقِيِّكَ حَتَّىٰ تُنَزِّلَ عَلَيْنَا كِتَابًا{93

***"Na wanasema: 'Katu hatutakuamini mpaka utububujishie chemche- mi kutoka ardhini mbele ya macho yetu, au ububujishe mito kwenye mabustani ya mitende na mizabibu; au utuangushie mbingu ikatike vipande vipande kama ulivyodai, au utuletee Allah na Malaika katikati yetu; au ujenge nyumba ya dhahabu, au upae mbinguni; wala hatutakuamini kupaa kwako mpaka ututeremshie Kitabu tukisome (na chenye kuthibitisha utume wako)...." (Surah Bani Isra'il, 17: 90-93).***

Ni dhahiri kwamba yale yote waliyoyasema yalikuwa udanganyifu mtupu, kwa sababu mitende na mizabibu haina chochote kihusianacho na Utume wa mtu na kuzifanya mbingu zipasuke vipande

vipande na kuanguka mchangani ni jambo haliendani na ujumbe wa Utume ambao lengo lake ni kuwaongoza watu. Miongoni mwa matakwa yao kuna jambo moja tu lenye hali ya kimiujiza, nalo ni kupaa mbinguni kwa Mtume! Na japo Mtume (s.a.w.w.) angaliufanya mujiza huu wasingalimwamini, kwa sababu, walishasema wazi kwamba ni lazima ateremshe Kitabu kitakachouthibitisha utume wake!

Kama Waquraishi wangalipenda kweli kweli kuuthibitisha ukweli wa madai ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), basi kule kupaa kwake kwenda mbinguni kungalitosha kuwa uthibitisho wake.

Hata hivyo, walisema kwamba hawatatosheka nako. Matakwa yao yote yalikuwa na malengo maalumu. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwajibu akisema: "Hakika mimi si chochote ila ni Mjumbe na siwezi kufanya mujiza wowote bila ya ruhusa ya Allah."5

## Kichocheo Cha Ukaidi Wa Machifu Wa Kiquraishi

Sehemu hii ya historia ya kiislamu ni moja ya mambo yahitajiayo majadiliano, kwa sababu mtu hufikiria ni kwa nini Waquraishi waligombana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kiasi hiki, ingawa wote walimtambua kuwa yu mkweli na mwaminifu na kwamba hadi kufikia wakati ule hawajaona kosa lolote kwake japo lililo dogo zaidi, na kila mara wamekuwa wakisikia maneno ya kusisimua na fasaha kutoka kwake, na wakimwona akitenda matendo yasiyo ya kawaida na yaliyokuwa nje ya epeo la kanuni za maumbile. Mambo machache yangaliweza kufikiriwa kuwa ndio chanzo au vyanzo vya kichocheo cha ukaidi huu.

## Waquraishi Walikuwa Wanamwonea Kijicho Mtukufu Mtume (S.A.W.W.).

Baadhi yao walikataa kumfuata Mtume (s.a.w.w.) kwa sababu walimwonea kijicho na walitamani kwamba wao wenyewe ndio wangaliishika kazi hii tukufu. Qur'ani tukufu inasema:

{وَقَالُوا لَوْلَا نُزِّلَ هَٰذَا الْقُرْآنُ عَلَىٰ رَجُلٍ مِنَ الْقَرْيَتَيْنِ عَظِيمٍ {31

***"Na wanasema: 'Kwa nini hii Qur'ani hakuiteremshiwa mtu mwenye uwezo mkubwa kutoka katika miji miwili hii?'*** (***Surah al-Zukharuf, 43:31***).

Wafasiri wa Qur'ani tukufu wanapoieleza sababu ya kufunuliwa kwa aya hii (yaani hoja ya Makafiri kuhusu ni kwa nini Qur'ani haikufunuliwa Makkah au Taifu) wanandika hivi.

Siku moja Ibn Mughayrah alikutana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akamwambia kwamba yeye (Walid) alifaa sana kuishika kazi ya Utume kwa kuwa yeye anao kipaumbele kuliko yeye (Mtume s.a.w.w) katika umri, utajiri na watoto.6

Umayah bin Abi Salt alikuwa mtu aliyekuwa akimzungumzia juu ya mtume kabla ya kuja kwa Uislamu na

yeye mwenyewe alikuwa na shauku ya kuishika kazi hii kuu. Hata hivyo, hakumfuata Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hadi mwisho wa maisha yake na alikuwa akiwashawishi watu kumwasi Mtume (s.a.w.w.)

Akhnas, aliyekuwa mmoja wa maadui wa Mtume (s.a.w.w.), alimwambia Abu Jahl: “Nini maoni yako kumhusu Muhammad?” Alimjibu akisema: “Sisi na Abdi Munaaf tuligombea utukufu na ukuu na tulikuwa karibu tu sawa nao na tulizitumia njia zote zilizowezekana ili kuwa sawa nao. Sasa ingawa tumekuwa sawa nao, wanasema kwamba ufunuo umemteremkia mtu wa familia yao kutoka mbinguni. Naapa kwa jina la Allah! Katu hatutamwamini.”[7]

Hii ni mifano inayoonyesha dhahiri kijicho cha machifu wa Kiquraishi. Vile vile iko mifano mingine iwezayo kuonekana kwenye kurasa za historia.

## Kuihofia Siku Ya Hukumu

Hiki kilikuwa kisababisho kilichokuwa na athari kuu zaidi cha ukaidi wa Waquraishi, kwa sababu walikuwa watu wakutaanisi, wenye ashki. Mwito wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ulikuwa unapingana na tabia za kale za watu hawa waliokuwa wakiufaidi uhuru kamili kwa karne nyingi zilizopita; na kuziacha tabia mbaya kunafuatiwa na taabu na kazi ngumu zaidi ya hapo, Kuzisikia aya zenye kuyahusu mateso, zenye kuwahofisha watu wanaotaanisi, wadhalimu na wajinga na adhabu kali, kulijenga hofu kuu nyoyoni mwao na kuliwafanya wawe na wasiwasi na wasiokuwa na raha.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipozisoma aya tulizozitaja hapo chini kwenye mikusanyiko ya kawaida ya Waquraishi, kwa sauti ipendezayo, kulitokea ghasia iliyozivuruga furaha zao.

Waarabu waliokuwa na kawaida ya kujiandaa kwa ajili ya kujikinga na aina zote za matukio, walikuwa wakitabiri kwa mishale wakipima ndege kwa mawe ili kupata usalama, na kufikiria kuja na kwenda kwa ndege kuwa ni dalili ya matukio, hawakuwa tayari kutulia mpaka wapate uhakika juu ya adhabu ambazo Mtume Muhammad (s.a.w.w.) aliwaonya juu yao. Hivyo basi, waligombana nae ili kwamba wasizisikie tena bishara na vitisho vyake. Hapa tunanukuu baadhi ya aya zilizozihangaisha mno akili za wale Waarabu wenye kutaanisi na wajinga:

{يَوْمَ يَفِرُّ الْمَرْءُ مِنْ أَخِيهِ {34

{وَأُمِّهِ وَأَبِيهِ {35

{وَصَاحِبَتِهِ وَبَنِيهِ {36

{لِكُلِّ امْرِئٍ مِنْهُمْ يَوْمَئِذٍ شَأْنٌ يُغْنِيهِ {37

***“Itakapokuja siku ya Hukumu mtu atamkimbia nduguye, na mama yake na baba yake, na mkewe na wanawe, Siku hiyo, kila mtu atakuwa na jambo lake mwenyewe”***
**(*Surah Abasa, 80:34-37*).**

Waquraishi walipokuwa wameketi kandoni mwa Al-Ka’ba wakinywa mvinyo mara kwa ghafla waliyasikia maneno haya:

{بِآيَاتِنَا سَوْفَ نُصْلِيهِمْ نَارًا كُلَّمَا نَضِجَتْ جُلُودُهُمْ بَدَّلْنَاهُمْ جُلُودًا غَيْرَهَا لِيَذُوقُوا الْعَذَابَ ۗ}56

***“.... ... .., Hivi karibuni tutawatupia Motoni, kila mara ngozi zao zitakapoteketea, tutawapa ngozi*** **(*nyingine*)** ***badala ya zile, ili waionje adhabu Yetu,....”***
**(*Surah al-Nisa, 4:56*).**

Maneno haya yaliwatia wasi wasi na mshtuko mno kiasi kwamba bila ya kujitambua waliviacha vikombe vyao (vya mvinyo) na wakaanza kutetemeka kwa hofu.

Pia zilikuwapo sababu nyinginezo zilizowafanya waache kuutambua ukweli wa Uislamu kwa mfano, siku moja Harith bin Nawfal mwana wa Abd-i Munaaf alikwenda kuonana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akamwambia: “Tunajua kwamba kile unachotuogofya nacho ni kweli na sahihi. Hata hivyo, kama tukiidhihirisha imani yetu kwako, Waarabu washirikina watatutoa kwenye nchi yetu.”

Aya zifuatazo zilifunuliwa ili kuwajibu watu hao:

{وَقَالُوا إِنْ نَتَّبِعِ الْهُدَىٰ مَعَكَ نُتَخَطَّفْ مِنْ أَرْضِنَا ۚ أَوَلَمْ نُمَكِّنْ لَهُمْ حَرَمًا آمِنًا}57

***“Na wanasema: ‘Kama tukiufuata mwongozo pamoja nawe, tutatole- wa nchini mwetu; je, hatukuwakalisha mahali patakatifu pa amani, . ..”*** **(*Surah al-Qasas, 28:57*).**

## Baadhi Ya Mikanusho Ya Washirikina

Wakati mwingine washirikina walisema: ‘Sham ndio nchi inayolea Mitume mapajani mwake na mpaka sasa bado haijawahi kuonekana kwamba mtu awe ameteuliwa kuishika kazi ya Utume kwenye jangwa hili (la Makkahh).” Kwa kuwafuatisha Wayahudi baadhi ya washirikina walisema: “Kwa nini hii Qur’ani iteremshwe kidogo kidogo? Kwa nini haikuteremshwa yote kamili kama Injili na Taurat?” Qur’ani tukufu inanukuu ukanushaji wao huo kwa maneno haya: **“Na waliokufuru wanasema: ‘Mbona hii Qur’ani haikuteremshwa kwake yote kwa mara wahyi mmoja tu?”**

Kisha inatoa jibu lifuatalo:

{كَذَٰلِكَ لِنُثَبِّتَ بِهِ فُؤَادَكَ ۖ}32

*“Tumeiteremsha hivyo ili tukuimarishie imani yako . . . .”*(*Surah al- Furqan, 25:32*).

Bila shaka mambo yasiyopendeza na matukio makali yana athari kubwa kwenye moyo wa mwanaadamu na chanzo pekee cha kuridhika kwa upande wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kilikuwa ni maneno mapya aliyoyasikia kutoka kwa Mola wake, ambaye amemwamrisha uvumilivu na ujasiri, na kwa njia hii akajenga moyo mpya muundo wake wote.
Ni kwa lengo hili kwamba Qur'ani tukufu ilifunuliwa kidogo kidogo.

Zaidi ya hapo, kwenye siku za awali za Uislamu, kwa desturi baadhi ya kanuni zilitambulika rasmi, lakini haikufaa kuziacha ziendelee. Hivyo basi, halikuwezekana kwamba Qur'ani tukufu ingaliweza kufunuliwa kwa ufun- uo mmoja tu.

1. Aa'laamul Waraa, uk. 27-28; na Bibaarul Anwaar, Juzuu 17, uk. 211-222.
2. Majma'ul Bayaan, Juzuu 10, uk. 387.
3. Kitabul Mu'jizatil Khaalidah, cha Allamah Shahristaani, uk. 66.
4. Siirah-I Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 293-294
5. Baadhi ya wamishenari wa Kikristo wamehoji juu ya msingi wa aya hii na nyinginezo kwamba, Mtukufu Mtume wa Uislamu hakuwa na muujiza wowote isipokuwa Qur'ani. Hata hivyo, uongo wa hoja hii, umedhihirishwa mwenye kitabu cha Kifursi (Kiirani) kiitwacho 'Risaalat-i Jahaani-i Pymbaran.'
6. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 361.
7. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 316.

# Sura Ya Kumi Na Saba: Kuhama Kwa Mwanzo

Kuhama kwa kikundi cha Waislamu kwenda Ethiopia ni uthibitisho wa dhahiri wa imani na uaminifu wao wa kina zaidi. Wakiwa na lengo la kuyaambaa madhara na maovu ya Waquraishi na kupata mazingira yenye amani itakayoruhusu kuzitekeleza ibada za dini yao na kumwabudu Allah aliye Mmoja tu, waliamua kuutoka mji wa Makkah na kuuacha utajiri wao, biashara zao, watoto wao na ndugu zao.

Hata hivyo, hawakujua wafanye nini na waende wapi, kwa kuwa waliona kwamba ibada ya masanamu ilikuwapo kila mahali katika Penisula ya Uarabuni yote na hapakuwapo mahali popote ambapo jina la Allah lingaliweza kutamkwa kwa sauti kuu au sheria za kiislamu kutumiwa. Hivyo, wakaamua kuyapeleka maoni yao yale kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambaye msingi wa dini yake umesi- mama juu ya: “..... **kwa hakika ardhi yangu ina wasaa, niabuduni Mimi tu.**” (kwa kuchagua maskani yatakayokuruhusuni kumwabudu Allah Pekee)” (**Surah al-Ankabut,** 29:56).

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitambua vizuri hali mbaya ya kuhuzunisha ya Waislamu. Ingawa yeye mwenyewe alipata msaada wa Bani Hashimu nao walimhami kutokana na kila aina ya madhara, wafuasi wake sana sana wao walitokana ni vijana wajakazi na watumwa na baadhi ya waungwana wasiokuwa na msaada wowote wa ulinzi. Wakuu wa Quraishi waliwatesa hawa watu wasiokuwa na msaada bila ya

kukoma, na ili kuzuia vita za kik- abila, machifu wenye nguvu wa makabila mbali mbali waliwatesa watu wa makabila yao waliosilimu. Maelezo ya mateso na maonevu ambayo Waquraishi wamewatendea watu, tayari yameshaelezwa kwenye kurasa zilizotangulia.

Ni kwa sababu hii kwamba wale wafuasi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walipomwomba ushauri kuhusiana na kuhama, aliwajibu akisema: "Kama mkisafiri kwenda Ethiopia, mtapata faida zaidi, kwa sababu ya kutokana na kuwapo mtawala mwenye nguvu na mwadilifu kule, hakuna yeyote ateswaye kule na ardhi ya nchi ile ni nzuri na safi na mnaweza kuishi pale hadi Allah Mwenyezi atakapokupeni auni."[1]

Bila shaka mazingira yaliyo safi, ambapo mtu mwenye kufaa na mwadili- fu yu katika usukani wa mambo, ni mfano wa Pepo, na lengo pekee la wafuasi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika kuiendea nchi ile ni kwamba waweze kuzitekeleza ibada zao kwa usalama kamilifu na utulivu wa akili.

## Kikundi Cha Kwanza Kwenda Ethiopia

Maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yenye kupenya yalikuwa na athari njema mno kiasi kwamba mara tu baada ya ushauri ule, wale waliokuwa tayari wamekwisha kujiandaa kabisa, waliifungasha mizigo yao na wakaenda Jiddah wakati wa usiku, imam wakiwa kwenye wanyama au wakienda kwa miguu bila ya maadui wao (waabudu masanamu) kutambua kule kuondoka kwao. Idadi kamili ya wale waliohama wakati huu ilikuwa kumi na walikuwamo pia wanawake wa kiislamu wanne.

Hapa inafaa kujua ni kwa nini Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuzitaja sehe- mu nyingine. Hata hivyo, mtu akizichunguza zile hali zilizokuwapo Uarabuni na kwenye sehemu nyinginezo wakati ule, basi siri ya kuichagua Ethiopia itadhihirika kabisa. Sababu yake ilikuwa kwamba kuhamia kwenye sehemu zilizokuwa zikikaliwa na Waarabu, ambao kwa kawaida walikuwa wakiabudu masanamu ilikuwa ni hatari.
Wenye kuyaabudu masanamu hawakupenda kuwapokea Waislamu, imma kwa sababu walitaka kuwaridhisha Waquraishi au kwa sababu waliipenda mno dini ya jadi zao.

Sehemu za Uarabuni zilizokuwa zikikaliwa na Wakristo na Wayahudi hazikufaa hata kidogo kwa kuhamia, kwa sababu walikuwa wakipigana na kugombona wenyewe kwa wenyewe kwa ajili ya kupenyeza kwao kiroho, na haikuwapo nafasi kwa mshindani wa tatu. Zaidi ya hapo, vikundi hivi viwili viliwachukulia watu wenye asili ya kiarabu kuwa ni duni na waliotezwa.

Yemen ilikuwa chini ya maongozi ya Mfalme wa Iran na watawala wa Iran hawakuwa tayari hata kidogo kuwaweka Waislamu nchini mle, kiasi kwamba Khusro Pervez alipoipokea barua itokayo kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), mara moja alimwandikia barua Gavana wa Yemen kumkamata yule Nabii mpya na kumpeleka Iran. Hira, nayo ilikuwa chini ya utawala wa Iran kama vile ilivyokuwa Yemen; Sham ilikuwa mbali kutoka Makkah. Zaidi ya hapo, Yemen na Sham zilikuwa masoko ya Waquraishi na zilikuwa na uhusiano wa karibu zaidi na watu wa sehemu hizi.

Kama Waislamu wangalikimbilia huko, watu wale wangaliwafukuza kutokana na ombi la Waquraishi, waliokukwa wametoa ombi la aina hiyo hiyo kwa Mfalme wa Ethiopia ambaye alikataa kulitimiza.

Katika siku hizo, safari ya baharini, hasusan na wanawake na watoto ilikuwa ni kazi ngumu isiyo kifani. Kuichukua safari kama hii na kuzitelekeza njia za kupatia mahitaji ya maisha ilikuwa ni dalili ya utii kwa Allah na imani halisi. Jiddah (na kwa mujibu wa kauli ya Jurji Zaydaan' bandari ya Shuaibiyah ya siku hizo) ilikuwa ni bandari ya kibiashara iliyoendelea, na kwa bahati, meli mbili za kibiashara zilikuwa tayari kung'oa nanga kutoka pale kwenda Ethiopia.

Wale Waislamu, wakichelea kufuatwa na Waquraishi, walilidhihirisha lengo lao na kuichukulia safari ile na waliipanda meli hiyo kwa haraka mno, kwa malipo ya nusu dinar. Taarifa inay- ohusu kule kuondoka kwa Waislamu vile vile iliyafikia masikio ya machi- fu wa Makkah na wakawatuma watu kwenda kuwarudisha, lakini walipofika kule bandarini, ile meli ilikuwa tayari ishaondoka pwani ya Jiddah nayo haikuweza kuonekana.

Kuwafuata wale waliochukua hifadhi kwenye nchi ya kigeni kwa ajili tu ya usalama wa imani yao, ni uthibitisho wa dhahiri wa uovu wa Waquraishi. Wahamaji hawa wamezitelekeza mali zao, watoto wao, makazi yao, na kazi zao lakini machifu wa Makkah hawakuwa tayari kuwaacha. Wazee wa 'Dar-un Nadwah' waliyachelea matokeo ya safari ile na wakalijadili jambo hili miongoni mwao, na majadiliano haya tutayaeleza baadae.

Watu wa kikundi hiki hawakuwa wa familia moja, na kwa mujibu wa kauli ya Ibn Hishamu[2] kila mmoja wa hawa watu kumi alikuwa wa familia tofauti.

## Kikundi Cha Pili Kwenda Ethiopia

Uhamaji mwingine ulifanyika baada ya huu wa kwanza na kiongozi wa msafara wa wahamaji wa kikundi cha pili alikuwa ni Bwana Ja'far bin Abu Twalib. Uhamaji huu ulitayarishwa kwa uhuru kamili na hivyo basi, baadhi ya wahamaji walifaulu kuwachukua wanawake wao na watoto pamoja nao.
Matokeo yake yakawa kwamba idadi ya Waislamu nchini Ethiopiua ilifikia themanini na watatu, na kama tukiwahesabu watoto waliochukuli- wa kule au waliozaliwa nchini mle, idadi yao itazidi hii.

Kama alivyoeleza Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Waislamu waliiona nchi ya Ethiopia kuwa ni nchi yenye kustawi na hali ya hewa tulivu na huru. Bibi Ummi Salama, mkewe Abi Salama, ambaye baadaye aliipata heshima ya kuolewa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anasema hivi kuhusiana na nchi ile:
"Tulipokaa Ethiopia tulijiona kuwa tuko chini ya ulinzi wa mlinzi aliye bora zaidi. Hatukupata taabu yoyote ile au kulisikia neno baya lolote kuto- ka kwa yeyote yule."

Kutoka kwenye beti za mashairi zilizotungwa na baadhi ya wahamaji hawa, inabainika kwamba hali ya hewa ya Ethiopia ilipendeza mno. Maelezo kwa kirefu yanaweza kuonekana kwenye Siirah-i Ibn Hisham.[3]

# Waquraishi Wapeleka Wajumbe Wao Kwenye Baraza La Ethiopia

Machifu wa Makkah walipopata taarifa juu ya uhuru na maisha ya amani ya Waislamu kule Ethiopia, miali ya chuki iliwaka nyoyoni mwao, wali- ingiwa na wasiwasi kutokana na maisha ya furaha waliyokuwa wakiishi huko, kwa kuwa nchi ile ilithibitika kuwa pepo kwa ajili yao. Waliogopa mno isije ikawa kwamba Waislamu wakapata kuwa karibu na Negus (Mtawala wa Ethiopia) na wakaweza kumvutia kwenye ile dini ya Uislamu na hivyo wakatayarisha kuivamia Penisula ya Uarabuni wakiwa na jeshi lililoandaliwa vizuri.

Wazee wa 'Darun Nadwah' walikutana tena na wakaamua kwa pamoja kuwapeleka wajumbe kwenye mahakama ya Ethiopia na kutayarisha zawadi zifaazo kwa ajili ya Mfalme na mawaziri wake ili kuipata hisani yao, na kisha kuwashtaki Waislamu wahamiaji hao kwa upumbavu na ujinga na kuzusha dini.

Ili mpango wao huo uweze kupata ushindi wa haraka waliwachagua watu wawili kutoka miongoni mwao wafahamikao kwa hila na vitendo vyao vya kuidanganyifu. Hapo baadae mmoja wao akaja kuwa mzinguaji katika nyanja ya siasa. Kura ziliwaangukia 'Amr bin Aas na Abdullah bin Rabi'ah. Raisi wa 'Darun Nadwah' aliwapa maagizo kwamba kabla ya kukutana na yule Mtawala wa Ethiopia kwanza waanze kuwapa zawadi wale mawaziri na kufanya mazungumzo nao kabla ya kumwona Mfalme na wajaribu kuwavutia kwao, ili kwamba watakapokutana na Mfalme, wao (mawaziri) waweze kuwaunga mkono. Baada ya kupewa maelezo mafupi juu ya jambo hilo, wale watu wawili waliondoka kwenda Ethiopia.

Wale mawaziri wa Ethiopia walikutana na wale wajumbe wa Waquraishi na wale wajumbe baada ya kutoa zile zawadi, walizungumza nao hivi: "Kikundi cha vijana wetu kimeyakana mafundisho ya jadi zao na wameizungusha dini iliyo kinyume na dini yetu na ile yenu. Hivi sasa wanaishi nchini mwenu. Wazee na machifu wa Waquraishi, kwa nia njema wanamwomba Mtukufu Mfalme wa Ethiopia kuwafukuza upesi iwezekanavyo.

Vile vile tunapenda kwamba baraza la mawaziri lituunge mkono mbele ya Mfalme. Na kwa vile tunautambua vizuri upungufu na njia na tabia za watu hawa, ingalifaa kwamba jambo hili lisijadiliwe kabisa pamoja nao, na kiongozi wa nchi hii vile vile asiwape nafasi ya kusikilizwa!"
Wale watu wenye choyo na wasioona mbali (yaani wale mawaziri) wali- wahakikishia uungaji mkono wao kamili. Siku iliyofuata wale wajumbe wa Waquraishi walikaribishwa kwenye Baraza la Kifalme na baada ya kutoa salaam zao na kuwakilisha ujumbe zawadi zao waliwasilisha ujumbe wao kwa yule Mfalme kwa maneno haya: "Ee Jalali Mtawala wa Ethiopia! Baadhi ya vijana wetu walio wapumbavu wamechukua hatua ya kuhubiri dini isiyoafikiana na dini rasmi ya nchi yako wala ile ya jadi zao. Hivi karibuni watu hawa wamekimbilia nchini mwako na wanapata faida visivyostahili kutokana na uhuru ulioko nchini humu. Wazee wa Waquraishi, kwa dhati kabisa, wanakuomba Jalali Mfalme, kwamba itolewe amri ya kuwafukuza ili waweze kurudi nchini mwao. . . ."

Mara tu baada ya hotuba ya wajumbe wa Waquraishi kuisha, sauti za mawaziri, waliokuwa

wamekizunguuka kiti cha enzi cha mfalme, zilipaa. Wote waliwaunga mkono wale wajumbe wa Waquraishi na wakayathibitisha yale waliyoyasema. Hata hivyo, dalili za hasira zilijidhihirisha usoni mwa yule Mtawala mwenye hekima na mwadilifu wa Ethiopia. Akiwapinga wajumbe wa baraza lake aliunguruma, akisema: “Hili haliwezekani! Siwezi kuwakabidhi watu hawa wawili wale watu waliokimbilia nchini mwangu bila ya kufanya uchunguzi ufaao. Ni muhimu kwamba hali na mambo yote ya wakimbizi hawa lazima vitazamwe.

Nami nitawarudisha kwao baada tu ya maelezo ya watu hawa wawili juu yao kuwa yamethibitishwa kutokana na uchunguzi. Kwa upande mwingine, kama yaliyosemwa na hawa watu wawili juu yao hayatokuwa kwenye msingi wa ukweli halisi, basi sitawatelekeza, bali nitawapa msaada zaidi!”

Baada ya hapo mjumbe maalumu wa baraza la mfalme alitumwa kwa hawa Waislamu wahamiaji nae akawaleta mbele ya Mfalme bila ya kuwapa taarifa za kabla. Bwana Ja’far bin Abi Twalib alitambulishwa kuwa ndiye mwakilishi wa Waislamu hawa. Baadhi ya Waislamu walikuwa na wasiwasi kuhusu jinsi atakavyozungumza na yule mtawala wa Kikristo wa Ethiopia. Ili kuwatoa wasiwasi, Bwana Ja’far aliwaeleza ya kwamba atazungumza na Mfalme yule sawa kabisa na vile alivyosikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akisema.

Mfalme wa Ethiopia alimgeukia Bwana Ja’far akasema: “Kwa nini mmeyakana mafundisho ya jadi zenu na kuifuata dini isiyoafikiana na dini yetu wala ile ya jadi zenu?”
Bwana Jafar akamjibu yule Mfalme, akisema: “Tulikuwa watu wajinga na tulikuwa tukiyaabudu masanamu. Hatukuacha kula mizoga. Daima tulijitia kwenye vitendo viovu. Hatukuwaheshimu jirani zetu. Wale waliokuwa wanyonge na wasiokuwa na msaada miongo– ni mwetu walionewa na waliokuwa na nguvu.

Tuligombana na kupigana na ndugu zetu, tuliutumia muda mrefu sana katika njia hii hadi mtu mmoja kutoka miongoni mwetu, aliyekuwa na maisha ya kabla ya hapo yaliyokuwa angavu mno na safi, aliamka na kutuita, kwa amri ya Allah, kumwabudu Mungu Mmoja na wa Pekee na akatukataza kuwahimidi masanamu kuwa ni jambo baya. Vile vile ametuamrisha kuvirudisha vitu vya watu vilivyowekwa dhamana kwetu, kuyaacha maovu, kuwatendea wema ndugu na majirani zetu, na kuacha umwagaji wa damu, kushughulika na mambo haramu, kutoa ushahidi wa uongo, kunyakua mali ya mayatima na kuwasingizia wanawake mambo mabaya.

“Ametuamrisha kusali, kufunga, na kulipa kodi kutokana na utajiri wetu (zaka). Tumemwamini na tukajishughulisha na kumhimidi na kumwabudu Allah, Mmoja tu. Tunaamini kuwa kile alichokitangaza kuwa halali, kuwa ni halali kweli. Hata hivyo, Waquraishi wamekuwa wakitutendea ukatili na wametutesa mchana na usiku ili kwamba tuikane dini yetu; na turejee kwenye ibada ya mawe na masanamu na kutenda kila aina za matendo maovu. Tumewapinga kwa muda mrefu hadi nguvu yetu ikamalizika. Tukiwa tumekata tamaa juu ya maisha yetu na mali zetu tumekimbilia Ethiopia ili kuiokoa dini yetu. Sifa njema za uadilifu wa Mtawala wa Ethiopia zimetuvutia kama sumaku, na vile vile, hivi sasa tunayo imani kamili juu ya uadilifu wake.”[4]

Hotuba ya Bwana Ja'far yenye mvuto na ya kusisimua, ilimvutia mno yule Mfalme, kiasi kwamba yeye Mfalme, akichuruzikwa na machozi machoni mwake, alimwambia Bwana Ja'far: "Hebu soma chochote kile kutoka kwenye Kitabu cha Mbinguni cha Mtume wenu."

Bwana Ja'far akasoma aya kadhaa kutoka Surat Maryam. Aliendelea kuzisoma aya hizo na akalieleza lengo la Uislamu kwa ukamilifu juu ya usafi wa Bibi Maryam na cheo cha juu cha Nabii Isa (a.s.). Alikuwa bado hajaimalizia Sura ile wakati yule Mfalme na maaskofu walipoanza kulia kwa sauti kuu na ndevu zao pamoja na kurasa za vitabu vilivyofunuliwa mbele yao vikalowa machozi yao!

Baada ya hili, kwa muda fulani hivi kilitawala kimya barazani mle na mvumo ulikoma. Kisha Mfalme akaingilia na kusema: "Maneno ya Mtume wao na yale aliyoyaleta Nabii Isa yametoka kwenye chanzo cha nuru kimoja na kilekile. Nendeni zenu. Sitawakabidhi kwenu katu!"

Kinyume na vile mawaziri na wale wajumbe wa Waquraishi walivyotegemea, mkutano ulimalizika kwa hali ngumu upande wao na haukuwapo mwali wowote wa matumaini uliosalia!

'Amr bin Aas' aliyekuwa mjumbe na mtu mwerevu, alifanya mazungumzo na yule mwenzie Abdallah bin Rabi'ah na akamwambia: "Ni bora kesho tuitumie njia nyingine na inawezekana kwamba njia hiyo ikamalizika katika maangamizo ya wahamiaji hawa. Kesho nitamwambia Mfalme wa Ethiopia kwamba kiongozi wa wakimbizi hawa anayo itikadi maalumu juu ya Nabii Isa isiyoafikiana hata kidogo na mafundisho ya Ukristo."

Abdullah alimkataza asifanye hivyo na akamweleza ya kwamba miongoni mwa wakimbizi wale walikuwapo watu walio ndugu zao. Hata hivyo, ushauri wake haukufaulu. Siku iliyofuata walikwenda kwenye lile baraza la Mfalme pamoja na mawaziri wote. Mara hii walijifanya kwamba ni wenye huruma na kuiunga mkono dini rasmi ya Ethiopia na kuzilaumu itikadi za Waislamu juu ya Nabii Isa na wakasema: "Watu hawa wana itikadi maalumu juu ya Isa zisizoafikiana hata kidogo na mafundisho na itikadi za ulimwengu wa Kikristo na kuwako kwa watu kama hawa ni hatari kwa dini rasmi ya nchi yenu. Ingalifaa kwako wewe Jalali Mfalme, kuulizia jambo hili kutoka kwao."

Wakati huu yule Mtawala wa Ethiopia mwenye hekima aliamua kulichunguza jambo lile pia na akaamrisha kwamba wale wahamiaji waletwe mbele yake. Wale Waislamu waliifikiria tena sababu ya kuitwa kwao tena. Ilionekana kana kwamba imefunuliwa kwao kwa mzinduo sahihi kwamba lengo la kuitwa kwao lilikuwa kuulizia kuhusu itikadi yao juu ya mwasisi wa Ukristo. Bwana Ja'far akatajwa tena kuwa ndiye mzungumzaji wao.

Ja'far alikuwa tayari kaisha waahidi marafiki zake ya kwamba atazungumza tu yale mambo ya habari ile aliyoisikia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Negus alimgeukia yule mjumbe wa wakimbizi na akasema: "Nini itikadi yenu juu ya Nabii Isa?"

Bwana Ja'far akajibu akasema: "Itikadi yetu juu ya Isa ni ile tuliyofundishwa na Mtukufu Mtume wetu.

Alikuwa mja na Mtume wa Allah. Alikuwa Roho na Neno la Allah ambalo kwalo Alimbariki Maryam."

Mfalme wa Ethiopia alifurahi mno kuyasikia maelezo ya Bwana Ja'far, na akasema: "Ninaapa kwa jina la Allah! Isa hakuwa na cheo cha juu zaidi ya hiki!" Wale mawaziri na watu waliopotoka hawakuupenda haya maoni ya Mfalme. Hata hivyo, licha ya maoni yao hayo, Mfalme alizisifu itikadi za Waislamu na akawapatia uhuru kamili! Akazitupilia mbali zile zawadi za Waquraishi mbele ya wajumbe wao na akasema: "Mungu hakuchukua hongo yoyote kutoka kwangu aliponipa mamlaka haya. Hivyo basi, haifai kwamba mimi nilimbikize utajiri kwa njia kama hii!"[5]

## Kurejea Kutoka Ethiopia

Baadhi ya watu waliohamia Ethiopia waliitoka nchi ile na kurudi Hijaz kutokana na taarifa za uongo kwamba Waquraishi wamesilimu. Waliporejea walitambua ya kwamba taarifa walizozipokea zilikuwa za uongo na shinikizo na maonevu juu ya Waislamu yalikuwa bado haya- jakomeshwa. Hivyo basi, wengi wao walirudi Ethiopia na ni wachache wao tu waliouingia mji wa Makkah, imma kwa siri au kwa kuwa chini ya ulinzi wa Quraishi mwenye nguvu.

Uthman bin Maz'un aliingia Makkah chini ya ulinzi wa Walid bin Mughayrah[6] na akasalimika kutokana na ukatili wa adui. Hata hivyo, aliweza kuona kwa macho yake mwenyewe kwamba Waislamu wengine walikuwa wakionewa na kuteswa na Waquraishi. Uthman alihuzunika sana kuuona ubaguzi huu. Hivyo basi, alimwomba Walid atangaze hadharani kwamba mwana wa Maz'un hayuko tena chini ya ulinzi wake, ili kwamba yeye nae aweze kuwa mwenye hali ile ile walimo Waislamu wengine, na ashirikiane nao kwenye huzuni na masikitiko yao. Hivyo Walid akatangaza msikitini akisema:

"Kuanzia muda huu Ibn Maz'un na hayuko chini ya ulinzi wangu." Na Uthman nae akasema kwa sauti kuu: "Nathibitisha hivyo." Mara tu baada ya hapo, Labid, mshairi wa Uarabuni aliingia msikitini na kuanza kuisoma Qaswida yake maarufu mbele ya ule mkusanyiko mkubwa wa Waquraishi.

Alisema: "Kila kitu si chenye uhakika na ni chenye kuidanganya akili, isipokuwa Allah tu." Uthman akasema: "Umesema kweli." Hapo Labid akaisoma sehemu ya pili ya ule mstari wa ubeti. "Baraka zote za Allah ni zenye kugeukageuka." Uthman akaingiwa na wasiwasi na akasema: "Umekosea. Mibaraka ya Ahera ni yenye kudumu na ya milele."
Labid aliuchukulia vibaya mkanusho wa Uthman na akasema: "Enyi Waquraishi! Hali yenu imebadilika.

Hapo kale mikutano yenu ilikuwa na mipangilio mizuri na wafuasi wenu hawakuhuzunika. Ni tangu lini hali yenu ikabadilika? Ni nani huyu?" Mmoja wa wale waliokuwapo pale akasema: "Yeye yu mpumbavu aliyeikana dini yetu na kumfuata mtu aliye kama yeye. Usiyasikilize maneno yake." Kisha yule mtu aliamka na kumpiga Uthman kofi la nguvu usoni mwake hadi ukageuka kuwa mweusi (kwa kuvilia damu).

Walid bin Mughayrah akasema: "Ewe Uthman! Ungelisalia kwenye ulinzi wangu yasingalikupata yote

haya."

Uthman akamjibu akasema: "Mimi niko chini ya ulinzi wa Allah Mwenyezi!" Walid akasema: "Niko tayari kukupa ulinzi tena." Uthman akamjibu akasema: "Sitaukubali hata kidogo."[7]

## Ujumbe Wa Wakristo

Matokeo ya kuhubiri Uislamu kulikofanywa na wahamiaji yalikuwa kwamba, ujumbe wa kuuliza juu ya Uislamu ulitembelea Makkah kwa niaba ya kituo cha kidini cha Wakristo wa nchini Ethiopia. Walikutana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) msikitini na wakamwuliza maswali fulani. Mtume (s.a.w.w.) alijaribu kujibu maswali yao kisha akawaomba wasilimu na akawasomea baadhi ya aya fulani fulani za Qur'ani tukufu.

Hizi aya za Qur'ani zilizibadili akili zao katika hali ambayo walianza kutiririkwa na machozi kutoka machoni mwao bila ya kukusudia na wakauamini Utume wake mara moja, na wakazithibitisha dalili zote za yule Mtume aliyeahidiwa ambaye bishara zake wamezisoma kwenye Injili.

Abu Jahl aliuchukia mkutano huu wenye shauku na uliomalizika kwa mafanikio. Kwa ukali mwingi, aliwaambia wajumbe wale: "Watu wa Ethiopia wamekutumeni katika ujumbe wa uchunguzi na haikuwa nia ya watu wale kwamba muikane dini ya jadi zenu. Mimi sidhani kwamba wako watu wapumbavu zaidi yenu kwenye uso wa ardhi hii."

Wale watu waliyatamka maneno ya upatanishi katika kumjibu huyu Firauni wa Makkah, aliyetaka kuificha miali ya jua yenye kutia nguvu, kama vile lifanyavyo wingu jeusi na hivyo wakaukomesha ugomvi ule.[8]

## Ujumbe Wa Waquraishi

Ujumbe wa watu wa Ethiopia ulikuwa njia ya kuwaamshia Waquraishi na wao nao wakaamua kufanya utafiti. Kikundi cha watu wakiwamo Harith bin Nasr na 'Uqbah bin Abi Mu'it walikwenda Yathrib (Madina) wakiwa ni wajumbe wa waquraishi kwa lengo la kwenda kuuliza maswali juu ya Utume na 'mwito' wa Muhammad kwa Wayahudi. Wanachuoni wa Kiyahudi waliwashauri wajumbe wale kwenda kumwuliza Mtume Muhammad (s.a.w.w.) maswali yafuatayo:- Ni nini uhakika wa roho?

Hadith ya watu waliotoweka kwenye siku za kale (watu wa pango). Ujasiri wa yule mtu aliyesafiri upande wa Mashariki na upande wa Magharibi wa ulimwengu (Dhulqarnayn).

Waliwaambia wajumbe hawa kwamba, kama Muhammad ataweza kuyajibu maswali haya, hawana budi kuwa na uhakika kwamba yu mteule wa Allah, lakini kama akishindwa kutoa majibu yaliyohitajika, hawana budi kumchukulia kwamba yu muongo astahiliye kuondoshelewa mbali upesi iwezekanavyo.

Wajumbe wale walirejea Makkah katika hali ya furaha mno na wakawaarifu Waquraishi juu ya maswali yaliyotajwa hapo juu. Hivyo, ukatayarishwa mkutano ambao Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) nae alikaribishwa. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwaambia kwamba alikuwa akisubiri ufunuo wa Allah

kuhusiana na yale maswali matatu.[9]

Ule ufunuo wa mbinguni ukafika. Jibu la swali la kwanza kuhusiana na roho liko kwenye Surah Bani Israil, 17:85. Na kuhusu yale maswali mengine mawili, yamejibiwa kwa kirefu mwenye Surah al-Kahf, aya ya 9- 28 na 83-98. Majibu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kirefu, juu ya maswali haya matatu yanapatikana kwenye vitabu vya tafsiri na hayahitaji kurudiwa hapa.

1. Siirah-i Hisham, Juzuu 1, uk. 321; na Tarikh-i Tabari, Juzuu 2, uk. 70.
2. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 245.
3. Siirah-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 353.
4. Tarikh-i Kamil. Juzuu 2, uk. 54-55.
5. Siira-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 338.
6. Siira-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 369
7. Siira-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 371.
8. Siira-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 392.
9. Siira-i Ibn Hisham, Juzuu 1, uk. 300-301.

# Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al-Itrah Foundation:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr

20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake

59. Umaasumu wa Mitume – Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume – Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah – Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah – Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliy onyooka
75. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al – Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali
87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi

98. Swala ya maiti na kumlilia maiti

99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)

100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu

101. Hadithi ya Thaqalain

102 Fatima al-Zahra

103. Tabaruku

104. Sunan an-Nabii

105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)

106. Idil Ghadiri

107. Mahdi katika sunna

108. Kusalia Nabii (s.a.w)

109. Ujumbe -Sehemu ya Pili

110. Ujumbe - Sehemu ya Tatu

111. Ujumbe - Sehemu ya Nne

112. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa

113. Shiya N'abasahaba

114. Iduwa ya Kumayili

115. Maarifa ya Kiislamu.

116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza

117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili

118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu

119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne

120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano

121. Johari zenye hekima kwa vijana

122. Safari ya kuifuata Nuru

123. Historia na sera ya vijana wema

124. Myahudi wa Kimataifa

125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi

126. Visa vya kweli sehemu ya kwanza

127. Visa vya kweli sehemu ya Pili

128. Muhadhara wa Maulamaa

129. Mwanadamu na mustakabali wake

130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza

131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili

132. Khairul Bariyyah

133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi

134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.

135. Yafaa ya kijamii

136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu

137. Taqiyya
138. Mas-ala ya Kifiqhi
139. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili

## Back Cover

Historia inatuambia kuhusu ustaarabu mkubwa uliopita hapo kale na mwishowe ukapotea. Hivi sasa tumebakiwa na masalio na magofu bubu yanayotukumbusha zama za kale za wanaadamu zilizochakaa. Imam Ali (a.s.) alimpa dokezo la fikra zake mwanawe ambalo ni lenye kuhusika na jambo hili.

Alisema: "Mwanangu mpenzi! Ingawa muda wa maisha yangu si mkubwa kama ule wa watu wengine waliofariki dunia kabla yangu, lakini nilijichukulia hadhari kubwa kujifunza maisha yao.
Kwa juhudi nyingi niliyapitia matendo yao na nilizifikiria fikra na matendo yao.

Niliyachunguza masalio ya vitu vyao visivyo na uhai na magofu, na nikayafikiria maisha yao kwa makini mno kiasi kwamba nilijihisi kana kwamba niliishi na kufanya kazi pamoja nao tangu kwenye zama za awali za historia hadi kwenye hizi nyakati zetu, na ninayajua yaliyowatendea mema na yaliyowadhuru."

Hakika sifa moja ya historia iangazayo mno ni kwamba, inazichukua taarifa za maisha ya watu wakuu wa kale. Hakika watu hawa waliiunda historia kwa kuwa walileta mapinduzi na mabadiliko kwenye mtindo wa maisha ya wanaadamu.

Miongoni mwa hawa watu wakuu, hakuna hata mmoja aliyeishi maisha yenye mambo mengi, ya kimapinduzi na yenye maana kama aliyoishi Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.).

Hakuna yeyote miongoni mwao aliyeziacha athari za kudumu kwenye jamii aliyojitokeza kama alivyofanya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Huu ni ukweli uliokubaliwa na karibuni wanahistoria wote - wawe ni wa Mashariki au wa Magharibi.

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com [16]
Katika mtandao: www.ibn-tv.com [17]

---

**Source URL:** https://www.al-islam.org/fr/ujumbe-sehemu-ya-kwanza-jafar-subhani#comment-0

**Links**

[1] https://www.al-islam.org/fr/person/jafar-subhani

[2] https://www.al-islam.org/fr/organization/al-itrah-foundation-0

[3] https://www.al-islam.org/printpdf/book/export/html/25265

[4] https://www.al-islam.org/printepub/book/export/html/25265

[5] https://www.al-islam.org/printmobi/book/export/html/25265

[6] https://www.al-islam.org/fr/person/dhikiri-u-m-kiondo

[7] https://www.al-islam.org/fr/tags/history

[8] https://www.al-islam.org/fr/tags/knowledge

[9] https://www.al-islam.org/fr/tags/shariah

[10] https://www.al-islam.org/fr/tags/arabs

[11] https://www.al-islam.org/fr/tags/surah

[12] https://www.al-islam.org/fr/person/imam-ali

[13] https://www.al-islam.org/fr/person/prophet-muhammad

[14] https://www.al-islam.org/fr/person/imam-jafar-al-sadiq

[15] https://www.al-islam.org/fr/person/prophet-ibrahim

[16] mailto:alitrah@raha.com

[17] http://www.ibn-tv.com